

13 MEI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Nne - Tarehe 13 Mei, 2013

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha, 2013/2014.

MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

13 MEI, 2013

**MHE. PAULINA P.GEKUL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI
YA UPINZANI WA WIZARA YA UJENZI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ujenzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 189

Fedha kwa Ajili ya Kuadhimisha Sherehe za Kitaifa

MHE. HENRY D. SHEKIFU (K.n.y. MHE. MARY P. CHATANDA) aliliza:-

Katika kuadhimisha sherehe mbalimbali za Kitaifa nchini Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana.

Je, Serikali itakuwa tayari kuokoa fedha kwa kuachana na Bajeti kubwa zilizotengwa kwa machapisho ya fulana (*T-Shirts*) na tafrija fupi ili fedha hizo ziweze kusaidia katika shughuli nyingine?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, URATIBU, SERA NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maadhisho ya sherehe za kitaifa nchini yamekuwa yakigharimu Serikali fedha nyingi sana. Hata hivyo Serikali inachukua hatua mbalimbali ili kupunguza gharama hizo, Ofisi yangu imeandaa mapendekezo ya kupunguza idadi ya namna ya kuadhimisha sherehe hizo kwa mwaka. Wizara zimeshatoa mapendekezo kwa Waziri Mkuu ya namna maadhisho ya sherehe mbalimbali zilizo chini ya Wizara hizo zingeweza kuadhimishwa sasa ili kupunguza gharama.

Kwa mfano baadhi ya sherehe za kisekta zimependekezwa kuanzishwa kila baada ya miaka mitatu mpaka mitano badala ya kila mwaka. Mapendekezo haya yanashibiri kujadiliwa katika vikao vya maamuzi ili yaanze kutumika rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imepunguza kwa kiasi kikubwa bajeti ya uchapishaji wa fulana, kanga na vipeperushi kama sehemu ya maadhisho ya sherehe za kitaifa. Sare zinazotolewa kama *T-Shirts* zinalenga makundi maalum tu ambayo ni muhimu kwa ajili ya ushereheshaji na kufikisha ujumbe mahsus (kauli mbiu) kuhusu maadhisho husika kwa wananchi. Aidha, tafrija fupi hufanyika wakati wa sherehe za Uhuru na Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tafrija hizi maalumu hasa kwa wageni maarufu wa Kimataifa ambao huwa wanaalikwa na Ikuu na ni wageni wa Mheshimiwa Rais.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa sherehe hizi ni muhimu na kufanyika Kitaifa pia ni muhimu, lakini hakuna umuhimu wa kuzihamisha kutoka eneo moja kwenda eneo lingine maana zikihamishwa inabidi kuweka miundombinu mipyä kwa ajili ya sherehe hizo, kama vile sherehe za mwenge. Hivi ni kwa nini tusiwe na eneo moja tukajua kuwa hili ndilo eneo litafanyika sherehe hizo ili kupunguza gharama? (*Makof!*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, URATIBU, SERA NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninapenda kumjibu Mheshimiwa Shekifu, swali lake la nyongeza kama ifauatavyo:-

Ni kweli kuwa baadhi ya sherehe huwa zina hama, zinazunguka kila Mkoa na lengo ni kuhamasisha wananchi wa maeneo mbalimbali ili waweze kushiriki katika kutekeleza shughuli zinazoendana na Sera za Sherehe zile. Kwa mfano sherehe za nanenane zinafanywa Kikanda zinazunguka na Mwenge madhumuni yake ni tofauti kabisa na sherehe zingine kwa sababu unahimiza upendo nanupendo huwezi

kuwa katika Mkoaa mmoja. Upendo uko kila Mkoaa na unahitaji kuhimiza upendo. Unazunguka kuhamisha matumaini kutoka Mkoaa mwagine kwenda Mkoaa mwagine. Kwa hiyo nilifkiri shughuli za mwenge haziwezi kulinganishwa sana na shughuli zingine. Lakini tunachoangalia katika madhimisho ya Sherehe ya nchi siku nyingine kwa mfano siku ya maziwa, siku ya maji, siku ya nyuki na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi zinaweza kuwa *fixed* katika kipindi fulani lakini baadhi ya sherehe zingine na pengine tunafikiru tunaweza kuangalia kuzunganisha. Kwa mfano Sherehe ya sabasaba sasa imekuwa ya maonyesho ya biashara. Lakini ukienda nanenane na yenyewe ina maonyesho ya biashara. kwa hiyo, kuna sherehe zingine ambazo tunaweza kuzunganisha zikafanyika mahala pamoja kitaifa na nyingine zikawa zinazunguka ili wananchi wote wapate bahati ya kuona na kuangalia maonyesho ya biashara. (*Makofii*)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, inashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na maadhisho ya sherehe mbalimbali ambazo Waziri amezitaja lakini kuna hili la uzinduzi wa mwenge wananchi wamekuwa wakichangishwa, lakini wakati huohuo Serikali imekuwa na ndimi mbili kwamba mchango wa mwenge ni hiari lakini wafanyabiashara na wananchi na ofisi mbalimbali wamekuwa wakiandikiwa na Serikali kwamba wachangie. Ninaomba nipate kauli ya Serikali kwa nini wananchi hawa wanachangishwa wakati kuna fungu linatengwa kwa ajili ya kazi hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, URATIBU, SERA NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na ninajua kuwa Mikoa huwa inachangisha fedha lakini moja ya kazi za mbio za mwenge siyo zile shamrashamra tu mbio za mwenge mara nyingi huwa zinafanya shughuli nyingine za kuhimiza maendeleo, kama alama ya kichocleo cha kuhimiza shughuli za maendeleo ya kujitolea wannchi katika maeneo yale. (*Makofii*)

Kwa hiyo, wakati mwingine Mikoa huwa wanachangisha fedha kukamilisha shughuli fulani ambazo kwa pamoja wamezianzisha ili angalau zihitimishwe na shughuli ya mwenge.

Mheshimiwa Gekul. Kuandikiwa barua na Serikali kuchangia siyo kosa maana hata kwenye arusi huwa tunaalikwa kuchangia na hatuchangi humu ndani kuna makadi mengi watu wanatuchangisha lakini hatuchangi,kama hupendi huchangi lakini kuandika barua ya mchango kwa Mkoa siyo mbaya. Lakini ungeniambia wanazimisha hili ni suala jingine.

Haturuhusu kulazimishwa lakini wananchi wanaruhusiwa kuchangia maendeleo yao kama pale Manyara wanavyochangia kujenga shule, Zahananti na miundombinu mingine kwa faida yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotolewa na Serikali ni kwa ajili ya kugaramia mahitaji ya wale vijana wanaokumbiza mwenge kitaifa, mafuta ya mwenge wenyewe na gharama za usafiri za wale vijana.

Lakini kwa maendeleo yanayohamasishwa na mwenge katika eneo lile wananchi lazima wachangie ili miradi yao waliyoibuni wao wenyewe iweze kukamilika.
(Makof)

Na. 190

Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Ngaramtoni

MHE. DKT. AUGUSTINE L . MREMA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga stendi ya mabasi katika Mji wa Marangu Mtoni ambao unakuwa kwa kasi na una magari mengi?

13 MEI, 2013

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt.Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Mji wa Marangu Mtoni unakuwa kwa kasi kubwa na kusababisha ongezeko la magari yanayotoa huduma katika maeneo hayo. Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imeshatembelea eneo hilo la Marangu Mtoni na kulikagua, pamoja na kuandaa michoro na gharama za ujenzi wa stendi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za ujenzi wa stendi hiyo zimekadiriwa kuwa shilingi 32,300,000/= pendekezo hili liko katika hatua za awali za kujadiliwa katika vikao vya Halmashauri ili mradi huo uweze kutengewa fedha na kutekelezwa ili kuondokana na msongamano mkubwa wa magari, pikipiki na biashara zilizopo katika eneo hilo. Mradi huu utakapokamilika unakusudiwa kuongeza vyanzo vya mapato kwa Halmashauri kutokana na huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha mpango huo unafanikiwa, Halmashauri imepanga kutumia wadau wengine wa maendeleo kwa kuzingatia Sera ya *Public Private Partnership (PPP)* ili kujenga na kuendesha mradi huo na kuufanya kuwa endelevu.

MHE. DKT. AUGUSTINE L . MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninaomba kuuliza swali lifuatalo:-

Kwa kuwa msongamano pale Marangu mtoni ni mkubwa na pale Marangu Mtoni ni Kituo cha barabara kubwa Himo, kwenda Kilema na kwenda Rombo.

Sasa swali ni kwamba badala ya kungojea Halmashauri ya Moshi ambayo haina hela tena kwenye jibu lako umesema wanapanga, ina maana hizo hela hazipo na mimi ningetaka ile stendi ijengwe haraka na mapema ili kuondoa huo msongamano pale.

Ninaomba kujua Serikali kuu ina utaratibu gani wa kusaidia hizi Halmashauri wanapokuwa na miradi mizuri na mikubwa kama huu wa kujenga stendi ya basi Marangu Mtoni. Mnawasaidiaje kutumia benki, kutumia Bank guarantee, pamoja na mambo mengine kama hayo ili miradi iweze kutekelezeka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini kama tunaziachia Halmsahauri uwezo hawana hili swali litasusua hata miaka kumi jibu wewe Nailbu Waziri unasemaje hapo (*Makofi/Kicheko*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri unasemaje kuhusu hilo. Naibu Waziri Majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaoomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, ninatambua ni Naibu Waziri Mkuu Mstaafu. Ni kweli kuwa Halmashauri zetu zina miradi mingi ambayo inaweza kutekelezeka kwa ngazi ya Halmashauri yenyelewe lakini iko ile miradi ambayo haiwezi kutekelezeka kutokana na gharama kuwa kubwa.

Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inao mpango ambao ni endelevu wa Halmashauri kuzitumia Bodi ya Mikopo ya TAMISEMI lakini LAPF pamoja na *TIB* na siku za karibuni hapa tumeingia makubaliano na *TIB*. *TIB* imekubali kukopesha Halmashauri kwa kupata dhamana kutoka TAMISEMI yenyelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunayo mifano ya Halmashauri ambazo zimejenga vituo vyake vya mabasi na miradi yake mingine kwa kutumia mikopo kutoka maeneo niliyoyataja kama vile Halmashauri ya Jiji la Mwanza wamejenga Kituo chao cha Mabasi lakini pia Moshi yenyelewe imejenga pale kupitia mikopo kutoka Bodi ya Mikopo.

Kwa hiyo, Halmashauri hiyo hiyo na kwa kuwa tayari imeshafanya *study* pale Marangu Mtoni inaweza kuingia utaratibu huu wa kukopa kutoka kwenye Bodi ya Mikopo au *LAPF* pamoja na *TIB* ambayo sasa imekubali kusaidia Halmashauri zote nchini kuzikopesha na kuendesha miradi ambayo ni mikubwa kwa kuandika maandiko ya pamoja kati ya *TIB* na Wataalamu walio katika Halmashauri yenyelewe ili kuratibu miradi hiyo iweze kutekelezeka utaratibu huo unaweza kusaidi Halmashauri zote nchini.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa stendi hii ya Marangu Mtoni ni sehemu ya kupitia kwenda Mlima Kilimanjaro ambako ni sekta ya Utalii, kwenda Kenya nchi ya jirani kupitia Rombo na kwa kuwa stendi hii inatakiwa ijengwe kwa kuangalia future zaidi ya miaka 20- 30 ijayo na hapa zimetengwa milioni 32.

Je, Serikali kuu itachangia utaalamu wa namna gani ili stendi ikitengwa miaka 20 ijayo angalau wafanye na eneo la ujenzi ni dogo wawewe kujenga *under packing facility* ya kisasa ambayo ina *complex* kwa ajili ya future ya miaka 20 au 30 ijayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na nimeona una wazo zuri na ninajua kuwa Mkoa wa Kilimanjaro una tataizo kubwa la ardhi. Kwa hiyo wazo la kujenga *underground station* ni wazo zuri sana, sasa ili kuweza kukusanya nguvu za kitaalamu kujenga kituo cha miaka mingi, bado nimeeleza kuwa kama mtaingia mikopo na *TIB* upo uwezekano Halmashauri yoyote ile zaidi ya Moshi

kuwa na kikao cha pamoja cha wataalam wetu wa Halmshauri lakini na wale wa *TIB* wakatengeneza andiko linaloweza kupendekeza ujenzi wa kituo cha kudumu cha miaka mingi na kwa gharama yoyote ile na bado *TIB* inaweza kutukopesha fedha tukajenga kituo cha aina ambayo mnakihitaji pale Moshi. Kwa hiyoo ni maamuzi yenu wenyewe huko Moshi. (*Makofi*)

Na. 191

Utekelezaji wa Mradi ya Maji katika Halmashauri ya Wilya ya Bukoba

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Kutokana na matatizo makubwa ya maji katika maeneo mengi ya Bukoba Vijijini, vijiji kumi vilipewa kipaumbele katika miradi ya maji, lakini ni vijiji vitano tu ambavyo utekelezaji wake umeanza.

(a) Kwa nini vijiji vya Kibona, Ibwera, Lukindo na Katale viliachwa katika utekelezaji huo?

(b) Ni lini utekelezaji wa miradi hiyo ya maji utaanza katika vijiji hivyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini imekamilisha usanifu wa miradi katika vijiji 10 walivyochagua kama vipaumbele vyao ambavyo ni Bintuntu, Kibirizi, Itongo, Lukindo, Katalale, Mashule, Kitanya. Ibwera

na Kyamulaile. Ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Mashule umekamilika mwezi Machi, 2013 na wananchi wanapata huduma ya maji. Halmashauri inakamilisha taratibu za kusaini mkataba na Mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa kijiji cha Kyamulaile na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa vijiji viwili vya Kibona na Ktahya zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miradi kwa vijiji vilivyobaki vya Bituntu, Kibirizi, Itongo, Lukindo, Katale na Ibwera utafanyika katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba kwa mwaka 2012/2013 ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 612.02 na hadi sasa kiasi cha shilingi milioni 416.8 sawa na asilimia 70 kimeshatolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. (Makof)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu, lakini ninapenda nimwulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama jibu ni hilo ni kijiji kimoja ambacho kimepata maji katika miradi hii ya Benki ya Dunia, pale Bukoba Vijijini tuna vijiji 92, kati ya vijiji 92 ni kimoja tu ambacho kimepata maji sasa bado hali ya maji ni mbaya sana na kuna dhiki kubwa ya maji.

Kwa hiyo, wananchi wa Bukoba Vijijini wamejipanga chini ya Uongozi wa Mbunge wao wamenunua mashine ya kuchimba visima ili waweze kupunguza tatizo la maji. Lakini kuwa na mashine ya kuchimba kisima haitoshi kuna mahitaji ya mabomba, mahitaji ya pampu, mahitaji ya mtandao.

Naomba kujua sasa, Serikali itatusaidiaje kutoa huduma katika kusaidia kusambaza maji katika vijiji kwa msaada wa wananchi wenyewe na mashine yao na nguvu zao?

Swali la Pili; Kata ya Maruku na Kanengereko Serikali ilijenga mtandao wa maji miaka ya sitini na sabini mwanzoni maji yakatoka katika shule, katika vijiji na maeneo mbalimbali, lakini kwa sababu ni muda mrefu mtandao huu umechakaa na maji hayatoki na dhiki ya maji ipo pale pale.

Wananchi wameunda umoja wa walaji wa maji chini ya Mhandisi wa Maji wa Wilaya na wanatambulika na wamebainisha kwamba inatakiwa kupatikana shilingi milioni 500 ili huduma hii irejee ya kutoa maji kwenye vijiji hivyo vyta Kata hizo mbili, wamejiunga na wamechanga hela kidogo kwa nguvu zao kwa kujitahidi wamefikisha kama milioni mia moja hivi.

Naomba kujua kama Serikali ipo tayari kutusaidia sasa, kuongezea kiasi kinachopungua cha milioni kama mia nne ili wananchi hawa tena warudishiwe huduma ya maji. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mbunge kwa swali zuri alilouliza. Kwamba mpaka sasa ni kijiji kimoja kimepata maji na ana vijiji vingi. Kama tulivyoeleza kwenye bajeti na baada ya kuongezewa fedha ni kwamba mwaka huu mpaka mwezi wa tisa tutakuwa tunakamilisha utekelezaji wa miradi ya vijiji vitano kila Wilaya na katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 vijiji vingine vitano vitaongezeka na hivyo kufika kumi(10).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kumhakikishia kwamba vijiji tutavipunguza na hii kasi itaendelea. Lakini kwa pamoja kwamba tutasaidiaje wale wananchi ambao wamechanga na ule mradi ambao umechakaa sasa hautoi maji ni kwamba katika Bajeti yetu tumetoa kipaumbele kwa miradi inayoweza kutoa matokeo ya haraka, miradi inayotoa matokeo ya haraka ni kama hii ambayo tayari imeshaanzishwa ipo ambayo ukiweka fedha inaanza kutoa maji moja kwa moja. (*Makofii*)

13 MEI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo miradi miwili kama alivyotangaza Waziri tutaichukua tutawasiliana ili tuone kwamba inaingia ili iweze kutekelezwa katika mwaka 2012/2013 na 2013/2014. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Kwa Wabunge wageni, mwaka 2000 Mbunge wa Bukoba Vijiji aliwa akiitwa Mheshimiwa Kinyondo Maheremu, ye ye aliwa anajiiwa Mbunge wa Vijiji vya Bukoba, siyo Bukoba Vijiji, kwa sababu baadhi ya Vijiji kule ni Miji midogo. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka.

Na. 192

Upatikanaji wa Michango ya Maji inayotolewa na Wananchi

MHE. CLARA D. MWATUKA aliuliza:-

Katika sehemu nyingi nchini wananchi huchangia fedha kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa huduma za maji. Hata hivyo michango hiyo hypotea pasipo kutimiza malengo yaliyokusudiwa:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha fedha hizo za wananchi zinafuatiliwa na kutimiza lengo husika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) aliujibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchangiaji wa wananchi katika miradi ya maji unazingatia matakwa ya Sera ya Maji ya mwaka 2002. Sera hiyo inawataka wananchi washiriki katika kupanga, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi

ya maji katika maeneo yao. Utaratibu huu wa kisera unasaidia wananchi kuona kuwa miradi hiyo ni ya kwao wenyewe na hivyo kufanya miradi kuwa endelevu.

Kulingana na Sera hiyo, kila mradi unatakiwa kuundiwa chombo cha watumia maji kwa mujibu wa sheria ya maji na usafi wa mazingira ya mwaka 2009. Serikali imeandaa na kusambaza mwongozo kwenye Halmashauri zote nchini kwa ajili ya uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazokusanya kutokana na michango ya jamii zinapaswa kutunzwa katika akaunti ya mradi husika. Chombo cha watumiaji maji kinapaswa pia kusoma taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi mitatu kwenye mkutano Mkuu wa Kijiji. Aidha, Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri anatakiwa kukagua matumizi ya fedha hizi zinazotokana na michango ya wananchi. Inapobainika kwamba upo ufujaji wa matumizi ya fedha hizo kuwa ni mabaya, wahusika huchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kwa Naibu Waziri.

Pamoja na majibu mazuri aliyonjibui, tangu wananchi walipochangishwa fedha hizi hivi sasa ni zaidi ya miaka mitatu au minne maji bado hajapatikana. Je, ni lini sasa hayo maji yatapatikana?

Swali la Pili; pamoja na kusema kwamba kunakuwa na chombo cha watumiaji hayo maji, tangu wamechangisha mpaka hivi sasa haijulikana ni kiasi gani kilipatikana kutokana na pesa zile ambazo walikatwa kwenye mazao yao kama korosho na ufuta, hawajui ni kiasi gani kilipatikana na kwamba kila wakiuliza ghalani ambako walitumia kukatwa hizo pesa majibu hayakuwa yanapatikana, wengine wakasema ni Mtendaji wa Kata, walipomwendea Mtendaji wa Kata majibu hayakueleweka.

Je, Serikali inachukua hatua gani sasa kupata jibu la ukweli juu ya hili ambalo walikuwa wanachangisha na huyu Mtendaji ambaye alikuwa anapokea hizo pesa? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza la namna ambavyo Kijiji kimechukua muda mrefu kutekeleza mradi wa maji huku kukiwa kuna michango ya wananchi. Hili lingeweza kumalizwa na Halmashauri yenyewe ambayo pia inafanya uratibu kama wananchi na wenyewe wangeweza kutoa taarifa kwenye Halmashauri yao. Kwa kuwa Mbunge wewe ni mmoja kati ya Wajumbe wa Baraza la Madiwani kwenye Halmashauri yako na unatoka kwenye maeneo ambayo yana matatizo ungeweza kuwa wa msaada mkubwa wa kuijulisha Halmashauri ili Mkaguzi wa Ndani aende kwenye vijiji husika kufanya ukaguzi wa ndani ili apate majibu ya namna gani fedha zilizochangwa na wananchi zilivyoweza kutumika. Ili sasa Mhandisi wa Maji katika Halmashauri ya Wilaya aweze pia kutekeleza mradi huo kwa haraka kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la makato yao na namna ambavyo utoaji wa taarifa haupo. Kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi, inapotokea kuna mtendaji ye yote kwenye kijiji na wamechangisha michango ya aina ye yote zaidi ya huu wa maji, bado mtendaji huyo kama ameshindwa kutoa taarifa kwenye Kijiji husika ya mapato na matumizi ya michango ya wananchi anapaswa kuchukuliwa hatua kali dhidi ya jambo hili.

Kama hili ndivyo lilitivo, sasa namwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Masasi ambako najua Mheshimiwa Mbunge anataka, kufanya ufuatiliaji kwenye vijiji vilivyotamkwa na Mbunge na Mbunge uwasiliane na Mkurugenzi kumwambia ni Kijiji gani ili hatua kali ichukuliwe dhidi ya Mtendaji huyo ambaye mpaka sasa ameshindwa kuchukua hatua kwa kushindwa kusoma mapato na matumizi kwenye mikutano mikuu ya kijiji. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Lema swalii la nyongeza.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Nabu Spika, nakushukuru. Tatizo kama hili lipo katika Jimbo la Arusha Mjini Kata ya Terati, ambako wananchi walichangishwa fedha miaka mitatu iliyopita na hawajawahi kusomewa taarifa ya mapato na matumizi ya jambo hilo. Lakini vilevile Diwani wa Kata hiyo pamoja na Kamati yake walienda kutafuta msaada kwa *Donors* na wakapata *pipe* za kuweka maji kutoka Kata ya Lemara mpaka Kata ya Terati, lakini mpaka leo tunavyoongea, michango waliyochanga wananchi pamoja na michango mingine ambayo ni takribani milioni thelathini hajulikani iliko. Nilikwenda na Mkuu wa Wilaya hapo kufuatilia jambo hilo kulikuwa na Mkutano mkubwa wa wananchi na bado Mkuu wa Wilaya akaagiza Diwani alete *statement* ya mambo yote kuhusu michango ya wananchi na mpaka leo hajafanyika na tunapoongea sasa hata *DC amekiri kwamba* jambo hilo halijafanyika.

Ninaomba Serikali itoe jibu kama ambavyo Naibu Waziri amesema kuhusu Mbunge mwenzangu.

NAIBU SPIKA: Sina hakika kama Naibu Waziri unajua hilo, basi tafadhali majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la uchangishaji michango kwenye maeneo yote ya vijiji ambayo yapo chini ya Halmashauri zetu na Kata zote zipo chini ya Halmashauri hizo hizo na michango hii ni halali.

Kitu ambacho kinatakiwa kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi kwamba michango ile ni lazima iweze kutolewa taarifa ya mapato na matumizi kwa ngazi husika, kama michango ilikusanywa na Mtendaji wa Kata kuna *WDC* ipo pale ambayo Diwani kama Mwenyekiti na wale Wenyevitii wa Vijihi ambao wamechangia michango ile wanapaswa kupata taarifa hizo. (*Makof!*)

Kama taarifa hizo hazipatikani sasa Diwani ambaye anaingia kwenye Halmashauri na kama Mbunge pale ulikuwa unafahamu jambo hili, bado mnawenza kulilingiza na kulitolea maamuzi kwenye Baraza lenu la Madiwani kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa pia kumekwishatolewa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya bado kuna haja ya kufanya ufuatiliaji kwa sababu Mkuu wa Wilaya ndiye msimamizi wa Serikali eneo lile na kama alishachukua yeye sasa naamini kwa kauli yangu sasa Mkuu wa Wilaya anaweza akafanya ufuatiliaji wa kina ili kupata matokeo sahihi ya kwanini michango hii hajenda kwenye maeneo husika.

Hii ni sambamba na swali lako la pili bado linaingia kwenye eneo lilelile kwamba ni lazima ukaguzi wa ndani ufanyike kupitia kwa Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa ili kubaini kiwango kilichoharibiwa na kutoweka, ili sasa hatua kali ziweze kuchukuliwa na uongozi stahiki ikiwemo na Mkurugenzi Mtendaji ambaye ni mwajiri wa watendaji wetu wa Kata na Vijiji pia.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na swali linalofuata nitambue uwepo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja nasi, kwa sababu wiki iliyopita kwa siku kadhaa hatukuwa nae. Karibu sana Bungeni. Sasa tuelekee Rau na Kishumundu swali la Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami. (*Makof*)

Na. 193

Ukarabati wa Barabara ya Rau Madukani - Kishumundu

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI aliuliza:-

Barabara ya lami kuanzia Rau Madukani hadi Kishumundu hukarabatiwa kwa kujaza kifusi badala ya kurudishia lami:-

(a) Je, utaratibu wa kukarabati barabara za lami ni kurudishia lami au kujaza kifusi?

(b) Je, Serikali sasa iko tayari kukarabati barabara hiyo kwa kuweka lami badala ya kutumia kifusi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Paul Cyril Chami, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Rau Mdukani Kishumundu ina urefu wa kilomita 10.0 barabara hii imekuwa ikihudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa muda wote kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kipande cha barabara hii ambacho kimewekewa lami ni kilomita 3.5.

Aidha, ni kweli kwamba kipande hiki cha barabara kiko katika hali mbaya kwa sasa kiasi cha kuhitaji matengenezo makubwa. Barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo kila mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2009/2010 zilitengwa shilingi 9.0, mwaka wa fedha 2010/2011 shilingi milioni 14.5, mwaka wa fedha 2011/2012 shilingi milioni 17.0 na mwaka 2012/2013 wa fedha zilitengwa shilingi 21.5. Fedha hizi zilipokelewa kama zilivyo kuwa zimeidhinishwa na Bunge na kutumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya mara kwa mara, sehemu korofi na matengenezo ya kawaida.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini iliyofanyika mwaka 2009/2010 katika barabara hii ilibaini kwamba zinahitajika zaidi ya shilingi bilioni 8 ili kuweza kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami umbali wa kilomita 10.0.

Hata hivyo, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa na inapitika katika kipindi chote cha mwaka.

Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, Halmashauri imeidhinishiwa shilingi milioni 46.2 ya fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na matengenezo ya muda maalum ya barabara hii sawa na urefu wa kilomita 10.0. (*Makofi*)

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nifanye masahihisho, kwanza mimi siyo Dkt. Paul Cyril Chami, mimi ni Dkt. Cyril August Chami.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali mawili ya nyongeza kwanza ni kwamba upo utaratibu kwamba barabara ikishajengwa kwa lami mara nyingi huwa inashughulikiwa na *TANROADS*, lakini kwa barabara hii ya Rau Madukani hadi Kishumundu imehamishiwa Halmashauri ambako hakuna fedha na ndiyo maana ikibanduka inarudishiwa kifusi.

Je, Waziri sasa atawaambia wana Moshi Vijijini kwamba barabara hii itarudishiwa *TANROADS* ili iendelee kukarabatiwa kwa lami badala ya kuwekwa kifusi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Waziri kwenye majibu yake amesema kwamba kipande ambacho kimewekwa lami ni kilomita tatu na nusu tu, lakini ukweli ni kwamba barabara yote kilomita 10 mpaka Kishumundu ilikuwa na lami lakini kutokana na kuwa chini ya Halmashauri imebanduka polepole mpaka imekuwa sasa inaonekana kama barabara ambayo haikuwahi kuwekwa lami.

Je, Waziri uko tayari kuja kutembelea Kishumundu ili ye ye pamoa na *TANROADS* na mimi tuweze kujihakikisha kwamba barabara hii ilikuwa na lami tangu miaka ya 1972? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niombe radhi kwa jina hilo na sasa tunalitambua kama ni Dkt. Cyril August Chami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ilikuwa na lami ambayo ilijengwa miaka mingi iliyopita, na ilipojengwa ilikuwa haijaingia kwenye utaratibu huu wa barabara kuwa chini ya *TANROADS*.

Fedha ambayo sasa hivi tunaitenga kama ambavyo tumeeleza kwamba tathmini ya mahitaji ya barabara hii kuirudishia kuwa kiwango kiwango cha lami kwa kilomita zote kumi ni zaidi ya bilioni nane, na kwa ngazi ya Halmashauri peke yake haina uwezo wa kutenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya ujenzi wa barabara moja ya kilomita 10 kwa kiwango cha lami.

Lakini pia barabara hii ili iweze kuingia kwenye mpango wa *TANROADS* kwa sasa siyo rahisi kwa sababu barabara hii ni ya Halmashauri ya Wilaya. Hata kama ilikuwa imejengwa kwa lami na kwa kuwa ujenzi wa muda mrefu baada ya kipindi kile cha uhuru.

Taratibu za kuihamisha kutoka ngazi ya Wilaya kwenda ngazi ya *TANROADS* ni lazima kwanza Baraza la Madiwani la Halmashauri husika lifanye maamuzi na wapendekeze, na wakishapendekeza ngazi ya Baraza la Madiwani litaingia kwenye Kamati ya ushauri ya Wilaya inayotambulika kwa jina la *DCC*. *DCC* nayo ikiipendekeza itakwenda kwenye ngazi ya Mkoa kwenye kamati ya ushauri ya Mkoa inaitwa *RCC*, *RCC* Meneja wa *TANROADS* Mkoa yupo, na Meneja wa *TANROADS* Mkoa anaweza kuipokea kwanza kama ana fedha.

Lakini mbili kama barabara hiyo inakidhi vigezo na vigezo muhimu vyta barabara kupandishwa kwenda *TANROADS* kwanza kwa idadi ya magari mengi yanayopita kwenye barabara hiyo.

Lakini pia matumizi makubwa ya kibashara kwenye barabara hiyo na idadi ya watu ambao wanaitumia barabara hiyo ndiyo baadhi ya vigezo ambavyo vinakidhi. Kama Meneja wa *TANROADS* kuititia *RCC* akiridhika na akiwa na Bajeti sasa inaweza ikapandishwa hadhi kutoka ngazi ya Wilaya ambako sasa barabara hiyo ipo na kuipeleka kwenye ngazi ya *TANROADS*.

NAIBU SPIKA: Maswali mawili mafupi ya nyongeza, Mheshimiwa Rajabu na Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa. Mheshimiwa Rajabu.

MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Kwa sababu tatizo hili la Moshi Vijijini liko *almost* katika Halmashauri zetu nyingi hapa nchini, na tumegundua kwamba fedha nyingi za mfuko wa barabara zinapelekwa katika Halmashauri zetu.

Je, Halmashauri zinakosa watalaam wa kushughulikia barabara hizi. Je ni lini Serikali itakuwa tayari kuunda kitengo kama *TANROADS* kudhughulikia barabara zetu katika Halmashauri?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba katika Halmashauri zetu Wahandisi au watalaam tulionao ni wale wale waliosoma na kubobe katika fani hizi na kwa hiyo wanao uwezo pia wa kufanya thathmini ya ujenzi wa barabara ya ngazi hizo, lakini pia kufuata vigezo vya watalaam ambao wanaweza kuijenga barabara yenye we kwa vigezo ambavyo vimeainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbili, tatizo hili ni kweli linafanana na barabara nyingine zote lakini nataka niwaambie barabara tulizonazo zimegawanyika katika maeneo manne, tunazo barabara za vijiji ambapo vijiji

vyenyewe vinashughulikia barabara hizo, tunazo barabara za Halmashauri ambapo Halmashauri zenyewe zinaratibu kuitia Wahandisi wenyewe, lakini pia tuna hizo za *TANROADS* na Barabara Kuu.

Lakini kwa ngazi ya Halmashauri zetu zinaratibiwa na Halmashauri na zinatangazwa kandarasi na wakandarasi wanaopatikana ili waweze kujenga barabara bora kwa kiwango anachokihitaji Mbunge ni suala la uteuzi wa Wakandarasi ambao pia wanaweza kujenga kwa kiwango kikubwa cha kutosha kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Halmashauri zinajenga barabara hizi kuitia mfuko unaoitwa *Road Fund* ambao upo kwenye Halmashauri. Kwa hiyo chombo unachokihitaji ambacho kwa ngazi ya Mkoa kinaitwa *TANROADS* huku sisi tuna *Road Fund* ambayo pia inashughulikia ujenzi wa barabara hizi ndogo. Kwa hiyo, wazo na kuunda chombo kingine zaidi ya hicho, inaweza kufanywa pia na Wizara husika.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, tatizo la Wilaya ya Moshi Vijiji linafanana na tatizo la Wilaya ya Mbeya Mjini, naomba kumwuliza Naibu Waziri, katika Kata ya Ruanda barabara ya Kabwe kupita llemi, mpaka kutokea Isanga, barabara ile ya lami imejaa kifusi na mashimo na inafukiwa ama inajazwa kifusi hicho kwa nguvu ya wananchi wenyewe.

Naomba sasa Naibu Waziri atueleze, kama alivyouliza Dkt. Chami, ni nini mkakati wa Serikali pamoja na kwamba amejibu ni Halmashauri, lakini tunavyoolewa barabara ikishakuwa ya lami kwa muda mrefu inahamia *TANROADS*? Naomba majibu Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Naibu Waziri majibu ya swali hilo la Wananchi wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi tafadhali majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza si kweli kwamba ikishajengwa barabara kuwa ya lami inahamia *TANROADS*. Barabara za lami zinaweza zikabaki Halmashauri. Lakini si sahihi barabara ikichakaa kuweka udongo kwenye barabara ya lami. Kwa hiyo naomba sana Wakurugenzi wa Halmashauri na Wahandisi watumie teknolojia sahihi inayokubalika katika matengenezo ya barabara.

Katika fedha za mfuko wa barabara tumetenganisha, barabara za lami na barabara za udongo au changarawe. Kwa hiyo, fedha inayotolewa kwa ajili ya lami basi watumile lami kutengeneza kipande ambacho kimeharibika kulingana na Sheria ya Mfuko wa Barabara. Ahsante sana.

Na. 194

Idara ya Usalama Kulinda Raslimali za Taifa

MHE. VINCENT J. NYERERE aliuliza:-

Je, Idara ya Usalama wa Taifa inatoa msaada gani kwa Taifa kuhakikisha kuwa Raslimali za Taifa hazimilikiwi kifisadi na wachache ili Taifa liwe salama kwa vizazi vijavyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA
ali jibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Idara ya Usalama wa Taifa yameainishwa katika Kifungu Namba 5 cha Sheria Namba 15 ya mwaka 1996 ya kuundwa kwa Idara ya Usalama wa Taifa. Majukumu hayo ni kukusanya taarifa za kiusalama kuzifanya uchunguzi na kuishauri Serikali kwa lengo la kuchukua hatua zinazostahili. Mionganoni mwa taarifa hizo ni pamoja na zinazohusu vitendo vya hujuma dhidi ya uchumi na raslimali za taifa kama vile kumilikiwa na watu wachache kwa manufaa yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo huchukuliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa raslimali zilizopo zinanufaisha taifa sasa na baadaye. Hivyo basi, Idara ya Usalama wa Taifa imekuwa ikitekeleza majukumu hayo kwa weledi na umakini mkubwa ili kuhakikisha linaendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu. (*Makofii*)

MHE. VINCENT J. NYERERE: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekirii kwamba Idara ya Usalama imekuwa ikifanya kazi kwa weledi na umakini mkubwa na kwa taarifa nilizonazo Idara ya Usalama wako katika Uwanja wa Ndege wa *KIA* na walitoa ushauri kwa Serikali dhidi ya ndege ya *Qatar* iliyotua tarehe 22 mwezi wa kumi na moja mwaka 2010 na kuondoka tarehe 25 mwezi wa kumi na moja mwaka 2010 ikiwa na wanyama. (*Makofii*)

Kwa kuwa Serikali ilipuuzia taarifa za Usalama wa Taifa. Ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watumishi wa Serikali?

Swali la pili, kama hatua hazijachukuliwa Serikali inawashauri nini wananchi wachukue hatua dhidi ya Serikali? Ahsante sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya msingi nimezieleza kazi za Idara ya Usalama wa Taifa na pengine kwa taarifa ya Watanzania nikazirudia.

Sheria ile inazungumza *Functions of the Service shall be nimatefsiri kwa Kiswahili.* Kukusanya habari zinazohusu Usalama na kumtaarifu Waziri au mtu ambaye anaona inafaa apewe.

Pili, kuwashauri Mawaziri kuhusu masuala ya Usalama yahusuyo Idara au Wizara zao. Tatu kushirikiana kadri inavyowezekana na vyombo vingine vya Serikali na Ofisi za umma ndani na nje ya Tanzania kama kuisaidia kutekeleza majukumu na mwisho kumtaarifu Rais au mtu mwingine, au Mamlaka kama Waziri anavyoelekeza kuhusu eneo liwezalo kuwa na vitendo vya ujasusi, kuhujumu uchumi na ugaidi. Idara ya Usalama wa Taifa haikamati mtu, haishtaki mtu. Kazi yake ni kukusanya habari na kushauri. Sasa inapokuwa imeshauri na akawa mtu hakufuata ushauri, Mamlaka iliyopo juu yake ndio inapaswa kumchukulia hatua. Idara ya Usalama kazi yake ni kutoa ushauri.

Sasa swali la pili unauliza kwamba inapofika katika hiyo wananchi wanafanyaje? Mimi naomba sana inapofika hatua kama hiyo Usalama wa nchi yetu hili ni suala la sisi wote, waliomo ndani ya Idara ya Usalama wa Taifa na wananchi wote kwa ujumla. Kinachotakiwa kufanya ni kutoa taarifa katika vyombo vinavyohusika na litaweza likachukulia hatua. Tunazo Kamati za Ulinzi na Usalama ngazi ya Taifa, tuna Baraza la Usalama wa Taifa, Wilayani kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa. Pale ambapo unaona kwamba suala hili huuridhiki nalo ni kupeleka katika chombo kinachohusika.

Ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ni mtu mzito sana kama unazo taarifa za aina hiyo niletee. Nitazifikisha kwenye Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa liweze kufanyiwa kazi.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwa kuwa chombo hiki ni muhimu sana katika ustawi na maendeleo ya nchi, kijamii na kiuchumi na kwa kuwa siku za hivi karibuni baadhi ya Wanasiasia, baadhi ya vyombo vya habari na baadhi ya wananchi wamekuwa

wakikishutumu sana chombo hiki. Jambo ambalo linaweza kupelekea kisiaminike ndani ya jamii na kwa kuwa ukweli wa tuhuma hizi wanazo, wanaotuhumu na labda na chombo chenyewe.

Sasa swalii, je ni lini chombo hiki kitachukua hatua ya kufanya uchunguzi au kama uchunguzi umeshafanyika ni lini taarifa za uchunguzi huo zitakapotolewa kwa umma ili hatua ziweze kuchukuliwa dhidi ya baadhi ya wanaotuhumiwa ndani ya chombo chenyewe au dhidi ya wale wanaotuhumu kwa njia ambayo inakifanya chombo kidhalilike. Lakini taarifa zao siyo za kweli na uchunguzi huo uwekwe kwa wananchi kwa namna ya kurejesha imani kwa jamii?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ni swalii moja tu. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikubaliane naye. Wako watu Wanasiasa kwa kujitafutia umaarufu au kwa kutafuta ile Waingereza wanasema *Scape Board* yaani kutafutia visingizio. Mtu umeshtakiwa unasema, nisingeshtakiwa Usalama wa Taifa.

Mtu umekamatwa una mali ya mtu, ukiulizwa Usalama wa Taifa. Nataka kusema hivi, hilo suala analosema ni kweli. Ninachotaka kusema ni kwamba unauliza lini chombo kitachukua hatua kufanya uchunguzi.

Nataka kusema hivi, baada ya kauli hizo za wanasiasa kutoka mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora, niliandaa maelezo ya kukanusha kwamba Idara ya Usalama wa Taifa kwa vyovyote vile haihusiki na tuhuma hizo.

Lakini asubuhi yake suala likawa limetinga Mahakamani. Kwa taratibu ya Sheria yetu katika nidhamu ya Utawala Bora ambayo ndiyo Wizara ninayoisimamia, siweza kuendelea na hatua zile kwa sababu suala liiliwa Mahakamani. (*Makof!*)

13 MEI, 2013

Na. 195

Mbegu Bora ya Mahindi Aina ya DKC 8053

MHE. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA aliuliza:-

Mbegu bora ya mahindi aina ya DKC 8053 inayozalishwa kuitia utafiti inastawi vizuri kijiji Mbola (*Millennium village*) Wilayani Uyui tangu mwaka 2006 na ina uwezo wa kutoa gunia 30-40 za mahindi katika eka moja; na sasa mbegu hiyo inatumiwa na baadhi ya ya wakulima Jimboni Igala katika Kata za Goweko, Igala, Nsololo na Kizengi kwa sababu ya ubora wake. Lakini bado Serikali inatoa ruzuku kwa mbegu ya Kilima ambayo ina uwezo wa kutoa gunia 18-22 kwa eka moja kwa kutumia mbolea ushauri wa Maafisa Ugani:-

Je, Serikali haioni itawaongeza kipato wakulima na maeneo hayo kwa kubadilisha mbegu ya Kilima na kuwauzia kwa ruzuku mbegu aina ya DKC 8053 au *pioneer variety* ili wawze kununua mbegu hiyo ambayo inavumilia ukame na ina mavuno mengi ikilinganishwa na Kilima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA aliibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Eng. Athuman R. Mfutakamba, Mbunge wa Igala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mbegu za aina ya DKC 8053 zinavumilia ukame na kutoa mavuno mengi ukilinganisha na mbegu aina ya Kilima ambayo hutoa mavuno machache kidogo zaidi. Hata hivyo, mbegu hiyo ya DKC 8053 imebainika kushambuliwa na wadudu wa hifadhi (*storage pest*) kwa haraka zaidi. Aidha, ladha ya unga wake haiwavutii sana wateja wengi na inatoa pumba nyingi wakati wa kukoboa ukilinganisha na mbegu nyingine au mahindi yatokanayo na mbegu aina ya Kilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha, wakulima wanufaika hupatiwa Seti (*package*) ya vocha tatu za mbolea ya kupandia, mbolea ya kukuzia na mbegu bora za mahindi yaani (Chotara au mbegu mchanganyiko (*OPV*) au mbegu bora za mpunga ambapo wakulima wa eneo husika huchagua aina ya mbegu wanayoihitaji baada ya kushauriwa na maafisa ugani waliopo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo utaratibu uliopo ni kwa wakulima wa Halmashauri husika ya Wilaya kuwasilisha Wizarani mahitaji halisi ya aina ya mbeguza mahindi wanazopendelea kwa mfano mbegu za DKC 8053 ili Wizara iweze kuwasiliana na kampuni ya mbegu husika ili wakulima hao waweze kusambaziwa mbegu hiyo katika utaratibu wa ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Wizara ni kuwapatia wakulima mbegu na mbolea kwa utaratibu ulio bora na ulio na maslahi mapana kwao na kwa maana hiyo Sekta ya Kilimo nchini. Aidha, mkakati huo utatokana na ushauri wa kitaalam kutoka kwa wataalam wa ngazi zote wakiwemo wakulima wenyewe, watafiti, wagani katika ngazi ya Wilaya. Mawakala wa mbolea, mbegu na madawa pamoja na watendaji wa Kurugenzi ya Maendeleo ya Mazao ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wakulima wa Wilaya ya Uyui kuwa kazi kubwa ya Serikali ni kuboresha mawasiliano baina ya wadau ili kuongeza uzalishaji na tija ya mazao mbalimbali nchini. (*Makofii*)

MHE. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa majibu mazuri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa mbegu bora ni sehemu ya kuongeza mazao.

Je, Serikali ina utaratibu gani kwa kukamilisha bwawa la Goweko na Igalula kwa ajili ya umwajiliaji?

Swali la pili, ni kule Mexco mbegu ambazo zinazalishwa na *Mosanto Agro Science*, *Dow Agro Science* pamoja na *Pioneer* pamoja na kufanyiwa majaribio, lakini Serikali ya Mexco imekataza kwa sababu ya *Pollination pollution* kwa sababu ya kuharibu mbegu asilia.

Je, tumefanya utafiti kiasi gani kuwa na mbegu zetu hizi zitahimili masuala ya tabia nchi na pia uwezekano labda wa kansa kwa hizi mbegu mpya ambazo hatuna uzoefu nazo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:
Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza kwa sababu swali lenyewe lilikuwa linahusu mbegu bora katika kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mahindi. Lakini Mheshimiwa ameulizia suala la bwawa la Goweko na bwawa la Igulula.

Naomba niseme tu kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba katika hii miradi ya umwagiliaji, kwa sasa hivi tuna skimu kama 160 hivi mbalimbali nchi nzima ambazo ziko katika hatua tofauti. Zingine zinakwenda kwenye utekelezaji nzuri, zingine utekelezaji wake siyo nzuri sana kama tulivyoona Wilaya ya Bahi wiki iliyopita.

Kwa hiyo, ninachoomba nimhakikishie kwa kuwa mimi na Wabunge wa Tabora tumekubaliana kwamba tutakwenda Tabora katika kipindi hiki au baada ya Bunge hili, pamoja na mambo mengine tutakwenda kufuatilia utekelezaji wa bwawa hili la Goweko na bwawa la Igulula ili tuone kama linakwenda vizuri au lina mushikeri ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la mbegu za mosanto na mbegu za GMO na kansa. Mimi naomba niseme tu kwamba hili jambo mimi nadhani kila sehemu linapatiwa tafsiri tofauti. Kwa sababu watumiaji wakuu wa GMO ni hao hao Wamarekani, hao hao wa Mexco, hao wa Afrika Kusini na mpaka sasa hivi hata kwenye *AG Index* wenzetu wastani wa umri wao ni miaka 80.

Sisi wastani wa umri wetu ni miaka 55. Sasa hatusemi kwamba matumizi ya GMO yanaongeza umri. Lakini mimi nadhani kuna maelezo mbalimbali ambayo wanasema labda inaongeza kansa. Mimi nadhani wasiwasi wa Mbunge alishaligusia kwamba labda zinapunguza pia nguvu za kiume.

Kwa hiyo, mimi naomba nimsihi tu kwamba hizi tafiti zote bado hazijafanyiwa uhakika sana na hata sisi hapa Tanzania watafiti wetu wanazifanyia kazi kwa bidii sana na kwamba tuna watafiti wenye uwezo mkubwa sana pale Mikocheni ambao watatupatia maelezo ya kutosha kuhusu matumizi au kutokutumia mbegu hizi hapa Tanzania.

Na. 196

Kuuwezesha Mkoa wa Rukwa Katika Nyanja ya Kilimo

MHE. ABIA M. NYABAKARI aliuliza:-

Wananchi wa Mkao wa Rukwa ni wakulima stadi wa mazao ya chakula, lakini bado hali ya maisha ya wananchi iko duni sana:-

Je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuupa Mkao kipaumbele katika kuwezesha Nyanja ya kilimo ili kuinua kipato cha wananchi, Mkao na Taifa kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
aliibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkao wa Rukwa ni moja ya mikoa ya kimkakati katika uzalishaji wa chakula ambapo kwa muda mrefu umekuwa ukizalisha siyo tu chakula kinachotosheleza mkoa huo lakini pia ziada inayozalisha mikoa mingine na pia Hifadhi ya Taifa ya Chakula.

Kwa kutambua hayo Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele katika maendeleo ya kilimo katika kanda hii kwenye *program* mbalimbali za maendeleo ya sekta ikiwa ni pamoja na za *ASDP, TAFSIP, SAGCOT* na kadhalika.

Aidha, Serikali imeondoa vikwazo vyatia wafanyabiashara kununua moja kwa moja mazao ya wakulima hatua ambayo imepanua ushindani naimeongeza bei ya mazao ya mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imetoa zaidi ya shilingi bilioni nne (4) katika kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi 2011/2012 kwa ajili ya miradi kadhaa ya umwagiliaji ikiwemo ya Sakalilo, Katuka, Singiwe, Maleza, Ulimi, Ng'ongo, Lwafi/ Katongolo. Miradi hiyo iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika kipindi hicho pia Serikali imetoa ruzuku ya pembejeo za kilimo (mbolea na mbegu bora) ambapo jumla ya kaya zipatazo 546,647 zimepatiwa ruzuku ya mbolea na mbegu bora katika kipindi hicho.

Aidha, katika kupanua wigo wa uzalishaji kwa lengo la kuhamasisha kilimo cha mazao mbadala, Serikali pia ilitoa ruzuku ya mbegu bora za mtama (tani 10) na alizeti (tani 20).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha mashamba darasa (FFS) 884 yanayowafikia wakulima 22,000 yenye lengo la kufundisha kanuni bora za kilimo zikiwa ni pamoa na teknolojia na matumizi sahihi ya pembejeo. Jumla ya vituo 10 vya rasilimali za kilimo za Kata (*Ward Agricultural Resource Centre (WARCs)*) zenye uwezo wa kuhudumia wakulima 8020 vimejengwa na vimetumika kuwapatia wakulima taarifa na teknolojia mbalimbali za kilimo. Serikali imehamasisha matumizi ya zana bora za kilimo ambapo wakulima wa Mkoa wa Rukwa wamenunua jumla ya matrektta 16 kupitia matrektta ya masharti nafuu ya SUMA JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua nafasi hii ya uzalishaji mkubwa wa chakula wa mkoa wa Rukwa, Serikali inapitia upya vigezo vikuu vinavyoboresha kilimo na kuangalia namna ya kufanya maboresho. Kuongeza tija, ufanisi wa miradi ya umwagiliaji, upatikanaji wa mbolea na madawa yenye viwango bora kwa wakati, masoko na bei za mazao ni mionganoni mwa masuala yanayofanyiwa kazi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wakulima wa Mkoa wa Rukwa kwamba Serikali inatambua mchango

mkubwa wa mkoa huo pamoja na mikoa mingine yenye uzalishaji mkubwa katika kulisha taifa letu hivyo itafanya jitihada za makusudi zitakazoongeza hamasa ya kuzalisha zaidi kwa ajili ya kujikimu na biashara.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Miradi aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri haijakamilika na sababu tuaambiwa kwamba mvua ni nyngi. Sasa mvua imekatika. Naomba uwaambie wana Rukwa ni lini miradi hiyo sasa itakamilika ili tusiendelee kuambiwa kwamba miradi iko katika hatua mbalimbali ya utekelezaji?

Swali la pili. Katika mwaka 2013/2014 Wizara itawezesha mafunzo ya ma-operator 136 na viongozi wao. Kuhusu uendeshaji, matengenezo na utunzaji wa mashine za kuvuna mpunga na usindikaji. Sasa swali langu nilikuwa nauliza. Je, katika hao watu 136 ni watu wangapi watakaochukuliwa katika Mkoa wetu wa Rukwa ukizingatia kwamba sisi ni wakulima stadi wa mpunga? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuta maeneo ya miradi haijakamilika ni kwa sababu kwenye miradi ya umwagiliaji, kuna baadhi ya miradi inaweza ikaanza kupata matumizi kabla haijafikia asilimia ya kukamilika kwake. Mingine haiwezi kupata matumizi kulingana na mazingira maalum ya mradi huo. Ndiyo maana kwenye swali lilitangulia labda niseme kwamba Wizara yetu baada ya kupitia baadhi ya miradi na kuona hatua mbalimbali na utekelezaji kama nilivyosema kwenye swali lilitangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo utekelezaji ni mzuri unaridhisha. Kuna baadhi ya maeneo pamoja na kwamba, pesa zimekwenda utekelezaji sio mzuri. Kwa hiyo, tulichofanya hivi visingizio mvua nyngi, sijui mafuriko, na kadhalika. Tulichosema ni kwamba, kila Kanda ya Umwagiliaji sasa ifanye tathmini ya miradi yake, ili tuone ni wapi pesa zimekwenda, zinatumika vizuri na ni wapi pesa zimekwenda hazitumiki vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo tumeamua kwamba, Mkoa huu wa Dodoma, kwa maana ya Wilaya ya Bahi, Kongwa, Chamwino na maeneo ya hapa, yapate kwanza kama *pilot study*, ili tuone utekelezaji wa miradi hapa kabla hatuiaenda kuona utekelezaji wa miradi mingine. Hapa tutapata mifano ya utekelezaji mzuri na utekelezaji mbaya. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Abia Nyabakari, atambue tu kwamba miradi ya Rukwa kwa umuhimu wa uzalishaji mkubwa unaofanywa Rukwa, tutaifuatilia kwa karibu na mimi mwenyewe nimepewa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la ma-*Operator*, wanaotakiwa ni 136, lakini ma-*Operator* wanaotakiwa wanatakiwa kuwa na uwezo wa ufahamu wa msingi, ili wapewe kazi ya kusimamia mashine hizi za kuvuna mpunga, hatuwezi tu tukamchukua mtu yeoyote. Sasa kama watu 136 wote watapatikana palepale Rukwa na Katavi, itakuwa ni vizuri, lakinji tutaangalia kwanza kwa Mkoa wa Rukwa na Katavi, ili wapatikane pale, ikishindikana tutatoa fursa kwa Mikoa mingine.

Na. 197

Mtandao wa Tigo Kupoteza Mawasiliano

MHE. ABBAS Z. MTEMVU aliuliza:-

Mnamo tarehe 13 Novemba, 2012 majira ya saa tano za usiku hadi tarehe 14 Novemba, 2012 mchana, mtandao wa *tIGO*, ulikuwa umepoteza mawasiliano na nyakati fulani kutopatikana kabisa:-

Je, Serikali, inaweza kutoa ufanuzi juu ya tatizo hilo?

WAZIRI WA SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa, Kampuni ya Simu ya *tiGO* ilipata tatizo la kutokuwepo kwa mawasiliano kuanzia usiku wa tarehe 13 Novemba, 2012 hadi asubuhi ya tarehe 14 Novemba, 2012. Tatizo liliababishwa na hitilafu ya umeme ambao nguvu yake ilikuwa kubwa na kuunguza mfumo wa umeme katika kituo kikubwa cha kampuni hiyo, kilichopo eneo la Saba-Saba, Dar-es-Salaam. Aidha, tatizo hilo liliababishwa pia kuungua na kuharibika kwa betri 4 ambazo zinatunza umeme wa kituo hicho. Baada ya kukosekana kwa nguvu ya umeme iliyosababishwa na hitilafu hiyo, ilipofika saa 12.37 asubuhi, tarehe 14 Novemba, 2012 tatizo hilo liliababishwa vifaa vingine muhimu vya kuunganisha mawasiliano kushindwa kufanya kazi. Vifaa hivyo ni pamoja na *Home Location Register*, *Bay Station Controller*, *Radio Network Controller* na *Mobile Switch Centre*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo hilo, Kampuni ya Simu ya *tiGO* kwa kuhusisha Wataalamu wake, ilifanya jithanda za makusudi kuhakikisha kuwa, mawasiliano yanarejea katika hali ya kawaida ambapo ilifanikiwa kurejesha tatizo la umeme ilipofika saa 1.45 asubuhi ya siku ya tarehe 14 Novemba, 2012. Aidha, kazi kubwa ilikuwa ni ya kuhakikisha kuwa, vifaa vya kiufundi vilivyotajwa hapo juu vinafanya kazi ipasavyo ambapo Wataalam hao walifanikiwa kumaliza tatizo hilo na huduma kurejea hewani ilipofika saa 5.19 siku hiyo ya tarehe 14 Novemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hilo liliababishwa pia wateja wa mitandao mingine kushindwa kuwasiliana na wateja wa *tiGO*. Hata hivyo, robo ya wateja wa *tiGO* ambao wameunganishwa na mitambo mingine ya Kampuni hiyo, iliyopo Mtaa wa Lugoda, Dar-es-Salaam, walikuwa wanaweza kupiga simu kwenda mitambo mingine.

Mnamo tarehe 15 Novemba, 2012 Wizara, illiandikia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), ili kupata maelezo ya kina juu ya tatizo hilo na namna walivyojipanga kuhakikisha kuwa, tatizo hilo halijirudii na kuleta usumbufu kwa wateja. Kufuatia barua hiyo, Kampuni ya Simu ya *tiGO*, ilitoa maelezo pamoja na hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa matatizo kama hayo yanapatiwa ufumbuzi Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, imeanza utaratibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa kampuni zote za simu za mawasiliano, kwa lengo la kulinda maslahi ya watumiaji.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali; Makampuni ya simu haya, yanapoingia mkataba na Serikali, ku-*operate* nchini mwetu yanatakiwa yawe na Mkataba Maalum wa *Service Level Agreement*.

Service Level Agreement hii, inasimamia *Quality Service* ambayo Makampuni haya yanatakiwa yaitoe kwa wale wateja wao na pale ambapo wanaposhindwa kutoa *Quality Service* yanatakiwa wapigwe *fine* kama wanavyofanya nchi nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi zinakusanya mpaka Dola milioni 50 kwa mwaka kwa Makampuni ambayo yanashindwa kutoa *Quality Service*. Nataka kujua je, Makampuni nchini mwetu yanapigwa *fine* ipi au yanaadhibiwa vipi yanaposhindwa kutoa huduma bora kwa wateja wao?

WAZIRI WA SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la ziada la Mheshimiwa Zungu, kama ifuatavayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Sheria yetu ya EPOCA na tuna *Regulations* za EPOCA, ambayo kazi yake kubwa inaangalia *Quality Service Agreement*. Kama Kampuni ya Simu imeshindwa kutekeleza *Quality Service Agreement* ambayo imewekwa kwenye Kanuni hizo za EPOCA, Kampuni hizo zinapigwa *fine; fine* ya kwanza inakuwa ni 5,000,000/= au kifungo miezi 6 ama vyote kwa pamoja.

13 MEI, 2013

Na. 198

Fidia kwa Nyumba Zilizoathirika na Ujenzi wa Barabara

MHE. PAULINA P. GEKUL aliuliza:-

Mradi wa Ujenzi wa Barabara na Minjingu – Babati – Dareda, umesababisha baadhi ya nyumba za wananchi kupata mipasuko katika mitaa ya Ngarenaro – Babati, Maisaka B. Mruki, kutokana na zoezi la ulipuaji:-

Je, Serikali, italipa lini fidia kwa wananchi ambao nyumba zao ziliathirika na mlipuko huo wa baruti?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Minjingu – Babati – Dareda yenye urefu wa kilometra 84.6 ni sehemu ya barabara ya Singida – Babati – Minjingu yenye urefu wa kilometra 223.5 ambayo, utekelezaji wake umekamilika na kufunguliwa na Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, mnamo tarehe 3 Novemba, 2012. Katika kipindi cha utekelezaji wa mradi huu ulipuaji wa miamba kwa kutumia baruti ulisababisha nyufa kwa baadhi ya nyumba za wananchi zilizokuwa karibu na maeneo ya ulipuaji kwenye Mgodi wa Mruki na Mtaa wa Mruki, Maisaka B, Ngarenaro, Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamiliki wote wa nyumba zilizoathirika kutokana na ulipuaji wa miamba hiyo, walishalipwa fidia zao stahiki kulingana na Sheria na Ripoti ya Mthamini wa Serikali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mgodi wa Mruki, jumla ya wamiliki wa nyumba 53 zilizoathirika na mlipuko walilipwa fidia ya jumla ya shilingi 78,281,651.95/=. Katika Mtaa wa Mruki, jumla ya wamiliki wa nyumba 29 walilipwa fidia ya jumla ya 13,284.33/=. Katika Mtaa wa Maisaka B, jumla ya wamiliki wa nyumba 5 walilipwa fidia ya jumla ya shilingi 2,477,700/=. Katika Mtaa wa Ngarenaro, Babati, jumla ya wamiliki wa nyumba 26 wanastahili fidia ya jumla ya 18,588,158.10 ambapo waathirika 15 ndio walikubaliana na tathmini ya nyumba zao na tayari walishalipwa fidia zao stahiki; Waathirika 11 bado hawajaafiki tathmini iliyofanywa. Hawa 11 watalipwa mara baada ya kukubaliana na tathmini.

MHE. PAULINA P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimwombe Waziri, afute kauli yake hiyo ya kusema kwamba, wamiliki wote wamelipwa. Kwa sababu, katika majibu yako ya msingi unajichanganya mwenyewe kwamba, kuna wengine hawajalipwa, wengine wamelipwa. Kwa hiyo, naomba ufute hiyo kauli wakati unarudi maana ni uwongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niulize maswali mawili ya nyongeza. Ili kuepusha usumbufu na udanganyifu katika ulipaji wa fidia, kimsingi wakati baruti hizo zinalipuliwa ilitakiwa wale Wakandarasi waende kwenye *site* waone nyumba za wananchi, *then* walipue, halafu baadaye warudi sasa waone kwamba, ni nyumba zipo zimeathirika wakati walishatembelea awali. Kinachofanyika, huu utaratibu unaofanyika sasa, hawatembelei nyumba za wananchi, wanafanya *post-mortem* wanaenda baada ya kulipua zile baruti, kitu ambacho kinasababisha kwamba, wanashindwa kubaini nani mkweli; naomba nipate Kauli ya Serikali, juu ya huu utaratibu unaotumika sasa ambao kwa kweli, hauwatendei wananchi haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Katika Ripoti waliyopelekewa wananchi wa Ngarenaro na wananchi wa Mruki, Ripoti ambayo imetoka kwa Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na madini walioenda kuthamini zile nyumba za wananchi kwamba, wanastahili au hawastahili fidia. Ripoti

ile imeweka wananchi katika *categories* 3; kwanza wanaostahili, pili wasiostahili, tatu wanaostahili, lakini wakajadiliane na Wachina kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu. Ni lini Serikali ya CCM imeikabidhi Tanzania kwa Wachina? Kwa sababu, wananchi wanastahili fidia, wanaambiwa wakajadiliane na Wachina. Kama hamjakabidhi taratibu za kuongoza nchi hii kwa Wachina, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Gekul, ameshakuja Ofisini kwangu mara tatu. Ameshawaleta watu ambao walikuwa wameathirika na tatizo hili na nikawaelezea na nikaagiza Wataalam wangu wakalishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni kwamba, Mkandarasi anatakiwa achukue tahadhari wakati analipua miamba, ili isileté athari kwa wananchi. Sasa inapokuwa imetokea tatizo hili ni lazima ifanywe tathmini. Na nilivyosema kwamba, wananchi wale ambao tumethibitisha kwamba, ile mipasuko ya nyumba zao inatokana na mlipuko ndio tumelipa. Kwa hiyo, sijasema uwongo, ndio ukweli wenyewe. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Serikali ya CCM, ndio maana imetunga Sheria na ikaweka utaratibu, ili kwamba, kusiwe kuna wananchi wanaoneewa. Tumeweka utaratibu kwamba, lazima baada ya mlipuko kutokea ifanywe tathmini, huwezi ukafanya tathmini kabla ya janga na si kila siku unapofanya mlipuko lazima nyumba zipasuke. Kwa hiyo, tumeweka utaratibu huo na unaenda vizuri na ndio maana watu wengi wamekubaliana na utaratibu huo na unaenda vizuri na ndio maana watu wengi wamekubaliana na utaratibu huo kasoro hao 11.

Sasa suala la hao 11 isiwe kwamba, ni tatizo la Serikali, tutalishughulikia na tuweze kuona ukweli uko wapi.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nyongeza, napenda kuongeza kwenye majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu letu la msingi tumeeleza wamiliki wa nyumba 53 walioathirika wamelipwa milioni 78.281 hizi zimelipwa na Serikali ya *CCM*.

Kwa hiyo, Serikali ya *CCM* inajali wananchi wake na ndio maana imelipa hizi fedha, lakini wale 11 ambaao walitishla kwenda Mahakamani na baadaye wakajitoa na baadaye hawakuridhika na ile tathmini, tunawasubiri.

Wakikubaliana na ile tathmini iliyofanywa kwa mujibu wa Sheria Namba 4 na Namba 5 ya Mwaka 1999 na kwa mujibu wa Sheria nyingine ya Ardhi ya Mipango Miji Namba 6 na Namba 7 na Namba 8 ya Mwaka 2007, wakikubali tutawalipa, wasipokubali, watafute utaratibu mwingine. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa Maswali na Majibu Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru, tumevuka hapo. Sasa Matangazo ya Kazi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake ya Miundombinu, kukutana saa 7.00 Chumba Namba 231. Kamati ya Miundombinu, saa 7.00 Chumba 231.

Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Katibu wa *TAPAC*, anawaomba Kamati ya Utendaji *TAPAC*, wakutane leo saa 7.00 Mchana, Ukumbi wa Pius Msekwa. Kamati ya Utendaji *TAPAC*, saa 7.00 Pius Msekwa. (*Makof*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, saa 7.00 mchana Ukumbi Namba 227. Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Ukumbi 227, saa 7.00 Mchana.

Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida Timu yetu ya *Bunge Sports Club* bado inafanya mambo yake kwa uhakika chini ya Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Idd Azzan. Juzi Jumamosi, walifanya ziara kule Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo na wakacheza Mechi zifuatazo:-

Mpira wa Kikapu (*Basket Ball*), *Bunge Sports Club* ilitoka sare kwa vikapu 12 kwa 12 na Hombolo. Katika mchezo huo wa kikapu, nyota alikuwa Mheshimiwa Kabwe Zitto. (*Makof*)

Mpira wa Pete (*Net Ball*), *Bunge Sports Club* ilishinda kwa mabao 32 Hombolo wakiwa na mabao 3. Nyota wa mchezo huo kwa upande wa mpira wa pete, alikuwa Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha na mfungaji bora alikuwa Mheshimiwa Rachel Mashishanga. (*Makof*)

Kwa upande wa Mpira wa Miguu, *Bunge Sports Club* walishinda bao 2, Hombolo wakawa na bao 1. Magoli ya *Bunge Sports Club*, yalifungwa na Mheshimiwa Injinia Athuman Mfutakamba na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali. (*Makof*)

Aidha, nyota wa Mchezo huo alikuwa ni beki wa kutumainiwa, asiyepitika kirahisi, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali. (*Makof*)

Kwa uhakika mafanikio yote haya yamepatikana kwa sababu ya Kamati ya Ufundii, ambayo inaendelea kuongozwa na Profesa Maji Marefu, ambayo inafanya kazi yake kwa uhakika. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Kabaka, anatutangazia kwamba, Maonesho ya Mashirika yetu mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii Nchini ambayo jumla yake ni 6, yanaanza leo pale viwanja vya *Nyerere Square*, kuanzia saa 6.00 Mchana huu.

Tunaomba Waheshimiwa Wabunge, kila tukipata nafasi tuweze kufika pale hadi tarehe 18, mfululizo wiki nzima. Mashirika yote yatakuwa pale, watatoa taarifa ya kazi zao, watatoa matarajio waliyonayo, watajibu maswali, kero zenu na pia, wanasa jili wanachama wapya ambao mtapenda kujunga nao.

Maonesho haya yatafunguliwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa wakati ambao tutatangaziwa hapo baadaye kidogo. Pamoja na Mifuko hiyo 6, lakini SSRA ambao ndio Viongozi wa shughuli nzima wakiongozwa na Bi. Irene Isaka, wapo pale kwa ajili ya kujibu maswali yenu yote Waheshimiwa Wabunge.

Kama Mheshimiwa yejote ana swali la ziada, anaweza akamwandikia au kumwona Mheshimiwa Waziri Kabaka, kwa maelezo ya ziada.

Waheshimiwa Wabunge, nataka tukumbushane kidogo Kanuni ya 142, kuhusu Wageni. Kanuni inasema hivi, "*Spika, anaweza kuwatambulisha wageni wote wa Kitaifa na Kimataifa waliomo katika Ukumbi wa Bunge. Spika, vilevile anaweza kuwatambulisha Wageni wengine waliomo katika Ukumbi wa Bunge, ambao:-*

- (a) Wanahuksika moja kwa moja na shughuli za Majimbo.
- (b) Wanatembelea Bunge kwa ajili ya ziara za mafunzo.
- (c) Wametoa mchango wa Kitaifa, unaoihitaji kuenziwa.

Sasa nimeona Waheshimiwa Wabunge, baadhi ya Wageni wanaokuja kwa *categoryya* wanaohusika moja kwa moja na shughuli za Majimbo, mmekuwa hamuwatambulishi. Vilevile wanaotembelea Bunge kwa ajili ya ziara za mafunzo, mmekuwa mnasahau kutuletea ili tuweze kuwatambulisha.

Kwa hatua hiyo sasa naomba niwatambulische wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo, ambao ni Madiwani 30 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Makete. Naomba msimame pale mlipo, Waheshimiwa Madiwani? (*Makofi*)

Madiwani? Hawapo? Ooh, bahati mbaya sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Hilo la kwanza, la pili ambalo ningependa kukumbusha ni Kanuni ya 99...

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa?

MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka tulipokuwa tunafanya *briefing* kwenye kikao cha kwanza, Mheshimiwa Spika, alisema kwamba ataangalia namna itakavyokuwa kwa ajili ya kutambulisha wageni ili kuokoa muda kwa Bunge, sasa sijui kama hiyo tena imerekebishwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pudensiana Kikwembe, una wasiwasi na uwezo wangu? (*Kicheko*)

Hizo ndiyo taratibu ambazo amesema Mheshimiwa Naibu Spika na wala hazipingani chochote na ninachokizungumza. Ambacho tumekifuta ni yale majina mliyokuwa mnatuletea kutambulisha watu ambao mna mahusiano nao binafsi.

Nilichokuwa nafafanua ni kanuni ambayo bado ipo na nimewasomea ilivyo, hii sijatunga mimi, kwa wageni wanaokuja kwa ajili ya mafunzo hapa Bungeni bado wanaendelea kutambulishwa na ni kanuni ya 154, bado ipo hapa, lakini ile habari ya mtoto wangu, mama watoto na kadhalika yale mambo ya mahusiano ambayo kwa kweli si lazima Bunge lijue, hayo ndiyo ambayo tumeyafuta.

Pia niwakumbushe Kanuni ya 99(14) hasa kwa Waheshimiwa Mawaziri, baadhi bado wanajisahau, wanajaribu kukumbuka kutambulisha familia na kadhalika, hilo limekatazwa kwa kanuni hizi.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba Katibu tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka
2013/2014 – Wizara ya Ujenzi**

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA
NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2012/2013. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Mpango na bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kunipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu vyema na kwa utekelezaji mahiri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 pamoja na mipango na programu mbalimbali za kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika kutafuta fedha za kutekeleza miradi iliyopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 ambayo pia inajumuisha barabara. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wamemsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Spika na wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa hekima, umahiri na busara mnazotumia katika kuiongoza Bunge hili Tukufu. Namwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia busara na hekima katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa kifo cha ghafla cha Mheshimiwa Mbunge

mwenzetu Hayati Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani kwa tiketi ya *CUF*. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu na wananchi wote wa Jimbo la Chambani, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini na Mheshimiwa Athuman Juma Kapuya, Mbunge wa Jimbo la Urambo Magharibi kwa kuteuliwa kuiongoza Kamati ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawapongeza wajumbe wote wapya walioteuliwa kuunda Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Ushauri wa Kamati na Wabunge wote kwa ujumla utaendelea kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Wizara ya Ujenzi ili kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika kumpongeza na kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya Mipango na Uchumi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba hiyo, ni matumaini yangu kuwa maoni yao yatasaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira na dhima ya Wizara; Dira ya Wizara ni kuwa na Barabara, Madaraja, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi zenye ubora wa kiwango cha juu, zenye gharama nafuu na zinazozingatia usalama na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, dhima ya Wizara ni kuwa na Barabara, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi zilizo na uwiano na ambazo zinakidhi mahitaji kwa viwango bora na kwa bei nafuu zinazoendana na mikakati ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na wakati huo huo zikiwa endelevu kiuchumi na kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi ina majukumu ya kusimamia Sera za Ujenzi na Usalama Barabarani; ujenzi na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali; pamoja na masuala ya ufundi na umeme. Aidha, Wizara inasimamia shughuli za usajili wa Makandarasi, Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi; masuala ya usalama barabarani na mazingira katika sekta; uboreshaji utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Wizara; pamoja na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imelenga kujenga barabara ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu ya mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kufanya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa; kujenga barabara za kupunguza msongamano wa magari mijini hususan katika Jiji la Dar es Salaam; kuhakikisha kuwa usafiri wa vivuko unaimarishwa katika maeneo yote yanayohitaji huduma hiyo na kusimamia ujenzi wa nyumba za Serikali na watumishi. Aidha, Wizara itaendelea kusajili na kusimamia Makandarasi, Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kwa kutumia Bodi husika pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaendelea kusimamia masuala ya usalama na mazingira katika barabara na vivuko pamoja na kufanya matengenezo na ukarabati wa Magari ya Serikali na Mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi husika katika kushughulikia masuala mtambuka kama vile kampeni za kupunguza maambukizi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI, uhifadhi wa mazingira, masuala ya jinsia pamoja na uendelezaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Wizara katika kufikia malengo; ili kuweza kutekeleza malengo yake, Wizara itaendelea kuzingatia kutekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2011/2012 – 2015/2016, Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ya Ujenzi inazingatia utekelezaji wa Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Miundombinu ya Usafirishaji (*Transport Sector Investment Program – TSIP*) ambayo ni programu ya miaka kumi (2006/2007-2016/2017) inayolenga kuimarisha na kuboresha miundombinu ya usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatekeleza Sera ya Taifa ya Ujenzi (2003), Sera ya Usalama Barabarani (2009) na Sera ya Ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*PPP*). Wizara pia itaendelea kusimamia utoaji elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya barabara kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 pamoja na sheria nyingine ili miundombinu ya barabara iweze kutunzwa na kudumu kwa muda uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara vile vile itaboresha mfumo wa upimaji magari ya mizigo kwa kuweka mizani itakayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (*weight-in-motion*) kwa lengo la kuzuia uharibifu wa barabara kutokana na magari yanayozidisha mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni pamoja

na kusimamia fedha za Mfuko wa Barabara zinazopelekwa Mikoani ili kazi za matengenezo ya barabara zinazotekelezwa zilingane na thamani ya fedha (*value for money*). Wizara pia itaendelea kutafuta vyanzo vipyta ili kupanua wigo wa Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kuzifanyia marekebisho sheria za kisekta ili ziweze kuendana na mazingira ya sasa na kufikia viwango vinavyokubalika Kimataifa na Kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itahakikisha kuwa Makandarasi, Wahandisi Washauri na Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa kizalendo wanahuishwa kikamilifu katika ujenzi wa miradi mikubwa hususan miradi ya barabara, madaraja, nyumba na vivuko inayogharamiwa na Serikali badala ya kutegemea kampuni za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuwajengea wananchi uzoefu stahili katika Sekta ya Ujenzi na kupunguza kasi na wingi wa fedha zinazotokana na vyanzo vyetu kuhamishiwa nje ya nchi kwa kulipia kazi za kampuni za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2012/2013. Ukusanyaji wa mapato; katika mwaka 2012/2013, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Sh. 15,628,580.00 kuititia Idara zenyet vyanzo vya mapato. Idara hizo ni Utawala, Huduma za Ufundsi na Menejimenti ya Ununuvi. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya Sh. 36,388,193.24 ziliikuwa zimekusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kukusanya fedha zaidi ikilinganishwa na bajeti iliyopangwa ni kuongezeka kwa makusanyo ya ada za usajili wa vyombo vya Serikali kufuatia zoezi la kufuta matumizi ya namba za kiraia kwenye magari, pikipiki, bajaj na mitambo ya Serikali na kusajiliwa kwa namba za Serikali. Zoezi hili lilianza tarehe 19 Novemba, 2012 na hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya magari, pikipiki, bajaj na mitambo ya Serikali iliyosajiliwa kwa namba za Serikali ni 2,268.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara ilitengewa kiasi cha Sh. 329,085,354,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2013, Sh. 257,177,456,588.75 zilikuwa zimetolewa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho ni asilimia 78.15 ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha zilizotolewa, Sh. 15,490,538,152.00 zilikuwa za Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Sh. 237,811,447,236.75 ni za Mfuko wa Barabara na Sh. 3,875,471,200.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, Taasisi na Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Wizara illidhinishiwa Sh. 693,948,272,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh. 296,896,892,000.00 zilikuwa fedha za ndani na Sh. 397,051,380,000.00 zilikuwa fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2013, Wizara ilishapokea fedha zote za ndani kiasi cha Sh. 296,896,892,000.00 na Sh. 236,782,437,956.41 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja; nchi ya Tanzania ina mtandao wa barabara wenyewe jumla ya kilometra 87,581. Kati ya hizo, kilometra 35,000 ni Barabara Kuu na za Mikoa zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Barabara zinazobaki ni za Wilaya na zinasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Aidha, kuna jumla ya Madaraja 4,880 katika Barabara Kuu na za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilipanga kukamilisha ujenzi wa barabara kuu zenye urefu wa kilometra 414 kwa kiwango cha lami, kukarabati kilometra 135 kwa kiwango cha lami pamoja na kujenga na kukarabati madaraja 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013, ujenzi wa kilomita 374.65 za barabara kuu kwa kiwango cha

lami na ukarabati wa kilomita 140.63 kwa kiwango cha lami ulikamilika. Kuhusu matengenezo ya Barabara Kuu, lengo lilikuwa ni kuzifanyia matengenezo kilomita 10,534.3 na madaraja 1,154. Hadi kufikia Aprili, 2013 kilomita 6,052.8 za Barabara Kuu na madaraja 652 yalifanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande Barabara za Mikoa, Wizara ilipanga kujenga kwa kiwango cha lami kilomita 31.9, kukarabati kwa kiwango cha changarawe kilomita 573.6 na ujenzi wa madaraja 27. Hadi kufikia Aprili, 2013, kilomita 8.23 zilijengwa kwa kiwango cha lami, kilomita 198.9 zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja nane ulikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matengenezo ya Barabara za Mikoa, Wizara ilipanga kuzifanyia matengenezo barabara zenye urefu wa kilomita 22,482 na madaraja 1,263. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 13,459.2 zilikuwa zimekamilika na madaraja 758 yalikuwa yamefanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kudhibiti uzito wa magari illendelea katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa kutumia mizani 26 ya kudumu na 17 inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi Aprili, 2013 magari yapatayo 2,321,526 yalikuwa yamepimwa ambapo magari 598,074 yalikuwa yamezidisha uzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni asilimia 25.76 ya magari yote yaliyopimwa. Jumla ya fedha zilizokusanya kutokana na tozo (kwa mujibu wa Sheria Na. 30 ya mwaka 1973) ya uharibifu wa barabara na malipo ya kupitisha mizigo mipana na isiyo ya kawaida ilikuwa ni Sh. 3,913,898,889.45.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza maandalizi ya kujenga barabara ya Dar es Salaam - Chalinze (*Express way*) kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na Kampuni binafsi. Kufuatia tangazo lilitolewa na Wizara kupitia *TANROADS*, Kampuni 19 zimewasilisha mapendekezo ya jinsi ya kujenga barabara hii kwa njia sita kuanzia Dar es Salaam

– Mlandizi na njia nne kuanzia Mlandizi - Chalinze. Kazi za kuchambua mapendekezo hayo ili kumpata mbia anayeweza kufanya kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa ujenzi wa barabara ya Bagamoyo-Makofia-Msata kilomita 64 ulisainiwa tarehe 15 Agosti, 2010 kwa gharama ya Sh. bilioni 89.608. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 55.4 za tuta la barabara, kilomita 51.2 za tabaka la chini, kilomita 51.2 za tabaka la juu na kilomita 51.2 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa barabara ya Usagara – Geita – Bwanga – Buzirayombo – Kyamyorwa kilomita 422 umegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ilihuisha ujenzi wa Barabara ya Kyamyorwa - Geita kilomita 220 ambayo ilikamilika Februari, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ilihuisha ujenzi wa barabara ya Geita - Usagara kilomita 90 ambapo ujenzi wake ulianza Februari, 2008 na umekamilika Januari, 2010. Sehemu ya tatu itahuisha ujenzi wa barabara ya Uyovu - Bihamamulo kupitia Bwanga kilomita 112. Mikataba ya ujenzi imesainiwa Oktoba, 2012 na Mkandarasi ameshapeleka vifaa na wataalam kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa barabara wa Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora kilomita 310.60 unahuisha ujenzi wa Barabara ya Tabora - Urambo kilomita 94, ujenzi wa daraja la Malagarasi na barabara zake za maingilio (*approach roads* – kilomita 48), barabara ya Uvinza – Kidahwe kilomita 76.6, Kigoma- Kidahwe kilomita 36 na Kaliua – Kazilambwa kilomita 56. Aidha, utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Tabora-Ndono kilomita 42; Gharama za ujenzi wa mradi huu ni Shilingi bilioni 51.35. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 19 za tuta la barabara zimekamilika.

(ii) Ndono-Urambo kilomita 52; Gharama za ujenzi

wa barabara ya Ndono – Urambo ni Shilingi bilioni 59.77. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 22 za tuta la barabara zimekamilika.

(iii) Kaliua – Kazilambwa kilomita 50; Mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Kaliua – Kazilambwa kilomita 56 umesainiwa tarehe 27 Machi, 2013 na kazi za maandalizi ya ujenzi zinaendelea.

(iv) Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi na barabara zake za maingilio, mkataba wa usanifu na ujenzi wa mradi huu ulisainiwa tarehe 21 Oktoba, 2010. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiuchumi (*Economic Development Cooperation Fund*) wa Korea Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa madaraja matatu ambapo moja lina urefu wa meta 200, la pili meta 50 na la tatu meta 25 pamoja na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 11 kwa kiwango cha lami. Kazi zinafanyika kwa utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (*Design and Build*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013 kazi za ujenzi wa daraja zimekamilika kwa asilimia 81 na ujenzi wa tuta la barabara, tabaka la chini na tabaka la juu umekamilika. Kwa awamu ya pili inayohusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 37 kwa kiwango cha lami, Serikali ya Korea Kusini imekubali kutoa fedha na Mkataba wa Mkopo wa Nyongeza (*Supplementary Loan Agreement*) umesainiwa tarehe 11 Desemba, 2012. Kazi za ujenzi zimeanza tarehe 4 Januari, 2013.

(v) Uvinza – Kadehwe; Mkataba wa ujenzi wa barabara ya Uvinza – Kidahwe kilomita 76.6 ulisainiwa tarehe 24 Juni, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 78.241. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 74 za tuta la barabara, kilomita 73 za tabaka la chini, kilomita 72 za tabaka la juu na kilomita 70.18 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Marangu-Rombo Mkuu na Mwika-Kilacha kilomita 32, mkataba ulisainiwa tarehe 13 Mei, 2008 kwa gharama ya Shilingi bilioni 25.075. Hadi kufikia Aprili 2013, jumla ya kilomita 32 za tuta la barabara, kilomita 32 za tabaka la chini, kilomita 32 za tabaka la juu na kilomita 29.3 za lami zimekamilika. Kwa barabara Sanya Juu (Siha) – Kamwanga kilomita 75, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Mbwemkulu kilomita 95 ulisainiwa tarehe 14 Mei, 2003 kwa gharama ya shilingi bilioni 39.239 na ulikamilika mwaka 2008. Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi haikupokea mradi huu kwa kuwa haukukamilika kwa kiwango kilichokusudiwa na hivyo kuwepo kwa marekebisho yanayohitajika kufanyika. Kazi ya kufanya marekebisho imekamilika na mradi umepokelewa na Wakala wa Barabara tarehe 21 Februari, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Dodoma – Manyoni kilomita 127, ulisainiwa tarehe 12 Machi, 2003 kwa gharama ya shilingi bilioni 63.888. Ujenzi wa barabara hii ulikamilika tarehe 22 Novemba, 2009 na kipindi cha uangalizi cha miaka mitatu kilikwisha Novemba, 2012 na mradi umepokelewa na TANROADS.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya Dumila – Kilosa kilomita 63 kwa kiwango cha lami umegawanywa katika sehemu mbili; Dumila – Rudewa kilomita 45 na Rudewa - Kilosa kilomita 18. Utekelezaji wa sehemu hizi mbili ni kama ifuatavyo:-

(i) Dumila-Rudewa kilomita 45; Mkataba wa ujenzi ni wa gharama ya Shilingi bilioni 41.929. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 44.72 za tuta la barabara, kilomita 31.85 za tabaka la chini, kilomita 0.3 za tabaka la juu na kilomita 0.3 za lami zimekamilika.

(ii) Rudewa-Kilosa kilomita 18; Usanifu umekamilika na Serikali inaendelea na juhudzi za kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi kwa upande wa mradi wa barabara ya Sumbawanga-Matai-Kasanga Port kilomita 112 ni wa Shilingi bilioni 133.286. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 38 za tuta la barabara, kilomita 27 za tabaka la chini, kilomita 12 za tabaka la juu na kilomita 12 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa mradi wa upanuzi wa barabara ya Kawawa Junction-Mwenge-Tegeta kilomita 17, sehemu ya Mwenge – Tegeta ulisainiwa tarehe 16 Desemba, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 88.403 kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan. Aidha, sehemu ya Mwenge – Kawawa Junction kilomita 4.3 itafadhiliwa pia na Serikali ya Japan.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 21.67 za tuta la barabara, kilomita 12.12 za tabaka la chini na kilomita 21.66 za tabaka la juu zimekamilika. Aidha, kwa sehemu ya Morocco – Mwenge malipo ya fidia kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 yamefanyika kwa nyumba zinazotakiwa kuondolewa ili kupisha ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mradi wa barabara ya Kyaka-Bugene kilomita 59.1, mkataba ulisainiwa kwa gharama ya shilingi bilioni 64.96. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 11.8 za tuta la barabara na kilomita 7.9 za tabaka la chini zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mradi wa barabara ya Isaka- Lusahunga kilomita 382 ni kufanya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na umegawanyika katika sehemu tatu (3). Utekelezaji wa sehemu zote tatu ni kama ifuatavyo:-

Lot 1: Isaka – Ushirombo Kilomita132; Mkataba wa ujenzi unagharimu Shilingi bilioni 145.329 na kazi zilianza tarehe 18 Februari, 2010. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 111.77 za tuta la barabara, kilomita 107.72 za tabaka la chini, kilomita 107.64 za tabaka la juu na kilomita 106.74 za lami zimekamilika.

Lot 2: Ushirombo – Lusahunga Kilomita 110; Mkataba wa ujenzi utagharimu Shilingi bilioni 114.556 na kazi zilianza tarehe 18 Februari, 2010. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 53.5 za tuta la barabara, kilomita 53.5 za tabaka la chini, kilomita 53.5 za tabaka la juu na kilomita 53.5 za lami zimekamilika.

Lot 3: Lusahunga – Rusumo/Nyakasanza – Kobero kilomita 150. Lengo la mradi huu ni kufanya usanifu wa kina wa barabara hili yenye urefu wa kilomita 150 kwa ajili ya kuikarabati kwa kiwango cha lami. Usanifu wa kina utakamilika katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kujenga barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora yenye urefu wa kilometa 264.35 kwa kiwango cha lami umegawanyika katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

Lot 1: Manyoni – Itigi – Chaya kilomita 89.35; Mkataba wa ujenzi ni wa gharama ya shilingi bilioni 109.642. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 39.8 za tuta la barabara na kilomita 2.9 za tabaka la chini zimekamilika.

Lot 2: Tabora – Nyahua kilomita 85; Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 kwa gharama ya shilingi bilioni 93.401. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 16.19 za tuta la barabara zimekamilika.

Lot 3: Chaya – Nyahua kilomita 90; usanifu umekamilika na ujenzi umepangwa kuanza mwaka 2013/2014 kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa

barabara ya Handeni – Mkata kilomita 53.2 ni wa gharama ya Shilingi bilioni 57.338. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 53.2 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mradi wa barabara ya Korogwe – Handeni kilomita 65, mkataba wa ujenzi ni wa Shilingi bilioni 63.199. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 59 za tuta la barabara, kilomita 52 za tabaka la chini, kilomita 51 za tabaka la juu na kilomita 50 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Ndundu - Somanga kilomita 60 unagharamiwa na Serikali ya Tanzania, Kuwait Fund na OPEC. Mkataba wa ujenzi ni wa gharama ya Shilingi bilioni 58.814. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 52.38 za tuta la barabara, kilomita 46 za tabaka la chini, kilomita 36.53 za tabaka la juu na kilomita 30 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Makutano – Natta – Mugumu /Loliondo – Mto wa Mbu kilomita 328, lengo ni kufanya usanifu wa kina ikiwa ni pamoja na maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa sehemu ya Natta – Mugumu - Loliondo kilomita 239 na Mto wa Mbu – Loliondo kilomita 213 ilisainiwa tarehe 26 Agosti, 2009. Utekelezaji wa mradi umegawanyika kama ifuatavyo:-

Lot 1: Loliondo – Mto wa Mbu kilomita 213; Usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na ujenzi utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Lot 2: Makutano - Natta – Mugumu kilomita 80; kazi ya usanifu wa barabara hii umekamilika na mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Makutano – Sanzate kilomita 50 ulisainiwa Machi, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Tanga - Horohoro kilomita 65 kwa kiwango cha lami, mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 22 Desemba, 2009 kwa gharama ya Shilingi bilioni 69.894. Mradi huu umeghamariwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko wa *MCC* ya Marekani na mchango wa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013, kazi za ujenzi wa barabara hii zimekamilika. Barabara ilifunguliwa rasmi tarehe 13 Aprili, 2013 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nzega - Tabora kilomita 115 inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na mradi umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Utekelezaji wa sehemu hizi ni kama ifuatavyo:-

(i) Nzega-Puge kilomita 56.2; gharama ya mradi huu ni Shilingi bilioni 66.358. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 13.5 za tuta la barabara zimekamilika.

(ii) Puge-Tabora kilomita 58.8; Mradi huu unajengwa kwa mkataba wa gharama ya Shilingi bilioni 62.737. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 23 za tuta la barabara na kilomita 2.9 za tabaka la chini zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya Sumbawanga - Mpanda- Nyakanazi kilomita 829 kwa kiwango cha lami umegawanyika katika sehemu kuu nne: Sumbawanga – Kanazi kilomita 75, Kanazi – Kizi - Kibaoni kilomita 76.6, Kizi – Sitalike – Mpanda kilomita 95 na Mpanda – Uvinza -Nyakanazi kilomita 582.4. Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Sumbawanga – Kanazi kilomita 75; gharama ya ujenzi kwa sehemu hii ni Shilingi bilioni 78.84. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 25 za tuta la barabara, kilomita 19.5 za tabaka la chini, kilomita 6.4 za tabaka la juu na kilomita 6.4 za lami zimekamilika.

(ii) Kanazi – Kizi – Kibaoni kilomita 76.6; Mkataba wa ujenzi unahusisha kilomita 76.6 kwa gharama ya Shilingi bilioni 82.841. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 19 za tuta la barabara zimekamilika.

(iii) Kizi – Sitalike – Mpanda kilomita 95; Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Sitalike – Mpanda kilomita 35 umesainiwa tarehe 22 Oktoba, 2012 kwa gharama ya Shilingi bilioni 37.097. Hadi kufikia Aprili, 2013 Mkandarasi ameshakamilisha maandalizi (*mobilization*) na ameanza kazi za ujenzi.

(iv) Mpanda – Uvinza -Nyakanazi kilomita 582.4; usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na ujenzi utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Nyanguge – Musoma kilomita 183, mkataba wa kazi kwa sehemu ya Simiyu/Mara border - Musoma yenye urefu wa kilomita 85.5 ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 85.368. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 75 za tuta la barabara, kilomita 61.45 za tabaka la chini, kilomita 50.97 za tabaka la juu na kilomita 45.56 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ujenzi wa mchepuo wa Usagara - Kisesa kilomita 17, mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 26 Machi, 2013. Mkandarasi yuko katika maandalizi ya kuanza kazi, kwa sehemu ya Nyanguge hadi mpakani mwa Simiyu/Mara, Serikali inatafuta fedha za ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa mradi wa barabara ya Mziha – Turiani – Magole kilomita 84.6 umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

(i) Magole – Turiani kilomita 48; Mkataba wa ujenzi ulisainiwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 41.89. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 34 za tuta la barabara na kilomita 0.24 za tabaka la chini zimekamilika.

(ii) Turiani – Mziha kilomita 36.6; kazi ya usanifu wa barabara hii imekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa barabara ya Bariadi-Lamadi kilomita 71.8, mkataba wa ujenzi utagharimu Shilingi bilioni 67.408. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Shinyanga – Mwigumbi – Maswa – Bariadi yenye urefu wa kilomita 171. Hadi kufikia Aprili, 2013 jumla ya kilomita 6.88 za tuta la barabara na kilomita 3.12 za tabaka la chini zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia (*Mafia Airport Access Road*) yenye urefu wa kilomita 14 yanaendelea. Mkataba wa ujenzi wa barabara hii umesainiwa Machi, 2013 kwa gharama ya Shilingi billioni 13.554 fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Dodoma – Chuo Kikuu cha Dodoma (*Dodoma University Road*) kilomita 12 itajengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani. Hatua za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya mradi huu zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa barabara ya Tunduma-Sumbawanga kilomita 223.0 unaoghamariwa kwa fedha za '*Millennium Challenge Corporation*' (MCC) ya Marekani umegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

(i) *Lot 1:* Tunduma – Ikana kilomita 63.7; Mkataba wa ujenzi wa sehemu hii ya barabara unagharimu Shilingi bilioni 82.52. Hadi kufikia Aprili 2013, jumla ya kilomita 43.75 za tuta la barabara, kilomita 26.34 za tabaka la chini, kilomita 24.88 za tabaka la juu na kilomita 1.3 za lami zimekamilika.

(ii) *Lot 2:* Ikana – Laela kilomita 64.0; Mkataba wa ujenzi wa sehemu hii ya barabara ni wa gharama ya Shilingi bilioni 76.076. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 55.1

za tuta la barabara, kilomita 45.04 za tabaka la chini, kilomita 43.66 za tabaka la juu na kilomita 43.39 za lami zimekamilika.

(iii) *Lot 3: Laela – Sumbawanga* kilomita 95.3; Mkataba wa ujenzi wa sehemu hii ya barabara ni wa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 97.141. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 44.3 za tuta la barabara, kilomita 41.9 za tabaka la chini, kilomita 41.76 za tabaka la juu na kilomita 33.76 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa barabara ya Kagoma- Biharamulo-Lusahunga kilomita 154 ni sehemu ya barabara ya Mutukula – Bukoba – Biharamulo – Lusahunga kilomita 294. Mkataba mpya wa kumalizia ujenzi wa sehemu ya barabara ya Kagoma – Lusahunga kilomita 154 kwa kiwango cha lami ulisainiwa tarehe 18 Juni, 2009 kwa gharama ya Shillingi billioni 191.454.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania baada ya *ADB* kujitoa. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 150.9 za tuta la barabara, kilomita 150.9 za tabaka la chini, kilomita 130.5 za tabaka la juu na kilomita 121 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Japani imetoa msaada wa fedha za kugharamia ujenzi na upanuzi wa barabara ya Bendera Tatu – KAMATA. Kazi ya kuondoa mali zilizomo kwenye eneo la mradi imeanza. Utaratibu wa kumtafuta Mkandarasi unaendelea nchini Japani na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa barabara ya Minjingu – Babati – Singida kilomita 223.5 unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na mchango wa Serikali ya Tanzania. Ujenzi wa sehemu tatu za Singida-Kateshi kilomita 65.1, Kateshi-Dareda kilomita 73.8 na Dareda-Babati-Minjingu kilomita 84.6 umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Minjingu – Arusha kilomita 104 inafanyiwa ukarabati kwa kiwango cha

lami kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa gharama ya Shilingi bilioni 75.511. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 12 za tuta la barabara, kilomita 10 za tabaka la chini na kilomita tisa za tabaka la juu zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa barabara ya lami ya Dar es Salaam – Tunduma (*TANZAM*) unahusisha ukarabati wa sehemu ya lyovi - Kitonga Gorge kilomita 86.3, Ikokoto - Iringa kilomita 60.9, mchepuo wa kuingia Iringa mijini kilomita 2.1 na Iringa-Mafinga kilomita 68.9. Mradi huu unagharamiwa kwa mkopo kutoka Serikali ya Denmark pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Sehemu ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto – Mafinga kilomita 149.6 umekamilika. Ukarabati wa sehemu ya Iringa – Mafinga kilomita 69.4, ulianza tarehe 9 Septemba, 2011 kwa gharama ya *Euro* milioni 38.5. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 70.1 za tuta la barabara, kilomita 54.64 za tabaka la chini, kilomita 53.91 za tabaka la juu na kilomita 53.11 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ukarabati wa barabara ya Korogwe - Mkumbara –Same kilomita 172 zimegawanyika katika sehemu mbili na utekelezaji wa sehemu hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Korogwe - Mkumbara kilomita 76; Mkataba wa ujenzi wa barabara ulisainiwa tarehe 16 Januari, 2012 kwa gharama ya Shilingi bilioni 62.866. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 19.1 za tuta la barabara, kilomita 14.2 za tabaka la chini, kilomita 13.7 za tabaka la juu na kilomita 3.4 za lami zimekamilika.

(ii) Mkumbara – Same kilomita 96; Mkataba wa ujenzi wa barabara ulisainiwa tarehe 16 Januari, 2012 kwa gharama ya Shilingi bilioni 65.130. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 3.3 za tuta la barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na ujenzi

wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi, kilomita 115 ambao umegawanywa katika sehemu tatu zifuatazo:-

(i) Mbeya-Lwanjilo kilomita 36; baada ya Mkandarasi wa awali (*Kundan Singh*) kushindwa kazi na kufukuzwa, Mkataba mpya wa ujenzi wa barabara ulisainiwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 55.385. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita tatu za tuta la barabara zimekamilika.

(ii) Lwanjilo-Chunya kilomita 36; Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Lwanjilo – Chunya utagharimu Shilingi bilioni 40.28. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita tatu za tuta la barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati na upanuzi wa barabara ya Chalinze - Segera hadi Tanga, ukarabati wa sehemu ya Chalinze – Kitumbi kilomita 125 umekamilika. Mkataba wa ukarabati wa sehemu ya barabara ya Kitumbi – Segera – Tanga kilomita 120 ulisainiwa tarehe 24 Desemba, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 67.237.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2013, upanuzi umekamilika kwa jumla ya kilomita 24.45 za tuta la barabara, kilomita 24.45 za tabaka la chini na kilomita 24.45 za tabaka la juu. Aidha, kilomita 90 za kuongeza tabaka la lami (*resealing*) zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Dodoma – Iringa kilomita 260 unagharamiwa na fedha za mkopo toka *ADB* na *JICA*. Mradi umegawanyika katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

(i) Iringa – Migori kilomita 95.10; Mkataba wa ujenzi wa sehemu hii ulisainiwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 84.216. Hadi kufikia Aprili 2013, jumla ya kilomita 58.7 za tuta la barabara na kilomita 39.1 za tabaka la chini, kilomita 10.7 za tabaka la juu zimekamilika.

(ii) Migori – Fufu *Escarpmment* kilomita 93.80;

Mkataba wa ujenzi wa barabara hii katika sehemu unagharimu Shilingi bilioni 73.612. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 56.4 za tuta la barabara na kilomita 25.3 za tabaka la chini, kilomita 9.4 za tabaka la juu zimekamilika.

(iii) Fufu *Escarpment* – Dodoma kilomita 70.90; Mkataba katika sehemu hii ya barabara unagharimu Shilingi bilioni 64.327. Hadi kufikia Aprili 2013, jumla ya kilomita 64.8 za tuta la barabara, kilomita 39.2 za tabaka la chini, kilomita 28 za tabaka la juu na kilomita 6.9 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Dodoma – Babati kilomita 261 umegawanywa katika sehemu zifuatazo:-

(i) Dodoma – Mayamaya kilomita 43.65; Mkataba wa ujenzi wa barabara hii ulisainiwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 40.609. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 25.75 za tuta la barabara, kilomita 20 za tabaka la chini, kilomita 18 za tabaka la juu na kilomita 17.35 za lami zimekamilika.

(ii) Mayamaya - Mela kilomita 99.35; Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Mayamaya – Mela imetangazwa Novemba, 2012 na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

(ii) Mela – Bonga kilomita 98.8; Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Mela – Bonga imetangazwa Novemba, 2012 na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

(iii) Bonga – Babati kilomita 19.2; Mkataba wa ujenzi wa barabara ulisainiwa tarehe 31 Mei, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 19.687. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 18.5 za tuta la barabara, kilomita 18.5 za

tabaka la chini, kilomita 18.5 za tabaka la juu na kilomita 18.2 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa barabara ya Masasi- Songea – Mbamba Bay umegawanywa katika sehemu zifuatazo:-

(i) Mangaka – Nakapanya kilomita 70.50; Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Mangaka - Nakapanya imetangazwa Mei, 2012 na mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*).

(ii) Nakapanya - Tunduru kilomita 66.50; Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Nakapanya - Tunduru imetangazwa Mei, 2012 na mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*).

(iii) Mangaka – Mtambaswala kilomita 65.50; Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Mangaka - Mtambaswala imetangazwa Mei, 2012 na mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*).

(iv) Tunduru – Matemanga kilomita 58.70; Mkataba ulisainiwa tarehe 24 Desemba, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 63.409. Mkataba wa ujenzi umefutwa tarehe 8 Januari, 2013 baada ya Mkandarasi *M/s Progressive – Higleg – Joint Venture (JV)* kushindwa kutekeleza mradi kimkataba. Taratibu za kumpata mkandarasi mwingine zinaendelea.

(v) Matemanga – Kilimasera kilomita 68.20; Mkataba ulisainiwa tarehe 24 Desemba, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 64.016. Mkataba wa ujenzi umefutwa tarehe 8 Januari, 2013 baada ya Mkandarasi *M/s Progressive – Higleg*

- *Joint Venture (JV)* kushindwa kutekeleza mradi kimkataba. Taratibu za kumpata mkandarasi mwingine zinaendelea.

(vi) Kilimasera - Namtumbo kilomita 60.70; Mkataba ulisainiwa tarehe 24 Desemba, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 53.229. Mkataba wa ujenzi umefutwa tarehe 8 Januari, 2013 baada ya Mkandarasi *M/s Progressive – Higleg – Joint Venture (JV)* kushindwa kutekeleza mradi kimkataba. Taratibu za kumpata mkandarasi mwingine zinaendelea.

(vii) Namtumbo – Songea kilomita 67.00; Mkataba wa ujenzi wa barabara ulisainiwa tarehe 25 Mei 2010 kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 46.963. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 66 za tuta la barabara, kilomita 58.5 za tabaka la chini, kilomita 55 za tabaka la juu na kilomita 52 za lami zimekamilika.

(viii) Peramiko – Mbinga kilomita 78.00; Mkataba wa ujenzi wa barabara ulisainiwa tarehe 2 Julai, 2010 kwa gharama ya Shilingi bilioni 79.803. Hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya kilomita 78 za tuta la barabara, kilomita 78 za tabaka la chini, kilomita 78 za tabaka la juu na kilomita 78 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja makubwa; katika mwaka 2012/2013, Wizara inaendelea na ujenzi na ukarabati wa madaraja ya:-

Kirumi kwenye barabara ya Makutano – Sirari, daraja la Nanganga kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, daraja la Maligisu (Mwanza) kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi - Maligisu, daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi - Ifakara – Mahenge, daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto-Inyonga, daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga-Manonga, daraja la Ruhekei kwenye barabara ya Mbinga-Mbamba Bay, daraja la Ruhuhu (Ruvuma) na ununuzi wa madaraja ya

Chuma ya dharura na mtambo wa kukagua madaraja (*Compact Emergency Bridges na Crane Lorry*). Utekelezaji wa ujenzi wa madaraja hayo umefikia hatua zifuatazo:-

(i) Daraja la Kirumi; Hatua za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina wa ukarabati wa daraja la Kirumi zinaendelea. Kazi za usanifu zinatarajiwaa kukamilika katika mwaka 2013/2014.

(ii) Daraja la Sibiti; Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 7 Agosti, 2012 kwa gharama ya shilingi bilioni 16.302. Hadi kufikia Aprili, 2013 Mkandarasi ameshakamilisha maandalizi (*mobilization*) na tayari kazi za ujenzi zimeanza.

(iii) Daraja la Kilombero; Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 24 Oktoba, 2012 kwa gharama ya Shilingi bilioni 53.214. Maandalizi ya kuanza ujenzi wa daraja yanaendelea.

(iv) Daraja la Maligisu; hadi kufika Aprili, 2013 ujenzi wa Daraja hili umefikia asilimia 90.

(v) Daraja la Kavuu; hatua za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa msingi na nguzo za daraja zinaendelea. Ununuzi wa vyuma vya daraja (Mabey parts) umekamilika.

(vi) Daraja la Mbutu; Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 27 Aprili, 2012 kwa gharama ya Shilingi bilioni 10.456. Hadi kufikia Aprili, 2013 kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 54.3.

(vii) Daraja la Ruhuhu; matayarisho kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja na bwawa la kumwagilia maji la Ruhuhu yanaendelea.

(viii) Ununuzi wa Madaraja ya Chuma ya Dharura na Mtambo wa Kukagua Madaraja (*Compact Emergency Bridges na Under Bridge Inspection Lorry*).

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za ununuzi wa Madaraja ya Chuma ya Dharura (*Compact Emergency Bridges*) zinaendelea na mkataba wa ununuzi wa Mtambo wa kukagua Madaraja (*Under Bridge Inspection Lorry*) umesainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa Daraja la Kigamboni, mkataba wa ujenzi ulisaniwa tarehe 9 Januari, 2012. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF). Mkandarasi ameshakamilisha maandalizi (*mobilization*) kwa asilimia 90 na ameanza kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kujenga Daraja katika Mto Ruvu kwenye barabara ya Dar es Salaam – Tunduma (TANZAM), ulikamilika mwaka 2009. Fedha za ndani zimetengwa katika bajeti ya 2012/2013 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai la Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Lengo la mradi huu ni kusanifu, kujenga na kukarabati barabara za Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara za Jiji. Hadi Aprili, 2013, hatua za utekelezaji wa miradi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo kwa kasi kutoka Kimara hadi Kivukoni, *Fire* hadi Kariakoo na Magomeni hadi Morocco unaendelea. Aidha, kazi ya ujenzi wa Karakana na vituo vya mabasi yaendayo kasi pamoja na uhamishaji wa miundombinu ya umeme inaendelea vizuri.

(ii) Ujenzi wa *Flyover* ya *TAZARA*: Maandalizi ya kumpata mkandarasi yanaendelea. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan kuitia Shirika lake la Maendeleo (*JICA*).

(iii) Ujenzi na upanuzi wa Barabara ya Gerezani (Bendera Tatu – KAMATA); Serikali ya Japani imekubali kugharamia mradi huu na taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea.

(iv) Barabara ya Kilwa (Bendera tatu – Mbagala Rangi Tatu): Ujenzi wa barabara hii umekamilika.

(v) Hadi kufikia Aprili, 2013, sehemu kubwa ya kazi kwa kiwango cha lami imekamilika kwa barabara ya Ubungo *Bus Terminal* – Mabibo-Kigogo *Roundabout* kilomita 6.4; Kigogo *Round about*-Bonde la Msimbazi –Twiga/Msimbazi *Junction* kilomita 2.7 na Barabara ya *Jet Corner* – Vituka – *Davis Corner* kilomita 10.3.

(vi) Kuhusu Usafiri wa vivuko/boti kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo; mkandarasi wa kujenga kivuko/boti chenye uwezo wa kubeba abiria 300 amepatikana. Usanifu wa maegesho matatu (*Magogoni, Jangwani Beach, Rungwe Oceanic*) unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na miradi mingine ya barabara za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

(i) Kazi za ujenzi zinaendelea kwa barabara ya Tabata Dampo – Kigogo na Ubungo *Maziwa Externa*/kilomita 2.25;

(ii) Kwa upande wa barabara za *Old Bagamoyo* na *Garden Road* kilomita 9.1, kazi za usanifu zimekamilika Februari, 2013; na

(iii) Kazi ya Usanifu imekamilika kwa barabara za Mbezi (*Morogoro road*) –Malamba Mawili – Kinyerezi - Banana kilomita 14; Tegeta – Kibaoni - Wazo – Goba - Mbezi Mwisho kilomita 20; Tangi Bovu-Goba kilomita tisa; Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni kilomita 2.6 na Kimara – Kilungule - *External Mandela Road* kilomita tisa. Hatua za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara mbalimbali. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika kwa barabara zifuatazo:-

(i) Mbinga – Mbamba Bay kilomita 66; Sehemu ya Signal - Ifakara kilomita 16.8, katika barabara ya Kidatu - Ifakara kilomita 30. Hii ni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami nyepesi. Barabara ya Turiani – Mziha kilomita 36.6; Barabara ya Mafinga – Igawa Kilomita 140.6; Barabara ya Chunya - Makongorosi kilomita 43; Barabara ya Same – Himo – Marangu kilomita 99.73; Barabara ya Mombo – Lushoto kilomita 32; Barabara ya Makambako – Songea kilomita 295 na barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili kilomita 140. Kwa barabara hizi, kazi inayofuata ni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea katika barabara zifuatazo:-

- (i) Barabara ya Mtwara – Mingoyo - Masasi (kilomita 200);
- (ii) Makongolosi- Rungwa-Itigi- Mkiwa (kilomita 413);
- (iii) Mpemba-Isongole (Tanzania/Malawi Border);
- (iv) Handeni – Kiberashi - Kibaya –Kwamtoro - Singida (kilomita 461); na
- (v) Bagamoyo (Makurunge) – Saadani – Pangani - Tanga (kilomita 178).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, taratibu za kuwapata Wataalam Washauri kwa ajili ya kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea kwa barabara zifuatazo:-

- (i) Matai- Kasesya (kilomita 50);
- (ii) Ifakara-Mahenge (sehemu ya Lupilo- Mahenge);
- (iii) Kibondo-Mabamba (kilomita 35);

- (iv) Omugakorongo – Kigarama- Murongo (kilomita 111);
- (v) Kyaka- Bugene/Benako (kilomita 124);
- (vi) Kolandoto- Lalago- Mwanhuzi –Oldeani (kilomita 328);
- (vii) Ipole – Rungwa (kilomita 95);
- (viii) Mtwara – Newala – Masasi (kilomita 209);
- (ix) Kidatu –Ifakara – Londo – Lumecha/Songea (kilomita 396) ambayo imepata ufadhili wa *ADB*na *JICA* kwa ajili ya Mtaalam Mshauri; na
- (x) Daraja la Wami.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko; katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia *TEMESA* ilipanga:-

- (i) Kuendelea na taratibu za kununua vivuko vypya vya Ilagala (Tani 50) Mkoani Kigoma, Kahunda/ Maisome (Geita) na kivuko cha mwambao wa Bahari ya Hindi kati ya Magogoni (Dar es Salaam) na Bagamoyo;
- (ii) Kukamilisha ukarabati wa vivuko vya *MV. Chato* (Geita), *MV Kome I* (Mwanza), *MV. Kilombero I* (Morogoro), *Mv. Geita* (Mwanza) na *Itungi Port* (Mbeya) pamoja; na
- (iii) Kujenga maegesho katika vivuko vya Msanga Mkuu (Mtwara), Ruhuhu (Ruvuma), Maisome/Kahunda (Geita) na Rugezi/Kisorya upande wa Ukerewe (Mwanza).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013, kazi za ujenzi na ukarabati wa vivuko ilikamilika kwa vivuko vifuatavyo:-

- (i) Ujenzi wa kivuko cha Kilambo Mkoani Mtwara;
- (ii) Ujenzi wa kivuko cha Ilagala Mkoani Kigoma umekamilika huko Uholanzi na kivuko kimewasili hapa nchini tarehe 26 Aprili, 2013;
- (iii) Ujenzi wa maegesho ya Nkome, Rugezi na Utete umekamilika; na
- (iv) Ukarabati wa vivuko vya MV. Chato, MV. Sabasaba na MV. Kyanyabasa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya vivuko na maegesho inayoendelea katika mwaka 2012/2013 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ujenzi wa Kivuko cha Kahunda-Maisome umeanza na utakamilika Desemba, 2013;
- (ii) Maandalizi ya Ununuzi wa kivuko cha Itungi Port (Kyela Mbeya) unaendelea;
- (iii) Ujenzi wa kivuko cha Msanga Mkoo (Mtwara) unaendelea Bandarini Dar es salaam;
- (iv) Ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Msanga Mkoo mkoani Mtwara upande wa Msanga Mkoo umekamilika na umeanza kwa upande wa Msemio;
- (v) Ujenzi wa maegesho ya Kahunda -Maisome na maegesho katika vituo vya Mharamba, Senga na Ikumbitare umeanza Machi 2013;
- (vi) Usanifu wa maegesho ya kivuko kwa ajili ya usafiri kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo unaendelea. Aidha, mzabuni amepatikana kwa ajili ya ununuzi wa kivuko cha Dar es salaam hadi Bagamoyo;
- (vii) Ujenzi wa uzio katika vivuko vya Magogoni Dar es salaam na Kinesi Mkoani Mara umekamilika;

(viii) Zabuni imetangwaza kwa ajili ya ukarabati wa vivuko vya MV. Kome 1, na MV. Kilombero I; na

(ix) Mkandarasi wa kukarabati kivuko cha MV. Geita amepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Majengo imeendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Viongozi na watumishi wa umma, majengo ya ofisi za Serikali na majengo ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013, ujenzi wa nyumba za viongozi katika Wilaya za Bahi (2) na Kondoa (1), jengo la ghorofa 18 barabara ya Chimara (DSM); na jengo la ghorofa nane barabara ya Haille Selasie Dar es salaam ulikamilika na yameanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Majaji; Dar es Salaam (2), Arusha (1), Songea (1), Tanga (1), Mbeya (1), Tabora (1), Mwanza (1), Iringa (1), Dodoma (1), pamoja na ujenzi wa nyumba za viongozi Ukerewe(2) na Mvomero (1) upo kwenye hatua za mwisho za kukamilishwa. Taratibu za zabuni kwa ujenzi wa nyumba zingine tano (Kagera, Shinyanga, Kilimanjaro, Mtwara na Dar es Salaam) zimeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa ya kupangisha kibashara Jijini Arusha (Wachaga Street na Simeoni Street) unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2014. Miradi ya ujenzi wa ghorofa lenye nyumba 16 za kupangisha kibashara eneo la SIDA – Dar es Salaam, ghorofa lenye nyumba nane, Mbezi Beach – Dar es Salaam na nyumba tatu Arusha upo katika hatua za umaliziaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bariadi, zahanati katika Manispaa

ya Lindi na zahanati katika eneo la Mwangaza Dodoma pamoja na ukarabati wa jengo la karakana za *MT. Depotna* Dodoma unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na utekelezaji wa Sera ya Usalama Barabarani ya mwaka 2009 kwa kutekeleza yafuatayo katika mwaka 2012/2013:-

(i) Kutoa elimu ya usalama barabarani kwa Shule za Msingi ili kupunguza ajali nchini;

(ii) Kuandaa na kuendesha kampeni za kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa usalama barabarani;

(iii) Kushirikiana na wadau muhimu kama vile Jeshi la Polisi, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu, Sheria na kadhalika katika kutoa elimu ya Usalama barabarani na kusimamila utekelezaji wa sheria zilizopo;

(iv) Kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara na kufanya tafiti za kutumia teknolojia ya kisasa katika kudhibiti uzito;

(v) Kuandaa taratibu za uanzishwaji wa Wakala wa Usalama barabarani; na

(vi) Kuandaa mapendekezo ya rasimu ya Sheria ya Usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara; katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, masuala yafuatayo yametekelawa ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara. Wizara imeteua Waratibu wa Mikoa katika mikoa yote Tanzania Bara ambao watakuwa na jukumu la kuhamasisha wanawake kushiriki katika kazi za barabara katika mikoa husika. Wizara imefuatilia kujua idadi ya kampuni za Makandarasi zinazomilikiwa na wanawake katika kila Mkoa ambao wako hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa jumla ya kampuni

za Makandarasi 125 zinamilikiwa na wanawake. Aidha, Wizara kupitia Kitengo cha Ushirikishaji Wanawake kimeendesha mafunzo kwa vikundi nya Wanawake na Makandarasi Wanawake 30 ili kuwaongezea uwezo wa kujenga na kuzifanyia matengenezo barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, washiriki wa warsha hiyo wamepata sifa ya kuanzisha Kampuni za Ukandarasi na kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi. Washiriki wa warsha hiyo walitoka Mikoa ya Kilimanjaro, Singida, Manyara, Tanga, Geita, Dar es Salaam, Katavi, Njombe na Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2012/2013, Wizara ilifanya kazi ya ufuatiliaji (*Monitoring*) kujua maendeleo na kiwango cha ushiriki wa wanawake katika miradi ya barabara. Wizara illweza kujua kiwango cha ushiriki wa wanawake kwenye miradi ya barabara hasa kwa wanawake wa kada za vibarua na wengineo ambao wanapata kipato kwa kazi za barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa Wizara katika Jumuiya mbalimbali za Kimataifa; katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kushiriki katika masuala yanayohusu Sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda na hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa EAC, Wizara imeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya barabara zinazounganisha nchi wanachama ukiwemo mradi wa ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga kwa kiwango cha lami. Mradi huu umekamilika na kufunguliwa rasmi na Wakuu wa Nchi za Tanzania na Kenya tarehe 28 Novemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa daraja la Rusumo linalounganisha Tanzania na Rwanda, usanifu wa barabara ya Bagamoyo – Saadani - Tanga, usanifu wa barabara ya

Arusha – Himo – Holili/Taveta na ujenzi wa Vituo vya pamoja vya mipakani (*One Stop Border Posts*) vya Namanga, Rusumo, Kabanga na Mutukula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia ilishiriki katika maandalizi ya Muswada wa Udhibiti wa Uzito wa Magari katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Vehicle Load Control Bill*, 2012) ambao unashubiri kuitishwa na Bunge la Afrika Mashariki. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi za *EAC* uliofanyika Nairobi tarehe 29 Novemba, 2012 ambao pamoja na mambo mengine ulipitisha miradi ya kipaumbele kwa ajili ya kuimarisha ufanisi wa huduma za bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara zetu, miradi iliyokubaliwa na Wakuu wa nchi za *EAC* ni barabara za kupunguza msongamano katika kuingia na kutoka Bandari ya Dar es Salaam; barabara ya Nyakanazi – Kasulu – Kidahwe – Mpanda; barabara ya Tanga – Saadani – Bagamoyo, barabara ya Nyanguge – Musoma – Sirari; barabara ya Lusahunga – Rusumo na barabara ya Nyakasanza – Kobero. Miradi hii ya barabara ijumuishwa kwenye mpango wa *EAC* wa kuboresha huduma za bandari na reli ambazo zinahudumia Tanzania na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *SADC*, mwaka 2012/2013, Wizara ilishiriki katika maandalizi ya Mpango wa Kuendeleza Miundombinu (*SADC Regional Infrastructure Development Master Plan*) ambao ulipitishwa na Nchi Wanachama wa *SADC* mwezi Agosti, 2012 Maputo nchini Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Mpango huu ni kuwa na miundombinu ya uhakika itakayozunganisha nchi wanachama ili kupunguza gharama na kurahisisha biashara. Mpango huo unahusisha uendelezaji wa miradi ya kipaumbele ya miundombinu katika Sekta za Nishati, Uchukuzi, Utalii, Maji, Mawasiliano na Hali ya Hewa. Miradi ya barabara inayojumuishwa katika Mpango Kamambe inahusisha:-

(i) Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze (*Expressway*- kilomita 100) kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa za Burundi, DR Congo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia;

(ii) Barabara ya Mtwara – Mbamba bay sehemu ya barabara ya Mbinga – Mbamba *Bay* (kilomita 66) inayoiunganisha Tanzania na nchi za Malawi na Zambia;

(iii) *TANZAM Highway* sehemu ya barabara ya Makambako – Songea (kilomita 289) inayoiunganisha Tanzania na nchi ya Msumbiji; na

(iv) Barabara ya Manyoni – Tabora – Kigoma sehemu za barabara ya Nyahua – Chaya (kilomita 90) na Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi (kilomita 310) zitakazoiunganisha Tanzania na nchi za DR Congo, Zambia na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi Wanachama kwa kushirikiana na Sekretarieti ya *SADC* zinaendelea na mikakati ya kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kamambe wa Kuendeleza Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Watumishi; katika mwaka 2012/13, Wizara imeendelea kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka jumla ya watumishi 25 katika mafunzo ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi 12 walishiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi 13 walipelekwa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watumishi wawili walipata mafunzo ya muda mrefu na watumishi wawili walipata mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi. Watumishi 10 walipata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 11 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Aidha, watumishi 20 walipandishwa vyeo, watumishi wawili walibadilishwa kada, watumishi watatu walithibitishwa kazini na watumishi 11 walijiriwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Kupambana na

UKIMWI. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara iliendelea kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na VVU kwa watumishi kwa kutumia wataalam kutoka Tume ya Kudhibiti Ukimwi (*TACAIDS*). Aidha, watumishi wameendelea kuhamashisha kupima afya zao pamoja na kuwapatia huduma ya lishe bora kwa watumishi walioathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita dhidi ya rushwa; Wizara katika mwaka wa fedha 2012/2013, iliendelea kuwaelimisha watumishi athari ya kutoa na kupokea rushwa pamoja na kuwahimiza kupambana na rushwa katika mazingira yote ya kazi. Elimu kuhusu mapambano dhidi ya rushwa ilitolewa kuititia vipeperushi, semina na mikutano mbalimbali kwa ushirikiano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*TAKUKURU*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEHAMA*); Wizara inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sera na mipango ya Wizara ya Ujenzi, umuhimu wa kutunza barabara na kuzingatia sheria na kanuni za matumizi ya barabara na sheria zingine zinazosimamia Sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEHAMA*) ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma kwa wakati. Tovuti ya Wizara imuboreshwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi. Wizara imeshiriki katika mikutano na mafunzo yanayolenga matumizi ya *TEHAMA* ili kuboresha utendaji wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara (*RFB*). Katika mwaka 2012/2013, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 429.664. Hadi tarehe 31 Machi, 2013, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya na kugawa kiasi cha Shilingi bilioni 333.7 ambazo ni sawa na asilimia 77.7 ya lengo la Shilingi bilioni 429.664 kwa mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine iliyofanywa na

Bodi katika mwaka 2012/13 ni kufuatilia na kukagua miradi ya matengenezo ya barabara inayotumia fedha za Mfuko nchi nzima. Kwa mwaka 2012/2013, Bodii liliifanya ukaguzi katika mikoa kumi na moja (11) ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Rukwa, Tabora, Dar es Salaam, Mwanza, Lindi, Mara, Katavi na Iringa. Pale inapobainika kuna udhaifu, mamlaka husika zilitaarifiwa na hatua stahiki zilichukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ufundii na Umeme; katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Ufundii na Umeme (*TEMESA*) imeendelea kusimamia uendeshaji wa vivuko 22 katika maeneo 15 hapa nchini kama ifuatayyo:-

- (i) Magogoni—Kigamboni- *MV. Magogoni*, Tani 500 na *MV. Kigamboni*, Tani 170;
- (ii) Ilagala (Kigoma)-*MV. Ilagala*, Tani 50;
- (iii) Kinesi—Musoma (Mara)-*MV. Musoma*, Tani 85;
- (iv) Ifakara—Ulanga (Mto Kilombero)- *MV. Kilombero I*, Tani 50, na *MV. Kilombero II*, Tani 50;
- (v) Kisorya—Rugezi (Mwanza/Mara)- *MV. Ujenzi*, Tani 50, na *MV. Sabasaba*, Tani 85;
- (vi) Rusumo - Nyakiziba (Mto Ruvuvu, Kagera)- *MV. Ruvuvu*, Toni 35;
- (vii) Kasharu - Buganguzi (Mto Ngono, Kagera)-*MV. Kyanyabasa*, Tani 7;
- (viii) Utete (Mto Rufiji)-*MV. Utete*, Tani 50;
- (ix) Pangani—Bweni (Mto Pangani – Tanga)-*MV. Pangani II*, Tani 50;
- (x) Kigongo—Busisi (Mwanza)-*MV. Misungwi*, Tani 250, *MV. Sengerema*, Tani 170, na *MV. Geita*, Tani 65;

(xi) Nyakaliro—Kome (Sengerema)-*MV.* Kome I, Tani 25 na *MV.* Kome II, Tani 40;

(xii) Ilunga - Kipingu (Mto Ruhuhu – Ruvuma)- *MV.* Ruhuhu, Tani 50;

(xiii) Bugolora—Ukara (Ukerewe/Ukara)-*MV.* Nyerere, Tani 25;

(xiv) Chato—Muhamamba—Zumacheli—Senga-Bukondo—Nkome-*MV.* Chato, Tani 75 na *MV.* Ukara, Tani 25; na

(xv) Kilambo - Namoto –*MV.* Kilambo Tani 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TEMESA* imeendelea kusimamia huduma za ukodishaji magari ya viongozi. *TEMESA* pia imetoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na mabarafu katika majengo ya Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Miradi ya kuboresha vituo na Vyuo vya Afya vya Mbeya, Mirembe (Dodoma), Tanga, Kairuki (Dar es Salaam), Sengerema, Rukwa na Mvumi;

(ii) Mradi wa maboresho ya *Theatre* katika Hospitali ya Mawenzi Moshi;

(iii) Mradi wa ujenzi wa Mahakama Kuu ya Shinyanga;

(iv) Mradi wa ukarabati wa Ofisi za muda za *TBA* Mkoa wa Njombe;

(v) Mradi wa usimikaji wa lifti katika jengo la Ofisi za Wizara ya Katiba na Sheria;

(vi) Miradi ya ununuzi na usimikaji wa jenereta katika Ofisi za Wizara ya Maji, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi

ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, *TANROADS*– Lindi, Chuo cha Uvuvi Mbegani na Chuo cha Maji;

(vii) Miradi ya ujenzi wa karakana za vyuvo vyaa maendeleo ya Jamii katika Mikoa ya Tanga, Tabora, Pwani na Mara;

(viii) Miradi ya ujenzi wa nyumba za Makazi ya Majaji katika Miji ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Tabora, Dodoma, Mbeya, Iringa na Mwanza;

(ix) Mradi wa ujenzi wa Ofisi za *SIDO* Mkoa wa Pwani; na

(x) Mradi wa ukarabati wa nyumba za makazi za Majaji Mikoa ya Mwanza, Iringa na Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13 Wizara kuititia *TEMESA* ilipanga kutengeneza magari katika Karakana zake zote zilizopo kila Mkoa. Hadi kufikia Aprili, 2013 *TEMESA* ilitengeneza magari 5,938. Matengenezo ya mifumo ya Umeme, Elektroniki Viyoyozi na Majokofu katika ofisi mbalimbali umeendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TEMESA* imeendelea kuimarisha karakana zake kwa vifaa vyaa umeme, elektroniki na mitambo. Mashine za kutambua matatizo ya Magari (*Computerised Diagonistic Machine*) imepatikana. Mashine nyingine 10 kama hiyo ziko katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya karakana 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilipanga kusajili Wahandisi 955, kampuni za ushauri wa kihandisi 25 na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa Wahandisi wahitimu 1,000. Hadi Aprili, 2013 Bodi ilisajili Wahandisi 838 na kampuni za ushauri wa kihandisi 10 na kufikisha jumla ya Wahandisi 12,102 waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali na kampuni za ushauri wa kihandisi 237.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati yao, jumla ya Wahandisi waliosajiliwa 10,694 ni wazalendo, na 1,408 ni wageni. Kampuni za ushauri wa kihandisi 169 ni za kizalendo na 68 ni za kigeni. Aidha, katika kipindi hicho, Bodi ilisajili Wahandisi Washauri 17 na kufanya jumla ya Wahandisi Washauri kuwa 386, kati yao 299 ni wazalendo na 87 ni wageni. Bodi ilifuta usajili kwa Wahandisi Washauri watatu na Kampuni ya Ushauri wa Kihandisi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi imetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:-

(i) Kusimamia mafunzo ya kuijendeleza kitaaluma kwa Wahandisi wote ili kuwafanya Wahandisi kwenda sambamba na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia na hivyo kuweza kufanya shughuli zao za kihandisi kwa ufanisi. Lengo pia ni kuwafanya Wahandisi kumudu ushindani unaoletwa na utandawazi. Wahandisi watalaan zaidi ya 3,000 wamenufaika na mpango huu.

(ii) Kukagua miradi ya ujenzi wa barabara na majengo ili kuhakikisha kuwa inajengwa na Wahandisi waliosajiliwa. Katika kipindi hiki, jumla ya miradi 504 ilikaguliwa. Aidha, Wahandisi wa kigeni 15 walibainika kufanya kazi bila usajili. Kati yao nane walikuwa na sifa na hivyo walisajiliwa na saba walikataliwa usajili kwa sababu hawakuwa na sifa za kutosha.

(iii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi wahitimu. Katika kipindi hiki Bodi ilisimamia mafunzo ya Wahandisi wahitimu 651. Kati ya Wahandisi hao, Wahandisi wahitimu 189 wa kike wanafadhiliwa na Serikali ya Norway.

Jumla ya Wahandisi wahitimu 2,224 wameshapitia mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003. Aidha, Wahandisi wahitimu zaidi ya 177 toka Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali wameshahitim mafunzo hayo na kusajiliwa na Bodi kama Wahandisi watalaan.

(iv) Kukagua miradi na kuhakiki kama Makandarasi wana Wahandisi wa kutosha na wenye uwezo kutekeleza miradi hiyo. Katika kipindi cha 2012/2013, Bodii likagua jumla ya miradi 104. Makandarasi waliobainika kutokuwa na Wahandisi wa kutosha, walielekezwa kuajiri Wahandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi. Katika mwaka 2012/2013, lengo la Bodi lilikuwa ni kusajili Wabunifu Majengo 18, Wakadiriaji Majenzi 25, Wataalamu wenye sifa za kati 31, Mafundi Sanifu saba, Warasimu (*Draughtsmen*) tatu na Kampuni za Ubunifu Majengo 14 na Ukadiriaji Majenzi tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013, Bodii lisajili Wabunifu Majengo 18 na Wakadiriaji Majenzi 25 na hivyo kufanya jumla ya wataalam wa fani hizo waliosajiliwa na Bodi kuwa 549 (337 ni Wabunifu Majengo, 211 ni Wakadiriaji Majenzi na *Building Surveyor* mmoja). Aidha, Kampuni 11 za Wabunifu Majengo na Kampuni tisa za Wakadiriaji Majenzi zilisajiliwa na kufanya jumla ya kampuni zilizosajiliwa kuwa 270.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi pia iliwasajili wataalam wa fani za sifa za kati 66. Bodi iliwafutia usajili Wabunifu Majengo nane, Wakadiriaji Majenzi saba, makampuni tisa na kusitisha usajili wa Mbunifu majengo mmoja kwa muda. Bodi pia ilisajili miradi ya ujenzi 774. Usajili wa miradi hiyo unasaidia kupatikana kwa taarifa za ujenzi kwa Serikali na pia wadau wote wa Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba shughuli za majenzi zinasimamiwa na kampuni za Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi waliosajiliwa, Bodii likagua miradi ya ujenzi 2,112 katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Tathmini ya ukaguzi huo imeonesha kuwa kuna uelewa mdogo kwa waendelezaji kuhusu umuhimu wa kutumia ushauri wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi katika kuendeleza miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wanachanganya taaluma hizi na Wahandisi au Makandarasi. Bodi ilichukua hatua za kuwaelimisha wadau husika umuhimu wa kuwatumia wataalam hao katika miradi ya ujenzi wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilipanga kusajili jumla ya Makandarasi 807 na kutathmini Makandarasi 587 ili kujiridhisha kama wana sifa na uwezo wa kuendelea kuwa katika madaraja waliyopo. Aidha, Bodi ilipanga kukagua miradi ya ujenzi 3,090 nchi nzima kwa lengo la kuhakikisha kwamba kazi zote zinafanywa na Makandarasi waliosajiliwa na pia kuwa Makandarasi wanafuata sheria na taratibu za usajili wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013 Bodi ilisajili Makandarasi wapya 813 na ilifuta Makandarasi 366 walioshindwa kuzingatia sheria na taratibu za ukandarasi. Hivyo hadi kufikia Aprili, 2013, Bodi ilikuwa na Makandarasi 6,991. Aidha, Bodi ilikagua jumla ya miradi 2,480. Katika miradi iliyokaguliwa miradi 1,672 sawa na asilimia 67.4 ilionekana kutekelezwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za usajili na miradi 808 ambayo ni asilimia 32.6 ilikiuka sheria na taratibu hizo. Makandarasi husika walichukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Makandarasi Namba 17 ya mwaka 1997 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 24 ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi pia imeendeleza programu za kuendeleza Makandarasi, kuimarisha Mfuko wa kusaidia Makandarasi wadogo na kukuza uwezo wa Makandarasi wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi. Katika mwaka 2012/2013 Baraza liliendelea kutekeleza majukumu yake ya kushughulikia maendeleo ya Sekta ya Ujenzi nchini. Baraza liliendesha mafunzo kwa wadau 163 wa sekta kuhusu shughuli za zabuni, menejimenti ya mikataba,

usuluhishi wa migogoro, menejimenti ya madai, gharama za ujenzi wa barabara, shughuli za matengenezo na ukarabati wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza liliandaa mafunzo maalum (*Tailor Made Course*) yaliyofanyikia Mtwara kwa ajili ya Halmashauri ya Mtwara, ambapo wadau 13 walipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya mitambo ya kisasa kwenye upimaji na ramani, usimamizi wa miradi ya ujenzi na usuluhishi wa migogoro ya miradi ya ujenzi. Aidha, Baraza lilitafiti zifuatazo:-

(i) Upimaji wa tija na ubora wa kazi katika Sekta ya Ujenzi;

(ii) Ushindani wa Makandarasi wazalendo katika kutekeleza miradi ya ujenzi ikillinganishwa na Makandarasi wa kigeni;

(iii) Kanuni za mikataba katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu (barabara na kadhalika); na

(iv) Usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa njia ya Kusanifu na kujenga (*Design and Build*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza katika mwaka 2012/2013, liliendelea kutoa ushauri wa kiufundi kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na *Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC)*, *National Ranch Corporation (NARCO)*, *National Audit Office (NAO)* na *Roads Fund Board (RFB)*. Aidha, Baraza lilihughulikia usuluhishi wa migogoro ya miradi ya ujenzi ipatayo 39.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Vikosi vya Ujenzi ni kufanya kazi za ujenzi na ukarabati wa majengo na shughuli zingine zinazohusiana na ujenzi. Aidha, Vikosi vina jukumu la kubuni na kutekeleza miradi yoyote ya kibiasahara

yenye mahusiano na kazi za ujenzi. Makao Makuu ya vikosi yapo Dar es Salaam. Vikosi vina matawi Arusha, Dodoma na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Vikosi vimekamilisha ujenzi wa maegesho (*Ferry ramps*) ya Rugezi kwa ajili ya Kivuko cha Rugezi – Kisorya, Ukerewe Mwanza. Aidha, Vikosi vimekamilisha ukarabati wa Ofisi zake Dar es Salaam na Mwanza na kuanza ukarabati wa Karakana za useremala (*Carpentry workshops*) Dar es Salaam na Dodoma. Vikosi vinaendelea na ujenzi wa nyumba za viongozi Dar es Salaam na Mwanza ukiwemo ujenzi wa nyumba za Majaji Dar es Salaam na Mwanza (*Phase I*).

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine iliyofanywa na Vikosi ni pamoa na ujenzi wa maegesho ya Kivuko cha Msangamkuu-(Mtwara), ukarabati wa Jengo la Hospitali ya Rufaa Mbeya, ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Nyumba za watumishi Siha (Kilimanjaro), ujenzi wa uzio katika Kivuko cha Kigamboni, ujenzi wa uzio katika eneo la kuegesha magari Kimara (Dar es Salaam) na ujenzi wa uzio katika Kiwanja cha Ndege cha Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi (*Tanzania Transportation Technology Transfer Centre*). Madhumuni ya Kituo hiki ni kuimarisha Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kusambaza teknolojia za kisasa kwa wadau wa sekta hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Kituo kilisambaza makala na taarifa 82 kwa wadau 94,500 zinazoelezea teknolojia mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi. Kituo kimeendelea na maandalizi ya Mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na uchukuzi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *Morgan State University* ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Chuo cha Ujenzi, Morogoro kilipanga kuendeleza ujenzi wa

jengo jipya la madarasa na karakana ya ufundi, kukarabati majengo matatu, pamoja na kununua samani na zana za kufundishia. Aidha, chuo kilipanga kufundisha jumla ya wanafunzi 780 katika fani za fundi stadi wa kazi za barabara, majengo pamoja na udereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2013, jumla ya wanafunzi wa fani za ujenzi 662 walipata mafunzo kama ifuatavyo:-

Basic technical course (224), Basic driving course (201), Passenger Service Vehicle (PSV) Driving course (140) na Technician Maintenance Management course (97).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Chuo kimefanya ukarabati wa majengo ikiwa ni pamoja na karakana ya umeme wa majumbani na magari. Aidha, ujenzi wajengo jipya ya karakana na madarasa unaendelea. Chuo kilinunua vifaa mbalimbali vyta kufundishia na matumizi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Matumizi Stahiki ya Nguvu Kazi - Mbeya. Katika mwaka 2012/2013, Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi-Mbeya (ATTI) kimetoa mafunzo kwa Wahandisi 18 kutoka Somalia na Mafundi Sanifu 30 kutoka nchini. Aidha, Chuo kimetoa ajira kwa wananchi 150 kuititia mafunzo ya vitendo kuhusu ukarabati na matengenezo ya barabara kwa Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo pia kimetoa elimu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa wanavijiji wapatao 550 waliopo jirani na kukarabati barabara za wanavijiji jumla ya kilometra 11 kwa kujitolea kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa utunzaji wa barabara zinazowazunguka. Aidha, Chuo kimefanya matengenezo na ukarabati wa jumla ya kilometra 88.5 kwa barabara za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato 2013/

2014; katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya Sh. 45,047,550.00 kutoka Idara zenyeye vyanzo vya mapato ambazo ni Idara za Utawala na Rasilimali Watu, Huduma za Ufundu na Idara ya Menejimenti ya Ununuzi. Sehemu kubwa ya mapato hayo itatokana na ada za kusajili magari, pikipiki, bajaji na mitambo ya Serikali kwa namba za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 ni Sh. 381,205,760,000.00. Kati ya fedha hizo, Sh. 21,211,514,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, Sh. 6,944,846,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi na Sh. 353,049,400,000.00 ni fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2013/2014. Vipaumbele vya miradi ya maendeleo itakayotekelawa na Wizara kwa mwaka 2013/2014 vimezingatia miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na wahisani, utekelezaji wa miradi iliyo katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Ujenzi imetengewa kiasi cha Sh. 845,225,979,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kat i ya fedha hizo, Sh. 448,174,599,000.00 ni fedha za ndani na Sh. 397,051,380,000.00 ni fedha za nje. Aidha, maelezo ya kila mradi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, vivuko na nyumba za Serikali, ujenzi wa Maegesho ya Vivuko Shilingi Milioni 5,990.00. Katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Ujenzi kupitia TEMESA itaendelea kujenga maegesho (*Landing Ramps*) ya vivuko ili vivuko viweze kuegeshwa kwa urahisi na usalama. Mradi huu umetengewa Shilingi milioni 5,990.00 kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

Ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Msanga Mkuu awamu ya II (Shilingi milioni 150.00), Ujenzi wa maegesho ya

Kilambo (Shilingi milioni 115.00), kumalizia ujenzi wa maegesho ya Ukara (Shilingi milioni 185.00) na kumalizia ujenzi wa maegesho Kilombero (upande wa Ulanga) (Shilingi milioni 50.00).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ujenzi wa maegesho ya Kahunda – Maisome umetengewa Shilingi milioni 854.00, ujenzi wa maegesho Itungi *Port* (Shilingi milioni 375.00), ujenzi wa maegesho Ilagala Shilingi milioni 250.00, ujenzi wa maegesho mwambao mwa bahari ya Hindi katika maeneo ya Magogoni, Jangwani *Beach* na Rungwe *Oceanic Shilingi* milioni 2,500.00 na kumalizia ujenzi wa maegesho ya Bugolora Shilingi milioni 54.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa sehemu ya Maegesho ya Kigamboni umetengewa Shilingi millioni 346.00, upembusi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya usafiri wa majini kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo Shilingi milioni 215.00 na ujenzi wa vituo vya kusubiria kivuko kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo katika maeneo ya *Govenor Jet* (Kivukoni), Jangwani *Beach* na Rungwe *Oceanic Hotel Shilingi* milioni 600.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembusi yakinifu kwa lengo la kuanzisha usafiri wa majini katika mwambao wa Ziwa Victoria ili kupunguza msongamano katika Jiji la Mwanza umetengewa Shilingi milioni 200.00. Shilingi milioni 96 zimetengwa kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa Vivuko Vipya - Shilingi Milioni 4,484.00. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu umetengewa Shilingi milioni 4,484.00 kwa ajili ya ununuzi wa Kivuko kipyta cha Dar es Salaam - Bagamoyo, boti ya uokoaji, mashine za kisasa za kukatia tiketi (*ticket vending machines*) kwa kivuko cha Magogoni na vifaa vya karakana za *TEMESA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukarabati wa Vivuko - Shilingi Milioni 2,102.2. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014,

miradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 2,102.21 kwa ajili ya ukarabati wa vivuko mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali - Shilingi Milioni 2,245.49). Miradi wa kujenga na kukarabati nyumba kwa ajili ya makazi ya Viongozi na Watumishi wa Serikali utaendelea kwa kutoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za Majaji pamoja na viongozi wengine wa Serikali wenyewe stahili ya kupewa nyumba na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 1,010.43 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba za Majaji katika Mikoa ya Kilimanjaro (1), Mtwara (1), Kagera (1), Dar es Salaam (1) na Shinyanga (1). Shilingi milioni 250.00 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bariadi Mkoani Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetenga jumla ya Shilingi milioni 220 ajili ya kufanya ukarabati pamoja na kuendelea na ujenzi wa uzio kuzunguka nyumba za viongozi katika nyumba za viongozi wa Serikali zilizopo Mikocheni, Kijitonyama na Msasani Peninsullar. Shilingi milioni 240.50 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa samani katika nyumba za viongozi wa Serikali wenyewe stahili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha Shilingi milioni 150.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa karakana za *TEMESA* na Shilingi milioni 40 kwa ajili ya ukarabati wa karakana na ofisi za Vikosi vya Ujenzi Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Shilingi milioni 140.00 zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Shilingi milioni 113.44 kwa ajili ya kazi za ushauri na Shilingi milioni 81.12 zimetengwa kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi kwa kuitia

Wakala wa Majengo imeanza kutekeleza mradi wa kujenga nyumba 10,000 kwa ajili ya kuishi na kuwauzia wafanyakazi wa Serikali. Wakala umesajili Kikosi cha Ujenzi (*Tanzania Building Agency Construction Company*); pamoja na kuwapatia mafunzo maalum wataalam wa vikosi vyta ujenzi vyta Jeshi la Polisi, Magereza, JKT na kikosi cha Wizara ya Ujenzi (*CSWS*) ambao watashiriki katika mradi huu. Maandalizi na mafunzo hayo ni kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa nyumba nyingi kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wakala umepata jumla ya viwanja 2,490 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 10,000 kama ifuatavyo:-

Arusha (29), Dar es Salaam (627), Dodoma (37), Geita (24), Iringa (54), Kagera (2), Katavi (100), Kigoma (164), Kilimanjaro (63), Lindi (41), Manyara (32), Mara (267), Mbeya (74), Morogoro (15), Mtwara (90), Mwanza (63), Njombe (102), Rukwa (70), Ruvuma (8), Shinyanga (131), Simiyu (308), Singida (22), Tabora (42), Tanga (123) na Pwani (2). Kati ya viwanja hivyo, jumla ya viwanja 413 vimepata hati miliki kama vifuatavyo: Dar es Salaam (314), Arusha (5), Iringa (53) na Lindi (41).

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wakala umeanza kazi ya ujenzi wa nyumba 132 kati ya nyumba 2,500. Nyumba 25 Bunju "B" DSM zimefikia hatua ya umalizaji. Nyumba 87 Bunju "B" Dar es Salaam; nyumba 20 katika Mikoa mipya ya Simiyu (4), Geita (4), Njombe (4), Katavi (4) pamoja na Chalinze, Pwani (4) zitaanza kujengwa katika mwaka 2012/2013. Mradi huu maalum utatumia fedha za Wakala zitokanazo na mauzo ya nyumba na mikopo kutoka Taasisi za Fedha. Baadhi ya Taasisi hizo zimeonesha nia thabiti ya kushirikiana na Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wakala utakamilisha mazungumzo na Taasisi za fedha ili kuweza kupata mkopo wa ujenzi; utakamilisha ujenzi wa nyumba 25 katika eneo la Bunju "B" na utaandaa upembuzi yakinifu na usanifu wa majengo kwa ajili ya ujenzi katika Mikoa

12 ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Mtwara, Iringa, Lindi, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wakala utaendelea na ujenzi wa nyumba 2,500 katika Mikoa ya Dar es Salaam (1,400), Arusha (150), Dodoma (250), Mwanza (150), Mbeya (150), Mtwara (100), Iringa (100), Lindi (50), Bariadi (50), Geita (50), Njombe (50) na Mpanda (50).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara na madaraja. Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (*Expressway*) kilomita 200, Sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (kilomita 100) – Shilingi Milioni 100. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (kilomita 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (kilomitam 100) kwa kiwango cha *Expressway*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya mradi huu utakaotekelawa kwa ubia baina ya Serikali na makampuni binafsi yameanza. Baada ya mradi kutangazwa Kampuni 19 zimewasilisha maombi ya kujenga barabara hii na kuonyesha jinsi ambavyo watatekeleza mradi huu. Uchambuzi wa maombi ya kampuni hizo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, kiasi cha Shilingi milioni 100.00 zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Awamu ya Kwanza itakayohusisha sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (kilomita 100).

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (sehemu ya Bagamoyo – Msata (kilomita 64) - Shilingi milioni 10, 885.24. Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Bagamoyo – Makofia - Msata (kilomita 64). Mkataba wa Ujenzi ulisainiwa tarehe 11 Agosti 2010 kwa gharama ya Shilingi milioni 89,610. Kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami inaendelea. Lengo pia ni kuendelea na usanifu wa barabara ya Bagamoyo – Sadani – Tanga (kilomita 178).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 10,441.10 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata (kilomita 64) kwa kiwango cha lami. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 444.14 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa barabara ya Bagamoyo – Sadani – Tanga (kilomita 178).

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Usagara – Geita – Kyamyorwa (kilomita 422) Sehemu ya Uyovu – Biharamulo (kilomita 112) - Shilingi Milioni 10,800.00. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo – Geita hadi Usagara (kilomita 310) na sehemu ya Uyovu - Biharamulo (kilomita 112).

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ilihuisha ujenzi wa Barabara ya Kyamyorwa - Geita (kilomita 220) ambayo ilikamilika Februari, 2008. Awamu ya pili ilihuisha ujenzi wa barabara ya Geita - Usagara (kilomita 90) ambapo ujenzi wake ulianza Februari, 2008 na umekamilika Januari, 2010. Awamu ya tatu itahusisha ujenzi wa barabara ya Uyovu - Biharamulo kuititia Bwanga (kilomita 112).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 8,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Uyovu – Biharamulo (kilomita 112), kiasi cha Shilingi milioni 800.00 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kyamiyorwa –Buzirayombo (kilomita 120) na kiasi cha Shilingi milioni 2,000.00 kimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho ya sehemu ya Geita - Usagara (lot 1 na 2) (kilomita 90).

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (kilomita 443) – Shilingi Milioni 51,669.34. Mradi huu unalenga kufanya usanifu na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kati ya Kigoma na Tabora (kilomita 443) pamoja na ujenzi wa daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi na barabara za maingilio ya daraja (kilomita 48).

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi wa daraja ilianza tarehe 2 Desemba, 2010 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2013. Ujenzi wa barabara ya Kidahwe - Uvinza (kilomita 76.6) ulianza tarehe 17 Desemba, 2010 na kazi za ujenzi zinaendelea. Ujenzi wa barabara za Tabora-Ndono (kilomita 42) na Ndono-Urambo (kilomita 52) ulianza tarehe 3 Januari, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 2,131.95 fedha za ndani na Shilingi milioni 10,693.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Kidahwe-Uvinza (kilomita 76.6). Kiasi cha Shilingi milioni 3,139.53 fedha za ndani na Shilingi milioni 10,130.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha Shilingi milioni 6,837.80 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tabora - Ndono (kilomita 42), Shilingi milioni 7,189.04 kwa ajili ya sehemu ya Ndono -Urambo (kilomita 52) na kiasi cha Shilingi milioni 4,848.02 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Urambo – Kaliua – Ilunde (kilomita 146). Barabara za Tabora – Sikonge (kilomita 70) na Uvinza – Malagarasi (kilomita 51) zimetengewa kiasi cha Shilingi milioni 6,700 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Marangu – Tarakea – Kamwanga/Bomang'ombe – Sanya Juu (kilomita 173) na Arusha – Moshi – Holili (kilomita 140) – Shilingi Milioni 11,133.63. Mradi huu unalenga kujenga barabara ya Marangu –Tarakea – Rongai – Kamwanga (kilomita 96) kwa kiwango cha lami na kukarabati barabara ya Arusha – Moshi – Holili pamoja na Arusha *By-Pass* (kilomita 140).

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa sehemu ya Tarakea – Rongai – Kamwanga (kilomita 32) ulikamilika Septemba, 2009 na ujenzi wa sehemu ya Tarakea – Rombo Mkuu (kilomita 32) ulikamilika Januari, 2011. Kazi za ujenzi wa

sehemu ya Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (kilomita 32) zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Septemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 488.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipia sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi wa Tarakea – Rombo na Shilingi milioni 2,146.00 ni kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Marangu – Rombo Mkuu na Mwika- Kilacha (kilomita 34).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kiasi cha Shilingi milioni 5,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu – Kamwanga (kilomita 75). Jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 fedha za ndani zimetengwa kuanza ujenzi wa barabara ya njia nne katika mradi wa Arusha – Moshi – Holili/Taveta-Voi sehemu ya Sakina-Tengeru (kilomita 14.10) na ujenzi wa Arusha *Bypass* (kilomita 42.41). Aidha, Shilingi milioni 2,500 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya KIA-Mererani (kilomita 26).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nangurukuru - Mbwemkulu (kilomita 95) – Shilingi Milioni 2,000.00. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo. Ujenzi wa barabara hii ulikamilika Januari, 2008. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho kwa Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Dodoma – Manyoni (kilomita 127) – Shilingi Milioni 1,309.28. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma - Manyoni (kilomita 127) kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*Design & Build*). Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na ulikamilika Novemba, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 1,309.28 fedha za ndani

zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini (kilomita 4.8) na kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mbwemkulu – Mingoyo (kilomita 95) – Shilingi milioni 1,000.00. Mradi huu umehusisha kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbwemkulu - Mingoyo yenyе urefu wa kilomita 95 kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*Design & Build*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es salaam – Lindi – Mingoyo na ujenzi wake ulikamilika Desemba, 2007. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, barabara hii imetengewa kiasi cha Shilingi milioni 1,000.00 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Manyoni – Singida. Sehemu ya Manyoni – Isuna (kilomita 54) – Shilingi Milioni 1,200 .00. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Manyoni - Isuna (kilomita 54) kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*Design & Build*). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi ulikamilika tarehe 7 Januari, 2011. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 1,200.00 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya *Port Access* (Nelson Mandela - kilomita 15.6) *Rehabilitation* – Shilingi Milioni 1,500.00. Lengo la mradi huu lilikuwa ni kukarabati na kuimarissha barabara ya Nelson Mandela (kilomita15.6) iliyokuwa imeharibika ili kurahisisha kupita kwa magari ya mizigo yanayotoka au kuingia Bandari ya Dar es Salaam na kupunguza msongamano wa magari kwa jiji la Dar es Salaam. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 1,500.00 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa malipo ya mwisho ya mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Dumila – Kilosa (kilomita 78) – Shilingi Milioni 6,000.00. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara Dumila – Kilosa (kilomita 78). Kazi ya ujenzi wa barabara ya Dumila - Rudewa (kilomita 45) ilianza Februari, 2010 na ujenzi unaendelea. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka 2013/2014, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 6,000.00 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga *Port* (kilomita 112) – Shilingi Milioni 11,241.37. Mradi huu unalenga kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Sumbawanga – Matai-Kasanga *Port* (kilomita 112) kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na unatekelezwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 8 Oktoba, 2009 na kazi ilianza Januari, 2010. Mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, kiasi cha Shilingi milioni 11,241.37 fedha za ndani kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Madaraja Makubwa (Nangoo, Kirumi, Sibiti, Kilombero Maligisu, Kavuu, Mbutu, Ruhuhu, Ruhekei na Momba na Ununuzi wa *Emergency Bridge Parts*) – Shillingi Milioni 21,500.00. Mradi huu ni wa kujenga/kukarabati madaraja makubwa kwenye barabara kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaraja hayo ni Daraja la Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, Daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi - Ifakara – Mahenge, Daraja la Maligisu (Mwanza) kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi - Maligisu, Daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto-Inyonga, Daraja la Ruhekei katika barabara ya Mbinga-Mbamba *Bay*, Daraja la Kirumi (Mara), Daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, Daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga-Manonga, Daraja la Ruhuhu (Ruvuma) na Daraja la Momba

kwenye barabara ya Sitalike-Kilyamatundu/Kamsamba - Mlowo (Rukwa/Mbeya Border). Aidha, mradi unahusisha kununua Madaraja ya Chuma ya dharura (*Compact Emergency Bridge*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Daraja la Nangoo limetengewa kiasi cha Shilingi milioni 500.00, Daraja la Maligisu Shilingi milioni 200; Daraja la Sibiti Shilingi milioni 3,000.00, Daraja la Kilombero Shilingi milioni 7,500.00, Daraja la Kavuu Shilingi milioni 1,000.00, Daraja la Mbutu Shilingi milioni 5,300.00, Daraja la Ruhekei Shilingi milioni 250.00, Daraja la Momba Shilingi 2,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Shilingi milioni 50.00 zimetengwa kwa ajili ya ununuza wa madaraja ya chuma ya dharura na mtambo wa kukagua madaraja (*Compact Emergency Bridge* na *Under Bridge Inspection Lorry*) na Shilingi milioni 200.00 kwa ajili ya usanifu wa daraja la Ruhuhu. Ukarabati wa daraja la Kirumi umetengewa Shilingi milioni 1,500.00. Fedha zote ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya *New Bagamoyo* (Kawawa Jct - Tegeta kilomita 17) – Shilingi Milioni 20,500.00. Lengo la mradi huu ni kupanua barabara ya kuanzia makutano ya barabara za Kawawa na Ali Hassan Mwinyi eneo la Morocco hadi Tegeta kutoka njia mbili hadi njia nne ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan kuititia Shirika la Maendeleo la JICA. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusisha mradi wa Mwenge – Tegeta (kilomita 12) na awamu ya pili ni mradi wa Kawawa Jnt – Mwenge (kilomita 4.2)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya Shilingi milioni 2,500.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 18,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya

kuendelea na ujenzi, kulipa fidia na kuhamisha miundombinu kwenye eneo la ujenzi (mabomba ya maji, nguzo na nyaya za umeme/simu na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (kilomita 178) – Shilingi Milioni 7,037.53. Lengo la mradi kwa mwaka 2013/14 ni kujenga barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (sehemu ya Kyaka-Bugene) yenyе urefu wa kilometra 59.1 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100. Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 15 Desemba, 2010 na kazi za ujenzi zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 7,037.53 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Isaka – Lusahunga (kilomita 242) na Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza - Kobelo (kilomita 150)- Shilingi Milioni 21,520.48. Lengo la mradi ni kufanya ukarabati wa sehemu ya Isaka – Lusahunga (kilomita 242) kwa kiwango cha lami kwa fedha za Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili za Isaka – Ushirombo (kilomita 132) na Ushirombo – Lusahunga (kilomita 110). Mikataba ya ujenzi wa sehemu hizi ilisainiwa tarehe 18 Agosti, 2009. Kazi ya ujenzi kwa sehemu zote mbili inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, barabara hii imetengewa fedha za ndani Shilingi milioni 12,512.72 kwa sehemu ya Isaka – Ushirombo na Shilingi milioni 9,007.76 kwa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga kwa ajili ya kuendelea na ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (kilomita 264) – Shilingi Milioni 22,499.57. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora kwa kuanzia na sehemu ya Manyoni – Chaya (kilomita 89.35) na sehemu ya Tabora – Nyahua

(kilomita 85) kwa kutumia fedha za ndani. Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 na kazi ya ujenzi inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2013/2014 kwa sehemu zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 10,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Tabora – Nyahua na Shilingi milioni 10,299.57 kwa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya. Kwa barabara ya Nyahua - Chaya (kilomita 90) kiasi cha Shilingi milioni 2,200.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Korogwe – Handeni (kilomita 65) – Shilingi Milioni 6,356.73. Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Korogwe – Handeni (kilomita 65). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi zinaendelea. Kwa mwaka 2013/2014 barabara hii imetengewa Shilingi milioni 6,356.73 kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mikoa Shilingi Milioni 31,915.27. Lengo la mradi huu ni kuzifanyia ukarabati barabara za Mikoa kwa kiwango cha changarawe, kujenga kwa kiwango cha lami na kujenga madaraja katika mikoa ya Tanzania Bara. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya kilometra 515.6 kwa kiwango cha changarawe na kujenga kilometra 35.5 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za ukarabati kwa kiwango cha changarawe zitafanyika katika Mikoa yote. Aidha, ujenzi wa madaraja 17 utafanyika katika Mikoa ya Katavi (1), Morogoro (1), Mbeya (3), Manyara (1), Ruvuma (2), Simiyu (4), Lindi (1), Mtwara (1), Geita (1) na Rukwa (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mwanza/Shinyanga *Border*–Mwanza (kilomita 10) Shilingi Milioni 50.00. Lengo la mradi huu ni kuendelea na ukarabati wa sehemu

zilizoharibika katika barabara ya Mwanza/Shinyanga Border - Mwanza kwa mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 50.00 za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Handeni – Mkata (kilomita 54) – Shilingi Milioni 4,484.75. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Handeni – Mkata (kilomita 54). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 28 Desemba, 2010 na umekamilika Novemba, 2012. Barabara hii imetengewa Shilingi milioni 4,484.75 kwa ajili ya kulipia sehemu ya madai ya mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mwandiga – Manyovu (kilomita 60) – Shilingi Milioni 1,234.35. Ujenzi wa barabara ya kutoka Mwandiga hadi Manyovu inayounganisha Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi kwa kiwango cha lami ulikamilika Oktoba 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka 2013/2014, barabara hii imetengewa Shilingi milioni 1,234.35 kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kupunguza msongamano ya magari katika barabara za Dar es Salaam – Shilingi Milioni 28,634.00. Ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ulianza katika mwaka wa fedha 2009/2010. Barabara hizo ni Ubungo *Bus Terminal* – Kigogo-Kawawa *Roundabout* (kilomita 6.4), Kawawa *Roundabout-Msimbazi Valley* – Jangwani/Twiga *Junction* (kilomita 2.7), Jet Corner – Vituka-Davis Corner (kilomita 10.3) na ujenzi wa mfereji wa Bungoni unaoanzia barabara ya Nyerere hadi Uhuru (Bungoni). Aidha, mradi wa mabasi yaendayo kasi (*Bus Rapid Transit Infrastructure*) na vituo vyake unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, kiasi cha Shilingi milioni 1,689.00 kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobakia kwa barabara ya Ubungo

Bus Terminal - Kigogo - Kawawa Roundabout, Shilingi milioni 605.00 kwa barabara ya Kawawa Roundabout - Msimbazi Valley - Jangwani/Twiga Junction na Shilingi milioni 1,290.00 kwa ajili ya barabara ya Jet Corner - Vituka - Devi's Corner.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha Shilingi milioni 3,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Ubungo Maziwa - External na Tabata Dampo - Kigogo, Shilingi milioni 5,000.00 kwa barabara ya Kimara - Kilungule - External, Shilingi milioni 6,000.00 kwa barabara ya Mbezi (Morogoro road) - Malambbamawili - Kinyerezi - Banana, Shilingi milioni 5,000.00 kwa barabara ya Tegeta - Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi/ Morogoro road, Shilingi milioni 3,000.00 kwa barabara ya Tangi Bovu - Goba, Shilingi milioni 1,500.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa barabara ya Kimara - Baruti - Msewe - Changanyikeni na Shilingi milioni 1,500.00 kwa barabara ya Kibamba - Kisopwa sehemu ya Kibamba - Mlonganzila (kilomita nne). Shilingi milioni 50.00 zitatumika kufuatilia na kusimamia Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Fly Over ya TAZARA na Shilingi milioni 3,000.00 zimetengwa kwa ajili ya maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Ubungo, Magomeni, Mwenge, Tabata/ Mandela na Morocco kwa kutumia mfumo wa Usanifu na Kujenga (*Design and Build*). Aidha, Shilingi milioni 1,000.00 zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Bendera Tatu - Gerezani (KAMATA) katika barabara ya Dar es Salaam- Mbagala (Kilwa road).

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwa viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, wasaidie kuondoa nyumba zilizojengwa kwenye hifadhi ya barabara ili miradi nilioitaja isije ikakwama kwa sababu ya watu waliojenga kwenye hifadhi ya barabara kwa kuvunja Sheria Na. 13 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ndundu – Somanga (kilomita 60) - Shilingi Milioni 5,287.74. Mradi huu unalenga kujenga barabara sehemu ya Ndundu hadi Somanga (kilomita 60) kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi zinaendelea. Barabara hii imetengewa Shilingi milioni 5,287.74 fedha za ndani katika mwaka 2013/2014, kwa ajili ya kukamilisha kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kidatu - Ifakara - Lupilo - Malinyi - Londo - Lumecha/Songea (kilomita 396) - Shilingi Milioni 1,600.00. Lengo la mradi huu ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kidatu hadi Lumecha/Songea chini ya msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na mchango wa Serikali ya Tanzania. Barabara hii imetengewa Shilingi milioni 100.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 1,500.00 fedha za nje kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Tabora - Ipole - Koga – Mpanda (kilomita 359) - Shilingi Milioni 2,000.00. Mkataba wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulisainiwa tarehe 8 Juni, 2009 na kazi zimekamilika. Lengo la mradi ni utayarishaji wa nyaraka za zabuni za ujenzi wa barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Makutano - Natta – Mugumu/ Loliondo – Mto wa Mbu (kilomita 452) – Shilingi Milioni 8,617.63. Lengo la mradi ni kufanya usanifu wa kina na kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa sehemu ya Natta - Mugumu (kilomita 50) na Mto wa Mbu – Loliondo (kilomita 213) ilisainiwa tarehe 26 Agosti, 2009. Kazi ya usanifu wa kina imekamilika mwaka 2011. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya

Shilingi milioni 5,617.63 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano -Sanzate (kilomita 50) na Shilingi milioni 3,000.00 kwa sehemu ya Mto wa Mbu – Loliondo (kilomita 213).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ibanda – Itungi/Kiwira Port (kilomita 26) – Shilingi Milioni 1,000.00. Lengo la mradi ni kufanya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni kiungo muhimu kwa bandari ya Itungi/Kiwira. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu umetengewa Shilingi milioni 1,000.00 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ukarabati ili kuiunganisha bandari mpya ya Kiwira.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nzega – Tabora (kilomita 115) – Shilingi Milioni 13,392.09. Mradi unalenga kujenga barabara ya Nzega – Tabora (kilomita 115) kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili za Nzega-Puge (kilomita 58.8) na Puge-Tabora (kilomita 56.10). Kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami inaendelea kwa sehemu ya Nzega – Puge na sehemu ya Puge-Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 6,696.05 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Nzega – Puge na Shilingi milioni 6,696.04 kwa sehemu ya Puge – Tabora .

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Sumbawanga – Mpanda - Nyakanazi (kilomita 829) – Shilingi Milioni 38,858.72. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Kasulu – Nyakanazi kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Sumbawanga-Kanazi (kilomita 75) na Kanazi-Kizi-Kibaoni (kilomita 75.6) zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 8,850.94 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa sehemu ya Sumbawanga-Kanazi, Shilingi milioni 8,850.94 kwa

sehemu ya Kanazi-Kizi-Kibaoni na Shilingi milioni 6,617.63 kwa sehemu ya Kizi-Sitalike-Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha Shilingi milioni 4,539.21 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mpanda-Mishamo (kilomita 100). Sehemu ya Kigoma – Nyakanazi imetengewa Shilingi milioni 10,000.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilomita 100 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nyanguge – Musoma (kilomita 183) na Mchepuo wa Usagara - Kisesa (kilomitam 17) – Shilingi Milioni 18,235.26. Lengo la mradi ni kuikarabati barabara ya Nyanguge-Musoma (kilomita 183) na kujenga kwa kiwango cha lami kilomita 17 za mchepuo wa Usagara - Kisesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa sehemu ya Simiyu/Mara Border – Musoma (kilomita 85.5) unaendelea. Maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Nansio - Kisorya - Bunda sehemu ya Kisorya - Bunda (kilomita 50) yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu umetengewa Shilingi milioni 9,735.26 kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ukarabati wa barabara ya Nyanguge - Musoma. Kiasi cha Shilingi milioni 4,000.00 kimetengwa kwa sehemu ya barabara ya Kisesa – Usagara Bypass kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kiasi cha Shilingi milioni 4,500.00 kimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nansio - Kisorya - Bunda sehemu ya Kisorya - Bunda (kilomita 50).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Magole - Mziha (Magole-Turiani kilomita 48.8) – Shilingi Millioni 6,266.84. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Magole – Mziha kwa kiwango cha lami. Jumla ya Shilingi milioni 6,266.84 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Magole - Turiani katika bajeti ya 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (kilomita 171) – Shilingi Milioni 11,965.65. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Mwigumbi- Maswa-Bariadi-Lamadi yenyenye jumla ya kilometra 171 kwa kiwango cha lami. Kazi zilianza tarehe 8 Julai, 2010 kwa sehemu ya Bariadi - Lamadi na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi (kilomita 100) yanaendelea. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, kiasi cha Shilingi milioni 6,465.65 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa barabara ya Bariadi - Lamadi. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 5,500.00 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi (kilomita 100).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Tabora - Ipole-Rungwa (Ipole-Rungwa – kilomita 95) – Shilingi Milioni 500.00. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Tabora - Ipole - Rungwa kwa kiwango cha lami kwa kuanza na sehemu ya Ipole - Rungwa yenyenye urefu wa kilomita 95. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na umetengewa Shilingi milioni 500.00 mwaka 2013/2014, kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia (*Mafia Airport Access Road* - kilomita 14) – Shilingi Milioni 2,471.17. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na Shirika la Misaada la Marekani (*MCC*) ni kwamba Serikali itajenga barabara hii na *MCC* itatoa fedha za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mafia. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 2,471.17 zimetengwa kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma (*Dodoma University Road* - kilomita 12) –

Shilingi Milioni 3,000.00. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Chuo Kikuu Dodoma kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Jumla ya Shilingi milioni 3,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Kigamboni – Shilingi Milioni 3,000.00. Lengo la mradi ni kujenga daraja litakalounganisha Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Kigamboni. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 3,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi. Mradi unajengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na NSSF.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Sam Nujoma (kilomita 4) – Shilingi Milioni 21.51. Lengo la mradi lilikuwa ni kupanua barabara ya Sam Nujoma kutoka njia mbili kuwa njia nne pamoja na njia za waenda kwa miguu kuanzia Mwenge hadi Ubungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu umegharamiwa na Serikali ya Tanzania na kazi za ujenzi wa barabara zilikamilika Julai, 2009. Shilingi milioni 21.51 fedha za ndani zimetengwa katika mwaka 2013/2014, kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Tunduma - Sumbawanga (kilomita 223) – Shilingi Milioni 57.88. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Tunduma – Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 223 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Marekani kuititia *Millennium Challenge Corporation (MCC)* na mchango wa Serikali ya Tanzania. Utekelezaji wa mradi umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni:-Tunduma – Ikana (kilomita 63.7); Ikana – Laela (kilomita 64.0) na Laela – Sumbawanga (kilomita 95.3).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 17.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuhamisha miundombinu katika eneo

la ujenzi na usimamizi kwa sehemu ya Tunduma – Ikana, Shilingi milioni 17.0 zimetengwa kwa sehemu ya Ikana-Laela na Shilingi milioni 23.88 kwa sehemu ya Laela – Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kagoma – Lusahunga (kilomita 154) – Shilingi Milioni 14,477.25. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Mutukula – Bukoba – Bihamarulo – Lusahunga (kilomita 294) iliyofanyiwa usanifu mwaka 1996 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Ujenzi wa sehemu ya barabara ya Mutukula – Muhutwe – Kagoma ulianza Machi, 2001 na ulikamilika Septemba 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali Benki ya Maendeleo ya Afrika ilitoa mkopo kwa ajili ujenzi wa sehemu ya Kagoma – Lusahunga (kilomita 154) kwa kiwango cha lami. Baada ya Mkandarasi *China State Construction Engineering Corporation Limited (CSCEC)* wa China kushindwa kutekeleza mkataba wa awali na kuondolewa, mkataba mpya wa kumalizia ujenzi wa barabara ya Kagoma – Lusahunga (kilomita 154) kwa kiwango cha lami ulisainiwa kwa fedha za Serikali ya Tanzania. Katika mwaka 2013/2014 barabara hii imetengewa Shilingi milioni 14,477.25 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Arusha – Namanga (kilomita 105) - Shilingi Milioni 3,517.12. Mradi wa Arusha – Namanga (kilomita 105) ni sehemu ya mradi wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaojumuisha nchi za Tanzania na Kenya. Kwa sehemu ya Tanzania, mradi unafadhiliwa na *Japan Bank for International Cooperation (JBIC)* kwa kushirikiana na Serikali za Tanzania. Kazi za ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami zimekamilika Desemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 1,228.12 fedha za ndani na Shilingi milioni 2,289.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Singida -

Babati – Minjingu - Arusha (kilomita 321) - Shilingi Milioni 26,396.39. Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Singida - Babati -Minjingu yenyе urefu wa kilomita 223 na kukarabati kwa kiwango cha lami sehemu ya Minjingu-Arusha yenyе urefu wa kilomita 98.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Singida - Babati - Minjingu umegawanywa katika sehemu tatu za Singida – Katesh (kilomita 65.1), Katesh – Dareda (kilomita 73.8) na Dareda – Babati – Minjingu (kilomita 84.6). Kazi za ujenzi zilianza tarehe 11 Machi, 2009 na zimekamilika Agosti, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hii inagharamiwa na ADB, JICA na Serikali ya Tanzania. Mkataba wa ukarabati wa sehemu ya Minjingu-Arusha umesainiwa tarehe 12 Mei, 2011 na kazi zinaendelea. Sehemu hii inakarabatiwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, kiasi cha Shilingi milioni 240.56 zimetengwa kwa sehemu ya Singida – Katesh, Shilingi milioni 336.00 kwa ajili ya sehemu ya Katesh – Dareda na Shilingi milioni 375.00 kwa ajili ya sehemu ya Dareda – Babati – Minjingu ili kukamillisha malipo ya Makandarasi wa sehemu zote tatu. Kiasi cha Shilingi milioni 444.83 fedha za ndani na Shilingi milioni 25,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara ya Minjingu hadi Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Msimba – Ruaha/Ikokoto - Mafinga (kilomita 219) – Shilingi Milioni 25,716.53. Lengo la mradi ni kufanya ukarabati wa barabara ya lami ya Dar es Salaam – Tunduma (*TANZAM*). Mradi huu unahusisha ukarabati wa sehemu ya Iyovi - Kitonga Gorge (kilomita 86.3), Ikokoto - Iringa (kilomita 60.9), barabara ya mchepuo kuingia Iringa mjini (kilomita 2.1) na Iringa-Mafinga (kilomita 68.9).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu unagharamiwa kwa mkopo kutoka Serikali ya Denmark pamoja na mchango

wa Serikali ya Tanzania. Aidha, maandalizi ya ukarabati kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mafinga - Igawa (kilomita 146) yanaendelea kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 5,516.53 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa kilomita 68.9 za Iringa - Mafinga. Aidha, jumla ya Shilingi milioni 200.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 20,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Mafinga-Igawa yenye urefu wa kilometra 146.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Korogwe - Mkumbara - Same (kilomita 172)- Shilingi Milioni 53,621.38. Mradi wa ukarabati wa barabara ya Korogwe - Mkumbara - Same (kilomita 172) ambayo ni sehemu ya barabara ya Segera - Moshi - Arusha unagharamiwa na Benki ya Dunia pamoja na Serikali ya Tanzania. Katika mwaka 2013/2014, kazi ya ukarabati wa barabara hii zitaendelea kama ifuatavyo:-

(i) Korogwe – Mkumbara (kilomita 76), Katika mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 100.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 32,671.38 fedha za nje zimetengwa kwa ajili kuendelea na kazi ya ukarabati wa sehemu hii ya barabara.

(ii) Mkumbara – Same (kilomita 96), katika mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 100.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 20,750.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili kuendelea na kazi ya ukarabati wa sehemu hii ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mbeya-Makongolosi (kilomita 115) – Shilingi Milioni 15,691.68. Lengo la mradi ni kujenga barabara ya Mbeya hadi Makongolosi (kilomita 115) kuititia Chunya kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Mbeya – Lwanjilo (kilomita 36); Lwanjilo-Chunya (kilomita 36) na Chunya-Makongolosi (kilomita 43).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014,

barabara hii imetengewa jumla ya Shilingi milioni 6,528.78 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mbeya-Lwanjilo; Shilingi milioni 5,008.00 kwa sehemu ya Lwanjilo-Chunya na Shilingi milioni 3,847.05 kwa sehemu ya Chunya – Makongolosi. Aidha, Shilingi milioni 307.84 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati sehemu ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Chalinze – Segera - Tanga (kilomita 248) – Shilingi Milioni 7,700.00. Lengo la mradi ni kuifanyia ukarabati na upanuzi barabara ya Chalinze - Segera hadi Tanga. Utekelezaji wa mradi umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni: Chalinze-Kitumbi (kilomita 125) na Kitumbi-Segera-Tanga (kilomita 120). Jumla ya Shilingi milioni 3,200.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 4,500.00 fedha za nje zimetengwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Kitumbi-Segera-Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Dodoma – Iringa (kilomita 260) – Shilingi Milioni 86,539.31. Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa (kilomita 260). Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea na ujenzi, katika mwaka wa fedha 2013/2014, kiasi cha Shilingi milioni 615.68 fedha za ndani na Shilingi milioni 30,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa sehemu ya Iringa – Migori (kilomita 95.1), Shilingi milioni 538.72, fedha za ndani na Shilingi milioni 28,000.00 fedha za nje kwa ajili ya sehemu ya Migori – Fufu Escarpment (kilomita 93.8) na Shilingi milioni 584.90 fedha za ndani na Shilingi milioni 26,800.00 fedha za nje kwa ajili ya sehemu ya Fufu Escarpment – Dodoma (kilomita 70.9).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Dodoma – Babati (kilomita 261) – Shilingi Milioni 56,992.41. Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati (kilomita 261). Utekelezaji wa mradi huu

umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni:-

- (a) Dodoma-Mayamaya (kilomita43.65);
- (b) Mayamaya-Bonga (kilomita198.15); na
- (c) Bonga-Babati (kilomita 19.2).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, kiasi cha Shilingi milioni 6,606.15 zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Dodoma – Mayamaya na Shilingi milioni 2,386.26 kwa sehemu ya Bonga – Babati. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mayamaya – Bonga ambayo imegawanywa katika sehemu mbili utaanza katika mwaka 2013/14 kama ifuatavyo:-

- (i) Mayamaya - Mela (kilomita 99.35); katika mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 500.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 25,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa sehemu hii ya barabara.
- (ii) *Mela - Bonga* (kilomita 98.8); katika mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 500.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 22,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa sehemu hii ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Masasi-Songea – Mbamba Bay (kilomita 659.7) – Shilingi Milioni 136,327.08. Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Masasi- Songea – Mbamba Bay (kilomita 649). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Shilingi milioni 533.88, fedha za ndani na Shilingi milioni 24,000.00, fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mangaka-Nakapanya na Shilingi milioni 532.57, fedha za ndani na Shilingi milioni 23,200.00, fedha za nje kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Nakapanya – Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shilingi milioni 532.93, fedha za ndani na Shilingi milioni 24,000.00, fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mangaka-

Mtambaswala na Shilingi milioni 3,567.32, fedha za ndani na Shilingi milioni 16,809.00, fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Tunduru-Matemanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu ya Matemanga-Kilimasera, Shilingi milioni 3,679.20, fedha za ndani na Shilingi milioni 14,944.00, fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. Aidha, Shilingi milioni 3,679.19, fedha za ndani na Shilingi milioni 13,715.00, fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Kilimasera – Namtumbo. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya fidia ni Shilingi milioni 17.00, fedha za ndani kwa barabara ya Songea – Namtumbo na Shilingi milioni 17.00, fedha za ndani kwa barabara ya Peramiho – Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Shilingi milioni 4,600.00, fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mbinga-Mbamba Bay na Shilingi milioni 2,500.00, fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Masasi - Newala – Mtwara (kilomita 209).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Barabara ya Uongozi *Institute*, Shilingi Milioni 1,500.00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye Chuo cha Uongozi pamoja na barabara zilizoko ndani ya chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 1,500.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia Chuo cha Uongozi pamoja na barabara zilizoko ndani ya Chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara – Shilingi Milioni 1,100.00. Lengo la mradi huu ni kujenga Makao Makuu ya Wakala wa Barabara pamoja na kuanza ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe na Lindi. Mradi huu

unagharamiwa kwa fedha za ndani. Usanifu wa jengo la Makao Makuu ya Wakala umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya Shilingi milioni 1,100.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama barabaran na mazingira. Usalama Barabarani - Shilingi Milioni 3,387.00; mradi huu una lengo la kuimarisha shughuli za kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara. Katika mwaka wa fedha 2013/14, kiasi cha Shilingi milioni 887 fedha za ndani na Shilingi milioni 2,500 fedha za nje zimetengwa. Kazi zitakazofanyaika ni zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa mizani ya kisasa inayopima uzito wa gari likiwa katika mwendo (*Weigh in Motion*) katika eneo la Vigwaza ambaao umetengewa Shilingi milioni 224 fedha ya ndani.

(ii) Uanzishwaji wa Wakala wa Usalama Barabarani nchini (*National Road Safety Agency*) ambaao umetengewa Shilingi milioni 293 fedha ya ndani na Shilingi 1000 fedha ya nje.

(iii) Utafiti na tathmini wa ajali za barabaran ambaao umetengewa Shilingi milioni 230 fedha ya ndani.

(iv) Ukaguzi wa hali ya usalama katika barabara (*Road Safety Audit*) Shilingi milioni 129 fedha ya ndani.

(v) Uwekaji Mfumo wa Taarifa za Ajali Barabarani (*Road Accident Information System*) ambaao umetengewa Shilingi milioni 11 fedha ya ndani na Shilingi milioni 1500 fedha ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usalama Barabarani na Mazingira - Shilingi Milioni 891.98; Mradi huu una lengo la kugharamia shughuli za Usalama na Mazingira pamoja na Marekebisho ya Mfumo wa utekelezaji wa shughuli katika maeneo haya. Mradi huu unagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na DANIDA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014 mradi huu umetengewa jumla Shilingi milioni 891.98. Kati ya fedha hizo Shilingi milioni 641.98 ni fedha za ndani na Shilingi milioni 250 fedha za nje. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 255 za ndani na Shilingi milioni 100 za nje zimetengwa kwa ajili ya kutoa Elimu ya Usalama Barabarani kwa shule za Nyanda za Juu Kusini Katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Katavi na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha Shilingi milioni 349.98 za ndani na Shilingi milioni 150 za nje zimetengwa kwa ajili ya kutoa Elimu ya Usalama Barabarani kwa umma kupitia vyombo vya habari, vipeperushi na kadhalika (*Road Safety Awareness Campaign*). Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 37 za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Menejimenti na Utunzaji wa Mazingira - Shilingi Milioni 200.00. Mradi huu una lengo la kuelimisha na kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika sekta ya Ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2013/14 kiasi cha Shilingi milioni 200.00, fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 kwa miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lingine ni kutoa mafunzo kuhusu tathmini na usimamizi wa mazingira katika sekta ya ujenzi kwa Wataalam wa *TANROADS*, *TEMESA*, *TBA*, Vikosi vya Ujenzi na wadau mbalimbali katika sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kujenga Uwezo (*Institutional Support*) - Shilingi Milioni 500.131; mradi huu unalenga kujenga uwezo (*capacity building*) wa wataalam wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, mradi huu umetengewa Shilingi milioni 200.131 fedha za ndani na Shilingi milioni 300.00 fedha za nje. Fedha hizo zitatumika kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani zao, pamoja na kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2013/2014, Mfuko wa Barabara unatarajiwa kukusanya jumla ya Sh. 504,306,000,000.00 ikilinganishshwa na Sh. 429,664,000,000.00 katika mwaka 2012/2013. Hii ni ongezeko la Sh. 74,642,000,000.00 sawa na asilimia 17.37.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, fedha hizi ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara na zinagawanywa kwa Wizara ya Ujenzi na TAMISEMI kwa kuzingatia Sheria ya Tozo za barabara ya mwaka 1998 kama ilivyorekebishwa mwaka 2006. Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi na Taasisi zake imetengewa Sh. 353,049,400,000.00 ikilinganishwa na Sh. 300,764,800,000.00 za mwaka 2012/13.

Katika fedha zilizotengwa chini ya Wizara ya Ujenzi, TANROADS imetengewa Sh. 314,535,652,200.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi imetengewa Sh. 34,948,405,800.00 kwa ajili ya kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara pamoja na ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara imetengewa Sh. 3,565,342,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 934,245,067.00 ni kwa ajili ya mishahara, Sh. 2,631,096,933.00 ni kwa ajili ya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya Barabara Kuu na za Mikoa katika Mikoa yote pamoja na barabara za Halmashauri za Wilaya. Aidha, fedha hizo pia zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Bodi ya Mfuko wa Barabara Dodoma na kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Wizara ya Ujenzi zitatumika kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

(i) Miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara Kuu ambayo imetengewa Sh. 9,126,610,000.00.

(ii) Miradi ya vivuko imetengewa Sh. 3,163,730,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 906,270,000.00 ni kwa ajili ya ununuzi

wa Kivuko cha Itungi Port na Sh. 787,950,000.00 ni kwa ajili ya ununuzi wa Kivuko cha Kahunda - Maisome. Ununuzi wa boti ya uokoaji (*Rescue boat*) kwa vivuko vya Ukerewe (Rugezi - Kisorya and Buolora-Ukara) umetengewa Sh. 469,510,000.00. Sh. 900,000,000.00 zimetengewa kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya vivuko na Sh. 100,000,000.00 ni kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi.

(iv) Sh. 1,325,370,000.00 zimetengewa kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya barabara, maandalizi ya Kanuni za Sheria ya Barabara, maandalizi na uchapishaji wa taarifa za kagazi za miradi ya barabara, uendelezaji wa teknolojia za ujenzi wa barabara, utoaji elimu kwa umma na kushiriki katika shughuli za Kikanda (*SADC, EAC, COMESA, Central Corridor* na kadhalika).

(v) Usalama Barabarani na Mazingira umetengewa Sh. 1,140,000,000.00.

(vi) Barabara za Mikoa zimetengewa jumla ya Sh. 20,192,695,800.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Matengenezo ya Barabara kwa Mwaka 2013/2014; Mpango wa matengenezo ya Barabara Kuu na Barabara za Mikoa kwa mwaka 2013/2014, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni jumla ya Sh. 314,535,652,200.00 Muhtasari wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Barabara Kuu: Kilomita 11,276.87 na madaraja 1,272 kwa Sh. 101,315,714,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara.

(ii) Barabara za Mikoa: Kilomita 24,489.09 na madaraja 1,305 kwa Sh. 162,103,560,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara.

(iii) Matengenezo ya Dharura na Tahadhari: Kiasi cha Sh. 6,871,541,200.00 zimetengewa kwa kazi hizi kutoka Mfuko wa Barabara.

(iv) Mradi wa Majaribio wa Kufanya Matengezo ya Muda Mrefu (*PMMR*): Kilomita 273 kwa sh. 2,324,837,000.00

(v) Matengenezo, Ukarabati na Ujenzi wa Mizani. Kiasi cha Sh. 3,500,000,000.00 kimetengwa kwa kazi hizi.

(vi) Kazi/Shughuli Zinazohusiana na Matengenezo zinazofanywa kutokea Makao Makuu: Kiasi cha Sh. 4,470,000,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara zimetengwa kwa ajili ya kuweka alama za barabarani na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Barabara ikiwa ni pamoja na kuweka alama za kuonyesha mipaka ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha hizo pia zitatumika kuandaa na kusimamia programu za matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa; kukusanya na kuweka takwimu za barabara na matumizi yake; kufanya kaguzi za hali na uimara wa madaraja; kufuatilia masuala ya usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kubaini maeneo hatarishi (*Black Spots*) na kuandaa hatua za kuchukua.

(vii) Usimamizi wa Kazi na Utawala. Kiasi cha Sh. 24,150,000,000.00 kimetengwa kwa kazi hizi.

(viii) Gharama za Uendeshaji wa Mizani (*Operational Costs*): Kiasi cha Sh. 9,800,000,000.00 kimetengwa kwa kazi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa kwa mwaka 2013/2014, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kama ifuatavyo:-

(1) Matengenezo ya Kawaida (*Routine Maintenance*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara mwaka 2013/2014 – Barabara Kuu: jumla ya shilingi milioni 24,291.040.

(2) Matengenezo Kawaida (*Routine Maintenance*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara mwaka 2013/2014 – Babaraba za Mikoa: jumla ya shilingi milioni 33,527.835.

(3) Matengenezo Maalum (*Periodic Maintenance*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara mwaka 2013/2014 – Barabara Kuu: jumla ya shilingi milioni 64,619.335.

(4) Matengenezo Maalum (*Periodic Maintenance*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara mwaka 2013/2014 – Barabara za Mikoa: jumla ya shilingi milioni 90,002.156.

(5) Matengenezo ya sehemu Korofi (*Sport Improvement*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara mwaka 2013/2014 – Barabara Kuu lami na Changarawe: jumla ya shilingi milioni 1,348.720.

(6) Matengenezo ya sehemu Korofi (*Sport Improvement*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2013/2014 – Barabara za Mikoa lami na changarawe: jumla ya shilingi milioni 16,279.01.

(7) Matengenezo ya Kukinga Madaraja (*Bridges Preventive Maintenance*) kwa Barabara Kuu na Barabara za Mikoa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara mwaka 2013/2014: jumla ya shilingi milioni 3,157.162.

(8) Matengenezo Makubwa ya Madaraja na Makalvati kwa Barabara Kuu na Barabara za Mikoa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara mwaka 2013/2014: jumla ya shilingi milioni 26,388.776.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Maalum wa Kitaifa wa Kuinua Matumizi ya Teknolojia ya Nguvu Kazi; katika mwaka 2013/2014, Chuo cha Matumizi Stahiki ya Nguvu Kazi (*Appropriate Technology Training Institute -ATT*) kitaendelea kutoa mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini kwa wananchi wapatao 2,500 ili kuwa na miundombinu bora na inayopitika kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mafunzo yatatolewa kwa wahandisi 44 kutoa ndani na nje ya nchi; Makandarasi 100, Wahandisi washauri 10 na Viongozi wa Vikundi 200, ili waweze kutoa huduma bora katika ujenzi, ukarabati na

matengenezo ya barabara kwa kutumia taaluma na ujuzi wa teknolojia ya nguvu kazi (*LB7*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za barabara nchini; katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake kushiriki katika kazi za barabara kwa kuendesha mafunzo ya ukandarasi kwa makandarasi wanawake na vikundi vya wanawake 25 kwa kutumia teknolojia ya Nguvu Kazi. Wizara itafanya ufuatiliaji wa maendeleo ya wanawake waliopatiwa mafunzo ya ushiriki katika kazi za barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake wengi zaidi kushiriki katika kazi za barabara kama Makandarasi na wafanyakazi katika ngazi mbalimbali za kazi za barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Watumishi; katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara itaendelea kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka katika mafunzo ya ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo yatakuwa ni ya muda mrefu na muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kuajiri watumishi wapya kukidhi mahitaji yake, kuwathibitisha kazini watumishi wanaostahili, Wizara itawapandisha vyeo watumishi wake kwa kadiri ya Ikama itakayotolewa na kutimizwa kwa sifa na masharti ya kupata vyeo kwa mujibu wa kada husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Kupambana na UKIMWI. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara itaendelea kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na VVU kwa watumishi pamoja na kuepuka kusambaza ugonjwa huo kwa kutumia vipeperushi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*), Wizara itaandaa semina

na mafunzo kwa watumishi na wataendelea kuhamasishwa kupima afya zao pamoja na kuwapatia huduma ya lishe bora kwa watakaothibitika kuathirika na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita dhidi ya rushwa; Wizara katika mwaka wa fedha 2013/2014 itaendelea kuwaelimisha watumishi athari za kutoa na kupokea rushwa pamoja na kuwahimiza kupambana na rushwa katika mazingira yote ya kazi. Elimu kuhusu mapambano dhidi ya rushwa itatolewa kuititia vipeperushi, semina na mikutano mbalimbali kwa ushirikiano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Mheshimiwa Naibu Spika, Habari, Elimu na Mawasiliano; katika mwaka 2013/14, Wizara itaendeleza mawasiliano na wadau wote ili kuboresha utoaji wa elimu na taarifa kwa umma. Wizara itaendelea kutoa taarifa za shughuli zinazotekelizwa na Wizara kuititia vipindi vya televisheni, redio, Tovuti (www.mow.go.tz) pamoja na machapisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuvipongeza vyombo mbalimbali vya habari, kwa ushirikiano wao na jinsi ambavyo vimikuwa vikifuatilia na kutoa taarifa za shughuli zinazohusu Sekta ya Ujenzi. Ushirikiano huu utaendelea kudumishwa ili kuhakikisha kuwa umma unapata taarifa za kutosha zinazohusiana na malengo, sera, sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa utekelezaji kazi katika Wakala / Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014. Wakala wa Barabara; katika mwaka 2013/2014, Wakala utaendelea kusimamia kazi za kukarabati, kujenga na kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa zenye urefu wa kilomita 35,000.

Matengenezo ya barabara kuu na mikoa yatahusisha matengenezo ya kawaida (*routine maintenance*) kilomita 30,656, matengenezo ya muda maalum na korofi kilomita 5,109.90 na madaraja 2,577. Mpango huu pia utajumuisha

shughuli za utawala na usimamizi wa kazi, udhibiti wa uzito wa magari, kazi za dharura, mradi wa matengenezo ya muda mrefu na kazi zinazosimamiwa toka makao makuu kuhusu mipango, usalama barabarani na hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala pia utaendelea kusimamia miradi ya ujenzi wa barabara kilomita 495 kwa kiwango cha lami, ukarabati wa kilometra 190 kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja 11 katika barabara kuu. Kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala umepanga kukarabati kilomita 867.60 kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilomita 66.1 kwa kiwango cha lami na kujenga/kukarabati madaraja 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala umeandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi 107. Kati ya watumishi hawa, 12 watahudhuria mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi, 20 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu (Shahada za Uzamili) na 75 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbalimbali ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Majengo ya Serikali. Katika mwaka 2013/2014, Wakala umepanga kutekeleza majukumu yake mbalimbali ikiwemo kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea, kununua viwanja zaidi mikoani ili kuuwezesha Wakala kujenga nyumba nyingi zaidi za Watumishi Mikoani, kufanya matengenezo ya nyumba za Serikali na kununua samani kwa nyumba za Viongozi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala utaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalam kwa miradi ya ujenzi wa nyumba za Watumishi na ofisi za Serikali kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ufundii na Umeme. Katika mwaka 2013/14, Wakala umepanga kuendelea na ununuzi wa Vivuko vya Kahunda – Maisome (Geita) na Itungi Port (Kyela – Mbeya); ununuzi wa boti ya uokoaji (rescue boat) na ununuzi wa kivuko cha Dar es

Salaam – Bagamoyo; ukarabati wa vivuko vya MV. Magogoni, MV. Geita, MV. Kome I na MV. Kilombero I; na ujenzi wa maegesho ya vivuko katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wakala utaendelea kukarabati karakana za Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma na kuzipatia vitendea kazi vya kisasa pamoja na kutengeneza magari ya Serikali katika karakana zote kila mkoa. Wakala pia utaendelea kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali pamoja na kukodisha mitambo mbalimbali na magari maalum ya viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mfuko ya Barabara; katika mwaka 2013/2014, Bodi ya Mfuko wa Barabara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, *TANROADS, EWURA* na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kufuatilia na kuweka mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato kwenye vyanzo vya mapato ya Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Bodi itaandaa mapendekezo ya kuboresha vipengele katika sheria iliyoanzisha Bodi ili kuboresha ufanisi wa utendaji wa Taasisi za barabara (*Road Authorities*) na Watendaji wanaosimamia matumizi ya fedha za Mfuko. Bodi itakamilisha uandaaji wa Taratibu za Sheria ya Mfuko wa Barabara (*regulations*) na miongozo mbalimbali ili kuboresha usimamizi wa Fedha za Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi itaimarisha ufuutiliaji wa matumizi ya fedha za Mfuko kwa kutumia wataalam washauri na wataalam wa ndani katika kufanya ukaguzi wa kiufundi wa ubora wa kazi (*value for Money*) kwenye mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi; katika mwaka 2013/14, Bodi ya Usajili wa Wahandisi imepanga kusajili Wahandisi 800, Mafundi Sanifu 200 na

kampuni za ushauri wa kihandisi 25. Aidha, Bodi itasimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitim 1,000. Idadi hii ni pamoja na wahandisi wahitim 651 wanaoendelea na mafunzo kwa fedha za Serikali na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi pia itafanya ukaguzi wa shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Bodi itatembelea na kukagua miradi ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na barabara za Halmashauri ili kutathmini hali ya uhandisi katika Halmashauri zote Tanzania bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuhakiki kama kazi zote za kihandisi zinafanywa na wahandisi wenyе sifa na waliosajiliwa na Bodi. Hii ni pamoja na kupata idadi kamili ya wahandisi walioko katika shughuli za kihandisi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi; katika mwaka 2013/2014, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi inatarajia kusajili Wabunifu Majengo (362), Wakadiriaji Majenzi (240), Mafundi Sanifu, Warasimu (*Draughtmen*), pamoja na kampuni za Wabunifu Majengo (200) na kampuni za Wakadiriaji Majenzi (101).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupanua wigo wa usajili, Bodi itasajili wataalum wenyе fani zinazoshabihiana na Kampuni za ushauri (*Interior Designers, Landscape Architects, Conservation Architects, Furniture Designers, Naval Architects, Building Surveyors, Building Economists, Project Managers and Construction Managers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Bodi itaendelea kuwawezesha wahitim kupata mafunzo kwa vitendo, ili kuhakikisha wanapata maarifa na usoefu unaokidhi haja ya Sekta ya ujenzi kulingana na sheria pamoja na kuwaelimisha

watekelezaji wa miradi ya ujenzi katika Mikoa ya Tanzania Bara kuhusu umuhimu wa kutumia wataalam waliosajiliwa katika miradi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Usajili wa Makandarasi; katika mwaka 2013/2014, Bodi ya Usajili wa Makandarasi imepanga kusajili jumla ya makandarasi 813 wa fani za Majengo, Majenzi (*Civil works*), Umeme, Mitambo, Kazi maalum (*Specialists*) Makandarasi wa muda (*Temporary Contractors*) na Makandarasi wanaofanya kazi kwa ubia. Aidha, Bodi itafanya tathmini (*Review*) ya vigezo vinavyotumika kusajili Makandarasi ili kuendelea kupata Makandarasi walio bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi pia itaendesha jumla ya kozi za mafunzo sita katika mikoa mbalimbali ya Tanzania na zaidi ya makandarasi 270 wanatarajiwa kuhudhuria mafunzo haya. Mafunzo yatalenga maeneo ya utawala/ udhibiti wa fedha, utawala wa biashara, usimamizi wa mitambo, matumizi ya Teknohana katika ujenzi, upangaji na udhibiti wa kazi za ujenzi. Ili kuhakikisha kazi zote zinafanywa na Makandarasi waliosajiliwa na Makandarasi wanafuata sheria na taratibu za usajili wao, Bodi imepanga kukagua miradi ya ujenzi 3,090 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na wadau wengine, Bodi itaendelea kusimamia mpango maalum wa kukuza uwezo wa Makandarasi wazalendo ukiwemo ujenzi wa daraja la Mbutu kwa mfumo wa Kubuni na Kujenga (*Design and Build*). Mradi huu unatekelezwa kwa ubia na Makandarasi wa kizalendo 13 na Wahandisi Washauri wazalendo wanne kwa lengo la kukuza uwezo wa wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi. Katika mwaka 2013/2014, Baraza la Taifa la Ujenzi limepanga kukamilisha Kanuni za Utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha Baraza (*CAP 162 Revised Edition 2008*), kufanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi. Aidha, itaratibu na kutoa

mafunzo, ushauri wa kiufundi kuhusu utatuzi wa migogoro katika sekta pamoja na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi (*Labour Based Technology*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi pia itaendelea na jitihada za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund (CIDF)*), kuratibu mfumo wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji (*Construction Sector Transparency Initiative (CoST)*); ikiwa ni njia mojawapo ya kupambana na rushwa katika sekta. Baraza vile vile, litaendelea kuratibu ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi na kuandaa majarida ya kiufundi kuhusu sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Nailbu Spika, katika mwaka 2013/2014, Bodi kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) na mwekezaji binafsi itaendelea na ujenzi wa jengo la ofisi la ghorofa 22 lililoko Barabara ya Samora, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vikosi vya Ujenzi; katika mwaka wa fedha 2013/2014, Vikosi hivi vitaendelea na ujenzi wa maegesho ya Kivuko cha Msanga Mkuu na maegesho ya Senga ya Kivuko cha Chato, ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi wa Serikali pamoja na kuendeleza viwanja 38 vinavyomilikiwa na Vikosi vya Ujenzi Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vikosi vitaendelea na maboresho ya kiutendaji kwa kufanya ukarabati wa karakana (*Carpentry Workshops*) zilizopo Dar es Salaam na Dodoma, ukarabati wa Ofisi zilizopo Dodoma na Arusha pamoja na kuongeza vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ujenzi – Morogoro; katika mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi 800 katika fani za ufundi stadi wa kazi za barabara, majengo pamoja na

udereva. Aidha, Chuo kitaendeleza ujenzi wa jengo jipya la madarasa na karakana ya ufundi pamoja na kununua samani na zana ndogo ndogo za kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia katika Sekta ya *Uchukuzi (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)*; katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kituo kimepanga kuendelea na jukumu la kusambaza teknolojia katika sekta ya barabara na uchukuzi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo kitaandaa warsha na mafunzo yanayolenga kutatua changamoto zinazoikibili sekta ya barabara na uchukuzi, kusambaza kwa wadau 120,000 jumla ya makala na taarifa 150 zinazohusu teknolojia mbalimbali katika sekta ya barabara na uchukuzi kwa ujumla pamoja na kuendelea kutoa huduma ya Maktaba ya Kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *Morgan State University* ya Marekani pamoja na wadau wengine kitaanza kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na uchukuzi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wabunge wote na Kamati ya Bunge ya Miundombinu, chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kwa michango, ushauri na ushirikiano waliotupa katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Wizara inaadidi kufanya kazi ushauri, na maamuzi ya Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti hii na katika fursa nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani zetu ziwaendee Washirika wetu wa Maendeleo waliochangia katika kutekeleza programu na mipango yetu ya sekta. Nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyochangia kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta yetu ni pamoja na Abu Dhabi, Denmark (*DANIDA*), Japan (*JICA*), Korea, Marekani (*MCC*), Uingereza (*DFID*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*),

Benki ya Dunia (*WB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Kuwait Fund na *OPEC Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha uongozi wa Wizara ya Ujenzi. Viongozi hao ni Mheshimiwa *Engineer* Gerson H. Lwenge, Naibu Waziri; Balozi Herbert E. Mrango, Katibu Mkuu; *Engineer* Dkt. John S. Ndunguru, Naibu Katibu Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Wenyeviti na Watendaji Wakuu wa Bodi za Mfuko wa Barabara, Usajili wa Makandarasi, Usajili wa Wahandisi, Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Baraza la Taifa la Ujenzi, *TANROADS, TEMESA* na *TBA*. Nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi na Taasisi zake kwa ushirikiano wao mkubwa. Nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu pamoja na uvumilivu walionao kwangu wakati nikitekeleza majukumu ya Kitaifa. Nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza sana Wabunge waliofanikiwa kurudi Bungeni baada ya *ku-appeal*. Wabunge hao ni Mheshimiwa Godbless J. Lema (Mbunge wa Arusha), Aeshi (Sumbawanga) na aishi na ataishi kweli kuwa Mbunge katika Jimbo hilo, lakini Mheshimiwa Kafumu alivyofumua na mpaka akaingia tena Bungeni kwa tiketi ya CCM na nina uhakika ataendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama alivyoahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Kafumu, Mheshimiwa Aeshi na nina uhakika, watashirikiana na Wizara yangu na napenda kuahidi kwao na kwa Majimbo yao kwamba tutatekeleza Ilani ya

Uchaguzi kama ilivyoanishwa kwenye ukurasa wa 62 - 72 katika kuyatekeleza yale yote waliyoyaahidi katika kipindi kifupi hicho kilichobaki. Nina uhakika Wananchi wa maeneo hayo wataendelea kutoa ushirikiano kwa Wabunge hawa kwa jinsi walivyoingia tena Bungeni kwa kishindo kikubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida 2013/2014; katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Ujenzi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 381,205,760,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo Sh. 21,211,514,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Sh. 353,049,400,000.00 ni fedha za Mfuko wa Barabara na Sh. 6,944,846,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2013/2014. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Ujenzi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 845,225,979,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh. 448,174,599,000.00 ni fedha za ndani na Sh. 397,051,380,000.00 ni fedha za nje.

MUHTASARI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA 2013/2014

A. Matumizi ya Kawaida

MAELEZO	KIASI (SHILINGI)
Mishahara	21,211,514,000.00
Mfuko wa Barabara	353,049,400,000.00
Matumizi Mengineyo	6,944,846,000.00
Jumla Fedha za Matumizi ya Kawaida	381,205,760,000.00

B. Fedha za Maendeleo

Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	448,174,599,000.00
Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo	397,051,380,000.00
Jumla Fedha za Maendeleo	845,225,979,000.00
JUMLA YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO	1,226,431,739,000.00

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa,
naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Ujenzi, Dkt. John Magufuli, kwa Hotuba yako. Hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa hotuba uliyotupatia.

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, naona anakuja Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Kapuya, Mwalimu wangu, karibu. (*Makofi*)

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika,
ahsante. Ndiyo raha ya kuwa na wanafunzi mpaka katika Bunge hili wenye vyeo vizito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013 na Kanuni ya 116

(11), naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Ujenzi kwa ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hiyo mbele ya Kamati yangu kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya 2012/2013 ikiwa ni pamoja na Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri wa Kamati na kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2012/2013. Wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imejitahidi kutekeleza ushauri na maagizo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2012/2013. Ukusanyaji wa mapato; Mfuko wa Barabara; Wizara ilijiwekea malengo ya kukusanya sh. 429,664,000,000/= za Mfuko wa Barabara ambapo hadi kufikia Februari 2013 kiasi cha sh. 285,595,022,000 za Mfuko wa Barabara zilikusanywa sawa na 66.5% ya malengo ya makadirio kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Idara na Vitengo vyenye vyanzo vya Mapato; katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya sh. 15,628,580.00 kupitia Idara na Vitengo vyenye vyanzo vya mapato. Idara hizo ni Utawala, Huduma za Kiufundi na Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi. Hadi kufikia Februari, 2013 jumla ya sh. 36,388,193.24 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 232.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili la makusanyo linatokana na zoezi lililoanza tarehe 19 Novemba, 2012 la kufuta matumizi ya namba za kiraia kwenye magari, pilipiki, bajaji na Mitambo ya Serikali na kusajiliwa kwa namba za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida; katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ilitengewa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sh. 329,085,354,000/=, hadi kufikia Februari, 2013 Wizara ilikuwa imepokea sh. 226,983,164,573.75/= ikiwa ni 69% ya makadirio yote. Kati ya Fedha zilizotolewa sh. 209,807,257,491.75/=, ni Fedha za Mfuko wa Barabara; sh.13,681,812,082.00/= ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na sh. 3,494,095,000.00/= ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo ya Wizara, Taasisi na Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2012/2013; katika Mwaka 2012/2013, Serikali ilitenga sh. 693,948,272,000/= za Fedha za ndani kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo hadi kufikia Mwezi Machi, 2013 kiasi chote sawa na 100% za Fedha zote za ndani zilikuwa zimeshatolewa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha zote za Maendeleo za mwaka 2012/2013, hajapata kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa bajeti na mpango wa bajeti kwa mwaka wa 2013/2014, Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato; katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Wizara kuitia Idara mbalimbali na Vitengo vyake inatarajia kukusanya jumla ya sh. 45,047,550/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na maendeleo; katika Mwaka wa fedha wa 2013/2014 Wizara imetengewa jumla ya sh. 381,205,760,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 845, 225,979,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hivyo makadirio kwa ajili ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 jumla ni sh. 1,226,431,739,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana

Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha katika sekta hii muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Kamati inaomba Serikali iendelee kuzingatia umuhimu wa sekta hii ili hatimaye barabara zote muhimu kiuchumi kama vile Kaliua – Usinge - Chagu, Mpanda Kaulia Kashishi Kahama nazo zikamiliike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kwanza, Miradi ya Maendeleo. Mpaka mwezi Machi, 2013 kati ya sh. 397,051,380,000/= za fedha za maendeleo zilizokuwa zinatarajiwa kupokelewa kutoka kwa wadau wa maendeleo ni sh. 16,360,803,000/= tu zilikuwa zimetolewa ambazo ni sawa na 4.1%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo huu unaonesha kuwa uwezekano wa kupata zote kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha ni mdogo. Kamati inashauri Serikali ipunguze utegemezi ambao mara nyingi umekuwa hautusaidii sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanasayansi maarufu, *Albert Einstein*, aliwahi kusema, nanukuu: "*I am thankful for all of those who said No to me. Its because of them I am doing it myself.*" Kwa tafsiri isiyo rasmi alisema "Nawashukuru wote walioniambia Hapana. Na kwa sababu yao nafanya mwenyewe."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wadau hao wanaelekea kusema Hapana tufanye wenyewe kwani tunaweza. Kwani maendeleo yetu yanatutegemea wenyewe kama mwanamzuki mmoja, Les Brown, alivyowahi kusema, nanukuu "*Accept responsibility for your life; know that it is you who will get yourself where you want to go, no one else.*" Tafsiri isiyo rasmi ni: "Kubali wajibu wa maisha yako. Fahamu kuwa ni wewe mwenyewe utakayejifikisha unakotaka kwenda na si mtu mwingine yejote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hali ya barabara Jijini Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na

msongamano mkubwa wa magari. Katika Taarifa ya mwaka 2012/2013, Kamati ilitoa ushauri kuhusu tatizo hili kubwa kiuchumi, kijamii na hata kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudimbalimbali zinazofanywa na Serikali za kutekeleza miradi ya kupunguza msongamano Jijini Dar es Salaam, Kamati inashauri kuwa wakati umefika kwa matatizo ya Dar es Salaam kutatuliwa kwa mkakati maalum na kwa mapana yake. Hili litawezekana ikiwa Serikali itatafuta Fungu Maalum (*Special Fund*) kwa ajili ya kuendeleza na kuboresha miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi mbalimbali duniani, mfano majirani zetu Kenya sasa wamefanikiwa kujenga miundombinu mizuri ya barabara za juu (*fly overs*) nydingi katika jiji la Nairobi na kupunguza msongamano mkubwa wa magari ndani ya Jiji hilo kwa sababu waliweka mkakati ikiwemo kuunda Wizara maalum ya Jiji la Nairobi na kutafuta mkopo kwa ajili ya Jiji hilo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati bado inaendelea kusisitiza uharakishwaji wa kuanzisha usafiri wa boti kutoka Bagamoyo mpaka Feri jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye maamuzi magumu na ya maendeleo sasa badala ya kubaki kulaumu umaskini na ufinyu wa bajeti. George Bernard Shaw aliwahi kusema, nanukuu: "*People are always blaming their circumstances for what they are. I don't believe in circumstances. The people who get on in this world are the people who get up and look for circumstances they want, and, if they can't find them, make them*" Tafsiri isiyo rasmi inasema: "Watu mara nydingi hulaumu mazingira walio nayo. Mimi siamini katika mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaosonga mbele katika dunia hii ni wale wanaosimama na kutafuta mazingira

wanayoyataka na kama hawayapati, wanayatengeneza, tutengeneze mazingira kwa kuona wenzetu wamefanya nini ili kupata mafanikio waliiyoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Kamati ilifanya ziara ya kutembelea ujenzi wa daraja la Kigamboni mwezi Aprili, 2013. Kamati ililelezwa kuwa matayarisho ya eneo la daraja yamekamilika na utaratibu wa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa Kurasini unaendelea. Upande wa Kigamboni uthamini wa mali katika eneo la ujenzi wa barabara ya maungio umekamilika na taratibu za fidia zinaendelea kwa ushirikiano na Wizara ya Ardhi na Serikali ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwani ujenzi wa daraja la muda umekamilika kwa asilimia 90%. Hata hivyo, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kupanua barabara zinazounganisha daraja hili. Aidha, katika kuhakikisha msongamano unadhibitiwa, Kamati inashauri katika makutano ya barabara ya Mandela na barabara ya Kilwa kujengwe barabara za juu (*fly over*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Miradi ya ujenzi wa barabara; tarehe 2 Aprili, 2013, wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Bajeti kwa kipindi cha 2013/2014, Kamati ililelezwa kwamba kiasi chote cha Fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo mpaka Machi, 2013 zilishatolewa kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo mazuri, kuwa fedha zote za ndani ziliikuwa zimetolewa kwa 100%, Kamati imepata taarifa kuwa hadi tarehe 8 Aprili, 2013 Wizara ilikuwa ikidaiwa sh. 348,666,029,178.53 kwa ajili ya fidia kwa wananchi, Makandarasi na Makandarasi Washauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpaka taarifa hii inasomwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu umepita mwezi mzima tangu tulipopata taarifa hiyo, Kamati inashauri kuwa wakati wa majumuisho ya mjadala wa bajeti ya Wizara hii ni

vizuri Bunge lako Tukufu lielezwe Serikali inadaiwa kiasi gani katika sekta ya barabara kutokana na bajeti ya mwaka uliopita wa 2012/2013 ili kujua iwapo bajeti inayopitishwa sasa itakwenda kujenga miradi iliyokusudiwa au ni kwa ajili ya kulipa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Kamati inazidi kusisitiza kuwa ili Serikali isielemewe na madeni yanayotokana na riba na adhabu zinazotokana na Mikataba ya kazi za ujenzi, ni vyema Serikali ikawa inatoa fedha kwa wakati muafaka kwa kuzingatia hatua za ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kumekuwa na changamoto zinazotokana na uvamizi wa maeneo ya hifadhi za barabara kinyume na Sheria ya barabara Na. 13 ya Mwaka 2007. Uvamizi huu unaleta usumbu na gharama kubwa katika ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo utekelezaji wa Sheria ya barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 una upungufu kiasi cha kutowatendea haki Watanzania wakati mwingine. Kifungu cha 16 cha sheria hiyo kinarejesha masuala ya fidia ya ardhi iliyochukuliwa na Serikali kwenye Sheria ya Uchukuaji Ardhi ya mwaka 2002 (*Land Acquisition Act, 2002-Chapter 118*).

Kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Uchukuaji Ardhi (2002), kinatamka kuwa pande zote zinazohusika katika uchukuaji wa ardhi, ndani ya majuma sita tangu notisi ya kutwaa ardhi husika ilipotolewa, ziwe zimeridhika na kiwango cha fidia kitakachotolewa kwa ajili ya eneo husika.

Aidha, kifungu 14(a) cha sheria hiyo kinatamka kuwa, tathmini ya ardhi inayotarajiwa kuchukuliwa itazingatia thamani ya ardhi hiyo wakati notisi ya uchukuaji wa ardhi hiyo ilipotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu umeonesha kuwa Sheria hii huwa inakiukwa mara kwa mara kwani Serikali

inatoa notisi ya kuchukua ardhi na hivyo kuzuia mmiliki wa eneo husika kutofanya shughuli yoyote ya maendeleo katika eneo husika. Tathmini inaweza kufanyika muda mrefu baada ya notisi kutolewa na malipo ya fidia kutolewa miaka kadhaa baada ya tathmini kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchelewesha tathmini na fidia kunasababisha wananchi walipwe fidia ndogo sana ikilinganishwa na bei ya soko ya eneo husika. Kamati inashauri serikali iwe kichocheo cha maendeleo ya wananchi, badala ya kuwa kichocheo cha umaskini kwa wananchi kwani tathmini na fidia zinazofanyika miaka mingi baada ya kutolewa notisi kunasababisha wananchi wapunjike na hivyo pesa wanazopata kama fidia kutokuwa na uwezo wa kujenga au kufanya maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini huu hautokani na fidia kwa majengo tu bali hata mazao ya kudumu kama miembe, minazi na kadhalika. Mbali ya fedha inayotolewa kwa mazao haya kuwa kidogo pia haizingatii ukweli kuwa zao husika lingemsaidia mmiliki kwa maisha yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro na mivutano mingi kutoka kwa wananchi inasababishwa na Serikali kutozingatia Sheria zilizotajwa hapo juu jambo linalopelekea wananchi kugoma kuondoka katika maeneo ya miradi na kusababisha kuchelewa kuanza kwa miradi Kama ilivyopangwa na Serikali. Kamati inashauri Serikali izingatie sheria wakati wa kutekeleza miradi yake na kuwa tayari kufanya tathmini na fidia mara baada ya kutoa notisi ya kuchukua eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vyombo vyaa usimamizi wa Sheria ya Barabara kuwa macho wakati wote endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara azuiwe au abomolewe mapema kuliko afike mbali au amalize kabisa ujenzi wake, baadae huleta misuguano isiyokuwa ya lazima kwani wananchi wengi wamekuwa wakiuliza wakati wa kujenga Serikali ili kuwa wapi? Kama hili litafanyika litakuwa fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inashauri Serikali ifanye kazi kama taasisi moja yenyе lengo moja la kuwahudumia na kuwaletea maendeleo Watanzania. Badala ya kuwa na umaja kila Wizara imekuwa ikifanya mambo yake bila mawasiliano na Wizara nyiningine na hata mawasiliano yanapofanyika utekelezaji haufanyiki kwa haraka kuendana hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; wakati Wizara ya Ujenzi ikishughulika na ujenzi na ulinzi wa barabara kwa kuhakikisha maeneo ya barabara hayavamiwi kwa namna yoyote ile, unaweza kuona nyumba zilizo ndani ya hifadhi ya barabara zimepewa hati miliki na Wizara ambayo ni sehemu ya Serikali hii hii, mabango ya matangazo ya biashara yanapotakiwa kuondolewa barabarani Halmashauri za Miji na Majiji hazikubaliani na suala hilo au katika upanuzi wa barabara uondoaji wa miundombinu ya maji na umeme pla unachelewesha sana kiasi cha kuchelewesha utekelezaji wa miradi husika na kuigharimu Serikali fedha zaidi katika miradi hiyo.

Hali hii pia inajitokeza kwenye utekelezaji wa Sheria ya Uuzaji wa Vyuma Chakavu inayosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini wanaoathirika zaidi na biashara hii ni Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi kwa miundombinu kung'olewa na kuuzwa kama chuma chakavu. Pamoja na malalamiko ya muda mrefu yanayotolewa na wadau mbalimbali kuhusu uharibifu wa miundombinu yetu inayogharimu fedha nyingi na usalama wa watumiaji wa barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria hii bado yanasuasua kwa vile Wizara inayoisimamia haiathiriki moja kwa moja na Sheria hii. Hali kama hii iko katika maeneo mengi hapa nchini. Kamati inashaurim linapokuja suala la maendeleo ya wananchi kuwa na umaja bila kuangalia maslahi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, matuta ya barabarani, kumekuwa na matuta makubwa mengi sana

katika barabara na hasa barabara kuu yaani *highway*. Matuta haya yamekuwa yakiambatana na matuta mengine madogo madogo yajulikanayo kama rasta.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yamekuwa yakileta madhara kwa afya ya binadamu kwani baadhi ya matuta yanakuwa makubwa sana, hayana alama na mengine alama zinakuwa zimepauka na kusababisha baadhi ya watu kutenguka migongo na shingo kutokana na kurushwa na magari yanapopita katika matuta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia magari ya mizigo matuta haya husababisha mizigo kuhama na kuyafanya magari yaelemewe na mizigo upande mmoja kitu ambacho huweza kusababisha ajali badala ya kuzuia ajali. Ni ukweli usiopingika kuwa matuta haya yamekuwa yakivunja na kuharibu vifaa mbalimbali vyataga magari pamoja na bidhaa zinazokuwa zikisafirishwa katika barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri matuta yapunguzwe sana kiidadi na ukubwa wake. Pia matuta ya rasta yaondolewe kabisa. Ikumbukwe kuwa Sheria ya barabara kuu (*highway*) duniani hairuhusu vitu hivi. Badala yake Kamati inashauri elimu itolewe kwa wananchi na wanavijiji wanaoishi pembezoni mwa barabara juu ya matumizi bora ya barabara na kusogea biashara zao mbali na barabara.

Mheshimiwa Spika, sita, Mizani za Barabarani, moja kati ya majukumu ya *TANROADS* ni ujenzi na utunzaji wa barabara kwa kudhibiti uzito wa magari ili kuhakikisha barabara zinadumu kwa muda mrefu, mizani ndicho chombo muhimu sana katika kudhibiti uzito wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa vituo vingi vyataga mizani, bado barabara hizi zimekuwa zikitengeneza matuta na mabonde, jambo ambalo linathibitisha kuwa ama ujenzi wa barabara hizi haukuzingatia viwango au magari yenye uzito kuliko uwezo wa barabara huendelea kupita siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili lisipotafutiwa ufumbuzi wa kudumu mapema, Taifa hili litakuwa linaendelea kutenga fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara zile zile kila mwaka. Kamati inashauri *TANROADS* itekeleze majukumu yake ya kusimamia barabara vizuri na endapo barabara zitaendelea kuharibika maofisa wa *TANROADS* waliopo katika Kanda husika wawajibishwe ili wengine waweze kuchukua nafasi zao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kwa kuwa magari mengi yanatoa mizigo bandari ya Dar es Salaam, Kamati inashauri kufungwe mzani nje kidogo ya bandari eneo la uhasibu ambao utatumika kupima uzito wa magari ya mizigo kabla ya kuanza safari ili endapo uzito utaonekana umezidi gari husika liweze kurudi na kupunguza mizigo kabla ya kuanza safari na kuharibu barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudzi za kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani, Kamati inaunga mkono wazo la Serikali kujenga mizani za kisasa mbali na barabara kuu, mizani hizi zitakuwa na uwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion*).

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili liharakishwe na mizani hizi zifungwe katika maeneo yote yenye kusababisha msongamano mkubwa wakati wa kupima magari na vituo vyake viwe mbali na barabara ili kuruhusu magari yasiyohusika kuendelea na safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko ya usomaji wa vipimo vya mizani kutofautiana kati ya mizani moja hadi nyingine. Yaani kama mizani ni saba, unaweza ukapata majibu saba ya uzito uliotofautiana na yanaweza kupishana kati ya tani mbili hadi tani sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linaashiria kuwa baadhi ya mizani zinakuwa na hitilafu au wafanyakazi wa mizani hufanya hila ili kujipatia chochote. Kamati inashauri ili

kuepuka vishawishi, rushwa na wizi wa fedha zinazotokana na tozo la faini kwa magari yanayozidisha mizigo, risiti za *TRA* za *electronic* zitumike badala ya risiti za kawaida kwani katika ulimwengu wa teknolojia kuna uwezekano wa kutengeneza risiti za kugushi na kuzitumia kupokea tozo kwa manufaa binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inashauri mizani ziwe zinafanyiwa matengenezo (*service*) mara kwa mara na (*certificate of calibration*) itolewe kila inapofanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Mizigo isiyo ya Kawaida (*Abnormal Load*) na *Winch*. Mizigo isiyo ya kawaida huingizwa kupitia Bandari yetu ya Dar es Salaam, baadhi ya mizigo hii husafirishwa kwenda katika miradi na uwekezaji mbalimbali nchini na mgingine hupelekwa nje ya nchi kama Zambia na DR Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mizigo hii huweza kufunguliwa na kupunguzwa endapo uzito umezidi, lakini mgingine haiwezekani kupunguzwa japo inakuwa imezidi uzito. Kwa sasa vibali vya kubeba mizigo isiyo ya kawaida hutolewa na Wizara, jambo ambalo huchukua muda mrefu na wakati mwingine inapokwama wasafirishaji wa mizigo ya aina hii wamekuwa wakipitisha Mombasa Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri, kwa kuwa mizigo hii siyo mingi sana, wasafirishaji wa mizigo hii waruhusiwe kubeba mizigo isiyo ya kawaida kwa kulipia tozo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vibali vyake vimekuwa vikitolewa na Wizara ya Ujenzi, lakini kwa kuwasiliana na *TANROADS*. Mawasiliano haya huchukua muda mrefu na kuna wakati vibali havitoki hadi baada ya wiki mbili mpaka miezi minne huku Mamlaka ya Bandari ikiendelea kutoza tozo kwa mwenye mizigo. Kwa majirani zetu Kenya vibali hivi huchukwa siku moja hadi mbili kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile vibali nya magari aina ya winchi na magari mengine ya kuokolea navyo vimekuwa vikichelewa kutolewa. Kamati inashauri, vibali hivi ambavyo hasa vinahusu maisha, vitolewe na *TANROADS* badala ya utoaji wake kuendelea kutumia Itifaki ya *SADC* inayotaka vibali vitolewle ndani ya masaa ishirini na nne tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vibali nya winchi au magari ya uokoaji vitolewe kwa mwaka mara moja ili kunapotokea ajali magari haya yawezekwenda haraka badala ya kusubiri mlolongo wa upatikanaji wa vibali. Kwani magari haya yanakwenda kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Wakala wa Ufundu na Umeme (*TEMESA*) inashugulikia matengenezo ya vyombo vyote nya moto na mitambo ya aina zote pamoja na mifumo ya umeme, viyoyozi na vifaa nya elektroniki na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za kihandisi katika maeneo hayo. Kwa kuaangalia majukumu hayo, Kamati inashauri kuwa *TEMESA* izidi kujengewa uwezo kwa kupatiwa wataalam wa kutosha na vifaa nya kisasa ili iweze kutengeneza magari ya Serikali kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ofisi nydingi na karakana za Wakala wa Ufundu wa Umeme (*TEMESA*) ni chakavu, Kamati inashauri, wakati Serikali inaendelea kuajiri wataalam wa kutosha na vifaa nya kisasa, ni vyema pia kuendelea na ujenzi pamoja na ukarabati wa karakana zote zilizo chini ya *TEMESA* nchini. Pia Kamati inashauri, ofisi zote za Serikali kuheshimu utaratibu na kwenda kutengeneza magari ya Serikali *TEMESA* badala ya kuyapeleka kwa mafundi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, Wakala wa Majengo Tanzania; katika Taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2012/2013, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Desemba 2012, Wakala umejenga nyumba za viongozi katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia majukumu

ya Wakala huu, Kamati inashauri uwezeshwe kifedha ili kusaidia kupunguza uhaba wa nyumba za viongozi pamoja na nyumba za watumishi wa Serikali. Pia Kamati inashauri kuwa Wakala huu ujiendeshe kibiashara kwa kujihusisha na usanifu wa majengo, kuchora ramani, kukopa benki kwa kuweka dhamana mali zake ikiwemo majengo na viwanja, kuingia ubia na wawekezaji wengine ili kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Na. 13 cha Sheria ilioanzisha Wakala za Serikali (*The Executive Agencies Act, 1997, Chapter 245*) kinatoa ruhusa kwa Wakala ikiwemo Wakala wa Ujenzi kukopa baada ya kupata kibali kutoka kwa Waziri anayehusika na masuala ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sheria hii na kwa kuwa Wakala huu una majengo ya kutosha upo uwezekano wa kuweka dhamana kwenye mabenki ili kupata mikopo ya kuendeleza miradi ya ujenzi. Kamati inashauri Wakala huu utafute mikopo ili uweze kujenga nyumba nydingi na kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Kamati inashauri Wakala wa Majengo Tanzania ujikite zaidi katika kujenga nyumba za ghorofa kwani zitasaidia kuchukua watu wengi zaidi katika eneo dogo na kufanya ardhi inayobaki itumike kwa ajili ya shughuli zingine za maendeleo. Ujenzi wa nyumba kama ilivyofanyika katika eneo la Kisasa hapa Dodoma siyo mzuri kwani umechukua eneo kubwa pasipo sababu. Ikumbukwe kuwa shughuli za binadamu zinaongezeka kila siku, lakini ardhi haiongezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, Bodi ya Usajili wa Makandarasi, shughuli za ujenzi zinahitaji Mkandarasi awe na mtaji mkubwa kutekeleza kazi za ukandarasi jambo ambalo limesababisha Makandarasi wengi wa Kitanzania wenyewe mitaji midogo kutoshiriki kikamilifu kutumia fursa za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kutekeleza ushauri wake uliotolewa mwaka 2012/2013, ambapo Bodi ya Usajili wa Makandarasi imeanzisha

Mfuko wa kusaidia Makandarasi wadogo wa ndani (*Contractors Assistance Fund- CAF*) kwa kutoa dhamana ya mikopo ya kukuza mitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulitekeleza hili, Makandarasi wa ndani 13 na Makampuni mawili ya Wahandisi Washauri wamepewa kazi ya ujenzi wa daraja la Mbutu. Kamati inashauri Serikali kuendelea kuwawezesha Makandarasi na Makandarasi Washauri wa Kitanzania kwa kuwashirikisha katika kazi kwani kwa kufanya hivyo tunaimarisha na kuzalisha wataalam bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja, Wahandisi na Mafundi Sanifu; kumekuwa na wimbi la kubadilisha Vyuo vya Ufundu kuwa Vyuo Vikuu na kusababisha kuwa na Taifa lisilo na idadi ya kutosha ya mafundi sanifu ukilinganisha na mahitaji ya soko. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa, isitishe utaratibu wa kubadilisha Vyuo vya Ufundu nya katika kuwa Vyuo Vikuu kwani kwa kufanya hivyo tunaondoa uwiano unaotakiwa baina ya Wahandisi na Mafundi Sanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na mbili, Bodi ya Usajili a Wabunifu Majengo na Wakadiriaji wa Majenzi; majukumu makuu ya Bodi hii ni kusajili, kusimamia, kuangalia na kuratibu mwenendo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Kampuni zinazohusiana na fani hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ina majukumu ya kukagua sehemu zinakofanya shughuli za ujenzi ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za majenzi zinasimamiwa na wataalam waliosajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia ujenzi wa maghorofa mijini ikiwemo Jiji la Dar es salaam unakua kwa kasi. Hata hivyo, baadhi ya majengo hayo yamekuwa yakiporomoka na kusababisha hasara kubwa ikiwemo kugharimu maisha ya watu kama ilivyotokea hivi karibuni Jijini Dar es slaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya hali hii ni kwamba,

Bodi haitimizi wajibu wake kama msimamizi na kama inasimimia basi inasajili Makandarasi ambao hawana sifa za kutosha. Kamati inashauri Bodi hii iwe makini katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuajiri ili maafa yanayotokea sasa yasiendelee kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya sh. 1,226,431,739,000/=. Kati ya hizo sh. 381,205,760,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 845, 225,979,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia na kujadili kwa Kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kifungu kwa kifungu na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu kuyajadili na kuyapitisha maombi ya fedha kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati namshukuru Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, Waziri wa Ujenzi akisaidiwa na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer Gerson Lwenge*, Mb, Katibu Mkuu Balozi Herbert E. Mrango, Naibu Katibu Mkuu Dkt. *Engineer John Ndunguru*, watendaji, watalaam wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha Taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu. Ninawashukuru wataalam bila kumsahau *Engineerwangu* wa Mkoa wa *TANROADSTabora*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa. Kwa nafasi ya kipekee napenda kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti; Mheshimiwa Prof.Juma Athuman Kapuya, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mjumbe; Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mjumbe; Mheshimiwa Clara

Diana Mwatuka, Mjumbe; Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo, Mjumbe; Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mjumbe; Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mjumbe na Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Aliko Nisukuma Kibona, Mjumbe; Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani, Mjumbe; Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mjumbe; Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mjumbe; Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura , Mjumbe; Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mjumbe; Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mjumbe na Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, Mjumbe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa, ninakuomba malizia tu, bila kutaja majina.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wengine ni Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mjumbe; Mheshimiwa Horoub Mohamed Shamis, Mjumbe na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashillilah kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Malizia tu.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU): Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii akiwemo Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Hosiana John kwa kuihudumia Kamati wakati wote hadi Taarifa hii kukamilika.

Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana wapiga kura wangu kwa ushirikiano wao na mshikamano wanaoendelea kunipa. Ni ushirikiano wenu ndio unaoniwezesha kuwatumikia kwa ufanisi zaidi

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi sana kwa Timu yetu ya *Azam* kwa kutufikisha hapo ilipotufikisha. Hawafanani na wale wengine ambao wamezoea kupanda mabasi tu kwenda Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile naomba nitoe ushauri wa bure kwa Mheshimiwa Ismaili Rage, kwamba tarehe 18 Mei, 2013, wale vijana wake watakuwa wanacheza na babu zao. Sasa si vizuri mtu mzima kumfunga tano tena, wawafunge tatu tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya kwa hotuba yako. Sasa moja kwa moja nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, naye si mwengine ni Mheshimiwa Said Amour Arfi, tafadhalii karibu sana.

MHE. SAID AMOUR ARFI (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI): Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na fadhila zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru nawe kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni 99(9), Toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la msingi la Wizara hii ni kusimamia tasnia ya ujenzi kwa ukamilifu wake ili kutoa matokeo bora na kuchochaea uchumi wa nchi yetu na kuwalettea maendelo watu wetu na kupunguza umaskini na kuwa na miundombinu yenye kukidhi viwango, ubora na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti 2012/2013, ukusanyaji wa vyanzo vya mapato katika idara na vitengo vya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2012/2013, ulivuka lengo la mwaka hadi kufikia Februari 2013. Walikusanya zaidi ya mara mbili ya lengo la makusanyo kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika Mfuko wa Barabara ulikusanya takriban asilimia 70 hadi Februari 2013. Ni dhahiri Mfuko wa Barabara nao utafikia malengo uliokusudia kwa mwaka 2012/2013 na kuvuka lengo, haya si mafanikio haba, hata hivyo, hayajakidhi wala kupunguza changamoto za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, Wizara imeendelea kupokea fedha kwa mtiririko unaoridhisha. Matumizi ya kawaida hadi februari 2013 ilipokea 69% ya fedha za matumizi na 100% ya fedha kwa ajili miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani zilizokuwa zimepokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matukio kadhaa yaliyotokea ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya kina na kutosheleza na hatua zilizochukuliwa ili kuzuia hali hii isijirudie tena na kuleta maafa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua majukumu ya Wizara hii pamoja na kuzisimamia Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii ikiwemo Baraza la Ujenzi (NCC), Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Bodi ya Usajili wa Wabunifu majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQSRB), pia Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na vyombo hivi kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na taratibu za miundo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamekuwepo matukio ya kujirudia ya kuanguka kwa majengo ya maghorofa yaliyokamilika na yanayoendelea kujengwa katika Jiji la Dar es Salaam na tukio la hivi karibuni jengo liliokuwa linaendelea kujengwa katikati ya Jiji la Dar es Salaam, Mtaa wa Indira Ghandi na kupoteza maisha ya Watanzania kadhaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa pole kwa wale wote waliopoteza ndugu na marafiki zao katika tukio hilo, Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tukio la kuanguka kwa ukuta katika kituo cha Mabasi, Ubungo na kuharibu magari na mali za Watanzania ambao walifika katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo kwa kujipatia huduma. Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa kwa tukio hilo ambalo lingeweza kuzuilika iwapo Mkandarasi angezingatia kanuni za usalama. Tunapenda kuwapa pole Watanzania wenzetu waliokumbwa na mkasa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pole na kufarjiana pekee haitoshi, bado tunajiuliza kama nchi, ni lini viongozi wetu wataheshimu, kuwajibika na kutekeleza majukumu yao na kuwa na ujasiri wa kutafuta mbinu za kutatua matatizo pindi tunapokutana na mambo magumu katika utendaji wetu na si kukimbia matatizo kwa kujificha chini ya migongo ya watendaji wengine na kutowajibika na uozo unaotokea katika Wizara tunazozisimamia na tukisubiri kusifiwa kwa mazuri yanayofanywa na watendaji hao hao na kukwepa lawama kwa mambo ya ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri anawasilisha hotuba yake ya bajeti kwa mwaka wa fedha uliopita alisema kuwa, naomba kunukuu: "Bodi itafanya ukaguzi wa kina katika taasisi za elimu ya juu zinazofundisha uhandisi ili kubaini kama vyuo hivyo vina sifa stahiki za kufundisha Wahandisi na iwapo Wahadhiri wanaofundisha Wahandisi wamesajiliwa na Bodi" (*Hansard ya Hotuba ya bajeti ya Waziri wa Ujenzi 2012/2013, ukurasa 162*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na nukuu hiyo

hapo juu, ni dhahiri kuwa, Wizara na Waziri wana hofu na aina ya vyuo vinavyotoa elimu ya uhandisi na pia wana hofu na Wahadhiri ambao wana jukumu la kufundisha Wahandisi hapa nchini kuwa hawana viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, tunataka kujua ukaguzi huo ulifanyika katika vyuo gani na hali ikoje na ni hatua gani zilichukuliwa dhidi ya vyuo ambavyo Wahandisi na Wahadhiri walikutwa hawana sifa sitahiki, kwani tumeendelea kushuhudia maafa yanayotokana na kazi mbalimbali zinazofanywa na Wahandisi hapa nchini mwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji kujua taarifa za uchunguzi wa kuanguka kwa maghorofa, Dar es Salaam ya mwaka 2006 na hatua zillizochukuliwa baada ya ukaguzi na nyumba ngapi zilizopaswa kuvunjwa. Kwa maelezo ya Waziri Mkuu Mstaafu rejea gazeti la Nipashe la 3 Aprili, 2013 ilionekana takriban maghorofa 100 katika Jiji la Dar es Salaam yalitakiwa kuvunjwa kwa upungufu na kutokidhi viwango ni maghorofa mangapi hadi sasa yamevunjwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza mambo yafuatayo:-

(i) Hatua stahiki za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa wahusika wa maafa haya na zionekane zimetendeka ili kujenga imani kwa Watanzania.

(ii) Bodi zote nilizozitaja hapo juu ziwajibike ipasavyo kila moja katika eneo lake na kusimamia kikamilifu wajibu wao kwa mujibu wa sheria na taratibu, vinginevyo hatuna sababu ya kuwa na Bodi za Kitaalam ambazo haziwezi kusimamia wanachama wao.

(iii) Tuangalie upya sheria zetu na ikiwezekana tuwe na mamlaka mahususi ya ukaguzi (*Inspection Authority*)

inayosimamia majengo hususan maghorofa yenye kuwa na wataalam wa fani zote kwa Miji na Majiji yetu badala ya Halmashauri zetu zinazotoa vibali na kushindwa kusimamia kutokana na ukosefu wa wataalam ili tuweze kujua ni nani wa kuwajibishwa.

(iv) Ukaguzi wa kina na wa kitaaluma ufanywe katika vyuo vyote vinavyotoa elimu ya uhandisi na kuona kama vyuo hivyo vina sifa za kutoa elimu hiyo kwa mujibu wa sheria na kama wahitimu wake wanasifa za kuwa Wahandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya ya fedha za barabara; katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012, tulihoji kuhusiana na fedha zilizokuwa zimetengwa chini ya fungu liliolojulikana kama *special road construction project* na tulisema ifuatavyo:-

Nanukuu *Hansard* ya tarehe 1 Agosti, 2011: "Mheshimiwa Spika, Miradi maalum ya ujenzi wa barabara (kasma 4168). Kitabu cha Miradi ya Maendeleo (sehemu-A juzuhu iv) katika fungu 98, kasma 4168, utaona kuwa mradi unaitwa "Miradi ya ujenzi wa barabara maalum" (*special road construction projects*) na fungu hili limetengewa kiasi kikubwa kuliko miradi mingine yoyote ya ujenzi wa barabara katika mwaka huu wa fedha kwani zipo jumla ya sh. 348,075,000,000/= na hizi zote ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika hizi ni fedha nyingi sana na hasa ikizingatiwa kuwa kitabu hicho kimeonesha miradi yote ya ujenzi wa barabara ambayo itatekelezwa katika mwaka huu wa fedha, ila hii miradi maalum haijaoneshwa ni miradi ya barabara gani na zitajengwa wapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kasma hii kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na 2010/2011 haikuwa imetengewa kiasi chochote cha fedha na ndio maana imetustua kuona mwaka huu fedha nyingi kiasi hicho zinatengwa kwa miradi isijojulikana kuwa itajengwa wapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia maelezo yaliyotolewa kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu juu ya mpango na bajeti ya mwaka 2011/2012, kasma 4168 haipo kwenye randama na hakuna maelezo yoyote ambayo yametolewa kuhusiana na fedha hizo ambazo zimetengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, tunataka kupata maelezo ya kina ni miradi gani hii ambayo haiwezi kuandikwa na inatengewa fedha nyingi kiasi hicho? Kwani hii italiwezesha Bunge kuweza kuitisha bajeti inayofahamu na kuisimamia Serikali kwa kuweza kufuatilia utekelezaji wa miradi husika”.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mjadala kuhusiana na hotuba ya Wizara ya Uchukuzi 2011/2012, ilipowasilishwa, Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe Salvatory Machemli alihoji fedha hizi na kusema, naomba kunukuu *Hansard* ya tarehe 3 Agosti, 2011:

“Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaja mwanzoni kwamba, reli inakuwa wakati watu wanaiangalia na Serikali haisemi kitu chochote, kazi yao kuomba Miongozo tu hapa, pesa zipo nyingi. Wakati nawasilisha hotuba yangu kwa Wizara ya Ujenzi, nilihoji kiasi cha pesa shilingi bilioni 348 ambazo hazikuoneshwa zinafanya kazi gani kwenye Wizara ile.

Mheshimiwa Magufuli jana wakati anafanya majumuisho hakutaja, amemeza tu japokuwa aliona ni chungu lakini akameza kama *Chloroquine*. Nataka sasa hizi shilingi bilioni 348 ambazo zimeoneshwa kwenye vote 4168 ambazo matumizi yake hayakuoneshwa basi wapelekewe reli ili tuimarishe reli, tuweze kuokoa barabara zetu kuliko kuziacha tu, jamaa wanatia mfukoni, wanachukua wanaweka waa, kama ilivyo kawaida yenu Chama cha Mapinduzi, mnakwenda kujenga Masinagogi Ulaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala huo

aliyekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe alijibu kuhusiana na hoja hiyo na kusema, nanukuu *Hansard* ya tarehe 3 Agosti, 2011

"NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mheshimiwa Mbunge asiendelee kupotosha na kujenga mahekalu hewani, nilitaka kumweleza kwamba hizo pesa zilizopitishwa hapa jana ni za Mfuko Maalum ambao unaisaidia Serikali pale ambapo mfadhilli wa nje kwa mfano, anaamua kufadhilli ujenzi wa barabara fulani na anasema Serikali ichangie ten bilioni, utaitoa wapi kama wewe huna Mfuko Maalum? Serikali ikaona logic ya kuweka Mfuko Maalum ili isitulazimu tena kuitisha Bunge kuitisha pesa hizo, sasa zianze kuleta maneno, kutufanya wote ni wahuni kama ye ye na hii siyo vizuri kusema kwamba tutapeleka hizo pesa wapi? Ahsante. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 4 Agosti, 2011 wakati wa kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa kauli ya serikali kuhusiana na fedha kuongezwa Wizara ya Uchukuzi na alisema, nanukuu hansard ya tarehe husika: "Kwa hiyo, baada ya Kamati ya Miundombinu kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kuishauri Serikali kuongeza bajeti hiyo kwa shilingi bilioni 95, jambo ambalo tuliliridhia na kulikubali, lakini hatukuweza kufikia kiwango hicho kama ilivyokuwa imeombwa.

Kikao cha jana kimewezesha Serikali kufanikiwa kupata fedha hizo ambazo zitatumika kwenye maeneo matatu yafuatayo:-

Reli ya Kati, Kampuni ya Ndege Tanzania na Usafiri wa Majini yaani Meli katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kiasi hicho cha shilingi bilioni 95 ni kiasi ambacho Wizara ilikuwa imeji-commit au imeahidi mbele ya Kamati kwamba, zikipatikana zitawezesha huduma za msingi katika maeneo hayo matatu kuweza kuendelea bila matatizo makubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Bunge likiwa limekaa

kama Kamati ya Matumizi wakati wa kupitisha Vifungu ya Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Tundu Lissu aliomba ufanuzi kama ifuatavyo: Nanukuu *Hansard*:

“.....Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nifafanuliwe, kama Bajeti ya Wizara ya Ujenzi mafungu yote yalishapitishwa, hii bilioni 95 iliyochotwa kutoka fungu la miradi maalum ya barabara na kuletwa kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara ya Uchukuzi ambayo ni *Vote tofauti kabisa zimechotwa kwa idhini ya Kanuni ipi*, mimi naomba nipewe angalau msingi wa kikanuni au wa kisheria wa kuchota fedha ambazo tayari zimeshatengwa na Bunge hili bila kupata *authorization* ya Bunge hili. Ahsante sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu yafuatayo yalitolewa, kwa mujibu wa *Hansard*:

“Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu alichokisema Mheshimiwa Tundu Lissu kipo ukurasa 276, Kifungu kidogo cha 4168. Hizi ni fedha ambazo zimewekwa katika Kifungu hiki katika Bajeti hii ya ujenzi, lakini ni Mfuko Maalum, hela hizi hazijawa *committed* kama unavyoziona. Ukiangalia miradi yote iliyomo katika kifungu hiki ina barabara tayari.

Fedha hizi ziliwekwa maalum kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya miundombinu hasa katika maeneo ambayo ipo miradi kadhaa ambayo tuna uzoefu, imekuwa inachangiwa na wafadhili, lakini hii tulifikiri sehemu nyine miradi hii imekwama kwa sababu sisi tulikuwa hatujitayarisha kuweka *counterpart fund*. Kwa hiyo, hizi fedha zimewekwa hapa kwa ajili hiyo, miradi yote ambayo Serikali ya Tanzania itafanya kutoka kwenye fedha za wafadhili, hizi ni fedha ambazo zimewekwa, ni fungu ambalo haliko *committed*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hizi fedha zimechukuliwa hapa zimepelekwa ujenzi kwa maana ya kwamba, ni fedha ambazo ziliwekwa kwa ajili ya Mfuko wa

Miundombinu. Zimekuwa voted, lakini Mheshimiwa Tundu Lissu atakuja kupata ukweli wa mambo haya yote wakati wa *Appropriation Bill. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya fedha hizi kupunguzwa, kiasi cha shilingi billioni 95 na kupelekwa Wizara ya Uchukuzi zilibakia kiasi cha shilingi billioni 252.975 katika kifungu hiki. Leo tumelazimika kulikumbusha Bunge kuhusiana na suala hili, kwani kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka husika wa fedha kuhusiana na kifungu hiki alisema, naomba kunukuu:

“Malipo ya madeni ya mwaka wa nyuma yaliyolipwa kwa fedha za 2011/2012 kwa kutumia jina la mradi usio halisi sh. 252,975,000,000. Miradi katika Wizara ilipewa namba 4168 kwa ajili ya kuitisha malipo ya madeni ya miaka ya nyuma kwa miradi inayoteklezwa na *TANROADS*. Namba hii sio halisi” (chanzo: taarifa ya CAG ukurasa 160, fungu 98).

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zilizopotea au kulipwa kifungu hewa ni sawa na fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya barabara zifuatazo kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014:-

(i) Barabara ya Usagara-Geita-Kyamyorwa (kilomita 422);

(ii) Barabara ya Kigoma-Kidahwe-Uvinza-Kaliua-Tabora (kilomita 443);

(iii) Barabara ya Nangurukuru-Mbwemkulu (kilomita 95);

(iv) Barabara ya Sumbawanga-Matai-Kasanga Port (kilomita 112);

(v) Barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora (kilomita 264);

(vi) Barabara ya Tabora-Ipole-Konga-Mpanda (kilomita 359);

(vii) Barabara ya Kidatu-Ifakara-Lupilo-Malinyi-Londo-Lumecha/Songea(kilomita 396); na

(viii) Kuondoa msongamano barabara za Dar (kilomita 102.15).

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi bilioni 252 ni nyingi kuliko fedha zilizotengwa kwa miradi niliyoitaja sasa hivi. Aidha, ni sawa na kusema kuwa barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 316.218 imepotea kwa kutumia mahesabu ya Wizara ya Ujenzi kuwa kilomita moja ya lami inajengwa kwa kiasi cha shilingi milioni mia nane (800,000,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sawa na kusema kuwa barabara ya kutoka Manyoni-Itigi-Tabora (kilomita 264) changanya na barabara ya kutoka Chunya -Makongorosi (kilomita 43) na Barabara ya Tangi Bovu -Goba (kilomita 9) zimepotea kutokana na ufisadi huu.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu yafuatayo kuhusiana na suala hili:-

(i) Fedha hizi zilizokuwa zimetengwa zilitumika kwa ajili ya kufanya shughuli gani? Kwani majibu yaliyotolewa na Wizara na Serikali Bungeni sio yaliyotolewa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(ii) Ni madeni gani yalilipwa kama kweli yalikuwepo au wajanja wachache walijinufaisha na wahusika wamechukuliwa hatua gani mpaka sasa?

(iii) Nini kauli ya Serikali kuhusiana na Ufisadi huu, mbele ya Bunge na Watanzania kwa ujumla.

(iv) Je, tunaweza kuendelea kuamini kauli za viongozi wa Serikali hii ndani ya Bunge kama hii ndio hali halisi?

(v) Nini kauli ya Serikali kuhusiana na Ufisadi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Barabara. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Mwenyekiti, Bodi na Watendaji wa Mfuko wa Barabara kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa uwazi na uwajibikaji. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kutafuta njia bora ya kuongeza mapato kwa Mfuko huu ili uongeze kasi ya kusaidia Ujenzi wa Barabara zetu na matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukusanya fedha za tozo kutoka Makampuni ya Uchimbaji wa Madini ambao ndio waharibifu wakubwa wa barabara zetu kwa kusafirisha mizigo mizito na magari makubwa na kufutiwa msamaha wa tozo hilo kama watumiaji wakubwa wa mafuta, huku wafanyakazi na wafanyabiashara wanatozwa tozo hilo kila wanaponunua mafuta. Kwa kutoa msamaha kwa makampuni haya yanaukosesha Mfuko wa Barabara kiasi kikubwa cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa Barabara. Pamoja na Mfuko wa Barabara kujitahidi kukusanya mapato kwa wingi, ila pia kasi ya matumizi ya fedha hizo kwa ajili ya masuala ambayo sio ya kujenga barabara moja kwa moja imeongezeka sana, kwa mfano, kwa mwaka huu wa fedha kwa mujibu wa randama kiasi cha shilingi bilioni 9.126 zilizotengwa ni kwa ajili ya miradi inayoteklezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (5.5.2.1 Barabara Kuu).

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo Kiasi cha shilingi bilioni 2.460 kitatumika kwa ajili ya matumizi ambayo siyo ya kujenga barabara moja kwa moja kama ifuatavyo:-

(i) Kifungu cha 2326, *training and Technical assistance TANROADS* Shilingi milioni 300.00, hizi ni kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kitaalam kwa wafanyakazi 100 wa *TANROADS*;

(ii) Kifungu 2326, *updating of draft design manual 1989 and economic analysis manuals for TANROADS*, shilingi milioni 300.00;

(iii) Kifungu 2326, vifaa vya maabara, ufuatiliaji na usimamizi wa kazi za ujenzi wa barabara shilingi milioni 500.00;

(iv) Kifungu 2326, kuandaa mpango mkakati wa *TANROADS* kwa kipindi cha miaka mitano shilingi milioni 100.00;

(v) Kifungu 2326, ufuatiliaji na usimamizi wa kazi za ujenzi wa Barabara *TANROADS* shilingi milioni 400.00; na

(vi) Kifungu 2326, ufuatiliaji na usimamizi wa miradi (*monitoring and other related activities*) shilingi milioni 860.00.

Jumla ni shilingi bilioni 2.460.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa barabara za mikoa, fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zitatumika kwenye mambo ambayo sio kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa moja kwa moja wa barabara ni kiasi cha zaidi shilingi bilioni 2.465. Kambi rasmi ya Upinzani, inataka kujua mambo yafuatayo:-

(i) Kwa nini fedha za Mfuko wa Barabara henzielekezwi zote kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara?

(ii) Mbona fedha kwa ajili ya kufuatilia na kusimamia miradi ni nyingi sana wakati kwenye mikataba ya ujenzi fedha za usimamizi wa mradi huwa zipo?

(iii) Je, ni kwa nini fedha kwa ajili ya mafunzo, uandaaji wa nyaraka mbalimbali za Wizara zisitokane na fungu la Serikali Kuu na fedha za Mfuko wa Barabara zikawa ni kwa ajili ya kuwekezwa zote kwenye sekta husika, yaani ujenzi na ukarabati wa barabara na si matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Kama Taifa tunapoteza wastani wa masaa manne kila siku za kufanya kazi ukiwa barabaran sawa na siku 112 za kazi kwa mwaka. Hiki si kiasi kidogo katika nchi maskini inayohitaji maendeleo kwa haraka kuzipoteza barabaran, badala ya kutumika katika uzalishaji na wafanyakazi kulipwa mshahara kamili wa masaa nane ya kazi wakati amefanya kazi kwa masaa manne tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa linapoteza kiasi kikubwa katika ujira, watumiaji wa barabara wanatoa fedha zaidi kufika mahali anapokwenda kwa kuchoma mafuta akiwa amesimama barabaran muda mrefu sana na hasara hii haipimiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

(1) Kasi ya Ujenzi wa Mradi wa *DART* (Mabasi yaendayo kasi Dar) iongezwe ili mradi huu ukamilike kwa haraka kupunguza tatizo la msongamano Dar.

(2) Miradi ya barabara za viungo (*Ring Roads*) ikamilishwe na kutazama barabara mpya zitakazosaidia kupunguza msongamano.

(3) Kutafuta fedha maalum (*Special fund*) hata kwa kukopa kwa ajili ya barabara za Dar es Salaam na kujijenga upya na kujenga barabara za juu (*Fly overs*) badala ya kusubiri wahisani hata kujenga kilomita tatu toka UDA depot/KAMATA junction tunasubiri fadhila na hisani, hii ni aibu kwa Taifa letu.

(4) Upanuzi wa barabara unaoendelea sasa uzingatie mahitaji ya baadaye na si sasa. Kila panapostahili tujenge njia zaidi ya mbili kila upande, tuachane na mazoea ya njia mbili twende njia tatu au nne kila upande wa barabara na jambo hili tunapendekeza lianzesasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa fedha zinazotengwa

katika bajeti za kila mwaka ya Wizara, hatuwezi kumaliza tatizo la barabara za Dar es Salaam. Serikali ichukue maamuzi magumu ya kuwa na fedha za kutosha (*special fund*) kwa tatizo la Dar es Salaam, Mji ambao unakua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali na Wizara hivi sasa kuwasilisha Bungeni mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa kukabiliana na changamoto za kukua kwa Miji ya Arusha, Mwanza na Mbeya na tatizo la msongamano ambao umeanza kujitokeza katika miji hiyo, ili tuweze kujiaandaa mapema, badala ya kusubiri mpaka hali iwe mbaya ndipo tuanze kuchukua hatua za dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujenzi wa daraja hili la Kigamboni Kambi Rasmi ya Upinzani inaipongeza *NSSF* na wadau wengine kwa kuona umuhimu wa daraja hili na kuchukua tahaadhari ya mahitaji ya baadaye kwa kuongeza njia katika kila upande wa barabara hiyo, lakini Wizara inapaswa kujipanga sasa namna ya kukabiliana kuyaondoa magari mengi yatakayokuwa yanatumia barabara hiyo, vinginevyo itakuwa haina tija kwa maana utakwenda kasi darajani unakuja kukwama uhasibu *junction* (*Mandela/Kilwa Road*) na UDA *Depot*(*Mandela road*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maelezo, ratiba na maandalizi ya kukabiliana na changamoto hiyo ili mradi huu uweze kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya ujenzi wa barabara. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, Wizara ilipokea fedha zote 100% kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa kwamba, fedha iliyoombwa haikutumika katika miradi mingi iliyoombewa fedha mwaka 2012/2013 na kutokamilika kwa miradi hiyo hususan barabara za Dar es Salaam kama vile barabara ya Kimara-Kilungule, Mbezi-Malamba Mawili-Kinyerezi, Banana-Tegeta, Kibaoni-Wazo-Goba, Mbezi Morogoro-Tangibovu-Goba na Kimara Baruti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamechoshwa na hotuba za Mawaziri zenyé matumaini, ahadi na maneno mengi huku wakijua na kuamini kwamba, hawatativiza wajibu wao na kulidanganya Bunge na kuwapa wananchi matumaini yasiyotekelvezeka. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri, miradi inayoombewa fedha na kuidhinishwa na Bunge itekelvezwe kwa mujibu wa mpango wa bajeti na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya barabara kuu, kadhalika haijengwi kwa kasi inayotakiwa, miradi mingi ambayo ilikuwa ikamilike mwaka 2012, 2013 na mapema 2014 bado haijakamilika hadi sasa. Ujenzi wa barabara nyingi katì ya hizo umefikia chini ya asilimia 50% ya ujenzi, kama Barabara ya Sumbawanga/Kibaoni, Sumbawanga/Kasanga, Tabora/Nzega, Tabora/Ndono, Ndono/Urambo, Kyaka/Bugene/Kasulo. Manyoni/Itigi/Chaya, Tabora/Nyahua, Korogwe/Handeni, Korogwe/Mkumbara, Mkumbara/Same, Mbeya/Lwanjilo, Lwanjilo/Chunya, Chalinze/Kitumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, orodha ni ndefu, lakini zipo pia ambazo zimejengwa kwa kiwango cha katì ya 45%-70%. Kadhalika orodha ni ndefu kwa ujumla, miradi yetu yote ya barabara haikamiliki kwa wakati ni pamoja na barabara ya Iringa/Dodoma/Kondoa/Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani na Watanzania kwa ujumla wanataka kujua juu ya masuala yafuatayo:-

(i) Kwa nini miradi hii haijakamilika kwa mujibu wa mikataba iliyopo, aidha wanataka kujua hasara inayopatikana kutokana na kutokamilika kwa miradi hii kwa wakati.

(ii) Gharama halisi ya miradi hii hadi sasa imeongezeka kwa kiasi gani kulinganisha na gharama za awali kutokana na kuchelewa kwa miradi hii?

(iii) Zipo taarifa kuwa baadhi ya miradi iliyokamilika na kutumika bado ina madeni, je, inadaiwa kiasi gani na lini Italipwa?

(iv) Watanzania wanataka kujua jumla ya riba na deni tunalodaiwa katika miradi ya barabara ni kiasi gani mpaka sasa na kuna mkakati gani wa kulipa deni hilo?

(v) Serikali itoe maelezo ya kina ni sababu zипi zilizopelekeea kampuni ya *Progressive* kupewa mkataba wa kujenga barabara ya Tunduma/Matemanga/ Kilimasera/ Namtumbo ambayo iligawanywa *lot* tatu na zote kupewa kampuni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi kampuni hiyo haikuwa na sifa ya kujenga barabara, katika nchi za Afrika, nani allitambua, nani allileta nchini, nani aliwasaldia kupata kazi na kwa nini wameshindwa? (*Makofii*)

Je, muda na hasara tunayopata kwa kuchelewa kwa mradi kwa hatua zilizochukuliwa nani analipa na nani kawajibishwa kwa uzembe huu?

(vi) Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara kutoa ratiba na mpango mkakati wa kufungua Kanda ya Kusini na Magharibi kwa barabara ya Masasi hadi Mbambabay. Tabora/Mbeya, Tabora/Mpanda, Mpanda/Kigoma na Kigoma/Biharamulo.

(vii) Ujenzi wa barabara uzingatie michoro, sheria za ujenzi wa barabara na kuondosha mara moja matuta madogo madogo katika barabara kuu, maarufu kama Rasta zinaleta uharibifu mkubwa kwenye vyombo vyya usafiri na inapokuwa lazima, wajenge *Bumps* zenyе uwiano kwa barabara zote na kuwepo alama za barabarani. Hakuna barabara kuu (*Highway*) yeyote duniani iliyo na rasta na *Bumpsila Tanzania*, tunaona *bumps* katika barabara za mijini na si *highway*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani

inaitaka Serikali miradi yetu yote izingatie mpango wa Taifa wa miaka mitano na uwezo wa kifedha wa nchi. Wataalam watimize wajibu wao na wasiwe watumwa wa kauli na ilani za kisiasa; Mwalimu alisema: "Kupanga ni kuchagua," ukishindwa kuchagua huwezi kupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROADS*. Wakala huu ni muhimu sana katika kusimamia na kuendeleza ujenzi wa Barabara nchini. Kwa mujibu wa Taarifa ya ukaguzi wa utendaji ya *PPRA* kwa 2011/2012, inasema kuwa *TANROADS* kwenye kipengele cha kusimamia ubora (*compliance level and Quality Control*) imepewa alama 45 kati ya 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *PPRA* imeshindwa kupata taarifa za kumbukumbu kwamba, *TANROADS* ina mpango wowote wa kusimamia ubora wa kazi kwenye mikataba inayotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwenye kipengele cha mikataba (*compliance on contracts Management*) imepewa alama sifuri (0) kati ya alama 100, kwa maana kwamba *PPRA* hawakuona ushahidi wowote kwamba, Mamlaka imekuwa ikisimamia mikataba kwa bidhaa na huduma zinazotolewa kwa mujibu wa mikataba na Wakandarasi

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba, kwa hali hii bado tutaendelea kushuhudia mikataba mibovu, ujuzi chini ya kiwango, hasara kwa Taifa na kupungua kwa kasi ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Ujenzi kushughulikia upungufu huo na kuondoa dosari zilizopo kwa kupata wataalam wenye sifa, uwezo na weledi katika maeneo yenye upungufu na kutoa fursa za mafunzo kwa wataalam waliopo, aidha uongozi na utawala uimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua barabara vijijini zinasimamiwa na Halmashauri zetu ambazo nyingi hazina uwezo mkubwa wa kifedha na pia hutengewa fedha kidogo na Mfuko wa Barabara kulingana na kazi kubwa wanayotakiwa kufanya ya kuhakikisha kuwa barabara zinapitika katika kipindi chote cha mwaka mzima. Aidha, wana ukosefu mkubwa wa nyenzo na wataalam. Kutokana na umuhimu wa barabara hizi kwa uchumi wa wananchi wetu ambao wanaishi vijijini, kwa mara nyingine tena Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuishauri Serikali na kupendekeza kuwepo na Wakala wa Barabara Vijiijini (*Rural Roads Agency*) kwa ajili ya usimamizi, ufanisi na ujenzi wa barabara bora vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, tutawenza kufungua uchumi wa vijijini kwani kutakuwa na wakala ambaye atakuwa na jukumu la kuhakikisha barabara zinafanyiwa matengenezo na ukarabati kwa wakati na hivyo kurahisisha uchukuzi wa mazao ya vyakula kutoka maeneo ya uzalishaji na kuweza kuwafikia watumiaji wa mazao hayo yakiwa katika hali ya ubora zaidi na hivyo yataweza kuongezewa thamani kulingana na ubora wake. Aidha, tutawenza kuchochlea uzalishaji kwa kiwango kikubwa, kwani maeneo mengi ya vijijini mazao huharibika kutokana na kukosekana kwa barabara na hivyo kuwakatisha tamaa wakulima/wazalishaji. Pia Taifa litakuwa na uhakika wa kwamba barabara/madaraja yatajengwa katika kiwango cha kuridhisha na thamani ya fedha, *value for money*, kuonekana na kupimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la vivuko na madaraja, juhudhi zimefanyika kwa kiwango ambacho siyo cha kuridhisha sana pamoja na changamoto zake. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara kuagiza na kusimamia kwa uangalizi mahususi kuhakikisha madaraja yote yanayojengwa yanakamilika kwa wakati. Ubora na usalama kwa vivuko vyetu vyote nchini uimarishwe, matengenezo yafanyike kwa wakati, vifaa vyta usalama viwepo vya kutosha, pia ukaguzi wa mara kwa mara uimarishwe na uthibiti wa idadi ya abiria na mizigo uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa mahitaji ya kipekee na haraka, Mv Ilagala ni kidogo na chakavu na kimikuwa kikiharibika mara kwa mara. Ni lini kivuko cha uhakika kitapelekwa licha ya kuwepo kwa ahadi nyngi, au kujenga daraja katika mto Malagarasi kama mto Kilombero ili kuondoa adha hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tulishauri kwamba, "Kikosi cha Wanamaji (*Navy*) kinatumika chini ya kiwango. Licha ya kikosi hiki kuwa na wahandisi wa usafiri majini waliobobe, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imikuwa ikitoa zabuni za kutengeneza vivuko kwa wakandarasi wengine kwa gharama kubwa wakati wanajeshi wenyewe taaluma hiyo wapo. Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa zabuni za kutengeneza vivuko kwa kikosi cha wanamaji kwa kuwa wana taaluma hiyo, na pia kwa kufanya hivyo wanapata nafasi ya kufanya mazoezi taaluma zao".

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jukumu la vivuko, madaraja na barabara liko chini ya Wizara hii ya Ujenzi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara kulifanyia kazi pendekezo hilo ili kuangalia ni kwa jinsi gani kamandi hii ya *navy* itakavyoweza kutekeleza jukumu hilo la utengenezaji na ukarabati wa vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha TEMESA ni muhimu sana katika kudhibiti matumizi bora ya fedha za umma katika matengenezo ya magari ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali yanagusa usafirishaji na upo mwanya wa ubadhirifu, wizi na matumizi mabaya katika gharama za uendeshaji wa sekta ya usafiri katika Serikali na kulipa gharama kubwa za matengenezo katika karakana na Makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba:-

(i) Serikali ifanye maamuzi bila ya kuchelewa kukiimarisha kitengo hiki kwa raslimali fedha na watu (wataalamu), nyenzo na majengo ya karakana ili magari yote yatengenezwe kupitia Wakala huu kama ilivyokuwa zamani na kupiga marufuku magari ya Serikali kufanyiwa matengenezo katika karakana binafsi.

(ii) Wakati Serikali inajipanga kutekeleza hilo, kama imeweza kusimamia kuagiza mafuta nchini kwa utaratibu wa *bulk procurement*, Serikali iiwezeshe TEMESA kufanya *bulk procurement* ya matairi ya magari kwa ajili ya Serikali. Jambo hili siyo gumu hata kidogo ili kuwepo na bei inayofanana, na ubora wa matairi kwa magari ya Serikali/ Halmashauri badala ya kila Idara, Wizara, Taasisi kununua kwa bei wanayoikuta sokoni na yenyе kupishana kwa kiwango kikubwa na ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita 2012/2013 Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake ya bajeti alisema kuwa Wakala wa Majengo uko katika mchakato wa ujenzi wa nyumba 10,000 katika Mikoa yote kwa ajili ya kuishi watumishi wa umma. Aidha, alisema kuwa katika mwaka huo wa fedha, Wizara kupitia Wakala wa Majengo, ilikuwa imepanga kujenga nyumba 2,500 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi huo zilikuwa tayari zimepatikana, kama mkopo kutoka kwenye benki za ndani ambao TBA ilikuwa imeomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri alisema katika hotuba yake ya bajeti kwamba, naomba kunukuu: "Aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Majengo, Tanzania imepanga kujenga nyumba 2,500 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara." (ukurasa 159 aya 230)." Hakika maneno haya yalikuwa faraja kwa watumishi na matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujuu majengo hayo 2,500 ambayo yalikuwa tayari yametengewa fedha kwenye bajeti iliyopita,

yamejengwa katika Mikoa gani na maeneo gani hapa nchini? Je, nyumba hizo wamepewa watumishi wa kada gani na ni vigezo gani vilitumika katika kugawa nyumba hizo kwa watumishi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kumekuwepo na malalamiko na kutokuridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Wizara na Taasisi zake hususan *TANROADS* kutowalipa wananchi fidia stahiki za haki na kwa wakati. Wananchi hawaridhishwi na kauli za viongozi wa Wizara hususan katika suala la kuwalipa wananchi fidia kwa mali zao wakipisha miradi mbalimbali za ujenzi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya ujenzi na hasa barabara za lami ni maendeleo kwa jamii pana na Taifa. Kwa mwananchi wa kawaida, maendeleo kwetu ni nyumba/shamba/ardhi yake hata kama nyumba ni ya miti, tofali za tope na kuezekwa kwa nyasi, kwake ni maendeleo na siyo barabara ya lami. Unapomvunja au kumnyang'anya ardhi yake, unamzidishia Mtanzania huyo umasikini kwa gharama ya maendeleo ya jamii pana. Kwa sababu yoyote ile, kwa namna yoyote ile, haki yake ni lazima. Narudia, ni lazima alipwe. Kitendo chochote cha kuvunja au kunyang'anya mali ya mtu ye yote ni dhuluma, kama inafanywa na mtu au Serikali ni dhuluma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kamwe haiwezi kukubali kushangilia au kushiriki katika dhuluma hii. Tunasema walipeni haki zao hawa Watanzania masikini amba mali mnazoziharibu na kuwanyang'anya ndiyo maendeleo na ustawi wa maisha ya familia zao. Kama kweli Serikali ya CCM inavyodai maisha bora kwa kila Mtanzania, basi boresheni maisha ya Watanzania hawa kwa kuwalipa stahiki zao ili waweze kupata makazi au ardhi mbadala. Waondoleeni Watanzania hawa mifadhaiko ya maisha na chuki dhidi ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula, nguo, malazi ni haki za msingi kwa kila binadamu. Hata kama ni kibanda ndiyo makazi yake, hakuna mtu ye yote mwenye haki ya

kumnyang'anya mwagine haki hizo bila ya kufidia au kumpatia makazi mbadala. Kilio cha fidia, fidia zisizostahiki, fidia za upendeleo na kutokulipwa ndiyo kilio cha Watanzania kila kwenye mradi wa ujenzi hususan barabara. Orodha ya wananchi wanaolalamika ni ndefu, kila palipo na mradi na hata waliokuwa tayari kupisha mradi kwa ahadi ya kulipwa wanaendelea kusumbuliwa na urasimu wa *Tanroads*, Wizara na Hazina; walipeni wananchi haki zao mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mihimili ya dola kila mmoja ufanye kazi bila kuingiliwa na kuheshimika. Wizara hii na *TANROADS* haipo juu ya sheria, inatakiwa kuheshimu sheria hata pale panapotolewa tangazo (*notice*) la kukusudia kuishtaki Serikali, kabla Serikali haijawasilisha majibu katika vyombo vyta haki, Wakala wa Barabara anavunja nyumba za Watanzania masikini, tena wenye hati miliki ya viwanja zilizotolea na mamlaka za Serikali hii kabla shauri kusikilizwa Mahakamani. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa haki za raia, kuheshimiwa utu wake na kusikilizwa. Wizara hii isiwaongezee Watanzania umasikini. Wakaazi wa Minsukumilo na Mpanda Hotel ni wahanga wa ubabe huu wa kutoheshimu mamlaka nyingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa sheria ni jambo moja, kusimamia sheria ni jambo lingine. Uungwana na lugha njema ni zaidi ya hayo, kwa kuwa Wizara ilishindwa kutambua na kuweka mipaka ya maeneo yao toka sheria ilipotungwa mwaka 1926. Leo wanamlaumu nani kuvamia maeneo yao? Sasa ndiyo wanakumbuka kwamba, wana maeneo ambayo tayari ni makazi ya wananchi, si kisingizio cha kuwapora haki zao. Kama wangeliweka mapema mipaka ya hifadhi ya barabara, wananchi wasingelijenga, wangeheshimu mipaka hiyo iliyouwepo, vinginevyo, Wizara inakwepa uzembe wake kwa kuwaadhibu Watanzania masikini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulipa fidia kwa wote, siyo watu wa Dar es Salaam tu. Msiweke matabaka, mnawalipa fidia watu wa Dar es Salaam, watu wa pembezoni huko Mpanda, Karagwe, Tunduru sijui na wapi hawalipwi. Watanzania wote wana haki

sawa mbele ya sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani hairidhiki na Watanzania masikini kutolipwa fidia katika miradi mbalimbali ya barabara nchini, fidia stahiki na kwa wakati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru, na pia niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mpanda Mjini kwa kuwa na imani kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Arfi kwa hotuba yako kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kuhusu Wizara ya Ujenzi.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba kipindi kilichopita wakati Mheshimiwa Arfi ameingia hapa Bungeni alikuwa na *afro* yenye nywele nyeusi tii, lakini sasa sijui nini kimetokea! Kweli kazi ya Ubunge ngumu! Mimi pia niliingia na *afro*, lakini leo hata nywele moja naitafuta, siiioni. Hii kazi ni ngumu! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana. Kwa muda huu tutapata wachangiaji kadhaa. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, kama uko kwenye orodha, jitahidi kuwepo kwa sababu ukirukwa jina itakuwa vigumu sana kupata nafasi, kwani maombi ya wachangiaji ni mengi sana katika hii Wizara na ningependa kadri iwezekanavyo watu wapate nafasi ya kuchangia. Kama tunavyoju, Wizara hii ni kubwa, wameomba bajeti ya Sh. 1,226,000,000,000/=. Sasa mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge na atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyogera.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyio mbele yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Magufuli na timu yake katika Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. Endeleeni, kazeni buti,

twende mbele. Kazi inaonekana na mwenye macho haambiwi tazama. Hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa mpya wa Simiyu nina ombi ambalo tumelileta Wizarani kuititia Bodi ya Barabara ya Mkoa. Kwa sababu huu ni Mkoa mpya na mtandao wa barabara katika Mkoa huu ni mpya, ni vyema tukauangalia kwa umakini. Tumependekeza barabara inayoanzia sehemu ya Magu kuja Sayaka, kwenda Salama – Kasoli – Nguliati – Bariadi kuelekea Gambasingu kwa ndugu yangu Mheshimiwa Cheyo, Kisesa – Mwandoya mpaka Mwanhuzi. Hii tukiendelea nayo na kazi nzuri inayoendela katika daraja la Sibiti tunaunganisha barabara ya Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka pale Sibiti unakwenda Kiomboi mpaka Misigiri au unaweza kuja mpaka Iguguno. Hii ni *short route* kabisa ya kwenda Singida. Pia tunataka tuunganishe na Mkoa jirani wa Arusha kutoka Mwanhuzi – Sibiti unaelekea Matala – Mang’ola – Oldiani – Karatu – Mto wa Mbu, tayari uko Arusha. Kwa hiyo, hilo ni ombi letu na tunaomba Wizara ilishughulikie mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nashukuru kuona fedha zimetengwa kwa ajili ya barabara ya Bariadi – Lamadi. Lakini huu ni mwaka wa nne tunajenga kilomita 71.8. Haya ndiyo nasema tujitahidi kukamilisha yale ambayo tumeyaanzisha kwa sababu unapochelewa gharama zinakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu, Mheshimiwa Arfi amelisema vizuri sana juu ya fidia kwa sehemu ambazo barabara hizi zinapita. Ni vyema hawa wananchi ambao wameguswa, wana haki ya kulipwa fidia, barabara imewafuata, kama ilivyotokea pale kwangu Dutwa na maeneo mengine ya barabara hii. Naomba Serikali iwatendee haki kwani wamevumilia vya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika eneo lingine. Ni kweli nimeona fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara niliyoisema ya kutoka Karatu – Odeani - Matala - Mwanhuzi - Lalago - Mhunze mpaka Kolandoto. Tumekuwa tukitenga fedha kidogo kidogo tangu mwaka 2008. Lakini naomba sana safari hii angalau kazi ambayo imepangwa kufanyika katika barabara hii tudhamirie kweli ifanyike na yenyewe iweze kufungua eneo hilo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunganisha hapa kwa upande wa ukanda huu, kile kiungo cha kutoka Usagala kuja Kisesa, ile *by pass*, tufanye kila linalowezekana; kwa hali ya Mwanza sasa hivi yale malori na mizigo mikubwa inayopita pale, ndani ya Jiji la Mwanza, jamani haiingii akilini mwangu kama ina mantiki. Tujitahidi, najua kuna tatizo la fidia, lakini tukiongea vizuri na wananchi hawa tukawalipa fidia, sidhani kama itakuwa tatizo. Pia *up grading* ya barabara kutoka Nyanguge mpaka Musoma, tuna kipande kile ambacho tumekianza, lakini hii barabara sasa hivi ina mawimbi mengi mno. Naomba Serikali iliangularie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara kutoka pale Makutano kuelekea Butiama kwenda Nyamuswa kwenda Nata – Mugumu – Loliondo mpaka Mto wa Mbu; tukifungua ile barabara, mimi nasema ukanda ule ni lazima tuufungue kama Serikali ilivyodhamiria. Fedha zimetengwa kwa usanifu huo, lakini tukamilishe hii kazi na baadaye tuhangaike kutafuta fedha. Lakini barabara ya Nyamuswa – Bunda – Mwibara – Kisorya – Nansio, ni vyema haya tukayaona kwa sababu ukishafungua ukanda ule utakuwa umefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana kwa eneo moja ambalo nasema ni la kiuchumi, tumelitengea fedha kwa ajili ya usanifu, lakini huu ukanda maalum wa kilimo wa SAGCOT ukitoka Kidatu ukaja Ifakara ukateremka mpaka Lupilo, Malinyi mpaka unakuja kuteremka Lumecha, Songea Mkoani Ruvuma hiyo. Ni ukanda ambao kwa kweli ni *grain basket* ya nchi hii. Nasema tujitahidi kwa uwezo wetu wote ili tuweze kuifungua hiyo njia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana kusikia barabara ya Mtamba Swala mpaka Mangaka, twende kwa rafiki yangu Injinia, maana ukitoka Mangaka – Lumesule kuelekea Tunduru, kipande kile jamani ambao tumetembea Tanzania hii, tuwatendee haki Watanzania hawa. Nia ni nzuri, lakini kama fedha ni za wengine nakubali, lakini tujitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nasema tufanye kila tunachowea kufungua kwa upande wa Magharibi, ningependa nianzie huku Mbeya; tumeanza vizuri Mbeya – Lwanjilo – Chunya – Makongorosi, twende sasa tunapanda Kambi Katoto twende mpaka Ipole twende mpaka Sikonge, Tabora twende mpaka Ndala na Nzega. Ndiyo utakuwa umekamilisha ndoto ya kuufungua ukanda huo. Mtu anayetoka Mbeya kwenda Mwanza, siyo lazima azunguke njia yote ile, lakini pia ni eneo zuri sana kwa biashara.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa wale Wabunge ambao hawajawafahamu Wabunge Maseneta, huo ndiyo uchangiaji. Unachangia kwa nchi, siyo ukisimama unaongea Jimbo lako, parokia, parokia, mwanzo mwisho. Mheshimiwa Chenge, endelea. (*Makofii*)

MHE. ANDREW M. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nimelisema hilo kwa sababu ni muhimu.

Sasa nikienda upande wa Magharibi, napongeza kazi nzuri ya Serikali inayofanyika kule, maana kuanzia Manyoni – Itigi kwenda Tabora kazi inafanyika jamani. Sehemu zote kwenda Kidahwe kuititia Kaliua tunafika huko. Lakini mimi naiangalia Nyakanazi – Kakonko mpaka Kibondo, ningelipenda kweli angalau, maana upande wa Kigoma - Kidahwe tumewaonjesha wananchi lami, lakini Nyakanazi – Kakonko – Kibondo kwa rafiki yangu Engineer Chiza, tuanze huko ili hawa watu na wenyewe tuwape matumaini, badala ya kuanzia huko kwingine maana na wenyewe ni Watanzania lakini angalau lami wameiona. Lakini hawa wa maeneo yale bado hawajaiona. Lakini maeneo yale hawajafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, la mwisho, hizi fedha za bajeti zinakuja kidogo kidogo. Nilikuwa najaribu kuangalia na amelisema vizuri sana Mheshimiwa Arfi kwamba barabara hizi tunazijenga kwa gharama kubwa sana. Sehemu kubwa ya madeni haya ni *penalties* za kuchelewa kumlipa mkandarasi na Mshauri. Kwanini tusifikirie mpango tukaongea na benki hizi, kwa sababu tunajua bajeti ya Serikali inakuja, ukiongea na benki una-/leverage, fedha zako zile za mwaka ukawaambia mimi nachukua mkopo huu kwa masharti ambayo tutaelewana ili *certificates* zinapoiva unawalipa wale Makandarasi na fedha za Serikali zikija unailipa benki kwa *rate* ambayo mmekubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Andrew Chenge kwa kutuwekea msingi mzuri sana wa mjadala unaoendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Agripina Buyogela, atafuatia Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza kabisa, naomba niwashukuru na kuwapongeza wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Vijiji kwa ushirikiano mkubwa na kwa namna wanavyonikubali kamanda wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niwapongeze sana Wizara ya Ujenzi kwa mara ya kwanza. Tangu nimeingia Bungeni siku zote nimekuwa ninalia na Wizara ya Ujenzi kila hotuba yao inapowasilishwa. Leo angalau wamepanga Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Nyakanazi. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maandiko matakatifu yanasema; "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Lakini pia yapo mengine yanasema: "Waheshimu watu wenye mamlaka." Ni maandiko hayo. Ujenzi wa barabara ya

Kidahwe – Nyakanazi ni ahadi ya Mheshimiwa, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninataka kujua na nipate majibu sahihi kutoka kwa Serikali, ni lini ahadi hii ya kiongozi ambaye ametajwa kwenye maandiko matakatifu itakamilika kuhusiana na ujenzi wa barabara ya Kidahwe - Nyakanazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema hayo kwa sababu Shilingi bilioni 10 ni fedha kidogo sana kwa kujenga barabara yenye kilomita 300. Ninahitaji wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho, atuambie ni mpango mkakati gani waliouweka wa kuhakikisha wanapata fedha za nje au mahali kokote ili kuhakikisha wanatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Serikali ya awamu ya nne ya kujenga barabara ya Kidahwe – Nyakanazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema mpende jirani yako kama nafsi yako. Kigoma tuko katikati. Ukiangalia kulia ndiko anakotoka Kiongozi Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukiangalia kushoto ndiyo anakotoka Waziri wa Ujenzi, ni jirani yetu. Sasa tunataka kuona tumsemee na mzee wetu Kiongozi wetu hapa Bungeni. Barabara ya Mpanda - Kasulu, inakamilika lini? Msituchonganishe mwisho tukakiuka maandiko matakatifu. Ukiangalia Mpanda ndiko anakotoka Kiongozi wa Serikali; Kigoma, Kasulu nilishawaambia hapa Bungeni, kule Jimboni kwangu wapo wananchi ambaao hawajui rangi la lami. Rangi ya lami inafananaje; hawajawahii kuiona kule Jimboni kwangu.

Kwa hiyo, ukiona napiga kelele hapa kwamba barabara itoke Mpanda ifike Kasulu, barabara ya lami itoke Kidahwe kwenda Nyakanazi, ninatafuta urahisi wa kwenda Jimboni kwangu kuwashawishi wananchi watoke kule wakifika Kasulu Mjini wajue rangi ya lami Mheshimiwa Magufuli. Leo miaka 50 ya uhuru bado kuna Watanzania ambaao hawajui rangi ya lami. Naamini ujumbe umefika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimesema leo naipongeza Wizara ya Ujenzi na naamini

sitakuwa na mengi ya kuzungumza, kwa sababu leo sili sana; mmeshanionyesha dalili, hata kama ni kunyonya kidogo, angalau siwezi kufa kwa niaba ya wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshawasilisha maombi, mimi wenyewe nilileta barua kwa Meneja Mkuu wa TANROAD, lakini pia Mkurugenzi wangu wa Halmashauri alileta barua. Kwa hiyo, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri ina barua mbili za maombi kuhusu barabara ya Makele - Kitanga ambayo mpaka leo hii tunaongea hakuna gari yoyote ambayo inaweza ikatoka Kasulu, Makele ikaenda Kitanga. Kule kuna Watanzania na mkijua Kitanga ipo mpakani; mimi nikienda kuhutubia Kitanga Warundi wanakuja kunisikiliza kwenye Mkutano wangu. Lakini huko kuna kijji cha Makele, Nyarugusu, Herushingo, Kigaje, Kitanga wote tumewaweka kwenye kisima ambao hawana usafiri wowote wa uhakika panapotokea tatizo. Wakati tukijua kabisa kwamba kule ni mpakani, mpaka ambao hauziliwi na kitu chochote, Warundi wanafua mto Malagarasi, Watanzania tunafua mto Malagarasi.

Naomba kilio hiki kwa niaba ya wananchi hao niliowataja mkisikie ndugu zangu. Najua siku zote mmekuwa mnatuambia na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ni msemajii mkuu wa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikifu. Naomba sasa kama imesikia isikie kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema sitaongea mengi, lakini naomba nitoe ombi mapema kwamba tunategemea kuanza ujenzi wa barabara. Ni vizuri mahali patakopita barabara, ule usanifu ufanyike mapema ili majumba yale yatakayopangwa kubomolewa, wale watu wataarifiwe mapema ili kuepusha vurugu. Kama ulishaona mahali pengine wanalalamika, usisubiri mahali unapotegemea kwenda kuanza ujenzi, nao waanze kulia kama wale. Sasa inakuwa ni utaratibu tu uliozooleka kwamba Serikali italipa, Serikali italipa, lakini hakuna namna Serikali inayopanga utaratibu wa kuweza kupunguza hizi kelele za wananchi wakati mnapofanya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisimamie kwenye kauli yangu kwamba sisemi mengi, ni vibaya nikipigiwa kengele ya pili. Nakushukuru sana na Mungu akubariki. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Buyogera, nakushukuru sana Mheshimiwa Kamishna. Sasa Mheshimiwa Halima Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Abdulkarim Shah ajiandae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami nitaongea kwa kadri uwezo utakavyoruhusu lakini na muda utakavyoruhusu vilevile.

Kwanza, nianze na barabara ya Mwenge/Tegeta Kibaoni. Hii barabara ni mradi mkubwa wa Kitaifa, lakini kuna changamoto moja kubwa ambayo kama tusipolangalia kwa makini tunaweza tukakuta kwamba barabara hii ambayo imejengwa kwa mabilioni ya Shilingi, Shilingi bilioni 88 kwa ujumla wake inaweza ikapotea na maji. Kwanza, kwa aina ya mwinuko ambao huko katika hilo eneo kunahitaji mapokeo mabaya na maji ambayo yanatoka maeneo ya Goba huko, Jimbo la Mnyika. Lakini kwa jinsi barabara inavyojengwa sasa hivi, hali iliyopelekea mvua iliyonyesha miezi kadhaa iliyopita, pale maeneo ya Mbuyuni barabara ilikatika na pale maeneo ya Afrikana vilevile barabara ilikatika. Sasa mimi kama Mbunge nilipeleka maombi kwa Mkurugenzi wa *TANROAD* kumtaka ahakikishe kwamba anajenga mifereji ya mapokeo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nikamshauri kwamba, kwa kuwa eneo la Afrikana kuelekea Salasala kuna maji mengi sana yanashuka, wakati Serikali ya Tanzania; kwa sababu naambiwa katika mkataba na Wajapan hakujajumuishwa ujenzi wa *service road*. *Service road* inabidi zijengwe kwa fedha za ndani. Sasa nilikuwa naiomba Serikali na namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa ujenzi wa *service road*, katika yale maeneo yenye mapokeo makubwa Afrikana, Salasala pale kwa kiasi kikubwa sana, mijenge hata mita 50 mbele za lami kuelekea ndani. Kwa sababu

mnafahamu ile barabara ya Afrikana kwenda Salasala ni barabara ya Halmashauri. Lakini katika kuokoa hii barabara yetu kuu na kwa kuwa *TANROAD* wana fedha nyingi, ni muhimu waende hatua moja mbele, lakini ile mifereji ya kule mbele kuweza kuleta maji huku chini, liwe jukumu la Halmashauri. Sasa tumeshaandika barua, tumeleta maombi kwenu, tunaomba myafanyie kazi ili zile Shilingi bilioni 88 zisipotee bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili *ringroads*, hizi barabara za pete; Jimboni kwangu ni katika maeneo ambayo yamebainishwa kama sehemu ya kupunguza foleni Mkoa wa Dar es Salaam. Lakini katika miaka yote, kama mitatu au minne iliyopita, tukija kwenye bajeti utaona barabara ambazo zitajengwa kwa lami, ziko kwenye mipango ya kujengwa kwa lami kama barabara za pete, utakuta barabara ya Tegeta Kibaoni, Wazo na Goba. Utakuta barabara ya Samaki, Wazo na Goba. Sasa ahadi hizo zimekuwa hazitekelezeki. Mwaka 2012 zilitengwa Shilingi bilioni 10 hapa, lakini ukiangalia kwenye barabara za Jimbo la Kawe hakuna chochote cha maana kilichofanyika, kuanzia pale Samaki, Mtongani, Kibaoni kwenda Wazo. Sasa hivi kutokana na mvua zilivyonyesha na hizi barabara zote zinahudumiwa na *TANROAD* hali siyo nzuri.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba hizi fedha ambazo zimetengwa sasa hivi Shilingi bilioni 28, nijue kwenye Jimbo la Kawe kuna mgao kiasi gani? Kwenye hiki kitabu cha Bajeti cha Mheshimiwa Waziri wanaeleza barabara nyingi hadi watu tunachanganyikiwa. Ukija kwenye utekelezaji, unashindwa kuhoji kipi kimekwenda wapi, kwa sababu zimetajwa barabara kibao. Kwa hiyo, mimi nataka kwa wananchi wangu wa Kawe kwa sababu ndio wamenileta hapa, tujue kama tuna kitu ama ndiyo imekula kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine nataka nijue kama kuna mpango wowote wa kuboresha ile *Old Bagamoyo Road*. Kwa sababu Halmashauri tulitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Maandazi *Road* ambao inaingiliana na

hiyo barabara ya *Old Bagamoyo Road* ambayo siku hizi nasikia inaitwa Mwai Kibaki. Sasa tumesitisha ule mpango tukiambiwa kwamba Serikali mnataka kuijenga *Old Bagamoyo Road* kuipanua, kwa hiyo tusije tukatupa fedha chini. Sasa nataka njue kama huo mpango upo na kama upo utaanza lini? Ili kama haupo, nikaihimize Halmashauri zile fedha tulizotenga kwa ajili ya barabara ya *Maandazi Road* Msasani zitekeleze wajibu wake au zifanye kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ni suala la Wakala wa Majengo. Mheshimiwa Waziri mwaka 2011 nilileta barua kwenye Wizara yake nilimkabidhi aliyekuwa Naibu wake Mheshimiwa Mwakyembe, Katibu Mkuu wa Wizara anajua na Mheshimiwa Waziri anajua kuhusiana na nyumba za lilikokuwa Shirika la Saruji ambalo lilibinafishwa mwaka 1997.

Kwa nyaraka ambazo mimi ninazo na kwa mkataba wa mauziano, zile nyumba za Shirika ambazo zinakaribia nyumba 150 kwa mantiki ya nyumba za makazi lakini pamoja na majengo mbalimbali kulikuwa kuna *dispensary*, vituo vya Polisi na majengo mbalimbali ya kijamii; kukawa kuna michakato ambayo inaendelea kwa sababu mkataba wa mauziano umelibainisha kwamba mwekezaji alipewa kiwanda, zile nyumba zimerudi Serikalini, na mwaka 2007 zile nyumba zilikabidhiwa *TBA*. Lakini tunavyozungumza mpaka sasa, licha ya kwamba kuna nyaraka mbalimbali, viambatanisho zaidi 14 ambavyo vinaonyesha kwamba kulikuwa kuna hatua za kugawa ile hati ili igawanywe mara mbili; Serikali ibaki na upande wake na kiwanda kibaki na upande wake. Sasa hivi mwenye kiwanda anadai kwamba lile eneo lote ni lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri aniambie kwa sababu nyaraka wanazo tokea mwaka 2011 na walikuwa wanapata kigugumizi sana na hapa tuna barua mbalimbali kutoka Wizara ya Miundombinu hii barua yenye Kumb. Na. 114/228/01/18 ya tarehe 07 Novemba, 2007 kutoka *PSRC* ikisema nyumba zimekabidhiwa *TBA*. Lakini vilevile kuna kumbukumbu ya Kikao cha Waziri Mkuu

ambacho kilifanyika tarehe 15 Februari, 2005 ambayo inasema kwamba kutokana na mkataba wa mauzo nyumba ama *residential at Wazo Hill* ziliondolewa na kukabidhiwa Shirika la Saruji Tanzania na hatimaye nyumba hizo zilikabidhiwa PSRC na ambazo baadaye zikakabidhiwa TBA.

Vilevile kuna nyaraka kutoka Kiwanda chenyewe ya tarehe 01 Oktoba, 1997 yenye kumbukumbu TPPCGM/12 ambayo na wao wanakiri kwamba hati Na. 42336 inatakiwa igawanywe mara mbili. Lakini vilevile kuna barua nyingine ambayo imetoka kwa Wakili wa Kiwanda cha Twiga kwenda *City Bank* ambayo inasema kwamba wanarejesha hati Wizara ya Ardhi ili itumie mamlaka yake kuigawa hiyo hati mara mbili na viwanja husika ni Na. 1, Na. 4 na Na. 7. Sasa nilikuwa naomba nipate kauli ya Serikali kwa sababu Watanzania ambao wamekuwa wanaishi kwenye hizo nyumba wamekuwa wanasumbuliwa sana. Najua Mheshimiwa Magufuli anakumbuka ile dhambi ya kuuzwa kwa nyumba za Serikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima tutakuomba hizo nyaraka kama zipo, kama baadaye utatupatia tutashukuru.

MHE. HALIMA J. MDEE: Hizi nyaraka zipo, Mawaziri ambao tunawaamini sana; Mheshimiwa Mwakyembe na Mheshimiwa Magufuli wanazo toka mwaka 2011, mali ya Serikali inataka kuchakachuliwa, wao wamekauka. Sasa sijui ule mkakati wa zile nyumba zilizouzwa za Serikali zilizozua malalamiko mengi kuna kitu kilicho jificha kuhusiana na hizi nyumba karibu 151. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha atuambie, kama waliziuza walimtumia utaratibu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala zima la hawa wasimamizi ama Bodi ya Usajili wa Makandarasi. Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumza; kuna nyaraka zinazoonyesha lile jengo ambalo lilivunjika lilitakiwa lijengwe ghorofa tisa. Nyaraka ambayo imetoka kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ghorofa tisa. Kuna nyaraka nyingine inaonyesha mawasiliano baina ya *Ladha Construction*

Limited, yule Mkandarasi na kwenda kwa Mkurugenzi wa *National Housing* wakizungumzia ghorofa 12. Lakini vilevile kuna nyaraka nyingine kutoka kwenye hiyo Kampuni ya *Ladha Construction* ikimwandikia Mkurugenzi wa *National Housing* kumwambia kwamba amepewa kibali cha kuongeza ghorofa kutoka 12 mpaka 16 na Manispaa ya llala. Sasa nilitaka kupata kauli ya Waziri; kwa kuwa Waziri Bodi yake ya Usajili ya Makandarasi pamoja na mambo mengine, inatakiwa isimamie Wakandarasi; kwa hiyo naomba Waziri ajibu kuhusiana na haya. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee. Nakushukuru sana na kama ikikupendeza, tutashukuru kama hizo nakala zitakuwepo, ili anapokujibu muwe mnaongea lugha moja.

Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Lakini kwa sababu dakika ni chache, niende moja kwa moja kwenye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuangalie ukurasa 15 wa hotuba ya Kambi ya Upinzani. Naomba ninukuuu ile para ya kwanza tu.

"Mheshimiwa Spika, wananchi wamechoshwa na hotuba za Mawaziri zenye matumaini, ahadi na maneno mengi huku wakijua na kuamini kwamba hawatatimiza wajibu wao na kulidanganya Bunge na kuwapa wananchi matumaini yasiyotekelezeka. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri miradi inayoombewa fedha na kuidhinishwa na Bunge itekelezwe kwa mujibu wa mpango wa bajeti na siyo vinginevyo". (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namweka Mwenyezi Mungu mbele nikizungumza hapa ili Mungu aamue nani mwongo kati ya Serikali yetu na hii *statement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwa miaka mitano. Nimeisimamia hii Wizara kwa miaka mitano. Naomba ni sema ukweli, kama tunasema ukweli, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa sana katika ujenzi wa barabara kwenye nchi hii. Tumwogope Mwenyezi Mungu na tuwe na hofu. Mimi mwenyewe tarehe 30 na 31 Oktoba, 2012 niliandamana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, tulikuwa na Waziri Magufuli. Tukaenda Rombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikiliza sasa. Tulipofika Rombo tulikwenda kufungua barabara ya kilomita 30; barabara ya lami. Barabara imejengwa kwa kiwango kikubwa! Barabara ya mfano ule nilliona Malaysia juzi. Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo lile ni mtu mwadilifu sana, alisimama, alitoa hotuba nzuri, alimsifu Mheshimiwa Rais, aliisifu Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hakuwa mnafiki. Wachaga ni watani zangu, hawajui kucheza ngoma. Siku ile walicheza ngoma mno! Wachaga walicheza ngoma na walicheza mpaka Msanja, leo unasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijengi barabara, unasema kauli kama hii! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kesho yake japo nilirudi nikalala kijijini kwangu ni mbali; kesho yake asubuhi niliungana na Mheshimiwa Rais tukaenda Hai. Tuko na Mheshimiwa Waziri Yule! Mimi nasema kwa vielelezo! Tumekwenda Hai kwenye Jimbo la Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Rais akafungua barabara ya Kwasadala - Masama kilomita 12 barabara ya lami.

Baada ya hapo, Mheshimiwa Freeman Mbowe akasimama mbele ya jukwaa akamsifu Mheshimiwa Rais, lakini akamwomba Mheshimiwa Rais amwongezee kilomita tano za lami na ile barabara aliyoiomba wala siyo *trunk road*. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongeza zile kilomita tano na akamwambia Mheshimiwa Magufuli ongeza hizo kilomita tano. Jamani tumwogope Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi naipongeza sana, Mheshimiwa Magufuli hongera, Naibu Waziri hongera, *Chief wa TANROAD* hongera! CCM tembeeni kifua mbele! Kazi imefanyika. Sasa nirudi jimboni kwangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hata kwangu imefanya kazi. Lakini naomba mjue kwamba asilimia 62 ya wananchi wangu wanaishi milimani. Barabara za milimani ni korofii, halafu kasoro kubwa ambayo labda hamjui, wananchi wangu wa milimani walijenga barabara zile wenyewe. Walianza kuzijenga wenyewe kwa mikono yao, hao mababu zangu walijenga kwa mikono yao! Kwa hiyo, wananchi wa Jimbo la Same Mashariki Milimani wanastahili pongezi sana jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Magufuli Waziri wangu, mimi nakuja kwa unyenyekevu, silalamiki. Nakuja kwa unyenyekevu! Kuna barabara inaitwa Hedaru – Vunta – Miamba. Barabara hii inaanzia Miamba, Sambweni, Mrinji, Ivuga, Mweteni, Bwambo, Vugwama, Idaruu, Kirangare, Njagu, Vunta mpaka Papaa. Hii barabara ni korofii sana. Ina miamba, ina mawe makubwa, ni barabara ngumu sana. Wananchi wanaishi kwenye hivi vijiji vyote ni tarafa nzima hii mnavyoiona. Wao maisha yao ni kubeba tangawizi vichwani kutoka Vunta mpaka Miamba kwenye kiwanda ambacho kimejengwa na wananchi. Siku nzima ndiyo atafikisha ule mzigo na inakuwa vigumu nywele kuota.

Barabara hii Mheshimiwa Magufuli nakunyenyekea kwa sababu najua wewe ni mchapakazi, una huruma. Barabara hii Halmashauri ya Wilaya ya Same hawana uwezo wa kujengwa na ndiyo maana hata siku moja hii barabara hajapita kitu chochote cha kuirekebisha. Mimi ni mwaka wa saba Mbunge wa Jimbo lile, nime-*takeover* kutoka kwa kaka Daniel Yona miaka kumi, nimemwuliza, anasema hata magari yenu ya kutengeneza barabara, haliwezi kupita kule. Barabara ile hata usemeje, siyo barabara ya kujengwa na Halmashauri ya Wilaya. Serikali yangu ya Chama cha

Mapinduzi nawasihi kwa unyenyekevu, nimeshafanya taratibu zote, barua imeshafika kwa Katibu Mkuu. Pandisheni barabara ile daraja iwe tu ya Mkoa japo wananchi wangu waweze kusafirisha mazao yao kupeleka kwenye kile kiwanda ambacho ni mali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sizungumzi kwa kulalamika. Huenda Mheshimiwa Magufuli, Naibu Waziri, Meneja wa *TANROADS* hawajafika. Lakini wakifika watajua wale wananchi wanastahili ile barabara ipandishwe daraja. Nawasihi kwa unyenyekevu, naishi Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kazi mnayoifanya ni kubwa, ringeni. Serikali ringeni nawaruhusu, lakini haka kabarabara nisaidieni kapande daraja tu. Kakikshakuwa *TANROAD*, basi wananchi wangu watakuwa wameokoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwape hadithi fupi sana. Siku moja nilikuwa naendesha gari kwenye barabara ya Kinondoni, pale makaburini. Nilikuwa nimewachukua wanawake wawili ndani ya ile gari. Tulipofika makaburini, mmoja akasema hivi; jamani lile kaburi zuri, halafu limewekwa marumaru, halafu limewekwa maua, na ni zuri sana. Akalisifu yule mwanamke. Yule mwingine akauliza kwani ni kaburi la nani? Mwenzie akamwambia lile ni kaburi la yule hawara wa mume wako, aliyefariki juzi. Akasema, kumbe ndiyo maana kunanuka hivyo! Yule yule aliyesifu lile kaburi, alipojua ni la mke mwenzie akasema linanuka. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, endeleeni kujenga barabara. Hakuna siku mtasifiwa kwamba mnafanya kazi. Watu hawamwogopi Mungu! Lakini naunga mkono hoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi endeleeni kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Huyo ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Mheshimiwa Abdulkarim Shah unafuata.

MHE. ABDUKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kunipa uwezo, afya na kuweza kusimama leo hapa kuweza kutoa maoni yangu au maombi kwa Wizara yetu hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, binafsi naomba nitumie fursa hii kuungana na Wabunge wenzangu kuipongeza Wizara kwa maana ya Serikali kwa mambo yote wanayoyafanya kwa nchi yetu. Hakika na upande wetu wa Mafia mambo mengi yanafanyika na kawaida ya binadamu, kuna hadithi inayosema mtu asiyeweza kumshukuru binadamu mwenzake kwa jambo lolote lile liwe dogo la kheri, kama hawezi kushukuru kwa hilo, basi hata Mungu mwenyewe ambaye haonekani hawezi kumshukuru. Kwa hiyo, jamani tuangalie kama alivyosema Mheshimiwa Anne Kilango, tumwogope na Mungu katika haya maelezo tunayoyatoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifungua kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 97 kuna mambo mazuri kabisa ambayo yameelekezwa na kutamkwa kwamba Mafia itapata barabara ya lami ya kilomita 14.3. Ni jambo la kushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Mafia. Lakini juu ya hayo, bado nazidi kuiomba Serikali kwamba mambo mengi mazuri huwa wakati mwингine vitu vidogo tu vinaleta hitirafu. Sasa naomba sana, tayari mkandarasi ameshafika, kampuni ya *CHICO* iko pale, vifaa vimeshafika, lakini fidia bado watu tumekuwa na wasiwasi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuambie fidia ile ya wale watakaoathirika na ujenzi wa barabara hii watalipwa lini ili tuweze kutoa muda wa wao kuhama au kuja kupata haki yao kulingana na taratibu zilivyowekwa. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inatoka Kijiji cha Utende kuja katika uwanja wa ndege wa Kilindoni wa mji wa Mafia. Lakini naomba niseme, uwanja mzuri uliojengwa na Serikali yetu pamoja na ufadhili kutoka *MCC* kwa maana

ya *Millennium Challenge Account Tanzania*, yote haya yanaweza yakaharibika kwa jambo moja dogo sana. Pale mwisho wa uwanja wa ndege ambapo ndipo kuna barabara hii inapita, barabara hii imekatika, daraja limechukuliwa na maji na pameharibika na hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, barabara hii itakuwa mtihani na bahati nzuri angalia kwenye picha utaliona lile, nimeliweka ili uweze kujionea mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilete ombi rasmi haraka iwezekanavyo ili hili eneo barabara yetu iwe nzuri lakini pia kuokoa mabilioni ya hela yaliyopelekwa kujenga uwanja ule wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, leo tarehe 13/5/2013 naomba sana na kwa heshima zote kaka yangu Mheshimiwa Magufuli na Serikali kwa ujumla, naleta ombi rasmi kwako kupitia Wizara yako na kueleza kuwa gati la Mafia linakamilika wakati wowote kuanzia sasa hivi. Lakini baada ya gati hilo kukamilika, tatizo kubwa ambalo tunalo ni usafiri wetu wa bahanini. Hivyo naomba katika program zako, kupitia vitengo vyako, basi sasa, hivi vivuko ulivyokuwa ukivitamka sehemu mbalimbali, Mafia tunahitaji kivuko. Kwa sababu mpaka sasa tunatumia mashua na boti za kienyeji kuvusha watu na hivi juzi tu, leo siku ya nne imetokea ajali, mashua ilikuwa inasafiri kutoka Mafia kuja Kisiju, imezama, ilikuwa na watu wanane, lakini saba tuliweza kuwaokoa. Mmoja, hadi hivi sasa hajapatiwana, mpaka hivi tunavyoongea.

Kwa hiyo, ni athari kubwa tunayoipata sisi wananchi wa Mafia na mali zetu. Naomba sana katika program yako tujue kwamba leo tarehe 13/5/2013 nalileta ombi hili rasmi kwako, Mafia sasa tuweze kuiangalia kwa mpango wa kuleta kivuko kwa ajili ya usafiri wa uhakika na salama kwa wananchi na mali zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ya kusema. La mwisho, nakuomba sana Mheshimiwa Magufuli, Naibu wako, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mtendaji wa *TANROADS, Road Fund Board* na Wakurugenzi wote wa Wizara, niko tayari kuchukua ndege keshokutwa au baada ya wewe kumaliza, twendeni

Mafia ukaone hali halisi ili utakapofika pale uone haya tuliyoyasema uweze na uweze kuchukua hatua za haraka kuweza kuokoa au kuboresha yale ambayo utayaona kule katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mafia, nazidi kutoa shukrani kwa Serikali, yangu ni hayo, sina zaidi kwa Wizara hii, bali kutakia kila la kheri viongozi wetu hawa, yale tunayoyaomba yaweze kutekelezwa. Nasema naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Owenya, dakika tano.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa wananchi wanaonisikiliza, naomba watambue kwamba ujenzi wa barabara ni kodi zao zinatumika bila kujali itikadi ya Chama kwa sababu kila Mtanzania analipa kodi na kodi hizo zinatengeneza barabara. Hivyo kwa wachangiaji kukaa hapa na kusema kwamba barabara zinajengwa na Chama cha Mapinduzi, siyo sahihi kwa sababu wananchi wote tunachangia katika ujenzi wa barabara hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kuanza niungane na Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kukubali kufungua barabara ya *Old Mosh*/kwa ajili ya watalii kuanza kupanda mlima. Lakini kwenye barabara ile, kuna ile inayoanza Kiboriloni kupitia Kikarara mpaka Kidia, hatimaye unafika *National Park*. Barabara ile ni mbovu sana na ni katika ya barabara ambazo ziko katika ahadi za Mheshimiwa Rais. Walisema barabara ile wataitengeneza kwa lami ambayo ni kilomita 10 tu, ni kama Shilingi bilioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinaonekana ni nyingi, lakini tutambue kwamba katika biashara ya utalii pia inaiingizia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. Ni mategemeo yangu Mheshimiwa Waziri atatenga fedha kwa ajili ya barabara hii kwa ajili ya watalii wale na kuweza kuongeza fedha na pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara hizi, *TANROADS* wanaweka matuta ambayo hayapo kwenye *standard*. Matuta yale ni makubwa sana na mengine ni makubwa kama kaburi. Sasa napenda kuuliza *TANROADS*, hakuna *standard* ya matuta hata kama wanabidi waweke matuta? Kwa sababu matuta yale yanaleta ajali, magari yanaweza kupinduka na ni hatari kwa maisha ya Watanzania.

Naomba nzungumzie kidogo Wakala wa Magari, *TEMESA*. *TEMESA* ipo karibu kila Mkoa na *TEMESA* ilianzishwa ili magari ya Serikali yaende yakafanyiwe *service* kule na kutengenezwa. Lakini badala yake sasa hivi gari ya Serikali ikataka kutengenezwa inabidi iende *TEMESA* ipate kibali iende ikatengenezwe kwenye *garage* za kampuni binafsi. Mimi napenda kujua, ni kiasi gani ambacho kimeshatumika kwa kutengeneza magari nje ya *TEMESA*? Kwa sababu fedha zile zinazotumika kutengeneza magari nje zingeweza kuimarisha ile mitambo, hata kama ni kuweka teknolojia mpya na kuleta hao Wachina waje kuwafundisha Watanzania, kwa kiasi kikubwa tunge-*save* fedha nyingi sana ambazo zingeweza kutusaidia sisi Watanzania na kuokoa fedha ambazo zinakwenda kutajirisha hao watu wa nje badala ya kazi hizo kufanyika na Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu bado muda unaniruhusu kidogo, naomba niongelee suala la msongamano katika Jiji letu la Dar es Salaam. Tatizo hili limekuwa ni sugu, watu tumekuwa tuki-*complain* kila wakati hapa! Kama Waingereza wanavyosema, *time is money*, lakini tumeona Watanzania wanapoteza zaidi ya masaa manne wakiwa njiani. Mvua zikinyesha Dar es Salaam, ina maana watu wanapoteza saa sita mpaka nane wakiwa njiani. Sasa mimi niiulize Serikali, kwanini isishughulikie kwanza zile barabara za pembeni au *feeder roads?* Wakizitengeneza kwa lami, watu wengi hawatatumia barabara moja na kuongeza msongamano. Lakini sasa hivi barabara inayotumika ni moja, msongamano ni mkubwa. Kwa mfano, barabara ya Mwai Kibaki, tumekuwa tukiizungumzia mara nyingi, kila siku wanairekebisha lakini tatizo liko palepale na Serikali ni hii hii moja.

Mheshimiwa Naibi Spika, mvua zikinyesha maji yanajaa tele! Tatizo ni nini? Kwanini tusiangularie jinsi ya kuhakikisha maji hayasimami tena pale *TMJ?* Imekuwa ni kero, kile kidaraja kiko pale, kuna siku ambayo itakuja kutokea ajali. Hivi tunasubiri mpaka ajali itokee ndiyo waweze kutengeneza lile daraja? Ni kitu kidogo sana kile. Kwanini hawaweki daraja katika ile sehemu ya *TMJ hospita?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naungana na Kambi ya Upinzani kwamba, naomba tupate Ripoti ya Tume ya Mheshimiwa Lowassa ambayo iliundwa wakati ule kuangalia ubora wa majengo katika Jiji la Dar es Salaam. Ile ripoti imeishia wapi? Au mtaunda tena *team* nydingine kuangalia ni nini kilichofanyika kwa hili jengo kubwa kuanguka? Maana mimi naamini kabisa kwamba Wizara ya Ujenzi ikishirikiana na Wakandarasi wa ndani wana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy, umeunga mkono au?
Ahsante sana.

*(Hapa Mheshimiwa Lucy Owenya hakusikika
kujibu chochote)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tutaendelea kuchangia tutakaporudi saa kumi na moja na wachangiaji wetu ataanza Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Eng. Eugen Mwaiposa na Wabunge wengine watafuata kama itakavyokuwa kwenye orodha yangu. Naomba tu yule ambaye yumo kwenye orodha, awepo kwa sababu akirukwa itakuwa ni vigumu kurudiwa tena.

Tangazo la Semina. Mheshimiwa Mama Anna Abdallah Mwenyekiti wa *TWPG* anaomba Waheshimiwa Wabunge wanawake wote kwamba ile semina yenu

inaendelea tena leo saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Nasikia baadhi ya Wabunge na wadau wengine wanalamika *TWPG* mnabagua. Kwanini hamwaliki?

Baada ya tangazo hilo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge liliahirishwa
mpaka Saa 11.00 jioni)*

(Saa 11.00 Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kuhusiana na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli - Waziri wa Ujenzi asubuhi ya leo.

Kama nilivyokuwa nimesema kabla ya kuahirisha asubuhi kwamba wachangiaji wetu tutaanza na Mheshimiwa Herbert Mtangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Mheshimiwa Herbert Mtangi, tafadhalii.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza jioni hii ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ukweli kwamba Wizara ya Miundombinu ni mionganii mwa Wizara zinazojitahidi sana hapa nchini. Mimi kwa nafsi yangu nasema katika tano bora, wao wanaongoza. Sina uhakika kama wapo zaidi ya hawa watano, lakini katika tano bora wao wako juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme, tulikubaliana kimsingi kwamba utekelezaji wa shughuli za barabara, kwanza tuangalie barabara za kitaifa, hayo makubaliano ni dhahiri. Mimi nilikuwepo katika Kamati ya Miundombinu, nimetembea sehemu nyingi za Tanzania, nimeona utekelezaji

wa ujenzi wa barabara katika ngazi hiyo ya barabara za Taifa; nenda Kaskazini, nenda Kusini, nenda katikati, Tabora na wapi barabara zinatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimkumbushe tu Mheshimiwa Magufuli kwamba zipo nchi ambazo zinatengeneza barabara vizuri sana hapa duniani. Nilipata nafasi ya kutembelea nchi ya Thailand na Malyasia hivi karibuni na kazi wanayofanya ni ya ajabu. Sikuona jina lako Mheshimiwa Magufuli kama ulitembelea kule. Lakini nataka nitoe mfano mfupi tu, barabara zap jinsi zilivyo.

Kwa mfano, barabara tuliyokuanayo ya Mandela Airport Mandela mpaka Mjini pale, wenyewe wanayo barabara kama hiyo, lakini juu ya barabara hiyo wana barabara nyingine mbili juu ya hewa, moja ya gari na nyingine treni ambayo inatoka Airport, itakwenda mpaka mjini na itapita Samora Katikati ya magorofa, inakwenda mpaka *Ocean Road*, hiyo ni njia ya barabara pamoja na treni. Ninaomba uende kule Malaysia na Thailand.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini najua dhamira na nia ipo. Hata kama tuna mipango, lakini bila kuweka dhamira na nia ya utekelezaji, hatutafika popote. Katika Wizara yako, nia na dhamira tunaiona ipo, tunategemea kazi itakwenda vizuri. Sasa baada ya kuona tumefanya kazi vizuri katika upande huu za Kitaifa, mwelekeo wetu sasa ni katika barabara za Mkoa. Hatujamaliza zile za Kitaifa. Najua wenzetu kule Babati bado barabara zao hazijakamilika, bado sehemu nyingine za Kusini hazijakamilika, lakini dhamira ipo umekwishaanza, msimamie itekelezwe.

Tukija katika barabara za Mkoa, sasa nirudi katika Jimbo langu la Muheza. Barabara za Mkoa zipo tano, lakini leo nitajikita katika barabara kubwa mbili. Nitajikita katika barabara ya kutoka Muheza kwenda Amani katika sehemu kubwa mbili; moja ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ahadi hii imetoka mwaka 2005, ameirudia tena mwaka 2010, lakini utekelezaji wake bado.

Hata hivyo, naona dalili zifuatazo ambazo zinaonyesha zipo dhamira za kutekeleza ahadi hiyo. Kwanza tunafanya ule upembuzi yakinifu.

Nilimwandikia Mheshimiwa Waziri barua nilipoambiwa kiasi cha fedha kilichopelekwa kilikuwa ni kidogo na hakitoshelezi, lakini baadaye namshukuru Mhandisi wa Mkoa wa Tanga alinikhakikishia kwamba fedha zimeongezwa. Kwa hiyo, ule upembuzi yakinifu kwa lengo la kuweka lami barabara hiyo unaendelea. Sasa ninaomba unifahamishe kwa uhakika kabisa, kwamba kweli upembuzi yakinifu unafanyika; lakini je, ni kweli utakamilika mwaka gani, na ni lini fedha zitatengwa ili kazi hiyo ya kuweka lami barabara hiyo ya kutoka Muheza kwenda Amani ikamilike?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magufuli hajawahi kufika katika barabara hiyo. Yeye miaka ile ambayo aliwahi kuwa Waziri wa Miundombinu wakati huo, alinisaidia kupata fedha ya kuweka lami kilomita moja na nusu ya hiyo barabara ninayoizungumzia leo. Tangu ameondoka, hazijatengwa fedha tena za kuweka lami katika barabara hiyo. Leo amerudi tena, na kauli yangu ni hiyo kwamba sasa unapata nguvu pia ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kuitekeleza. Naomba nifahamishwe ni lini upembuzi yakinifu utakamilika na lini lami itaanza kuwekwa katika barabara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara hiyo pia nimesema nitazungumzia katika maeneo makubwa mawili. Eneo la pili ni kwamba bado barabara hiyo inahitaji matengenezo makubwa kabla ya kufikia hatua ya kuwekewa lami. Alikuwepo mkandarasi, wote tunamjua, nilimsema sana hapa, ameondolewa. Sasa barabara inasimamiwa na *TANROADS* wenyewe, wameweka Wakandarasi wawili. Mmoja ni katika sehemu ya barabara inayotoka *Boza Junction* kuja Muheza na Mkandarasi huyo huyo pia ndiye anayeendelea na sehemu kubwa ya barabara ya kutoka Muheza kuelekea Amani. Yupo Mkandarasi mwingine ambaye anatoka eneo la Kibaoni – Amani kuelekea kwa Mkoro amshamba ya chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima niseme kwamba utendaji wa kazi bado haujaridhisha. Utendaji bado hauridhishi! Leo nashukuru nimepigilwa simu wiki iliyopita na wananchi wangu wa kule sehemu za Amani, wameniambia wamemwona mtu mmoja yuko kule anafanya ukaguzi wa hiyo barabara. Wao hawakumjua ni nani, lakini mwisho wa yote, nimetambua kwamba aliye kwenda kule ni Mheshimiwa Wanyanche ambaye ni Kiongozi wa hali ya juu sana katika Mfuko wa Barabara. Kwa nini amekwenda kule? Amekwenda kule nina uhakika, kwasababu amesikia hali ilivyokuwa mbaya ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia, Mheshimiwa Waziri mwenyewe bado hajafika kule. Aliyewahi kwenda kule wakati huo alikuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mwakyembe. Siku aliye kwenda kule ilifika mahali nikawaomba wananchi wangu, nikasema hebu sasa mruhusu aishie hapa, kwa sababu hali ya hatari huko mbele kama ataendelea kwenda lakini tunasahau Amani ndiko inakotoka chai kwa wingi na inailetea fedha za kigeni Taifa hili la Tanzania, leo tunaiachia Amani izame, uchumi wetu utakuwaje kama hata Watanzania wenyewe hatuthamini fedha za Kigeni zinazozalishwa katika eneo kama lile la Amani?

Mheshimiwa Naibu Spika, maziwa yanaharibika barabarani, magari hayawezi kwenda pamoja na mazao mengine mengi, tunajisahau, wataalamu na usomi wetu! Mimi naomba nchi hii tuendelee kuiendesha kwa hekima na busara.

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji wa ile kazi kwa Wakandarasi hawa wawili, ninaomba uimarishwe. Katika kipindi kilichopita, fedha zilitengwa, Wakandarasi walikwenda. Huyu wa Barabara ya Amani kweli alijitahidi, alipanda kule kabla ya mvua hazijanyesha ili aanze kazi mlimani halafu ashuke bondeni. Lakini yalitokea matatizo, walifika kule, mtaalamu mmoja wa Wizara ya Maliasili akamfukuza Mkandarasi kwa kumyima kifusi. Sasa utatengenezaje barabara kwa kiwango cha udongo bila ya kifusi, wakati mimi kama Mbunge, nilikuwa nina barua ya

ridhaa ya kuruhusu kifusi kuchukuliwa kwa ajili ya utengenezaji wa barabara ile. Lakini akafanya maamuzi yale ye ye peke yake bila hata kunishirikisha, na Mkandarasi yule akaondoa vifaa akaenda eneo lingine la barabara leo mvua inanyesha barabara haipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mhandisi Mkuu wa Mkoa, tulishirikiana na amefanya jitihada, tumepata maeneo na tatizo la kifusi pengine litakuwa limekwisha. Lakini barabara ingekuwa pengine imekwishatengenezwa, sasa hajatengenezwa. Naomba sana fedha za kutosha zitengwe ili barabara hiyo itengenezwe iweze kupitika kabla ya utekelezaji wa kuweka lami barabara hiyo.

Vilevile na barabara hii ya *Boza Junction* kuja Mkuzi hadi Muheza, ni sehemu ya hiyo barabara. Tunaomba fedha za kutosha zitengwe. Nimetazama katika viambatanisho, nimekuta kuna maeneo yanaonyesha kuna fedha. Lakini kiwango cha fedha ambacho naona zimewekwa, hazitoshelezi kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka kabla hajawekwa lami. Kwa kweli watu wa Muheza wanasikitishwa sana kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa mara ya pili mfululizo hajatekelezwa. Kilomita zenyewe ngapi? Wala hazitishi! kilomita 34 tu ndiyo zinatuhangaisha miaka 20 sasa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alione hili kuwa ni muhimu na kuhakikisha kweli kwa heshima ya Mheshimiwa Rais ahadi ile inatekelezwa. Lakini kwa heshima pia ya mchango wa fedha za kigeni zinazotoka kwenye mashamba makubwa sana ya chai ambayo ni makubwa hapa nchini, nenda utapata data zote, fedha za kigeni tungezikusanya fedha hizo zingetosheleza kutengeneza barabara hiyo. Lakini kwasababu ya Utaifa, fedha hizo zinakwenda katika sekta nytingine, lakini tunaisahahu Amani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana. Inatosha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Herbert Mtangi. Kama nilivyosema mwanzo, mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Eugine Mwaiposa.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Naomba kuahidi kwamba nitajaribu kuwa mzalendo kama ulivyoelekeza na nitafuata hatua za *Senator Chenge* katika kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Bunge hili limeanza nimekuwa nikifuatilia kwa karibu sana hotuba za wenzetu Wapinzani na hata leo hii nimemsikiliza kwa makini sana Msemaji aliyekuwa akiwasilisha kwa niabaya ya wenzetu wa Upinzani. Nasikitika kusema kwamba wenzetu wamekuwa wakilia na kunug'unika tu tangu Bunge linaanza mpaka leo hii.

Sasa ndugu zangu, Waheshimniwa Wabunge, sote tunaelewa; mimi natoka kule kwetu Mara, Kiswahili sikijui zaidi, lakini Mheshimiwa Shekifu atanisaidia, kuna msemo unasema, "Ukiona watu wazima wanalia, ujue wamekamatwa pabaya." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba wenzetu wamekamatwa pabaya. Kasi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi siyo kasi waliyoitegemea, ni kazi kubwa kweli kweli. Naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara hii ya Ujenzi kuititia kwa Jemedari wetu makini sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote walioko katika Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Naomba niseme kwamba wenzetu nyie mmetubeba kidedea, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana kwa utekelezaji mzuri wa llani yetu ya Chama cha Mapinduzi na hasa ile Ibara ya 62 mpaka 72 mmeitekeleza kwa umakini mkubwa. Lakini nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri

sana anayoifanya na kubwa ya kuzunguka duniani kote kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha na kuendeleza miradi yote ya barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Bunge hili Tukufu, kwa niaba ya Wakuu wa Wilaya wote na Wakuu wa Mikoa wote, naomba nimwahidi Mheshimiwa Rais, lakini Mheshimiwa Waziri kuwa sisi Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa tutaendelea kusimamia llani ya Chama cha Mapinduzi vizuri, na tutaendelea siku zote kuwaambia wananchi siku zote kuwaambia wananchi ukweli wa namna ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza ahadi zilizopo kwenye llani.

Mimi ningependa kuongelea zaidi ahadi za Mheshimiwa Rais, lakini kama muda utaniruhusu, ningependa pla kuongelea Wakala wa Majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze sana, kwa upande wa ahadi za Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika, lakini zipo ahadi nyingi kwa upande wa madaraja, kwa upande wa vivuko zimetekelvezeka kwa asilimia mia kwa mia. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, hakuna sababu yoyote ya kulalamika. Ahadi zimetekelvezwa vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natumie fursa hii kuleta salamu za wananchi wangu wa Mkoa wa Mara, wamenituma nije nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutimiza ahadi aliyowaahidi ya kuwapatia kivuko cha Rugezi – Kisorya, lakini vilevile kivuko cha Musoma – Ukerewe. Wananchi wangu wa Mkoa wa Mara wamefurahi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuahidi kwamba nitachangia kwa mtindo wa *Zigzag*, naomba vilevile nichukue fursa hii kuleta salamu za wananchi wa Wilaya yangu ya Meatu, wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuikamilisha ahadi yake na kuwapatia daraja la Mwanuzi. Daraja hili la Mwanuzi ni daraja ambalo limewasaidia sana wananchi wa Wilaya ya Meatu japokuwa yapo marekebisho

madogo ambayo yanatakiwa kufanyika na tayari nimekwishaongea na Injinia Kenti, Injinia mahiri sana anayesimamia Wakala wa Barabara wa Mkoa wangu wa Simiyu na tayari tumeshapata fedha Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kupitia Bunge hili Tukufu, umetupatioa fedha kwa ajili ya matengenezo ya dharura kwenye radaja lile. Kwa hiyo, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nashukuru sana kwa ujenzi wa daraja la Mto Sibiti. Daraja hili ni muhimu sana kwa kuufungua Mkoa wa Simiyu, lakini vilevile ni daraja muhimu kwa wananchi wote wanaotoka na kuingia kwenye Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie sasa utekelezaji wa ahadi wa Rais kwa upande wa barabara. Naomba Waziri afahamu, hapa kidogo kuna kigugumizi. Tangu nimekaa hapa Bungeni, sijawahi kuona majibu mazuri na yaliyosawia yakitolewa kuhusiana na ahadi za Rais kwa upande wa barabara. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, sote tunakubaliana, wenzetu wa upinzani wamekusafia sana na sisi wenzako tunakusifia zaidi, tunakuomba ulichukue suala hili kama suala la dharura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo ahadi ya Mheshimiwa Rais ya siku nyingi sana kwa wananchi wa Wilaya ya Butiama. Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa atatupatioa barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 194 kutoka Musoma Mjini kwenda Mugango, kwenda Makojo, kwenda Bukima mpaka Kusekela. Mheshimiwa Waziri unaifahamu vizuri barabara hii; barabara hii inapoteza fursa nyingi sana za kiuchumi kwa Mkoa wa Mara. Nakuomba leo utakapokuwa unahitimisha uniambie ili wananchi wa Wilaya ya Butiama waweze kuelewa ni nini hasa kinaendelea kwenye ahadi hii ya Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kumekuwa na utekelezaji wa kigugumizi na hasa kwa barabara zinazotakiwa kushirikiana kati ya Wizara ya Ujenzi lakini TAMISEMI. Tumeahidiwa; kila Mbunge hapa anaweza

kusema; barabara za lami kwenye Miji yetu. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Meatu katika Mji wa Mwanuzi, mpaka leo hii tunadai kilomita tatu za lami tumeahidiwa na Mheshimiwa Rais na hatujui zitatekelezeka lini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika Mji wa Bunda, kwenye Jimbo la Mheshimiwa Wasira ameahidiwa kilomita tatu lakini mpaka leo hii hajajulikana ahadi hiyo itatekelezeka lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya barabara ya Kisorya – Bunda.

Katika ukurasa wa 95, nieleze tu wasiwasi wangu. Barabara hii siyo tu kwamba inatoka Nansio, Kisolya Bunda, barabara hii inatoka Nansio Kisolya Bunda mpaka Ikitu au Nyamswa. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba inapoanza kukatwakatwa vipande namna hii, hata kama vipande hivi ni kwamba fedha iliyotengwa ni kwa ajili ya vipande hivi, lakini tunaiomba kwenye kitabu itokee barabara nzima, itaje mpaka Nyamswa inakoishia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana nia ya Serikali kwa kutaka kuufungua Mkao wetu mpya wa Simiyu. Naomba Mheshimiwa Waziri utambue kwamba Mkao wa Simiyu ni moja ya Mikoa ambayo ina fursa nyngi sana za kiuchumi na ingeweza kuchangia kwenye pato la Taifa kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia katika kitabu cha hotuba kwenye barabara za Mikoa na *trunk roads*, kusema ukweli Mkao wa Simiyu bado haujafunguka. Ningombaa sasa Mheshimiwa Waziri, ipo barabara ilianza kufanyiwa upembuzi yakinifu

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Filikunjombe.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nashukuru kupata nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa mimi sina hofu wala sina kipingamizi, wala sidhani kama kuna mtu ambaye atapinga kabisa kwamba Wizara hii ni kati ya Wizara ambazo zimechapa kazi sana na kwa kweli Wizara hii inafaa sana kupongezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pungezi zangu hiso, naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia barabara zilizopo katika Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ukonga asilimia 99 barabara zake ni za changarawe, lakini ni barabara ambazo zinawasumbua sana wananchi kutoka huko kuja Mjini. Nadhani wiki mbili zilizopita nilisimama hapa nikaeleza tatizo la barabara za Ukonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara kwa sababu angalau naona barabara ya kutokea Ukonga, Mombasa, Kivule kwenda mpaka Msongola ziko kwenye mpango. Lakini hapo hapo namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba kuna barabara yangu moja ambayo tulipokuwa tumekaa kwenye vikao vya *Road Board*, nafikiri ilikuwepo. Sasa hapa sijui kama imesahaulika au vipi! Ni hii barabara ya kutokea Banana inaingia Kitunda, Kivule inakwenda kukutana na hiyo

barabara niliyomaliza kuitaja, zinakwenda kuungana na barabara kubwa ya Msongola. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba barabara hiyo kama imesahaulika iwekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napongeza pia kwamba barabara hii tayari Serikali imekwishaonyesha nia ya kujenga kwa sababu daraja la kuanganisha Kivule, Msongola, Majohne na Msongola tayari limekwisha kuanza kazi na linajengwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana sasa hiyo barabara ya kutokea Banana iweze kuingia kwenye mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko barabara nydingine pia ambayo siioni hapa, barabara ya kutoka Chanika, inakwenda mpaka Nzasa halafu inakwenda kuungana na barabara nydingine za Kisarawe. Barabara ile hali yake ni mbaya mno! Kwa hiyo, naomba pia kama hii barabara imesahaulika kutokana na jinsi ambavyo tulikuwa tumeleta maombi yetu kutoka kwenye *Road Board*, basi nayo iweze kuwekwa kwenye mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la barabara ambazo zimewekewa mpango wa kupunguza foleni. Nimekuwa naongea sana kuhusu hizi barabara. Ukiangalia uhalsia wa jinsi bajeti zinavyokwenda, barabara zinazohesabika kwamba ni za kupunguza foleni, nyangi zinasukumwa kwenye maeneo ya Kinondoni, Kawe na sehemu nydingine kama vile Ubungo na kadhalika. Barabara nydingine za Ukonga kwa kweli zimesahaulika sana. Lakini ni barabara ambazo zingesaidia sana kupunguza foleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, foleni sasa hivi katika Jimbo la Ukonga zimekuwa ni kubwa sana hasa baada ya kuweka zile taa za barabarani. Lakini pia barabara imekuwa ni moja tu, hii ambayo inayotoka *Airport* kuelekea mpaka Msongola.

Kwa hiyo, kama tungeweza kufungua barabara nydingine za ndani, nadhani zingeweza kusaidia sana kupunguza foleni katika Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba wapo watu ambao wamehamishiwa Jimbo la Ukonga wakapelekwa katika maeneo ya Pugu Kinyamwezi pamoja na Viwege. Wale watu hawana barabara kabisa! Najua na ninatambua kabisa kwamba hili ni jukumu la Manispaa, lakini Manispaa za Dar es Salaam zimelemewa. Asilimia 95 ya barabara za Dar es Salaam ni za changarawe na barabara zote hizo zimeachiwa Manispaa za Dar es Salaam. Inakuwa ni vigumu sana kuweza kutekeleza au kufanya kazi barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, pamoja na kwamba kuna utaratibu wa kubadilisha barabara hizi ili ziweze kwenda Serikali Kuu, zile taratibu kusema kweli tayari zimekwishapitwa na wakati. Hebu sasa Serikali ije na utaratibu mpya wa hizi barabara ili angalau mzigo uweze kupungua kwenye Manispaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukisema kwamba barabara ambayo inatakiwa ipande daraja ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa au Wilaya, utakuwa unaumiza sana Jiji la Dar es Salaam. Barabara zilizo nyingi zinakosa vigezo hivyo, lakini ni barabara za msingi sana na muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongelea barabara hizo, naiomba Serikali itafute utaratibu mpya wa kuangalia upya changamoto ambazo zipo kwenye miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam ni Jiji ambalo tunaweza kusema ndiyo nchi. Kwa hiyo, naomba Serikali ije na mpango wa kuliangalia vizuri zaidi Jiji hili la Dar es Salaam hasa katika changamoto ambazo zipo za foleni na miundombinu kwa ujumla. Nadhani hata Kamati iliongelea jambo hili kwamba unapoangalia katika nchi zinazotuzunguka, wakatoa mfano wa Nairobi, kuna mpango mkakati maalum kwa ajili ya kushughulikia Jiji lile na kweli wamefanikiwa sana. Kwa hiyo, naomba sana, hebu tuweke

utaratibu wa kulishughulikia Jiji la Dar es Salaam kwa sababu asilimia kubwa ya mapato ya nchi yanapatikana pale ili kuweza kurahisisha kuongeza mapato hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nije na wazo kwa Mheshimiwa Waziri lakini na Serikali kwa ujumla wake. Kwa sababu kumekuwepo na changamoto kubwa sana, siyo Jimbo la Ukonga tu, lakini ni nchi nzima, changamoto ya Miundombinu. Ni kwa nini Serikali sasa isije na mpango wa kuwaruhusu wawekezaji wa ndani wafanyabiashara wakubwa waweze kuwekeza kwenye barabara, ili baada ya barabara hizo kujengwa, wale waweze sasa kukusanya fedha kwa kipindi kitakachokuwa kimekubalika mpaka watakapomaliza kulipa deni lao hilo ambalo wametumia kujenga barabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, njia hii imesaidia nchi nyingi sana na ni njia ambayo ingeweza ikalitoa Taifa hili kwenye changamoto kubwa tulizonazo za barabara.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika akishirikiana na Watendaji wake aweze kuja na mpango huo ili hata zile barabara nyingine ambazo ni za ndani ambazo zingeshughulikiwa na Manispaa ambazo hazina fedha za kutosha, basi waweze kujitokeza watu ambao wana fedha zao ili waweze kujenga na baadaye *ku-recover* fedha zao kutokana na matumizi ya barabara hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba tu Waziri, chonde chonde, hizo barabara zangu tatu nilizozitaja naziomba zirudi kwenye mpango kama ambavyo zilikuwa zimepangwa kwenye *Road Board* ya Dar es Salaam na barabara hizo naomba tu nirudie, ni barabara ambayo inaanzia Chanika kuelekea Nzasa, halafu inakwenda kutokea Kisarawe. Barabara zote hizo tatu niliziomba ili zipandishwe daraja, lakini naona ilishindikana.

Barabara nyingine ni barabara ya kutokea Banana inakuja Kitunda, Kivule inakwenda Msongola. Barabara

nyingine ni hiyo ya Banana ambayo ambayo imekwishajengwa kwa lami sasa kilomita moja, na inakuja mpaka Mazizini, Kivule inakuja kuungana na hiyo nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Eugen Mwaiposa. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Deo Filikunjombé, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kusema machache kuhusu Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kwa niaba ya wananchi wa Ludewa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Magufuli na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana Waziri wa Ujenzi Dkt. Magufuli kwa sababu mwaka 2012 kwa mara ya kwanza ulitutengea fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na *detailed design*, fedha ile ikawa haitoshi; nimepitia kitabu hiki na makabrasha ninaiona Ludewa inatokea kwenye maeneo kadhaa. Mimi kwa niaba ya wananchi nimeridhika, na kikubwa kwa kweli ni ile dhamira ya kweli ya kuhakikisha kwamba ile barabara ya kutoka Njombe - Ludewa hadi Manda nayo inajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya lami kutoka Njombe, Itoni, Ludewa, hadi Manda ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Ludewa kwa sababu maendeleo yetu ya kijamii tukiwa na barabara ya lami yataongezeka kwa sababu tutaweza kusafiri kwa urahisi zaidi, lakini pia tutaweza kusafirisha mazao yetu kama vile chai, mbao, kilimo pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya lami kutoka Njombe hadi Ludewa mpaka Manda ni muhimu na itachangia sana katika uendelezaji wa miradi ya Liganga na Mchuchuma. Lakini pia barabara hii ya kutoka Njombe hadi Ludewa itachangia sana katika kukuza utalii katika milima ya *Livingstone* na zile fukwe zinazovutia sana kule Manda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wenzetu wanasherehekea miaka 50 ya uhuru na kushangalia, sisi Ludewa tulikuwa tunaangalia tu, tulikuwa tunatazama tu. Lakini kwa hakika niseme bayana, sisi kwetu leo tukipata barabara ya lami ndiyo na sisi tutaanza sasa kusherehekea miaka 50 ya uhuru. Vile vile niseme bayana, ni bahati mbaya sana katika Mkoa mzima wa Iringa, Wilaya zote zina barabara za lami. Ukienda Kilolo Wilaya mpya, ukienda Iringa Mjini, ukienda Mafinga, ukienda Iringa Mjini, ukienda Njombe ni Wilaya moja tu ndiyo ilikuwa haina lami. Kwanza hii siyo haki na huu siyo upendo. Sasa kwa haya ninayoyaona kwenye kitabu hiki na kwa haya yanayotokea na sisi sasa tutaanza kufaidi na matunda ya uhuru na hatimaye wenzenu mtakapokuwa miaka 50 sisi tutakuwa mwaka wa kwanza au wa pili, lakini basi siyo neno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa nashukuru kwa yanayotokea, kikubwa ninachokiona hapa ndani, tunaomba sana sasa upembuzi yakinifu ukamilike. Nimeona fedha nyine zimetengwa mwaka huu. Tuongeze kasi, mimi najua Mheshimiwa Magufuli ukiamua unaweza, hata kuifanya barabara hii ijengwe kwa *design and build* wakati mmoja, najua ukiamua unaweza. Tunachokitaka sisi Ludewa, tunaomba kauli yako sasa ni lini ujenzi wa lami utaanza, na hasa ukizingatia kwamba miradi ya Liganga na Mchuchuma iko tayari na itaanza kutekelezwa hivi karibuni?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Ludewa kuishukuru sana Wizara na Kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutujengea barabara ya kutoka Ludewa hadi Lupingu. Tulipewa fedha mwaka 2012 hazikutosha, nimeona kwenye

kitabu hiki tumetengewa fedha nyingine kwa ajili ya kukamilisha barabara ile iende hadi Ziwa Nyasa. Naomba nitumie fursa hii kuomba fedha nyingine kwa ajili ya barabara ya kutoka Mlangali kwenda Lupila kuititia Lupanga, lakini barabara hiyo pia inakwenda mpaka kule Ikonda.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Mkia kuititia Lugalawa, Mundindi, Mavanga hadi Madaba nayo ni muhimu, tunapopata fedha naomba mtutengene ili barabara hii nayo iweze ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hatua hii Waziri Magufuli nataka nikutie moyo, pamoja na Naibu wako kwamba mnafanya kazi vizuri, na kwa niaba ya wananchi wa Ludewa sisi tunasema tutazidi kuwaombea muwe na afya njema, mzidi kufanyakazi kwa niaba ya Chama chetu cha Mapinduzi. Mheshimiwa Magufuli ni jembe letu, tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu, hata kesho na keshokutwa ukiomba nafasi nyingine kubwa kidogo kuliko ya sasa hivi hiyo, basi ujue wananchi wa Ludewa tupo nyuma yako. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutenga fedha za barabara ya lami kwa ndugu yangu Mbunge wa Mwibara Kangi Lugola; ye ye pia naye amekuwa akilia sana kila mwaka. Nimesoma kwenye kitabu humu mmetenga fedha kwa ajili ya barabara kutoka Kisolya mpaka kule Bunda. Kwa niaba yake nataka nikushukuru sana, na hii ndiyo tunaisema kwamba Mawaziri muwe mnakumbuka na Wabunge pia, siyo mnabebana Mawaziri kwa Mawaziri peke yenu, Hapana! Kwa niaba ya Mheshimiwa Lugola, nakushukuru sana, naomba kwa niaba ya wananchi wa Ludewa nitumie fursa hii pia kukukaribisha Ludewa. Sisi Ludewa ni watu wakarimu, njoo ututembelee, uone hali halisi ya kilio chetu. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza naunga mkono bajeti hii asilimia mia moja kwa mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Aah, leo hapa! Ngoja nikae vizuri. Mheshimiwa Juma Njwayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha na Mheshimiwa Zabein Mhita ajiandae.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote mimi naomba kutangaza kwamba naunga mkono hoja ya bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Lakini naomba kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mimi sielewi kwanini barabara ya Ndundu Somanga kwenda Lindi haikamiliki! Kuna ahadi nydingi. Mheshimiwa Waziri alikwenda kule akatuambia siku 180, zimepital! Akasema Juni, 2012, hajjakamilika! Akasema Juni, 2013, dalili iliyopo kule, hiyo Juni 2013 haitakamilika. Hivi Mkataba wa Serikali na Kampuni ya Karafi ukoje? Uko *endless!* Hauna *timeframe?* Mimi naomba tuimalize! Wananchi wanapata kero sana kwenye kipande kile cha kilomita 30 kilichobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ujenzi unaendelea pale, lakini unachukua muda mrefu kiasi sasa kuna kudharaulika kwa Serikali pasipo na sababu ya msingi. Mheshimiwa Waziri uwabane wale wasimamizi, uwabane wale wakandarasi na ufanye *visit* ya mara kwa mara pale ili tumalize ile kero. Hakuna sababu za msingi wananchi kuendelea kunya yasika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi Jimboni. Moja ya mambo ambayo ni siasa kwenye Mkao wa Mtwara ni barabara ya Mtwara, Tandahimba, Newala hadi Masasi. Leo nafurahi kuona kuna Shilingi billioni 2.5 hapa zinazomalizia upembuzi yakinifu na *design* pamoja na kwamba kutafanywa mambo ya tenda. Lakini ombi langu, Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni akiwa Newala, Tandahimba alisema kabla hajatoka, ni lazima aweke jiwe la msingi la ujenzi wa barabara ile. Naomba Mheshimiwa Waziri usimwangushe Rais. Ukimwangusha Mheshimiwa Rais, maana yake umeiangusha CCM na mimi na wana-CCM wenzangu tunaoipenda CCM hatutakuwa tayari, tutakushikia bango wewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi fulani naomba pia mipango iende sawasawa na suala la Daraja la Mwiti pale; Daraja lile limetengewa shilingi milioni 90 za mwaka jana na sijaona umeongeza kitu hapa. Ninachotaka kusema, hesabu za haraka haraka tu milioni 90 haziwezi kumaliza daraja lile. Kwa kuwa tutakuwa na bajeti mwishoni kule, hebu tafuta tafuta namna, utenge hela ya kutosha pale, upembuzi yakinifu na *design* ukamilike tungojee pesa za kuanza ujenzi wa lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kusema kwenye barabara hiyo kwamba, Wananchi wamekuwa wakipata shida sana hasa wakati wa mvua. Utaratibu uwekwe wa kupunguza kero kwa Wananchi wakati mvua inaponyesha. Ile barabara inapitisha kiwango kikubwa cha korosho zinazosafirishwa kwenda Bandarini Mtwara. Hata ukitengeneza katika muda mfupi tu unakuta imeharibika na wakati wa mvua kero inakuwa kubwa. Ni vyema ukawekwa utaratibu sasa wakati utaratibu wa kujengwa kwa lami ukiwa unaendelea. Hivi sasa Wananchi wanapotumia barabara ile tuwamalizie tatizo, tuwa-rescue mara moja wanapokuwa kwenye adha. Wanakaa barabarani kwa muda mrefu, jambo ambalo linaleta kero. Mimi naomba tutengeneze utaratibu wa haraka wakati haya mambo mengine yanakwenda, lakini tuweze kutatua adha iliyopo ya kukaa muda mrefu njiani. Kilomita 209 tu, haziwezi zikatushinda Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia kidogo Kivuko cha Msangamkuu - Msemo. Nimeona kwenye bajeti hapa kwamba, Kivuko kipo Bandarini Dar es Salaam na kwamba ujenzi wa gati kwenye sehemu ya Msangamkuu umekamilika bado Msemo. Natoa rai na naomba jambo hili lifanywe haraka. Mahali pale pakiwa na tufani kidogo panawazamisha Wananchi; ni *distance* ndogo sana, lakini imekuwa ikileta adha na imekuwa ikileta vifo kwa Wananchi. Tufanye haraka, tuwakomboe Wananchi wale. Tusifikie mahali pa kuona Wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi wanadharauliwa kwa sababu tu ya uendaji wa pole pole kwenye miradi na mipango yetu. Mheshimiwa Waziri ni jembe, sidhani kama haya yanaweza yakamletea ugumu

wa kufanikiwa. Achape kazi, awasimamie vizuri, tuepukane na hizo kero kwa Wananchi walioko kwenye maeneo yetu yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwamba, niliomba tujengewe barabara ya lami kutoka Mtama kuelekea Tandahimba na Newala, kuelekea Mkwiti labda niseme kwa ufupi; mahali ambapo palikuwa pakileta adha sana ya vifo na upotevu wa mali kwa Wananchi. Barabara hiyo sasa ina lami kilometra saba. Ni jambo la kupongeza, naishukuru sana Serikali. Nataka kutoa pendekezo kwamba, uzuri wa barabara ile unachafuliwa na kutokuwa na daraja kwenye eneo la Mto Lukuledi. Unapotoka tu pale Mtama unaenda Kinolambelo pale kuna daraja la muda mrefu la ovyo ovyo limekaa pale, haliletii taswira nzuri. Hela itafutwe, ijengwe barabara ile ili iendane na matengenezo yaliyofanywa kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri hapa, ametaja mpango wa kuwatumia Wakala wa Majengo (*TBA*) kujenga nyumba kwa ajili ya Wananchi, nikiwa na maana wafanyakazi na zingine kukopeshwa. Mimi natoa rai, jambo hili lisiishie mikoani tu. Pale kwenye nyumba 100, *let say* Mtwara kukiwa na nyumba 100, tutoe angalau nyumba 20 kwa kila Wilaya za Mkoa wa Mtwara. Maana wafanyakazi wanaoishi kule Wilayani Tandahimba, Newala, Masasi, Mtwara Vijijiini na Nanyumbu, nao wana adha ya mahali pa kuishi vyema. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tuwafikirie hali hiyo iwe hivyo hivyo Pwani, iwe hivyo hivyo Dodoma na mahali pengine kwenye Wilaya zao waangaliwe hawa na ujue wafanyakazi wengi wapo Wilayani huko na ndiko utumishi uliotukuka uliko. Kwa hiyo, tuwape kipaumbele, tuwape nafasi na wao wanufaikie na rasilimali yetu hii tunayoitengeneza kwa ajili ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia tuangalie suala la Mizani. Watu wengi wanaosafiri kwenye mabasi wakifika kwenye Mizani wanapata shida sana. Utaratibu wa

kwenye Mizani uangaliwe upya. Hatuna sababu ya kuwapa adha Watanzania au watu mbalimbali wanaotumia barabara zetu kwenye Mizani. Tuangalie utaratibu ambao utarahisisha na utafanya wanaotumia mabasi kwenda haraka kwenye safari zao badala ya hali iliyoko sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumalizia kwa kusema, Serikali ya CCM lazima itikiswe sana, maana ndiyo yenyewe mwembe. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njwayo, nakushukuru sana.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njwayo nakushukuru. Mheshimiwa Ignas Malocha, atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Mhita. Mheshimiwa Malocha!

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Vilevile niungane na wenzangu, kwa pongezi ambazo wamezitoa kwa Wizara ya Ujenzi. Kwa kweli lazima tukubali kwamba, Wizara hii inapongezwa mahali pote ndani ya Bunge hata nje ya Bunge na ni Wizara ambayo inatupa heshima kubwa sana. Tunampongeza Mheshimiwa Waziri Magufuli na Naibu Waziri. Tunampongeza vilevile Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, maana ndiye mtafutaji wa hizi fedha. Hongereni sana na tunaomba muendelee na mtindo huu. Wananchi wanasesema Magufuli akishika Wizara yoyote huchangamka na hii ndiyo hali halisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali namna ambavyo inajitahidi kuweka mtandao wa barabara za lami kuzunguka karibu mikoa yote. Naomba sasa lengo liliowekwa na Serikali likamilike kwa wakati, nikiwa na maana kwamba, barabara za Mkoa wa Rukwa kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, Sumbawanga – Mpanda zilikuwa zikamilike mwaka 2012 zinachelewa kukamilika. Hii tunajua ni hasara kwa Serikali kwa sababu gharama

zinaongezeka kutokana na malighafi. Kwa hiyo, tunaomba Serikail izingatie mikataba ambayo iliwekwa ya kumaliza hizo barabara.

Mheshimiwa Naiu Spika, pamoja na mtandao wa barabara za kuunganisha mikoa, lazima tuzame kwa undani zaidi nia yake ni nini? Nia yake ni kuwaondolea Wananchi adha, wakulima wa vijjini waweze kupata barabara nzuri kwa maana ya kusafirisha mazao yao na kuondoa umaskini. Barabara zikiwa ni za lami halafu barabara za vijjini kilometa zaidi ya 100 siyo nzuri, nadhani tutakuwa bado hatujawasaidia hawa wakulima. Kilomita 100 barabara ni mbaya. Sasa Mwananchi huyu ataendelea kulanguliwa tu, pamoja na kuwa na barabara ya lami. Barabara ya lami itaendelea kuwa na unafuu kwa wale wale wenyenye unafuu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ielekeze nguvu zake katika kuimarisha barabara za vijjini ili kuunganisha na hizi barabara za lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda kusisitiza hilo. Vilevile hizi barabara ambazo zinatengezwa na Halmashauri, kwa kweli zinatengenezwa katika kiwango kidogo sana na si kwa makusudi yao. Halmashauri zinapewa hela kidogo sana na ndiyo maana hata barabara zao hazina viwango. Kwa mfano; nichukulie Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, ina urefu wa kilometa 1,004, inapewa shilingi bilioni moja, ukigawanya unakuta kila kilometa unatengeneza labda kwa shilingi laki tisa. Sasa hiyo barabara itakuwa na kiwango gani! Kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalie uwezekano wa kuzipatia hizi Halmashauri fedha za kutosha ili ziweze kutengeneza barabara vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, llingine, napenda kuipongeza Serikali, nimesoma kwenye Kitabu, imetenga bajeti kwa ajili ya Daraja la Mto Mombasa. Naipongeza sana, Daraja hili limekuwa ni kilio cha muda mrefu, likikamilika utakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa Wananchi wa Rukwa hata Mkoa wa Mbeya kwa sababu linaunganisha Mikoa yote miwili na ni ukanda wenyenye uzalishaji wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, napenda kuiomba Serikali izingatie maombi maalum yanayoletwa na Halmashauri. Kutokana na uchache wa fedha ambazo wanapewa, wanalazimika kuandika maombi maalum ili wawewe kutengeneza zile barabara ambazo hazijapatiwa fedha. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itilie maanani ili kuziwezesha Halmashauri hizi barabara zote ziweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni fidia za nyumba au mali za Wananchi. Serikali imepanua barabara zake mpaka kufikia mita 30 kwa 30 kila upande, lakini barabara hizi zimekuta Wananchi. Cha kushangaza ni kwamba, barabara au nyumba ya Mwananchi inawekwa alama ya kijani, Mwananchi huyo anaambiwa asiendeleze. Sasa asiendeleze kwa muda gani na Mwananchi huyu ni mkulima, akae muda wote akisubiri bila kujua ni wakati gani atapewa fidia aweze kuendeleza nyumba! Dalili hii ni kuendelea kuwaweka Wananchi kwenye umaskini. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho atoe *time frame*, wale Wananchi waendelee kusubiri kwa muda gani kwa sababu wao ni wakulima, mtu ameshauza mazao yake anataka kujenga nyumba, amejenga anaambiwa asimame asiendeleze mpaka lini? Kwa hiyo naiomba Serikali iweze kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, naishukuru Serikali mwaka jana tuliomba fedha upande wa Barabara ya Kalambazite – Illemba, tulipewa na mwaka huu nimeona kwenye kitabu tumeongezewa. Vilevile Barabara ya Miangalua – Chombe, tuliomba fedha mwaka jana na mwaka huu tumeongezewa. Kwa kweli naishukuru sana Serikali. Naamini kweli hii ni Serikali makini na ni Serikali sikivu, ambayo inasikia kilio cha Wananchi na Watanzania mnapaswa kuiunga mkono kwa asilimia 100. Wala msidanganyike, hii ndiyo Serikali inayosikiliza Wananchi na kutekeleza malalamiko yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naipongeza Wizara na Hotuba ya Wizara kwa asilimia 100. Ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Nakushukuru sana Mheshimiwa Ignas Malocha. Sasa Mheshimiwa Zabein Mhita, atafuatiwa na Mheshimiwa Highness Kiwia.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi naomba nichangie hoja iliyo mbele yetu hususan barabara ya kutoka Dodoma kuititia Kondoa hadi Babati, ambayo Mheshimiwa Rais wetu alitoa ahadi kwamba, itajengwa kwa kiwango cha lami mwaka 2005 na kwa mara ya pili tena mwaka 2010. Umuhimu wa barabara hii unafahamika sana, inatoka Cairo mpaka Cape Town. (*Makof!*)

Katika nchi zote ambazo barabara hii imepita, tayari kuna lami, isipokuwa kutoka Dodoma – Kondoa – Babati, kilomita 261 tu. Nianze na barabara sehemu ya kutoka Dodoma mpaka Mayamaya, ambayo ni kilomita 43. Barabara hii ilianza ujenzi tarehe 20 Juni, mwaka 2011, lakini mpaka ninapoongea ni kilomita 17 tu ndizo ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami. Miaka miwili kilomita 17!

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, barabara hii nimepita sana mimi; hii sehemu ya lami, ina mawimbi na wala haijatulia. Nasema hivi kwa sababu ile barabara ya kutoka Bicha mpaka Kondoa imetulia, lakini hii haijatulia. Tatizo nini; mkachunguze.

Katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka jana, Serikali ilitufahamisha kuwa fedha kwa ujenzi wa barabara kutoka kipande cha Mayamaya - Bonga imekwisha tengwa, lakini hadi sasa barabara hiyo haijaanza ujenzi. Katika swali langu namba 65 mwezi Aprili mwaka huu, nilihoji kuhusu barabara hii; nikajibowi kwamba, tathmini ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya barabara hii imeanza. Tathmini imeanza na wala haijakamilika mwaka mzima. Mwaka mzima ndiyo tathmini imeanza, kweli barabara hii itakamilika? (*Makof!*)

Wananchi wa Jimbo la Kondoia Kaskazini na Kusini ni hodari sana ni wakulima hodari, wanalima alizeti, wanalima ufuta, mbaazi na karanga, lakini wanapata matatizo kusafirisha mazao haya katika masoko na tunafahamu barabara nzuri inainua uchumi wa Wananchi. Hivi Wananchi hawa wa Kondoia na Chemba kweli uchumi wao utainuka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Kolo lilivunjika tangu mwaka 1997 hadi sasa ninapoongea, miaka 16 daraja hili halijajengwa. Kipindi cha mvua daraja likijaa maana yake hamna atakayepita pale mpaka maji yapungue, wakati mwingine inachukua mpaka saa kumi. Sasa je, Serikali ina mpango gani kuhusu daraja hii?

Kabla barabara hii haijaanza kujengwa, Serikali illituambia itaanza kwa kujenga madaraja, nikajua daraja la Kolo linajengwa. Baadaye tena wakasema hapana, hatuanzi na madaraja, tunaanza na barabara, miaka 16 daraja halijajengwa, linawapa adha kubwa sana Wananchi wa Jimbo la Kondoia Kaskazini. Sasa adha hii itaisha lini? Watu wanangojea mto upite, maji yapite siyo mto. Maji katika mto yapite ndiyo na wao wavuke; kweli? Wenzangu wameshukuru, wana sababu za kushukuru; mimi nashukuru kwa lipi? Pamoja na kwamba, napenda sana kushukuru, lakini nashukuru kwa lipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii barabara inatoka Mtundwa mpaka Kashi na inapita katika Vijihi vya Salare, Bumbuta, Mahongo, Ata, Madisa, Nachenge, Mitati, Hurui hadi Kashi. Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba, Barabara hii itachukuliwa na *TANROADS* mwaka 2010 hadi sasa haijainuliwa hadhi pamoja na kwamba suala hili limeshafikishwa katika *Road Board* ya Mkoa wetu lakini bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hivi; namwomba Mheshimiwa Waziri, tafadhali, utakapokuwa unajibu, naomba ujibu hizi hoja ambazo nimezitaja hapa ili waajiri wangu, tena kwa dhati, kwa uhakika, kwa ukweli pamoja na Wananchi wa Chemba, Wananchi wa Kondoia,

hawa ndiyo waajiri wangu mimi Wananchi wa Kondoa, nataka wapate majibu sahihi ili na mimi niweze kuunga mkono hoja. Wale wakiridhika nimeridhika, wale waajiri wangu wasiporidhika na mimi sitaridhika. Vilevile kuna hii barabara inayotoka Bicha mpaka Kondoa, nimesema ni nzuri lakini fupi mno. Tunaomba basi mtuongeze kilomita tano kama mlivyoongeza kule mahala; waliomba kilomita tano mkawapa na mimi naomba kilomita tano Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zabein wapi huko? Endelea Mheshimiwa kuchangia. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. ZABEIN M. MHITA: Kwa kuwa ile barabara ni fupi hata kama ni ndefu inakuwa kama mtu ambaye amenyolewa nusu kichwa, hata kama amenyolewa vizuri nusu kichwa haifai; hebu isogezwe kilomita tano mbele na Wananchi wa Kondoa nao wajisikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tumezungumzia kwa muda mrefu sana na utakumbuka katika Bunge la Tisa, tarehe 2 Julai, Bajeti ya Miundombinu ilisitishwa kutokana na bajeti finyu ya kuhusiana na hii barabara. Bajeti ile ilahirishwa mpaka Serikali ilipotafuta pesa, lakini barabara hii pamoja na kutafuta pesa bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakiunga mkono Kondo na Chemba na mimi naunga mkono. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zabein Mhita, sijawahi kukuona ukiwa mkali namna hiyo. Tunaendelea, baada ya Mheshimiwa Zabein Mhita, nilisema Mheshimiwa Highness Kiwia na Mheshimiwa Henry Shekifu ajiandae.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa fursa niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Nami nitumie fursa hii kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Dokta Magufuli, kwa kuweza kunipandishia hadhi barabara katika Jimbo langu la llemela, yenye umbali

wa kilometra 18 kutokea National – Buswelu – Illemela mpaka Muhonze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, kupanga ni kuchagua, lakini pamoja na shukrani hizi, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, barabara hii au uteuzi huu wa barabara kwa ngazi ya Mkoa, unaambatana na masikitiko makubwa sana kwa Wananchi wa Wilaya ya Illemela, hususan wale ambao makazi yao na waliositishwa kuendeleza makazi yao, kwa barabara ya awali iliyokuwa imependekezwa kupandishwa hadhi ya Mkoa; Barabara ya Kiseke – Buswelu – Muhonze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa, Barabara hii sasa ipo katika utekelezaji, Barabara hii ya National – Muhonze, ukweli ni kwamba, yako maisha ya watu wengi sana kwa upande wa barabara ya awali iliyokuwa imepitishwa ambayo yamerudi nyuma kwa kiasi kikubwa sana. Hivi sasa wameshindwa kuendeleza makazi yao kutokana na barabara hiyo kutokuingia katika mpango wa utekelezaji wa mwaka uliokusudiwa. Barabara hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameipitisha kwa sasa, kimsingi, ningombwa wakati anahitimisha awasaidie Wananchi wa Illemela, waweze kuelewa vigezo alivyovitumia akaiacha barabara ya awali ambayo ina wakazi wengi sana, ina vigezo na tayari kuna Wananchi ambao walitishishiwa makazi yao kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo na hawaelewi hatima ya barabara hiyo na hawaelewi hata hatima ya malipo ya fidia zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya kilometra 18, ambayo Mheshimiwa Waziri anaifahamu vizuri kabisa, aliitembelea mwenyewe na alijionea hali halisi ilivyo, inaungana na barabara ya awali ya *Airport by pass - Kayinze*, ambayo inaungana na barabara ya sasa iliyopandishwa hadhi ya Muhonze, ambayo ina takribani ukijumlisha ni zaidi ya kilometra 40. Barabara hii pamoja na kuwa imepandishwa hadhi ya Mkoa kwa muda mrefu sana, lakini imekuwa na ukarabati mdogo, ukarabati wa kawaida. Nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba, barabara hii ukijumlisha na hizi

kilometra 18 za sasa, unazungumzia zaidi ya Kata tano ambazo zinaguswa na barabara hii na inaunganisha zaidi ya Kata tano. Ninaomba, ni muda mrefu sasa na hiki ni kilio cha Wananchi wa Kata ya Ilemela, Kata ya Buswelu, Kata ya Nyakato, Kata ya Bugogwa na Kata ya Sangabuye; barabara hii sasa tuijenge kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo maombi ya Wananchi wa Ilemela, kwa sababu ina vigezo vyote. Kwa kutokufanya hivyo, tutakuwa hatuwatendei haki Wananchi hawa. Maeneo haya sasa yamekwisha endelezwa vyta kutosha na barabara hii ikijengwa kwa kiwango cha lami, tutakuwa tumechochea maendeleo kwa Wananchi wa Manispaa ya Ilemela kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Barabara ya Buzuruga – Pasiansi – Kaloleni – Sanga; barabara hii hivi sasa ipo katika hatua za mwisho na kwa mwonekano ni kana kwamba, imekamilika, lakini barabara hii ina upungufu mkubwa sana. Pesa ambazo zimetumika hapa ni nyingi sana na sidhani kama itakabidhiwa katika hali iliyonayo sasa. Tutakuwa hatujawatendea haki Wananchi wa Manispaa ya Ilemela. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa nafasi yake kabla barabara hii haijakabidhiwa, aitembelee ajionee mwenyewe; madaraja yako chini ya kiwango, nguzo za barabara zimeanza kumomonyoka na inajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa nafasi yake afanye kila linalowezekana kabla ya makabidhiano ya barabara hii ambayo imegharimu zaidi ya bilioni 6.5, yenye urefu wa zaidi ya kilometra 14. Aitembelee, ajionee mwenyewe na ajiridhishe, maana upungufu ni mkubwa na maeneo mengi yako chini ya kiwango. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Barabara za Kata, kwa maana ya Barabara za Halmashauri, kutokana na hali halisi jinsi ilivyo. Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, ilikwisha wasilisha maombi maalum zaidi ya mara mbili kwa ajili ya ujenzi wa Barabara za Kata, Barabara za Halmashauri, lakini mpaka sasa hakuna hata shilingi moja ambayo imetolewa. Ukweli ni kwamba, barabara ninazozitungumzia

zilikuwepo na sasa hazipo. Maana yangu ni kwamba, barabara hizi zimeharibiwa na mvua kwa kiasi kikubwa sana na Manispaa ya llemela baada ya mgawanyo ni Manispaa mpya, haina uwezo wa kuzikarabati hizi barabara kwa uwezo wake kuititia *own source*. Kwa hiyo, naomba sana, pamoja na maombi ya Halmashauri ya Manispaa ya llemela, ambayo mpaka sasa hayajapata kibali, maombi maalum; kwa kuwa, barabara hizi hazipitiki kiasi ambacho sasa Wananchi wangu wamesahau hata salamu ninapokutana nao, suala la kwanza badala ya salamu ni barabara zetu vipi!

Pamoja na maombi maalum ya Halmashauri, naomba kufanyike tathmini ya kina ya barabara hizi. Kwa sababu, kama mwaka jana pesa kutoka Mfuko wa Barabara iliyokusudiwa ilikuwa ni shilingi milioni 725 na bado hazikuweza kutosheleza kitu na Mwaka huu wa Fedha ni shilingi milioni 525. Upungufu huu ni mkubwa sana pamoja na madhara ambayo yameshajitokeza ya mvua. Kwa hiyo, *ni-declare* kabisa kwamba, kutokukubali maombi maalum ya Halmashauri ya Manispaa ya llemela ni kuwaacha Wanalllemela katika hali ngumu sana. Niseme barabara hizo katika kiwango zilichofikia sasa hivi, hazina tofouti na barabara za kuititia ng'ombe. Hata hiki kiasi cha shilingi shilingi milioni 525 ambazo ndiyo ruzuku, haziwezi kutengeneza hata mitaro kwa kiwango cha asilimia 20 cha Barabara za Manispaa ya llemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi ni kwamba, barabara hizi ninazozizungumzia za Manispaa ya llemela, awali kulikuwa kuna unafuu kidogo, kulikuwa kuna *relief*, kwa sababu tulikuwa chini ya Mpango wa TSCP, Mpango wa kuendeleza Majiji kwa upande wa barabara. Sasa baada ya mgawanyo, llemela imeondoka katika Mpango huu na ukizingatia kwa sehemu kubwa tulikuwa tunafanya *sharing* hata kwa upande wa vifaa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ambako ndiko sasa wamebaki na vifaa vingi, ikiwa ni pamoja na magreda. Kwa hiyo, ndiyo kusema kwamba, llemela wako *empty*, hawana kitu chochote, kuititia *own source* hawana uwezo wa kutengeneza barabara zao. Naomba hili liangaliwe sana, kwa sababu hakuna namna naweza

nikaunga mkono hoja hii kama sitapata uhakika *in details* wa namna ambavyo barabara zangu za Manispaa ya llemela zinakwenda kupatiwa ufumbuzi, hususan barabara ambazo nimezieleza, kwa sababu, kupertia *own source* Manispaa ya llemela hawana uwezo wa kutengeneza barabara zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha, hatima ya Wananchi ambao wamesitishwa kuendeleza makazi yao kwa zaidi ya miaka sita sasa wa Barabara ya Kiseke, Barabara ya Mwanza – *By Pass* – Kayenze, inayotokea Sangabuye, basi ijulikane; kama wanaruhusiwa kuendeleza makazi yao au kama ni kulipwa fidia, basi ni lini watalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kiwia. Mheshimiwa Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassari na Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani ajiandae.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi na namshukuru Mungu pia. Nianze kwa kusifu sana na nisingerudia sana wenzangu walivyoisifu Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri. Ni semet tu Mgema akisifiwa, basi tembo asilitie maji. Kazi ni nzuri na kwa Serikali nzima napenda kusema, kumbe inawezekana. Hela za maendeleo kwa Wizara hii zimetoka mwezi Machi zote asilimia mia moja. Tufanye nini kwa Chama cha Mapinduzi? Lazima tukipe heshima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe maelezo kwamba, mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Tanga. Haya ninayoyazungumza, ninataka kuthibitisha kwamba, Mkoa wa Tanga ni ngome ya Chama cha Mapinduzi na ili tuweze kufanikiwa, nimwombe ndugu yangu Magufuli, ili iweze kuendelea kuwa ngome na bahati nzuri wewe ni mkereketwa wala siyo wa kuiga, unaonekana katika sura yako, wa CCM. Sasa nakuomba, Mheshimiwa Mntangi,

alitaja Barabara ya Amani – Muheza, kura zetu zitapungua pale kama barabara ile haitatengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulipata kura nyingi sana kwa Barabara ya Horohoro kuja Tanga, leo tunaringa; upande wa Tanzania una heshima kuliko upande wa majirani zetu, endeleeni na kazi hiyo. Vilevile nashukuru kwa sababu upembuzi yakinifu unafanyika kwa Barabara ya Magole – Turiani – Mziha – Handeni na inajengwa sasa. Barabara ile ikikamilika, sisi wa kutoka Tanga kuja Dodoma hatutapata matatizo. Naishukuru tena Serikali, kwa Barabara ya Handeni – Kiberashi – Songe – Kibaya – Kondoia hadi Singida. Barabara ile ikijengwa, ambayo ipo katika mpango, nina uhakika Kanda ya Kati na Kanda hii ya Pwani, zitafikika kwa urahisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kwa kirefu kidogo kuhusu bajeti na kazi nzuri inayofanywa katika Kanda hii ndogo ya Tanga. Sasa nije katika Jimbo langu; kwanza, ninashukuru sana utendaji mzuri wa *TANROAD* Mkoa wa Tanga; Injinia wetu Ndumbalo pamoja na Makandarasi, kuna Mkandarasi mzuri sana anaitwa Ndugu Nguzo, ametutengenezea barabara vizuri sana, kwa viwango vinavyotakiwa na viwango ambavyo huwezi ukauliza, barabara ya kutoka Magamba kwenda Mlela. Mimi napenda irekodiwe, *value for money* pale imeonekana, thamani ya fedha imeonekana, sasa naomba mwendelee hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba kabla sijaenda kwenye mambo mengine na unajua kwamba, nitazungumza hili; upandishaji wa daraja barabara ya kutoka Mashewa, ambayo iko Korogwe kuja Milingano, ambayo iko Jimbo la Bumbuli, kuja Mlola Jimbo la Lushoto, kwenda Ngolo Jimbo la Lushoto na kufika Mlalo, Jimbo la Mheshimiwa Ngwilizi, barabara hii ni ya uchumi kwetu, tunaomba sana ipandishwe daraja. Hili nimekuomba mara nyingi, nimeombwa tangu nikiwa Mbunge mpaka 2005, nimerudi tena umeniahidi na ninawaarifu Wananchi wa Jimbo la Lushoto kwamba, jamani

eeh, ahadi hii kwa Waziri, ipokeeni ni ndugu yetu ataitekeleza. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nige pia katika barabara ya kutoka Lushoto kwenda Mombo kupitia Doch, ni barabara ya mkato ambayo ndiyo inaweza kutuunganisha kama itatokea tatizo la barabara kuu ya lami kutoka Mombo kwenda Lushoto, hii ndiyo barabara pekee ya kutoka Mombo – Doch – Lushoto, ambayo inaweza kutufikisha Lushoto. Vinginevyo, juzi tu kama wiki mbili zilizopita mvua zilizidi Lushoto ikawa kisiwa, barabara hii ndiyo iliyotumika. Tunaomba sana ikiwezekana barabara hii itiliwe mkazo na itengenezwe ili iwe barabara ya kudumu kutufikisha Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ambayo ninaomba na ipo katika matengenezo ni barabara ya kutoka Lushoto kwenda Magamba. Barabara ile illanza kujengwa mwaka 2004, sasa ni karibu miaka kumi, kilometra tatu tu ndiyo zimejengwa. Tunaomba, tafadhal sana barabara imalizike, kwa sababu gharama zinazidi kukua. Sasa inaonekana ni aibu na kule wanakaa Viongozi wetu, basi, unajua kule Lushoto ni kama *Small Switzerland*, kule ni *Switzerland*, wengine mnaweza kuja kutembelea kidogo; sasa kule wanakaa Viongozi, tunaomba basi muione hiyo *Small Switzerland*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kukizungumzia sasa, pengine ni maeneo mengine, utekelezaji wa miradi kwa viwango na kwa wakati. Kwa mfano, barabara hii ya kutoka Same kuja Korogwe, ambayo sasa hivi ipo katika matengenezo; barabara hii kwa mwenendo inavyokwenda naona haitakwenda kufuatana na malengo. Mkandarasi anachukua muda mrefu na ninaomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko, waende kwa wakati, barabara imalizike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningelizungumzia kwa kifupi sana ni Mamlaka zilizopo chini yako, nitazungumzia Mamlaka moja tu *TBA*. *TBA* iliwahi kuzungumzwa hapa ndani na Mheshimiwa Maua Daftari

kwamba, haijali mtu. Mimi nakuomba, hebu chunguzeni hii Mamlaka, *Agency* hii, mwone *Management* pamoja na utendaji wake. Maana ikishaanza kutajwatajwa na Waheshimiwa haijali utu, kama haijali utu wa Mbunge, huyu wa Mwananchi wa kawaida utaujali vipi? Ni kitu kinachosikitisha sana. Kwa hiyo, ninaomba kauli hizi siyo za utani ni kauli za ukweli, pelelezeni kama *Management* haiwezi kuangalia matatizo ya Wananchi, basi hizi juhudzi zote mnazofanya zitaonekana hazifai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema, kwa mara ya kwanza, Kamati zote zilizotoa maelezo, Kamati ya Kudumu na Kambi ya Upinzani, wamesifu sana na wameshauri vizuri. Tunaomba chukueni ushauri wao, ili ushauri ule ukitekelezwa utapunguza malalamiko kutoka kwa Wananchi. Masuala ya mizani angalieni, rushwa, akiba ya barabara ni kweli ni mali ya Serikali, lakini kule kuwarusha Wananchi, kuvunja nyumba zao, kitu hiki hakitujengi kama Chama, kinatumiza sana. Hebu tutafute njia, kama walivyofanya Barabara ya Horohoro – Tanga, Wamarekani walitoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia; hebu tujitahidi tulipe fidia. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, juzi Rais, alipokuja kufungua barabara ile, Wananchi walilipwa kifuta jasho, wale waliovunjiwa nyumba zao; ilihamasisha sana na Wananchi wataendelea kukipenda Chama chao na Serikali yao, endeleeni katika maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua ni kazi ngumu, lakini bila kufanya hivyo, tutafanya kazi nzuri, lakini Wananchi hawataona watafikiria kabisa kwamba, hatuwasaidii. Kama mwenzetu alivyosema, kama mtu unamvunjia nyumba yake, hata ukimpelekea barabara ya lami, hataiona umuhimu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni matuta ya barabara, ni eneo ambalo linalalamikiwa; ni muhimu kwa kweli, lakini basi hebu jengeni matuta ya barabara kwenye barabara kuu yanayofikia *standard*. Siyo matuta ambayo gari likiingia linavunja watu na lenyewe linavunjika. Mimi nafikiri tukienda hivyo, tutajengea heshima Serikali yetu na ninaamini

jinsi tunavyokwenda na jinsi Wizara inavyofanya kazi, hakuna mtu asiyekiri kwamba, kumbe inawezekana. Tukiwa *serious*, tukifuatilia kwa kasi nzuri na kwa uzito unaostahili, tunaweza kufanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nashukuru sana utendaji na nawaomba sana niwaambie wenzangu walioko kule ng'ambo; "Kiatu cha mtoto hakivaliwi na mtu mzima." CCM ndiyo baba yetu, haiwezekani kiatu cha mtoto na ukimwona mtoto mkorofi anavaa kiatu cha mtu mzima, atavunjika mguu. Sasa naomba tuvae kama utani tu, lakini naomba tuelewe wazi kwamba, tunatekeleza yale tulioyahidi na tuna uwezo na hakuna atakayetuweza; nguvu ipo, nia ipo na uwezo tunao. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shekifu kwa mchango wako. Mheshimiwa Nassari, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Ramo Makani.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nafikiri nina dakika kumi.

NAIBU SPIKA: Dakika kumi ndiyo.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nikaweka wazi kufuatia maneno yaliyosemwa na baadhi ya Wabunge wenzetu hapa asubuhi, akiwemo jirani yetu, Mama Anne Kilango, ametupiga sana Kambi ya Upinzani, lakini pengine hakutuelewa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kufanya *clarification* kabla ya kufanya siasa za Jimbo ni vyema kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nikaweka wazi. Tulichokisema Kambi ya Upinzani, alichokisema Mheshimiwa Said Amour Arfi hapa asubuhi ni kwamba, Serikali yetu imekuwa ikitoa hatuba za matumaini kwa Watanzania. Serikali yetu imekuwa ikitutajia miradi mingi na pesa nyingi kila mwaka, lakini inapofika mwisho wa mwaka wa fedha, miradi hii inakuwa hajatekelezwa wala pesa hazijatolewa na ndiyo sababu tukasema hivi; kwamba, kuliko kutenga kuwafurahisha

Watanzania kwa miradi kumi ya barabara ndani ya mwaka mmoja wa fedha ni vyema tukawatengea miradi miwili ama mitatu tukaitekeleza kuliko miradi kumi halafu isipate fedha wala isitekelezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano mzuri tu ameniandikia Mheshimiwa Mhonga, mwaka 2010/2011 zilitengwa shilingi bilioni sita kwa ajili ya Barabara ya Kigoma – Mdawe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi kwa kilomita 310 na zikatengwa shilingi bilioni sita ambazo kimsingi zisingetosha. Bado hazikutolewa na mpaka leo tunavyoongea hapa, hazijawahi kutekelezwa, barabara hajajengwa. Mwaka 2010/2011, tumekwenda 2011/2012, tumekwenda 2012/2013, hazijawahi kutolewa ndio tulichokisema. Kwamba, kuliko kuwapa imani Watanzania ni vyema tukawatajia miradi miwili ama mitatu ambayo tuna uhakika Serikali ina uwezo wa kuitekeleza kuliko miradi kumi, kuwapa matumaini Watanzania halafu mwisho wa siku hakuna hata mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niendelee na siasa za Jimbo. Juzi, mwanzoni mwa mwaka huu wakati tunazindua Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, ambacho ni Chuo kikubwa, kinatumika na nchi za Afrika Mashiriki na Kati. Chuo ambacho Serikali imekubali ku-/invest zaidi ya shilingi bilioni 56 kukijenga. Mheshimiwa Rais, alikuja kukizindua na Mheshimiwa Magufuli, Wazi wa Ujenzi. Mheshimiwa Rais, alisema kwamba, kwa ubora wa Chuo hiki, kwa umuhimu wa Barabara ya Nelson Mandela inayotoka Usa River mpaka Arusha Mjini kuelekea Mushono, mwaka huu wa fedha itengewe fedha ikamilike kwa sababu wanaosoma pale ni Chuo cha Kimataifa, ni watu kutoka Mataifa mengi ya Afrika na nje ili Taifa letu liweze kupata heshima.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu leo hii, kwenye Hotuba hii ndefu ya Mheshimiwa Magufuli, namheshimu sana, ndani yake unaisoma mwanzo mpaka mwisho zaidi ya kurasa 270 huoni ni wapi barabara ile imezungumziwa. Barabara ambayo ujenzi wake siyo zaidi ya shilingi bilioni sita. Ninashindwa kuelewa kitu kimoja; hivi kwenye hii nchi mkubwa ni nani kati ya Rais na Waziri? Kama Rais anamteua

Waziri halafu anampa maagizo na Waziri anakubali tena kwa nderemo nyingi! Mheshimiwa Magufulsi siku ile ulizungumza tukiwa mimi na wewe pale Nelson Mandela Arumeru, lakini cha ajabu haipo humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunashindwa kuelewa na ubaya mkubwa ni huu; wewe unaifahamu vizuri Arusha, barabara pekee ambayo inaunganisha Arusha na Mikoa mingine ni Barabara Kuu ya Kaskazini ambayo inatokea Cairo mpaka Afrika Kusini. Barabara hii inapita kwenye Jimbo langu, inapita Arusha Mjini, inapita Arumeru, inakwenda Moshi kuelekeea Afrika ya Kusini. Cha ajabu miaka mingi barabara imekuwa ina-stack kwa sababu ni barabara moja, ina daraja moja, linaitwa Nduruma. Mwaka juzi kuna gari liliharibika pale la gesi, barabara ikashindwa kupitika, watu wameshindwa kwenda *Airport Kilimanjaro*, *Airport Arusha*, tuna wageni ambao wanalala kwenye hoteli za kitalii Arumeru, wanatakiwa wafanye mikutano Arusha Mjini walishindwa. Kuna barabara nzuri ya Old Arusha - Moshi, ambayo ndio hii ya Nelson Mandela, kilomita tisa pekee, lakini cha ajabu leo hii huku haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni barabara pekee, ni *alternative road* ya Mkoa wa Arusha, ukizingatia wageni waliloko kwenye Mkoa wetu, ukizingatia viwanja vya ndege hivi viwili, ukizingatia idadi ya Mabalozi wanaokuja na Mikutano Mikuu ya Kimataifa inayofanyika Arusha, inaunganisha Arumeru na Arusha Mjini, kwa sababu wakati mwingine wanafanya Arusha Mjini wanalala Meru, wanafanya Meru wanalala Arusha Mjini, haipo kwenye bajeti hii. Sasa Mheshimiwa Magufulsi, nakuheshimu sana Daktari wangu, hebu tuambie tu kwamba hivi kweli umepuuza agizo la bosi wako Mheshimiwa Rais Kikwete ama ni kwa sababu Arumeru sasa hivi inaongozwa na CHADEMA nikiwepo mimi au tatizo ni nini?

Nilikuandikia ki-note leo asubuhi hujanijibu, naomba unijibu kwenye majumuisho ya hotuba yako, kwa sababu baada ya hapo nakwenda kuonana na Mheshimiwa Rais Kikwete, siku si nyingi nina *appointment* naye, nitamwuliza

kwamba yule Waziri wako uliyemteua amekataa maagizo yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu, kuna barabara nyingi ambazo tunazzungumzia; kwa mfano, kuna *by pass road* kwenye mradi mkubwa wa Afrika Mashariki ambao wenzetu Wakenya wameingiza vimiradi vidogo ndani yake, vingi kweli, ambao ni mradi wa *donors*. Sasa huo mradi una *by passya* Arusha ambayo inatokea TPRA - Ngaramtoni inazunguka Magereza, Uwanja wa Ndege wa Arusha mpaka inakuja kutokea Usa River. Mradi huu ulipaswa kutengewa pesa na kweli humu ndani umeandikwa, lakini umegawanywa kwenye vipande vitatu, kwa maana ya kutoka Arusha Mjini barabara nne mpaka Usa River kipande cha kwanza, kutoka Usa River mpaka Holili au Voi, mradi wa tatu ni huu wa *by pass*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Magufuli, anisikilize vizuri kwamba, tunaomba Miradi hii itakapoanza iende kwa wakati mmoja, tufikirie habari ya *compensation* tunavyozidi kusubiri, lakini vilevile ni vyema tukafikiria kwamba Mkoa wa Arusha unazidi kutanuka. Arusha imeshajaa, ni mji mkubwa, mji wa Kitalii, ukitaka kutanua barabara leo Arusha kilomita mbili unaweza ukalipa mabilioni ya pesa, kwa sababu ya kutanua barabara, ni vyema mradi ukaenda haraka ili tuzuie *compensation* kubwa baadaye na tuangalie historia, tukumbuke Mataifa ya wenzetu. Nimefanya tafiti, ukiangalia Japani, Mji Mkuu ulikuwa ni Kyoto lakini baadaye walivyoona wamejaa wakaanzisha New Tokyo, ukiangalia Marekani walianzisha New York kwa sababu hii; kuna umuhimu wa kuanzisha New Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Jimbo langu la Arumeru, kuna hii barabara inayotokea Mwamela Junction kwa maana ya Njia Panda ya Mwamela mpaka kwenye geti la *Arusha National Park*, ambayo *TANROADimechukua*, lakini kila mwaka wanatengeneza wakitengeneza zaidi ni mita 100 peke yake. Sasa barabara ndogo ya lami nyepesi inachukua miaka sita mpaka saba; kwa nini? Ni vyema tukafikisha pale

tunapopasa kufikisha kwa maana ya *TANROAD* kufikisha getini, watu wa TANAPA wachukue kazi yao na kutoka kwenye geti upande wa pili mpaka Ngarenanyuki, *TANROAD* muweze kumalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu ni hiki, unatengeneza barabara ya kutoka Mwamela Junction kuelekea Arusha National Park unawaachia TANAPA wamalizie, halafu unachukua mita 200 mbele yake, halafu unaiacha Barabara ya King'ori Kibaoni ambayo inaunganisha Kata ya King'ori – Leguluki. Inaunganisha Kata ya Ngarenanyuki lakini inaunganisha Wilaya tatu, inaunganisha Arumeru – Sia – Longido halafu unaiacha na barabara hii unaiachia Halmashauri ambayo kimsingi haitumii kuingiza vipato. Barabara hii inaingizia vipato Serikali Kuu kwa sababu ni barabara ambayo inakwenda kwenye Hifadhi ya Taifa ya Arusha, ni barabara ambayo inakwenda Mlima Meru, ni barabara inayounganisha Wilaya zaidi ya moja kwa maana ya Wilaya tatu, lakini haipewi kipaumbele. Tumeipigania kweli lakini inaonekana Wizara imekuwa kichwa ngumu kuiingiza kwenye barabara za *TANROADS*. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa heshima kubwa tunaposema mambo hapa hatusemi kwa sababu ya kukikomoa Chama cha Mapinduzi. Tunapozungumza hapa hatuzungumzi kwa sababu eti wewe unatokea chama fulani; siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nchi ni ya kwetu sote, leo mko CCM, kesho itakuja CHADEMA, keshokutwa Chama kingine hatujui ni kipi. Tunazungumza mambo ya Kitaifa, tunatamani kuona Taifa letu liki-nourish.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari, ongea mambo ambayo ni ya kweli. Endelea. (*Kicheko*)

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na umetumia sekunde zangu kadhaa, naomba uniongezee. Nikwambie tu ukweli, nazungumza mambo ya Jimboni kwangu Arumeru, nayafahamu, siongei mambo ya Kongwa unayoyafahamu wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, pale mnapofanya mambo mazuri tunashukuru, Mheshimiwa Magufuli nimekuandika *ki-note* kukushukuru Barabara ya Kilala – Nkwaranga imekamilika na ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa sababu ya Hospitali kubwa ya KKT ambayo inahudumia watu wengi kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapowashukuru mkubali na tunapowakosoa vilevile ni vyema mkakubali, kwa sababu lengo letu ni kuijenga Tanzania iliyo moja. Pia ni vyema tukachukua mawazo yetu, kwa sababu hii Tanzania ni ya kwetu sote, tunaunganisha Wilaya tatu barabara inakuwa *despised simply because an MP is from CHADEMA; why?* Wanasiasa ni sisi, hawa akina mzee Lyatonga hawa walikuwa CCM, wameenda NCCR, leo wako TLP, ni walewale. Dokta Slaa alikuwa CCM ameona haiendi amekuja CHADEMA, wanasiasa ni sisi, Mheshimiwa Magufuli kesho utakuwa CHADEMA, huwezi kujua, tutengenezeeni barabara zetu tusonge mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sitaki kuchukua muda mrefu ni vyema nikaeleweka tu. Ninaomba Mheshimiwa Magufuli aniambie kuhusu Barabara ya Nelson Mandela kutoka Moshoro kupita Arumeru kuelekea Usa River, barabara ya Tengeru ya kilomita moja inayounganisha kutoka Tengeru mpaka Barabara ya Nelson Mandela ni vyema ukatuambia kama kweli hivi umekiuka maagizo ya bosi wako Mheshimiwa Kikwete ama pengine mliongea *chamber court* ili kutafuta kura Arumeru siamini sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Barabara ya King'ori. Barabara hii inaunganisha Wilaya tatu. Barabara hii inaunganisha Kata zaidi ya tatu. Barabara hii ina umuhimu mkubwa kwa uchumi wa Taifa letu, kwa sababu inakwenda kwenye Hifadhi ya Taifa, inakwenda kwenye hoteli kubwa za kitalii ambazo zinaingiza pesa nyingi kwenye Taifa letu. Vilevile ni vyema tukakumbuka kwamba, kuna wapiga kura ambaao walimwingiza Mheshimiwa Rais Kikwete madarakani mwaka 2010, ambaao wanategemea kuona ikirekebishika, la sivyo, ameongea Mheshimiwa Shekifu kwamba, Barabara ya

Morogoro imewapa kura, mimi niwaambie ukweli msipotengeneza Barabara za Arumeru zitazidi kuwanyima kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nikusemee na wewe kwamba, kule Kongwa pia siyo kwema sana, nimepita kwa sababu upo kwenye Kiti unashindwa kuzungumza; Mheshimiwa Magufuli ni vyema ukinikumbuka Nassari, umkumbuke na Mheshimiwa Ndugai. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Nassari, kwa nasaha zako kwamba leo unaweza ukawa chama hiki kesho chama kile, kwa hiyo, siyo ajabu Mheshimiwa Nassari uchaguzi ujao akawa CCM. (*Kicheko*)

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Siyo kweli.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani*. Unajua Waheshimiwa wengi hamfahamiani majina, baada ya Mheshimiwa Ramo Makani atafuata Mheshimiwa Magolyo, sijui wangapi mnafahamu Mheshimiwa Magolyo, mtamwona.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya afya na uhai. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuwa mmojawapo kati ya wachangiaji jioni hii. Labda nianze na jambo ambalo sikuliweka kwenye orodha ya mjadala, lakini nimelazimika kulisema sasa hivi baada ya mchango uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili Bajeti ya Taifa, bajeti kwa kifupi tu maana yake ni mpango wa mapato na matumizi. Yote hii ni mipango ambayo unajiwekea malengo ili uweze kuyafikia. Ni kweli kwamba, utafika wakati unaweza usifike kwenye malengo kama ulivyojikadiria, lakini ukijiwekea lengo dogo maana yake ni kwamba, unajiwekea mpango ambaa haukuwezeshi kufika kule unakotaka kufika kwa

haraka. Ni busara na hekima kujiveka lengo kubwa ili uweze kujitahidi kufikia kwenye lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye zile nilizojiandaa nazo. La kwanza, michango mingi iliyopita inazungumzia juu ya suala la ujenzi wa barabara, lakini ni ujenzi mpya wa barabara. Mimi nataka nizungumzie juu ya suala la matengenezo ya barabara ambazo zimekwishajengwa (*maintenance*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa tukaanza kujijandaa kwamba ujenzi wa barabara kilomita 11,000 ambalo ndio lengo, utaibua kazi nyngi za matengenezo baada ya muda mfupi; na kwa hiyo ni vyema kama Taifa tukajiandaa, namna ya kuweza kushughulikia kazi za *maintenance*. Kwa sasa kwa kuwa *maintenance* inabebwa na *Road Funds* kupitia *RFB*, kupitia Sheria ya Mfuko wa Barabara, napendekeza kama ilivyokwisha pendekezwa hapo nyuma ni lazima tuangalie namna ya kuweza kuuboresha Mfuko huu, kuboresha mapato yake ili tuweze kusimamia vizuri matengenezo ya barabara. Tuboreshe chanzo kilichopo lakini pia tubuni vyanzo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara ni jambo moja, lakini unapozungumzia matengenezo ya barabara, yako mambo ambayo ni vyema tukayazingatia kwa kuwa sasa hivi tunashuhudia barabara zilizokwisha kamilika zikiharibiwa na huku tukiwa tunazitazama tu. Mifano michache ni udondoshaji wa vitu kwenye barabara, ambao unasababisha barabara kuharibika mapema. Watu wanabeba zege bichi, yaani *green concrete* na kudondosha kwenye barabara, watu wanachimba barabara kwa sababu mbalimbali kama kuitisha mabomba na sababu nyngine nyngi na kadhalika, lakini pia ubebaji wa madini ya ujenzi ikiwepo udongo, mchanga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza, kwa sababu ya muda niseme kuwa, kuna haja ya kuanza kutilia mkazo suala la uelimishaji wa watumiaji wa barabara. Pia licha ya

uelimishaji, tuweke mpango mkakati, Serikali ijpange kutengeneza utaratibu wa kuwabaini wachafuzi na waharibifu wa barabara wa makusudi. Njia mojawapo inaweza kuwa na *moving cameras* baada ya kutayarisha *whistle blowers* na namna nyingine ambayo tunaweza tukajipanga nayo ilimradi taarifa zikifika mahali panapohusika wahuksika wachukuliwe hatua. Mpango huu unaweza kusimamiwa na Wizara, lakini pia kupitia Bodi mbalimbali zinazohusika na ujenzi wa barabara na mpango huu ukisimamiwa vizuri unaweza pia ukaleta hata ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la wataalam, nataka niseme kwa kifupi kwa sababu muda hautoshi; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unatutaka tukifika mwaka 2015 tuwe na wataalam, wahandisi na wabunifu na wasanifu majenzi 88,000. Kwa takwimu zilizoko kwenye Ripoti ya Wizara ambayo ni taarifa ya bajeti aliyosoma Mheshimiwa Waziri mpaka sasa hivi ukijumlisha *architects* na *engineers* wote wanafika 12,600, unaweza kuona mtihani tulionao. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa ya kuweza ku-*train* wataalam hawa kwa ajili ya ujenzi wa barabara na majenzi mengineyo. Ku-*train* siyo tu darasani, siyo *formal education* peke yake, pia kuna *training* kwa maana ya mafunzo kwa vitendo. Sasa tutumie miradi mikubwa iliyopo nchini kuweza ku-*train* watu ambao watakuja kusimamia *maintenance* huko siku zijazo. Miradi mikubwa kama ujenzi wa Daraja la Kigamboni, ujenzi wa Daraja la Malagarasi na miradi mingine mingi tu mikubwa ambayo kutokana na muda siwezi kuitaja yote, itumike kama *facilities* za kuweza ku-*train* watu ambao baadaye wanaweza kusaidia Taifa hili katika kusimamia *maintenance* na pengine ujenzi wa miradi mipya ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo; hivi sasa kila mtu anazungumzia juu ya suala la jengo lilitlobomoka na kuua watu na kuleta uharibifu wa mali. Kila mmoja anasukuma mpira kwa mtu mwagine akidhani kwamba, mtu mwagine ndiyo ana wajibu zaidi kuliko yeye. Nchi inaendeshwa kwa kanuni na taratibu ambazo zinafuatia Sheria ambazo zote zimedondoka kutoka kwenye Katiba. Kwa sasa ningeweza kusema tu kwa kifupi ili tuweze kuelewana kabla ya kuulizana

nani afanye nini, taratibu za ujenzi wa jengo, usimamizi wake unaenda katika hatua zote za ujenzi ikiwemo kuchimba msingi kujua umekwenda chini kiasi gani kadiri mtu aliyesenifu amesema, namna ya kuweza kujua kwamba zege lile na vitu vyote vinavyotengeneza zege, zikiwemo kokoto, ubora wa kokoto, ubora wa mchanga, ubora wa maji yanayotumika, uchanganyaji, usafirishaji, kwa hiyo, utawenza kuona ni namna gani ili kuweza kusimamia vizuri jengo, unatakiwa kuwa na watu hao kwenye jengo lile wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tujiulize Bodi ya Usajili ya Wahandisi ambayo ipo Makao Makuu Dar es Salaam, Bodi ya Usajili ya Wasanifu na wabunifu majenzi wapo Dar es Salaam, ukiwahesabu wote wanaweza wakawa 30 au 50, kama watakuwa wengi sana; wanaweza kusimamia ujenzi wa majengo nchi nzima kwenye Halmashauri zote? Jibu haiwezekani, ndiyo maana kama Taifa na kama Mataifa mengine yote Duniani, utaratibu uliowekwa ni kuzihusisha Halmashauri za Miji inayohusika kuzi-*empower* kuwa na wataalam na kuwa na Sheria ambazo hizo ndiyo zinazowawezesha kusimamia ujenzi siku hata siku, hatua hata hatua, kila siku wanakagua na kwa kweli huruhusiwi kuendelea kujenga kwenye hatua inayofuata kabla hujakaguliwa na kuidhinishiwa kwamba, unaweza kuendelea kujenga na ndiyo maana unapewa mamlaka ya kutoa vibali. Utatoa kibali kwamba, ujenzi uendelee lakini utatoa kibali cha kwamba jengo limekamilika, sasa linaweza kutumika na kadhalika

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi tu kwa sababu ya muda, niseme kwamba, hatuwezi kukwepa; ni lazima tuzihusise Halmashauri zetu, hata kama mtu atataka *ku-disown* atakuwa anafanya hivyo kwa makosa, ni Halmashauri ndiyo wanatakiwa kusimamia. *Building Regulations* zimesema hivyo, kwa bahati mbaya zilifutwa wakati Fulani, marekebisho yalifanyika hayakukamilika. Nataka nitoe wito kwa Serikali sasa hivi, vyombo vyote vinavyosimamia majenzi vitawenza tu kufanya kazi kwa kugawana majukumu kisheria na hatuna sheria moja inayogawa madaraka na mamlaka na mipaka. Kwa hiyo, tunahitaji Sheria moja itakayozunganisha Sheria

hizi moja moja zilizoko kwa wataalam wote na vyombo vingine ikiwemo *National Construction Council* na wengineo ili waweze kujua nani anatakiwa kufanya nini, wakati gani na wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri ninayo taarifa na niliwahi kushiriki huko siku za nyuma kabla sijaangia Bungeni, tayari tunayo Rasimu ya *Building Act*, ambayo inapanga watu wote kulingana na nafasi zao. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho, atueleze utaratibu wa uwepo wa Sheria ya Majenzi au Sheria ya Majengo umefikia wapi na Serikali itakamilisha lini utaratibu huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende Jimboni. Kwanza kabisa, naomba niipongeze Serikali, tayari barabara ya Mjimwema au pacha ya Mindu kwenda Ngapa mpaka pachani mpakani na Nachingwea, imeshapandishwa daraja, imepandishwa hadhi na kuwa sasa ni Barabara ya Mkoa. Nashukuru sana kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, sasa tunasubiri utekelezaji wa kujenga barabara ile kwa sura na kwa utaratibu utakaofanana na Barabara ya Mkoa, tofauti na ilivyokuwa hapo kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Namtumbo – Tunduru, yamesemwa mengi lakini nataka niseme kama Mbunge na kama mtu ambaye hili ni eneo langu ambalo nimebobeza kwa kiasi Fulani; naipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kumsimamisha Mkandarasi, *MS Progress*, kutokana na utendaji kazi wake mbovu ambaulikuwa unasababisha mradi ule usiweze kuendelea. Hatukufika hapo kirahisi, tumefanya mambo mengi kuititia ukaguzi na kuweza kupima uwezo wa mkandarasi kama anaweza kuendelea kujenga barabara ile kama ana matumaini yoyote ya kuweza kukamilisha kazi. Hili halitokani na upungufu wa taratibu za kumpata Mkandarasi. Ripoti ya Kambi ya Upinzani inazungumza alipatikanaje?

Alipatikana kwa *International Bidding Process*. Kazi zilitangazwa Kimataifa, watu wakaomba, wakawa *evaluated* kuititia *papers* na kadhalika na huo ndiyo utaratibu wa

kawaida Dunia nzima. Sasa, Mkandarasi anaweza kuwa mzuri leo wakati wewe unamtafuta, baada ya miezi miwili, mitatu au baada ya mwaka mmoja, akaflisika au akapata changamoto nyingine yoyote ile. Ndiyo maana unatakiwa usimamie kazi yako *on continuous basis*, kwa kumwangalia kila siku anafanyaje kazi ili akibadilika wakati ana kazi yako mkononi, uchukue hatua. Hivyo ndivyo Serikali ilivyofanya, kwani imechukua hatua baada ya kumwona ha-perform kama alivyotarajiwa wakati anaomba kazi. Kwa hiyo, isisomeke vibaya kwamba, labda Serikali ilikosea sana kumpa kazi, hapana haikuwa hivyo, nimelifanya kazi suala hili kwa kina kama Mbunge wa Jimbo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni *misleading* wanasema; kwa nini alipata *lots* zote tatu? Suala siyo *lots*, *lots* zile zote ukizijumlisha, nilikuwa nafanya hesabu hapa ni kilometra 187.6. Ukichukua *lots* zote tatu; Tunduru – Matemanga, Matemanga – Kilimasela na Kilimasela – Namtumbo, zote zina jumla ya kilomita 187.6. Barabara inayotoka Iringa - Dodoma ina *lots* mbili; moja Iringa – Migori na nyingine Migori - *Fufu Escapement*, ukizijumlsha *lots* hizo unapata kilomita 188.9. Kwa hiyo, *lots* siyo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa *Eng. Ramo Makani.*

Sasa kabla hatujaendela na mnajua matangazo mengine hayawezi kusubiri kwa sababu ya umuhimu wake; Mheshimiwa Profesa Majimarefu, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wapenzi wa *Club* ya Simba, kukutana kesho kule eneo la siri Msalato kwa ajili ya Mkakati wa Mechi ya Jumamosi wa kuifunga Yanga. (*Makofii*)

Haikueleweka nirudie, inatosha *eeh!* Mheshimiwa Magolyo.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Huyo ni Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige!

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Naomba nikushukuru sana kwa kuniita kwa jina langu halisi la kweli, jina ninalolipenda sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nimpongeze sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. John Magufuli, pamoja na Naibu wake na Wizara nzima kwa ujumla, kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya katika usimamizi wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya barabara. Kipekee, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa bidii na juhudikubwa anazofanya kutafuta fedha. Katika miaka mwili mfululizo, tumekuwa tukitenga zaidi ya shilingi triliioni 1.2, kwa ajili ya barabara. Katika historia ya nchi yetu, hajjawahi kutokea wakati wowote ambapo eneo hili la barabara limewekewa kipaumbele cha namna hii. Naomba nipongeze sana Serikali, karibia kila sehemu sasa kuna Mkandarasi na kama unavyoona hali ya Bunge, karibu kila Mbunge amefurahi. Napongeza sana juhudii hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, nilitaka niombe baadhi ya maeneo ambayo kwa maoni yangu yanahitaji kutazamwa kwa macho yenye huruma zaidi ifanyike hivyo. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa maeneo mbalimbali, kwa kutambua juhudii zilizofanyika na fedha zilizotengwa kwenye maeneo yao. Ninaamini kwamba na sisi pengine kwa mwaka utakaofuata, tutakapokuwa tumepata kipaumbele kuliko ilivyo hivi sasa, tutajumuika au mtatuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kahama tulikuwa tumeahidi kuanza upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara kuu tatu. Ipo barabara ya kutoka Kahama kuititia Mgodi wa Bulyanhulu hadi Mkoa mpya wa Geita katika Mgodi wa Geita. Kuna barabara nyingine

inaanza Kagongwa - Bukene kwa rafiki yangu Mheshimiwa Zedi, Mambali hadi Tabora. Pia kuna barabara inayounganisha Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Katavi, yaani barabara ya kutoka Kahama kuititia Uyogo - Kaliuwa mpaka Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni mwaka wa tatu, hii ni bajeti ya tatu ya utekelezaji wa llani yetu, tulitegemea katika hatua ya sasa, angalau kungekuwa kumeanza kutengwa fedha kwa ajili ya upembizi yakinifu. Nimeangalia kwenye vitabu suaona fedha zilizotengwa kwa ajili ya upembizi yakinifu na kuanza ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nizungumzie barabara inayounganisha Mkoa wa Shinyanga na Geita. Barabara hii iko *busysana* na imekuwa kero kwa Wananchi kwa muda mrefu. Pia, hii barabara inahudumia Mgodi wa Bulyanhulu na Mgodi wa Geita. Migodi ambayo kwa kiasi kikubwa, inatumia mafuta katika uendeshaji wake hasa Mgodi wa Bulyanhulu, sehemu kubwa ya madini yanasafirishwa katika mfumo wa mchanga, yaani *copper concentrate* kwenye malori. Hivyo, ni barabara ambayo inapitisha malori mengi sana na imekuwa kilio la Wananchi tangu mgodi ulipoanzishwa mwaka 2000 kwamba, barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami.

Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, mwaka 1997, Mgodi ulipokuwa ukianza, walikubaliana na Wizara ya Ujenzi mambo mawili: Kwanza, walikubaliana barabara hiyo itengenezwe na Mgodi wenyewe ili waweze kuitumia; na pili, yalikuwepo makubaliano kwamba, utaanza ujenzi wa kiwango cha lami ili kuweza kuhudumia Mgodi huo wa Bulyanhulu na Mgodi wa Geita. Toka mwaka 1997 mpaka hivi sasa, hakuna kilichofanyika katika uelekeo wa kuweka lami kwenye barabara hiyo. Mwaka 2007, Mheshimiwa Rais alikuja Kahama, akafika kijijini kwangu Segese, Wananchi wakamsomea risala wakamweleza masikitiko yao kwamba, wanapata shida sana kutokana na vumbi linalotimuliwa na malori yanayopita kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Miundombinu wakati huo alikuwa kaka yangu Mheshimiwa Chenge; Mheshimiwa Rais akawaelekeza kwamba, watakaporudi Dar es Salaam suala hili Waziri akaliangalie akiwa Wizarani, aone nini cha kufanya mapema iwezekanavyo ili kuondoa kero hii kwa Wananchi. Toka mwaka 2007 mpaka leo mwaka 2013, miaka sita baadaye, hakuna kilichofanyika na Wananchi wanaendelea kuteseka na kilio ni kilekile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana kilio hiki cha Wananchi ambacho baadaye kilikuja kukubalika na kuingizwa kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2010 - 2015, kwamba barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami; ianzé kuonekana ikitekelezwa. Najua juhudzi zinazofanywa na Serikali, lakini sidhani Wananchi wa kawaida huko vijijini kama wanaweza wakatuelewa. Niseme tu kwamba, pamoja na kwamba tumejenga barabara nydingi maeneo mengi, kila eneo lina matatizo yake na mimi nilidhani ni vizuri maeneo haya ambayo yana Barabara Kuu za Kitaifa lakini zenye Uchumi wa Nchi kama hii inayounganisha migodi miwili, ni vizuri ikapewa kipaumbele. (*Makofî*)

Naomba nzungumzie suala la kuweka kipaumbele; kuna maeneo mengine nadhani ni kwa sababu tu ya kutaka kuonekana tunafanya vizuri katika kila eneo; kwa mfano, kuna barabara nyininge ukiziangalia zinaunganisha Kata na Kata kwenye maeneo fulani hapa nchini na kuna maeneo tumetajiwa zinaongezwa kilometa tano. Ukizisikiliza kilometa tano hizo zinaenda kwenye eneo ambalo linaunganisha kijiji na kijiji na wala siyo Mkoa na Mkoa. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, tafadhalii sana, tuzingatii vipaumbele tulivyojiwekea kwamba, barabara zinazounganisha Mikoa na Barabara Kuu za Kiuchumi kama barabara hii ziweze kupewa kipaumbele kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuleta maombi ya Wananchi wa Jimbo la Msalala pamoja na Wilaya nzima ya Kahama. Wilaya ya Kahama kama mnnavyojua, inazalisha dhahabu lakini iko *busy* sana kwa shughuli mbalimbali. Ule Mji wa Kahama hauna barabara

ya lami, ukiacha iliyoanza kujengwa hivi sasa. Mheshimiwa Rais, aliahidi kujenga barabara ya lami Mji wa Kahama tangu mwaka 2005, kipindi cha kampeni. Ujenzi wa barabara hiyo umekuwa ukienda kwa kusuasua sana. Leo miaka saba, karibia inaenda kuwa miaka tisa au minane, ujenzi wa barabara ya kilometra tatu haujakamiliika wakati matarajio yetu yalikuwa angalau ujenzi ungekuwa umefika kilomita sita sasa, kwa maana ya barabara inayotoka Fantom kwenda Mwanza na barabara nyingine inayotoka Nyihogo hadi kule *Mongoro Ginney*. Barabara hizi ambazo ndiyo zinapita katikati ya Mji ilikuwa ni ahadi ya Rais, lakini utekelezaji wake unakwenda polepole.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewasilisha maombi *TANROAD* Mkoani, kwa ajili ya kupandisha barabara itakayounganisha Halmashauri mpya ya Msalala. Naishukuru Serikali kwani tumekubaliwa kuanzisha Halmashauri ya Msalala kuanzia tarehe moja mwezi Juni, siku chache zijazo na Makao Makuu ya Halmashauri hii yatakuwa Busangi. Busangi pale patakuwa hapana mawasiliano ya moja kwa moja kutoka pale kwenda Mkoani na tukawa tumependekeza iwepo barabara ya kutoka Didia, Jimbo la Solwa; ipite Isakajana, ipite Buluma, ipite Mwakuba, ipite Nduku, ipite Ngaya, ipite hadi Busangi, Makao Makuu ya Halmasahuri, iende Ntombo iungane na ile barabara inayotoka Kahama kwenda Geita. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeboresha na kuunganisha Halmashauri hii ya Msalala ambayo ni maarufu kwa uzalishaji wa mpunga na dhahabu kama nilivyokwisha kueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba niwasilishe maombi hayo na kwa mara nyingine, napongeza sana juhudhi zinazofanyika, lakini naomba mwakani barabara hizi nilizozitaja zionekane, kwani bado bajeti mbili tu; Bajeti ya mwaka 2014 na bajeti ya mwaka utakaofuata. Kama hatutaweza kutenga fedha mwakani, maana yake kutakuwa na tatizo. Mimi ni semet tu kwamba, pengine katika bajeti hiyo, nitakuwa mkali zaidi kwa sababu sasa tutakuwa tunaenda kwenye kipindi ambacho ni cha

kufanyiwa maamuzi katika mambo tuliyoahidi na haitakuwa vizuri tukafika mwisho bila kutekeleza ahadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii kwa sababu kazi iliyofanyika ni kubwa, maeneo mengi yametekelozwa, naamini na langu litatekelezwa, kwani wanasema dalili ya mvua ni mawingu. Kwingine kumetekelozwa na mimi naamini katika muda mfupi ujao barabara hizi nilizozitaja zitaanza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishia hapo, nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala. Sasa namwita Mheshimiwa Kaika Telele, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Hilda Ngoye ajandae.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nzuri sana inafanywa na Wizara hii na wala siyo siri, mwenye macho haambawi tazama, wote tunaona ni kazi nzuri, nchi nzima inaonekana kuna vumbi mpaka Jiji la Dar es Salaam kuna vumbi, maana yake kazi nzuri inafanyika huko ya kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtando wa barabara hapa nchini ni kama mishipa ya damu kwenye mwili, ni kazi kubwa inafanyika na mimi naunga mkono. Hata hivyo, mwaka jana wakati nachangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 26 Juni, 2012 nilizungumzia barabara hii ya Mto wa Umbu – Loliondo, kilometra 213, ambayo pia ipo katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nashukuru kwamba, barabara hii imetengewa hela; barabara nzima ya kuanzia Mto wa Mbu mpaka Mkoa wa Mara, imetengwa shilingi bilioni 8.6, lakini sijajua vizuri kama pesa hizi zote zitakuwa nusu kwa nusu kwa Mkoa wa Arusha na nusu nyingine Mkoa wa Mara. Naomba baadaye Mheshimiwa Waziri anifafanulie vizuri.

Itoshe tu kusema kwamba, Marehemu Baba wa Taifa, zamani enzi hizo miaka ya themanini, alitamani sana kuunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha kwa barabara ya lami. Hii azma leo inaonekana katika Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwamba ana mkakati wa kuunganisha mikoa yote ya Tanzania Bara kwa barabara za lami na hiyo kazi inaonekana ikifanyika. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Barabara ya Makutano – Nata – Mugumu – Loliondo – Mto wa Umbu, kama kuna barabara ambayo imepoteza *calories* nyingi sana za Mheshimiwa Rais ni hii. Kwani Rais ametumia nguvu nyingi, maelezo mengi kushawishi na kuelimisha watu mbalimbali waliopinga barabara hii walio ndani na nje, kujaribu kuwaambia kwamba kwa kweli pamoja na kwamba ana heshimu rasillimali za Taifa kama vile wanyamapori, mazingira, lakini vilevile amesema ana dhamana ya kuleta maendeleo kwa Wananchi wanaopakana na maeneo yenye wanyamapori kama vile Loliondo na Musoma.

Kwa hiyo, ametumia nguvu nyingi sana na kama mtakumbuka, kuna wakati alikuja Mheshimiwa Hilary Clinton, hawajasema tu, lakini ajenda iliyojificha ilikuwa ni juu ya barabara hii. Kwamba, kwa nini Tanzania ijenge hii barabara. Rais alifanya kazi kubwa na wataalam wake, amemwelimisha na amerudi kwao ameelewa. Sasa Mheshimiwa Magufuli, naomba tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kama ulivyofanya, kutengea hela barabara hii, lakini pia Mheshimiwa Rais alisema nina dhamana ya kuleta maendelo kwa watu wanaopakana na maeneo ya wanyamapori ambapo ni Loliondo na maeneo mengine.

Dhamira hiyo njema ya CCM imeoneshwa pia katika llani ya mwaka 2010 - 2015. Niseme tu kwa kifupi manufaa ya barabara hii. Barabara hii ikikamilika, italeta mabadiliko makubwa kiuchumi na kijamii kwa Wananchi ambao watapitiwa na hiyo barabara. Vilevile usafiri wa mabasi na malori utakuwa rahisi, nauli zitashuka kutoka Loliondo kuja Arusha, lakini pia bei za vitu madukani na katika masoko

itapungua. Pia, itakuwa ni njia mbadala, badala ya Watallii kungia tu kupitia Lango la Ngorongoro watakuwa na *option* nyingine ya kupita njia hii kuelekea Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilzungumzia barabara hii mara nyingi, lakini pia barabara hii itaweza kusafirisha mazao ya mifugo na kilimo kwenda katika masoko huko Arusha na maeneo mengine ya Moshi, Musoma na Mwanza. Vilevile Wananchi watapata urahisi wa kufikia huduma za afya na Hospitali za Rufaa, hasa KCMC Moshi na maeneo mengine. Usafirishaji wa mitambo na mafuta ya *generator* kwenda Loliondo itakuwa ni rahisi. Maafisa wa Serikali na Magari ya Serikali yatapita kwa urahisi zaidi. Masuala ya Ulinzi na Usalama katika eneo la *Lake Natron* yataangaliwa zaidi barabara hii itakapokamilika, kwa sababu *Lake Natron* ni *Economic Zone* kwa Mkoa wa Arusha; ni eneo ambalo ni muhimu sana. Pia barabara hii ikikamilika, Wananchi watakuwa wanapita saa 24 badala ya kupita Lango la Ngorongoro ambapo saa 12.30 litakuwa limafungwa kwa sababu ya masharti ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Engineer Urassa kutoka *TANROAD*, alipita kuangalia barabara hii ili kuona ni wapi Wananchi watafidiwa kama kuna mali zozote za Wananchi sehemu ambapo barabara hii itapita. Nafikiri wakashakamilisha utafiti huo, basi taarifa itaandikwa halafu Serikali itaona jinsi gani iwafidie watu hawa. Hata Wananchi wangu wa pale Wasso Mjini wameanza kubomoa nyumba zao ili kupisha ujenzi wa barabara hii. Naomba fidia itayarishwe kwa ajili ya Wananchi hao.

Terehe 2 Agosti, 2012 wakati Mheshimiwa Rais alipofika Loliondo kugawa mifugo kwa Wananchi walioathirika na ukame, alisema kwamba, kwa sababu barabara hii ni ndefu na wafadhilli hawatatupa fedha, tutatumia fedha za ndani, lakini tutaanza ujenzi wa barabara hii kuanzia Loliondo hadi Wasso kwa kilomita 50 kuelekea Sale karibu na Sekondari kwa bajeti hii ya 2013/2014. Bajeti ya mwaka 2014/15 tutajenga kilomita nyingine 50. Tutakwenda polepole hivyo, mpaka tumalize barabara hii, kwa Mheshimiwa sababu Rais

ameendelea kuonesha kwamba ana nia njema ya kujenga barabara hii na ni vizuri tukamuunga mkono kwa barabara hii kuitengea fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi kwa Mheshimiwa Waziri; barabara hii kuna maroli makubwa, mabasi na magari ya watalii yanapita, lakini imeharibika kuliko maelezo. Naomba ututafutie fedha, uipe *TANROAD* Arusha, waendelee kutengeneza au kuikarabati ili wakati tunaendelea kusubiri hizi taratibu za lami zikamilike, barabara hii iendelee kukamilika. Ninakuaminia kwa sababu wakati ule ulinipa shilingi milioni 100 za kutengeneza barabara ile *junction* kutoka Sale kwenda kwa Babu wa Loliondo. Umenipa hiyo fedha, naomba hizi zingine pia zisaidie ukarabati huu, nina hakika ukinisaidia, tutaendelea kuwa na imani na Serikali yetu na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro. Sasa namwita Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Cynthia Ngoye na Mheshimiwa Jerome Bwanausi ajiandae.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli, kwa kweli tunajivunia kama Watanzania. Lazima niseme kwamba, kwa upande wa Mkoa wa Tabora, bado Mheshimiwa Magufuli hajatutendea haki. Hakuna Mkoa wowote ambao unaweza ukawa na maendeleo kama haujafunguliwa na barabara. Ukiangalia historia ya Mikoa yote, Mikoa kwanza unafunguliwa na barabara ndiyo unafungua *channel* za biashara, za wawekezaji, *channel* za kila kitu. Mikoa wa Tabora bado tunaendelea kudumaa kimaendeleo kwa sababu bado tuko kisiwani, hatujafunguliwa hata upande mmoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali mengi tumeuliza hapa Bungeni kuitia kwa Wabunge mbalimbali, ni lini Barabara za Mkao wa Tabora zitakamilika? Majibu ambayo tumekuwa tunapewa ni kwamba, hata Ijumaa, Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba, Barabara za Mkoa wa Tabora zitakamilika ndani ya mkataba. Ningependa kuuliza leo hapa; hivi ni mkataba upi huo wakati barabara zote za Mkoa wa Tabora mikataba ilishapitiliza muda wake? Mikataba mingi ilikuwa inaishia mwaka 2012, mikataba mingine inaishia mwaka huu mwezi wa nne, mkataba mmoja umeisha mwezi wa tano, mikataba ipi ambayo sasa imewekwa ambayo labda sisi Wabunge hatujui kiasi kwamba, tutategemea kwamba ipo mikataba ya kumalizia barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia tu barabara moja ya Tabora - Ndono, mkataba wake umeisha tarehe 4 Januari, 2013. Mheshimiwa Rais ameweuka Jiwe la Msingi tarehe 9 Januari, 2013, sasa nikawa najuliza; hivi ujenzi umeisha, barabara ilitakiwa ikabidhiwe Serikalini, leo inawekwa Jiwe la Msingi; hivi kweli *are we serious?*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ituambie, Barabara za Mkoa wa Tabora hasa zitakamilika lini, kama kuna mikataba ambayo hatujui tuelezwe kwa sababu mikataba yote ilishapita muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013, Wananchi wa Wilaya ya Kaliwa, wakati huo ilikuwa ni Kata ya Kaliwa, walibomolewa nyumba zao kwa madai kwamba kuna upanuzi wa barabara kwa wakati ule, hawakulipwa chochote na wamefutilia kwa muda wote wa miaka kumi mpaka sasa, hawakuwahi kulipwa chochote. Pamoja na kufuatilia katika ngazi zote mpaka kwenda Mahakamani, lakini mpaka leo Serikali haijawapa chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha, mwaka huu wa 2013, Watalaamu wa Mkoa wamefika pale Kaliwa wakati wanapima kwamba barabara itapita wapi wanasema, barabara haitapita kabisa maeneo ambayo watu walivunjiwa nyumba zao, inapita pembezoni kabisa ya

Mji wa Kaliuwa. Ningependa Serikali, iwajibu Wananchi wa pale Kaliuwa, nini hatima ya wale walibomolewa nyumba zao mwaka 2003 na mpaka leo hawakulipwa chochote; lakini pia ni kwa nini Serikali ilichukua jukumu la kubomoa nyumba za watu wakati ilikuwa haijafanya *decision* barabara itapita wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na tetesi mbalimbali kwamba, ilikuwa ni mashinikizo ya Wanasiaya, mmojawapo akiwa ni Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo husika na Wananchi wamekuwa wakisikitika. Tunataka *commitment* ya Serikali, nini hatima ya madai ya Wananchi wote 23 walibomolewa nyumba eneo la Kaliuwa ambao mpaka sasa wanalia hawajawahi kupata haki zao, wakati Serikali inasema inahamisha barabara kutoka pale inapeleka upande mwingine? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara inayoanzia Urambo kwenda mpaka Ulyankulu na nyingine inaanzia Kaliuwa – Uyumbu, kilomita 60 kwenda Mpanda. Barabara hizi kwa kuititia Kikao cha Mkoa, tuliomba Serikali wakubali kuweka kwenye *TANROAD*. Kwa muda wote, barabara hizi zimekuwa zinanyanyuliwa tuta tu, haziwekwi angalau changarawe, kwa hiyo, zinabomoka kweli kweli, zinakuwa kwenye hali mbaya sana.

Mwaka huu Wananchi wa kilomita 60 walitengwa kabisa na wenzao wa Kaliuwa, wakati Kaliuwa ndiyo huduma zote za Hospitali, za masoko zinapatikana. Kutohana na uharibifu wa barabara, akina mama walijifungulia barabarani kwa kukosa huduma ya kuja Kaliuwa kwa ajili ya matibabu. Kwa hiyo, tunaomba sana barabara hizi ambazo zipo ndani ya *TANROAD*, waangalie angalau sasa ziingie kwenye changarawe na *then* ziende kwenye lami, tofauti na kupandisha tuta ambalo mvua zikija nyingi zinabomolewa, matatizo yanabaki palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitishwa na jinsi ambavyo Mkoa wa Dar es Salaam na hasa upande wa Kariakoo, sijui utaratibu gani unaotumika, nimekuwa naona

nyumba ambazo ni za kawaida kabisa, zinabomolewa zinanunuliwa, wanapandisha roshani za ghorofa mpaka 16 na kuendelea. Sasa ninachojiliza, miundombinu ya majitaka ni ileile, sijui jinsi ya kuhimili udongo pale ni ileile, sijui uwezo wake ni kiasi gani, lakini nashangaa kwamba; Serikali inawezaje kuruhusu, jengo dogo la nyumba ya kawaida, libomolewe ipande roshani ya ghorofa 16! Miundombinu ni ileile, tunashuhudia wakati wa mvua, Kariakoo inatapakaa kinyesi kila mahali kwa sababu miundombinu hajarekebishwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunaomba Waziri atuambie ni utaratibu gani ambaao unafuatwa na Serikali wa kuhakikisha kwamba ujenzi wa nyumba kubwa za maghorofa unaenda sambamba na kuboresha miundombinu ya majitaka ili ziweze kuendana na pia kuachana na nyumba kubomoka? Tumeshuhudia utendaji mbovu ndani ya wataalamu wa ujenzi, kwenye Halmashauri zetu, kwenye Manispaa kama ilivyotokea juzi Dar es Salaam, jengo limebomoka kwa sababu kibali kimetolewa, hakuna aliyefuatilia.

Mtu anaomba kibali cha ghorofa kumi, amejenga ghorofa 16, ina maana watalamu wanakaa maofisini! Kwa hiyo, tunaomba wataalamu wasikae maofisini, waende *site*, kama wamempa mtu kibali cha kujenga ghorofa kumi, wafuatilie kweli ghorofa kumi ndiyo zile, siyo baadaye tumeshapoteza maisha ya watu, madhara makubwa, tunaanza kusema, aliomba kumi tumeshangaa amejenga 16; huu ni udhaifu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo mafupi, nashukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ahsante sana, tunakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Ngoye.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Nami ni mmoja kati ya wale ambaao nathamini sana kazi ya Wizara hii ya Ujenzi,

wanafanya kazi nzuri na ni nchi nzima. Pamoja na hisia hizo ambazo kwangu mimi ni za kupongeza kwa namna nyiningine, lakini nilikuwa naomba sana wakati mwингine ahadi zinazotolewa tujaribu kuanza kuzitekeleza kwa namna ambayo inaonesha kwamba tuko *serious*.

Nataka nizungumzie habari za Barabara ya Katumba na kuendelea mpaka Rwanwa, mpaka Tukuyu. Barabara hii ilikuwa katika ahadi za Mheshimiwa Rais mwaka 2005/2006 na ameendelea kuahidi hivyo kwa muda mrefu. Nataka tu nichukue nafasi ya ku-appreciate kwamba, ni kweli Wizara ya Ujenzi ilianza kuchukua hatua zote zanazotakiwa kabla ya kuanza ujenzi. Upembuzi yakinifu umefanyika na upembuzi wa kina umefanyika, lakini tangu hatua hizo zimekwisha, mpaka leo madaraja yaliyoahidiwa kwamba yataanza kujengwa, ambayo ni sahihi kabisa, mpaka leo hayajaanza kujengwa. Sasa leo barabara kweli itaanza kujenga kwa lami kama madaraja hayo hayajajengwa; itawezekana? (*Makofii*)

Mwaka 2011/12, ahadi ilitolewa hapa Bungeni ya kutoa shilingi milioni 600, lakini hazikutolewa. Kwa hiyo, hata daraja moja halijajengwa. Mwaka wa nyuma vilevile zilitolewa ahadi hivyo hivyo za kuanza kujenga haya madaraja mawili ya Mwalisi na Mbaka, hayakujengwa wala fedha haikutolewa; mimi hadithi hii siielewii!

Mwaka huu hapa ninaona zimetolewa shilingi milioni 110, haitawezekana kujenga madaraja hata kama zitatolewa. Nashangaa sana kwa nini barabara hii baada ya kukamilisha hatua zote inalegalega namna hii kuanza kujengwa? Mimi nasifu kazi ya Wizara hii, lakini basi tuangalie pande zote za kona ya nchi hii ili barabara ziwe zinajengwa kwa uwiano. Mara nyangi tumepewa ahadi kwamba itajengwa barabara; mpaka lini? Sasa nataka nilitaarifu tu Bunge lako Tukufu, barabara hii inakwenda kwenye maeneo ya kiuchumi makubwa sana. Gesi mnayoiona hapa nchini, ikiletwa kutengeneza soda kwenye viwanda na inayosafirishwa kwenda nchi zingine za nje, inatoka katika Wilaya ya Rungwe katika maeneo haya ninayoyazungumzia. Inashindwa kusafirishwa kwa sababu barabara ni mbaya

sana na udongo wake ni *volcanic* na mvua za Rungwe ni kati ya milimita 2500 mpaka 2800 kwa mwaka.

Kwa hiyo, barabara ile ni chafu kila wakati, watu tunapita kwa matatizo makubwa. Ukiacha mambo ya gesi, vilevile kuna viwanda vinavyosindika chai katika maeneo hayo na ujuavyo Zao la Chai lazima liwe *transported* kila siku na chai isagwe kila siku. Sasa tusipoitengeneza hii barabara; maana yake nini?

Mimi naamini Wizara ya Ujenzi ina nia nzuri, naomba nia hiyo ikamilike, kwa sababu ya umuhimu wa hizi barabara. Ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa ahadi nyingi, lakini vilevile tujaribu kuangalia maeneo mengine ambayo yana matatizo zaidi kuliko mengine. Kwa hiyo, nilitaka hili lifahamike vizuri sana kwa Mheshimiwa Waziri na kwa kweli Wananchi wa kule walipoona *feasibility study* na *design* imekamilika, walijenga matumaini kabisa kwa Serikali yao. Sasa ni miaka mitatu tangu hatua hizo zikamilike, hakuna kinachoendelea, kila siku ni kelele tu, kwenye RCC ni kelele, naona jambo hili bila shaka litafikia mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika Kikao cha RCC Mbeya, tulikubaliana kwamba, baada ya kuona kuna tatizo kubwa sana la msongamano wa magari katika Jiji la Mbeya, tulikuwa tumependekeza kwamba, barabara ya zamani ya lami iliyokuwa inapita kuanzia eneo la Mlima wa Nyoka, basi iendelezwe hiyo ambayo inapita maeneo ya Uyole ya zamani mpaka Iyunga, mpaka Mbalizi, ikiunganishwa kwenda huko Tunduma na Zambia. Haya maelezo yamekuwa ya siku nyingi sana, yameletwa kwenye Wizara, lakini hatuoni kinachoendelea. Tunaomba sana watu wa Mkoa wa Mbeya, mtusaidie kuondoa ule msongamano, magari makubwa yanapita kwenda Malawi, kwenda Zambia, magari madogo na kila mtu siku hizi anataka kununua magari mawili, matatu, basi ni msongamano ambao hauleti amani kabisa katika kutumia barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho nililotaka kulizungumzia katika hoja hii, ni kweli kwamba, barabara

zinajengwa, ni vizuri, lakini naanza kupata mashaka juu ya uimara wa hizo barabara. Ukipita katika sehemu nyingi, utaona matuta, matuta, baada ya miaka miwili tu barabara imeshapata matuta, kweli huo ndiyo ubora au ndiyo kumaliza fedha za Wananchi tu! Barabara inajengwa, mwakani viraka, keshokutwa viraka tena sehemu nyingine, ukitoka Dar es Salaam ukifika pale eneo lile la Ruvu unakuja kule darajani, ile sehemu ni karibu kila mwaka inatengenezwa, lakini angalia matuta yake yalivyo, haifai kabisa!

Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri anapowabana hawa Makandarasi, awabane vilevile hawa *Consultants*, nao pia wana hoja ya kujibu, kwa sababu wanapitisha tu malipo yafanyike, lakini hakuna ubora wowote unaoonekana katika baadhi ya barabara ingawa nyingine ni nzuri. Mimi namsifu sana Mkandarasi aliyejenga barabara kutoka Uyole kuelekea mpakanı na Malawi. Barabara ile imedumu, hivi sasa mwaka wa 20, imeanza sasa hivi tu kuanza kidogo kidogo kupasuka katika maeneo ambayo watu wanachoma moto na magari yao, lakini *otherwise*, uimara wa barabara ile ni mzuri sana.

Mimi nimeshauri kwamba, tutafute Makandarasi wa aina hiyo, utaambiwa kwamba ni wa gharama sana, ndiyo, lakini kitu kizuri ni kile chenye gharama. Afadhali tujenge barabara ambazo zitakuwa na uimara na zitadumu kwa muda mrefu hata kama gharama hiyo itabidi tuitoe. Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe sana, barabara siyo nzuri sana wala siyo imara sana.

Wengine wanaochafua sana barabara na hili nalizungumza kila mara, watu wanafikiri nalizungumza kwa sababu tu ni masuala ya uharibifu wa mazingira. Mheshimiwa Waziri, shirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kukomesha kabisa tabia ya watu wanaoacha majani na matawi na nini barabarani. Wanachafua barabara zetu, zinaharibika, wanayaacha hapo wanakwenda zao, sasa huo siyo utunzaji mzuri wa barabara; ndiyo ni vizuri kuwa na barabara, lakini tunapofika mahali barabara imechafuka, umeweka alama za barabarani eti matuta! Wapi duniani hapa watu wanatumia majani kama alama za barabarani?

Hakuna! Wapi hapa duniani watu wanatumia matuta makubwa kuwa alama za barabaran? Hakuna! Ni hapa hapa Tanzania, kwa nini tunatumia fedha nyingi na kuharibu barabara zetu. (*Makofi*)

Baada ya maneno haya mafupi, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Cynthia Ngoye ahsante sana. Mheshimiwa Jerome Bwanausi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Aden Rage.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kuweza kupata nafasi ya kuchangia kwenye Hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Magufulli na Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara, kwa jinsi ambavyo kwa kweli wameonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaunganishwa na barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais, aliyekuteua kukurudisha kwenye Wizara hii na juhudhi kubwa anazofanya za kuhakikisha kwamba, fedha zinapatikana ili barabara hizi ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba, juhudhi zinazofanywa na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kuhakikisha wanasmamia barabara zinazojengwa hapa nchini ni kubwa sana. Hata pale ambapo Wakandarasi wanakuwa hawakufanya kazi vizuri, mmekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba, barabara hizi zinarudiwa; kwa kweli nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niishauri Wizara, badala ya kusubiri Wakandarasi wamalize barabara na baadaye zianze kufumuliwa upya, ni vizuri Wizara ya Ujenzi ikaweka mkakati wa kuhakikisha Kitengo cha Ukaguzi wa Barabara wakati zinajengwa kiweze kuimarishwa. Kwa sababu barabara hizi zinapokuwa zimekamilika na baadaye

kufumuliwa; kwa mfano, tumeshuhudia barabara ya Mbagala, barabara ya kule Sekenke, lakini pia kutoka Nangurukuru hadi Mbwenkulu, ililetä adha kubwa na usumbufu mkubwa sana kwa Wananchi wakati iliporudiwa kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni juu ya miradi inayoendelea katika Mikoa ya Kusini. Napongeza juhudzi zinazofanywa na Serikali yetu, lakini naiomba Wizara, iongeze kasi ya usimamizi wa miradi inayofanywa katika Mikoa ya Kusini. Tumekuwa tukilalamika kwa muda mrefu sana juu ya barabara ya Ndunu – Somanga. Mheshimiwa Waziri nimemsikia juzi akiahidi kwamba, mpaka Desemba barabara hii itakuwa imekamilika. Katika barabara ambazo Serikali imetoa ahadi nydingi na kuchelewa kutekelezwa ni barabara hii ya Ndunu – Somanga. Ningewomba Mheshimiwa Waziri, ahadi hii iwe ni ya mwisho kwa Wananchi wa Tanzania na Wananchi wa Kusini kwamba, kweli iwe Desemba, hii barabara ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunao Mradi wa Barabara ya Ulinzi. Umuhimu wa barabara za ulinzi, Mheshimiwa Waziri alishawahi kulieleza Bunge hili, lakini lipotatizo la utekelezaji wa barabara ya kilomita 297 ya kutoka Mangamba kupitia Tandahimba, Newala hadi kwenye Jimbo langu kwenye Kata ya Sindano, Mnavila, hadi Mchaulu, hadi kwenye Jimbo la Nanyumbu. Barabara hii imesahaulika kabisa, nimeona hapa imetengewa shilingi milioni 140, nimekuwa nikijuliza; millioni 140 hii ni ya kufanya nini kwenye kilomita 297? Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, awaambie Wananchi wa Kusini kuhusu barabara hii ya ulinzi; je, itaweza kutengenezwa kwa kiwango kinachostahili? Kwa sababu, baadhi ya madaraja kwenye barabara hii ya ulinzi, ambayo inapakana na Tanzania na Msumbiji, yaling'olewa na hatujui yalipelekwa wapi na kuleta adha kubwa sana Wananchi wa vijiji vya ulinzi ambavyo vilikuwa vimeanzishwa wakati ule wa vita ya Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningetaka nilichangie ni juu ya barabara ya kutoka Mtwara –

Tandahimba – Newala – Nagaga – Chingutwa hadi Masasi, ambayo nashukuru imetengewa shilingi milioni 2500 kwenye Bajeti hii. Naamini hii inawezekana ni kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu, lakini kwa takribani sasa miaka mitatu tangu tuingie hapa Bungeni, barabara hii imekuwa ikisemwa tu na mpaka leo hii tunavyosema, huyo mtaalamu wa kufanya upembuzi yakinifu hajapatikana hadi sasa.

Ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri, nia ya Serikali na ahadi ya Rais ilikuwa barabara hii iwe imeshaanza kutengenezwa kabla ya 2015. Naomba kasi iongezwe ili hii barabara ianzé kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni juu ya kuiombea hii barabara ambayo nimesema ni ya ulinzi, ilishawahi kuombwa na Kamati ya Ushauri ya Mkuu wa Mkoa kwamba, iingizwe kwenye Mpango wa Barabara Kuu, kwa sababu hadi sasa hii barabara imeachwa haishughulikiwi na Serikali Kuu wala haishughulikiwi na Halmashauri zetu. Kwa hiyo ni imani yangu, wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atalizungumzia hilo kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Jimbo langu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, pamoja na Meneja wa TANROAD, kwa jinsi wanavyoshughulikia barabara mbalimbali kwenye Mkoa wetu na hususan katika Jimbo la Lulindi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa unyenyekevu mkubwa sana, tunalo tatizo kwenye Mto Mwiti, katika Kijiji cha Nakalola hadi Kanyindi, pale tunahitaji daraja na pale kumekuwa ni tatizo kubwa sana linalofanya Wananchi wasipate mawasiliano na upande mwagine.

Tumepeleka mapendekezo ya kuomba pesa hizi TANROAD, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, ombi hili ulipe kipaumbele, kwa sababu Halmashauri yetu ya Masasi, haina uwezo wa kujenga daraja hilo. Ukiachilia mbali daraja ambalo lipo kwenye Barabara ya Newala – Masasi, ambalo limetengewa Sh. 90,000,000, tunakushukuru sana, pale Chilungutwa naamini patajengwa. Hili lingine, tunakuomba

sana Mheshimiwa Waziri, ulifanyie kazi ili kuhakikisha Wananchi wa maeneo haya wanapata kipaumbele katika kuhakikisha wanasonga maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sina mengi ya kuchangia kwenye Wizara zaidi ya kuipongeza, waongeze kasi ili maendeleo yapatikane. Naamini yataweza kupatikana kwa juhudzi za uongozi thabiti wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuokoa muda wako, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jerome Bwanausi. Mheshimiwa Ismail Aden Rage, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ningependa kuungana na Wabunge wenzangu wote, kuunga mkono hoja ya Wizara hii. Vilevile nampongeza kaka yangu Kamanda Magufuli, kwa kazi nzuri anayoifanya. Hata hivyo, leo hii nilitaka kujikita katika Barabara za Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchaguliwa kwa kishindo kuititia Tiketi ya Chama cha Mapinduzi, ndani ya siku 107 niliuliza swali la kwanza Bungeni hapa, lilikuwa Swali Na. 77, kwa mujibu wa *Hansard* niliyonayo hapa. Wakati ule Naibu Waziri wa Ujenzi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Maswali yangu nilitaka kuelewa, je, Barabara za Tabora zitakwisha kwa wakati uliopangwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri bila kuwa na wasiwasi na hofu, alinijibu na ninao ushahidi wa *Hansard* hapa kwamba, Barabara za Tabora zitakwisha kwa wakati uliopangwa. (*Makofii*)

Tarehe 15 Februari, niliuliza tena swali lingine hapa hapa ndani ya Bunge, lilikuwa Swali Na. 77. Niliuliza kuhusu Barabara za Tabora kwamba nillalamika Barabara za Tabora

zinasuasua. Safari hii alinijibu mwenyewe kaka yangu Magufuli, akisema kwamba, tangu amekuwa katika Wizara ile, wameshafukuza Makandarasi 2,900. Akatoa tahadhari kwa Makandarasi wa Tabora, wasipomaliza kazi zao kati ya mwaka 2013 na 2014 wajиandae kufukuzwa na wao. (*Makofi*)

Tarehe 12 Juni, 2012, niliuliza tena swalı katika Bunge hili hili, kuhusiana na Barabara za Tabora. Nikatoa taarifa kwamba, Makandarasi wale wanasuasua na hawafanyi kazi yoyote ya maana. Kaka yangu Injinia, Mwanachama mwenzangu wa Simba, Mheshimiwa Gerson Lwenge, akanijibu naye kwamba, usiwe na wasiwasi, barabara zako zitakwisha kwa wakati uliopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spka, Tabora ni Mkoa ambao Wabunge wote 11 ni Wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Nilisikiti sana, Kiongozi mmoja wa Upinzani, alikuwepo Tabora wiki mbili zilizopita akasema maneno ambayo kwa kweli yalitufedhehesha. Nikaona anaji-*contradict* yeye mwenyewe. (*Makofi*)

Tarehe 31 Oktoba, Rais alipokuwa anafungua kule Hai, Kiongozi huyu alimsifia Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kufunguliwa barabara zake. Kwa hiyo, alipofika Tabora akaponda kwamba eti Barabara za Tabora haziwezi kujengwa mpaka Wapinzani washike Mkoa wa Taboara. Ninataka kuwaambia hiyo ni ndoto na wasahau kabisa, Tabora ni ya CCM na itaendelea kuwa chini ya CCM. (*Makofi*)

Ninataka nimpongeze Mheshimiwa Andrew Chenge, leo asubuhi alipokuwa anachangia ametoa ushauri mzuri sana. Kwamba, hizi barabara zinazochelewa sasa hivi, ambazo tayari Serikali imeshaingia mikataba na Wakandarasi, ni vyema Serikali ikatafuta pesa Benki ili kuhakikisha Miradi hii inakwisha. (*Makofi*)

Ninasema hivyo kwa sababu nimejaribu kufanya mahesabu kidogo hapa kwa barabara za Mkoa wa Tabora; Barabara ya Nzega - Puge, ambayo imechelewa kwa miezi

22, kama itaendelea kujengwa kwa sababu muda wake ulitakiwa uishe tarehe 2 Mei, wameongezewa waendelee kujenga, kwa hiyo, Serikali itapata hasara siyo chini ya shilingi bilioni 2.3.

Barabara ya Puge – Tabora, itakapokwisha Serikali itapata hasara siyo chini ya shilingi bilioni 2.8. Tabora – Nyahua shilingi 146,000,000. Tabora – Ndono, shilingi bilioni 3.9. Ndono – Urambo watapata hasara kiasi cha shilingi bilioni 1.4. Hivi sasa Miradi minne kati ya miradi mitano ya Tabora yote imeshakwisha mikataba yake. Ina maana ya kwamba, Mkandarasi ataendelea kufanya kazi lakini kwa kuwa tumechelewesha malipo, atadai *interest*. Sasa ninaishauri Serikali yangu, kwa nia nzuri na kwa uwezo ambao ninamwamini Mheshimiwa Dkt. Magufuli na hasa nimefarijika juzi aliponihakikishia ndani ya Bunge hili kwamba, bararara hizi zitakwisha kwa wakati unaotakikana.

Nami nina imani hiyo kwa sababu tarehe 5 Januari, 2013 katika Viwanja vya Chipukizi, alikuwa amefuatana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Magufuli bila hofu na kwa kuwa ninamwamini, sina wasiwasi hata kidogo, aliwaahidi Wananchi wa Tabora, mimi sina kusudio la kutoa shilingi hata siku moja. Ninamwomba atakapokuja kutoa majumuisho, awahakikishie tu Wananchi wa Tabora kwamba, Serikali ya CCM pekee ndiyo yenyе uwezo wa kuwajengea barabara za lami na tutazipata kama alivyoahidi kabla ya mwaka 2014 kwisha. Nina imani kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka vilevile kuongelea juu ya fidia. Kuna barabara inayotoka Tabora kwenda Ndono, Wananchi wa pale wengine wamelipwa fidia wameafiki na wengine hawakuafiki, kwa sababu ya soko la maeneo yale, *market value*. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri, bahati nzuri kwa Mkoa wa Tabora tumepata bahati, tunaye *Regional Engineer* mzuri sana, msikivu, ana nidhamu ya hali ya juu; hebu tuangalie hizi fidia ambazo tumeahidi tutawapa Wananchi tuweze kuwapatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono Bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimwa Rage. Mheshimiwa Selemani Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia ni mmoja kati ya Wabunge ambao tunaridhishwa kiujumla na kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara ya Ujenzi, katika kuhakikisha kwamba, nchi yetu inakuwa na barabara nzuri zinazopitika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, ninapenda nitumie fursa hii na mimi kama mmoja wa Wabunge wa Mkoa wa Tabora, niombe kwa dhati kabisa, Waziri, kaka yetu, ambaye tunamwamini na tunaridhishwa sana na kazi zake, Mheshimiwa Magufuli, asikie kilio cha Wabunge wa Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora kwa upande wa barabara tumeachwa nyuma. Mkoa wa Tabora ni mkubwa, kwa eneo la ardhi Mkoa wa Tabora ni asilimia kumi ya nchi nzima ya Tanzania. Pamoja na ukubwa wake wote huo, ndiyo Mkoa ambao ukiingia Makao Makuu ya Mkoa kutokea upande wowote ule unaingia ukiwa unaingia kwa barabara ya vumbi. Makao Makuu ya Mkoa wa Tabora, huwezi kuingia kwa lami, sehemu zote unapopita ukiingia unaiingia kwa bara ya vumbi. Inatia aibu na tunaomba kama nilivyosema, tuna imani na Wizara na tunamwamini Mheshimiwa Magufuli, tunaomba safari hii kilio cha Wanatabora kisikike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 7, 8 na 9 Januari, 2013, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya ziara Mkoani Tabora, aliongozana na Mheshimiwa Magufuli na Wabunge wote wa Mkoa wa

Tabora tulikuwepo. Kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais aliifanya ni kuzindua na kuweka Mawe ya Msingi barabara hizi lakini na kutoa uhakika kwa Wanatabora kwamba, barabara hizi zitakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Tabora wanayo imani kubwa sana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kwa hiyo, hatutaki muda uende, ahadi hii ambayo Wananchi wana imani nayo kubwa sana ishindwe kutekelezeka; itakuwa ni aibu na hatutakuwa na mahali pa kuweka sura zetu. Tunamwoba Mheshimiwa Magufuli, tunaiomba Wizara ya Ujenzi na tunaiomba Serikali ya CCM ambayo tunaiamini sana, kuhakikisha kwamba Barabara za Mkoa wa Tabora safari hii, zote tatu, zinakamilika kwa kiwango na kwa matarajio ambayo Wananchi wa Tabora wanayo. (*Makofi*)

Kaka yangu Mheshimiwa Ismail Aden Rage, amezungumza mengi, kwa hiyo, sipendi sana kurudia, lakini nadhani Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni msikivu, Serikali ya CCM ni sikivu, haya yote ambayo Wabunge wa Tabora tumeyasema kuhusu barabara, safari hii yatafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mhehimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la Mfuko wa Barabara. Tunafahamu kwamba, Bararaba za Halmashari zetu zinakarabatiwa kwa kutumia fedha ambazo zinatoka katika Mfuko wa Barabara. Rai yangu hapa ni kwamba, Wizara igawe fedha hizi kwa kuzingatia *net-work* ya barabara katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano wa Wilaya yangu ya Nzega; Wilaya ya Nzega, ina *net-work* ya barabara ya kilometra 760, lakini utakuta fedha za Mfuko wa Barabara ambazo tunapata kwa ajili ya kukarabati Barabara ya Nzega; kwa mfano, Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, tulipata shilingi milioni 772. Fedha hizi zinatosha kuhudumia asilimia 50 ya barabara zote zilizoko ndani ya Wilaya ya Nzega. Kwa hiyo, fedha tunazopata zinaweza kuhudumia asilimia 50 tu.

Tatizo lingine, mpaka mwaka unaisha, kwa mfano, mwaka 2012/2013, mpaka mwezi Aprili, 2013 ni Sh. 344,000,000 tu ambazo zimepokelewa, ambazo ni kama asilimia 45. Kwa hiyo, kwanza, fedha zinazokuja zinatosha nusu tu ya *net-work* nzima ya barabara. Halafu hata hizo nusu, mpaka mwaka unafika unakuta ni asilimia 40 au 50 ya hizo nusu ambayo ndiyo inafika. Kwa hiyo, unakuta hakuna namna ambayo tunaweza kuhakikisha barabara zetu zinakuwa katika hali nzuri. Kwa hiyo, Mfuko wa Barabara uzingatie *net-work* ya barabara katika Halmashauri husika, angalau fedha zinazokuja ziwe katika asilimia ya kutosha, angalau asilimia 80 – 90 ya kuweza kuhudumia barabara ambazo zipo katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Magufuli kwamba, kuna barabara inayotokea Tabora inapita Mambali, inapita Bukene, Itobo na Kahama. Barabara hii imetajwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwamba, katika kipindi hiki cha awamu ya nne, itafanyiwa upembizi yakinifu, kama maandalizi ya kuitafutia fedha ili sasa iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa tatu sasa sijaona mpango wowote wa makusudi wa Wizara hii kutafuta fedha ili barabara hii ambayo itatoka Tabora mpaka Kahama, kwa rafiki yangu Mheshimiwa Maige, iweze kufanyiwa upembizi yakinifu, kwa maandalizi sasa ya kutafutiwa fedha ili ijengwe kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo ni rai yangu kwamba, kama nilivyosema mwanzo, ninamwamini sana, ninakubali utendaji kazi wa Mheshimiwa Magufuli, kwa hiyo, jambo ambalo limetajwa katika Ilani ni jambo ambalo kwa namna yoyote ile lazima litekelezwe. Kwa hiyo, fedha zipatikane, barabara hii ifanyiwe kazi, ili mwishoni mwa Awamu ya Nne, barabara hii iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kiujumla, kama tunataka kuwasaidia Wananchi wetu hasa wanaoishi maeneo ya vijijini, basi barabara kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia, ndiyo mishipa ya damu

katika uchumi. Kwa sababu moja ya sababu inayofanya kilimo chetu kisiwe na tija, ni kwamba, katika maeneo ambako wakulima wetu wapo hakufikiki, hakuna barabara. Kwa hiyo, kwanza, upelekaji wa pembejeo unakuwa mgumu, lakini hata wakulima wakilima, yale mazao yao hawawezi kuyafikisha sokoni ambako kuna bei nzuri wapate tija. Kwa hiyo, kama hakuna barabara maana yake una-*paralyse* hata uchumi.

Kwa hiyo, maeneo ambayo uzalishaji unatokea, mazao hayawezi kwenda katika eneo lingine na hata namna ya kuwasaidia wakulima kwa maana ya kufikisha huduma za ugani, mbolea na mbegu bora haitawezekana. Tunapozungumzia barabara, maana yake tunazungumzia uchumi. Tuchukue barabara kama ni nyezo muhimu ambayo inaweza kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kwa maana yoyote ile ni kwamba, kuna kila sababu ya kutoa umuhimu mkubwa wa kuhakikisha barabara zetu hasa za maeneo ya vijijini ambako uzalishaji unafanyika, zinakuwa katika kiwango ambacho kinapitika muda wote.

Mheshimiwa Niabu Spika, ninaomba nimalizie kwa kumkumbusha na kurudia tena kauli yangu ya mwanzo; niungane mkono na kama yangu Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, amezungumza vizuri sana, amesitisizia sana umuhimu wa Barabara za Tabora. Kwa niaba ya Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, tunakuomba usikie kilio cha Wabunge wa Tabora. Sikia kilio cha Wananchi wa Tabora. Mkoa wa Tabora ni mmoja kati ya mikoa ambayo siku zote unatoa kura nydingi sana kwa Chama cha Mapinduzi, tunaiamini Serikali, tunakuamini Mheshimiwa Magufuli, barabara za Tabora safari hii zikamilike.

Ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.
(Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zedi. Watani zangu wote mmesikika jamani. Ahsante sana. Hata Kongwa hakuna lami jamani siyo Tabora tu.

Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu. Mheshimiwa Machali na wengine, kesho tarehe 14 Mei, 2013 nitawakumbuka ambao hamkupata nafasi leo, tutaendelea na uchangiaji wetu na kumalizia kesho asubuhi. Kesho jioni tutapitia mafungu ya Wizara hii.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwakumbushe kwamba, Randama ya Fungu Na. 98 ipo na mimi ninazo nakala za ziada hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge yejote, kesho wakati tunaendelea ukihitaji kuangalia angalia, ni vizuri kupitia, kwa sababu maelezo mengi sana ya maswali ambayo Wabunge wanapenda kuuliza ya Fungu hili kwa nini limefanya hivi, limefanya vile au lina madhumuni gani, maelezo yote yako ndani ya Randama. Kwa hiyo, kesho wakati wa Mafungu, yale maswali tuliyoyazoea ya rejareja yale hatutayaruhusu. Yale ya mtu sema usikike, kwa sababu maelezo yako ndani ya Kitabu hiki na tutakuwa na muda wa kutosha asubuhi, kama nilivyosema mimi ninayo nakala hapa; Mbunge yejote atakayehitaji nitaweza kumwazima akaangalia na mwingine pia, tunazo nakala zingine za ziada.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata vikaratasi vingi ambavyo vimekuwa vikiulizia Kanuni ya Mavazi na Wabunge wengi wakiulizia uvaaji wa *combat* ndani ya Ukumbi wa Bunge, endapo ni sawa au siyo sawa. Endapo jambo hili linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kila mmoja aende kusoma Kanuni ya 149(a) kwa akina mama na 149(b) kwa akina baba. Ni vizuri kila mtu ajisomee mwenyewe halafu apime, aone mavazi anayokuja nayo humu ndani ni sawa sawa au siyo sawa sawa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, huwa ni aibu kwa Mbunge kutolewa Bungeni kwa sababu ya mavazi, umevaa ambavyo sivyo; ni aibu sana kwa wapiga kura wako, siyo vizuri Kiti kufanya hivyo. Tunatakiwa kusoma tu na kupima kama unaona ni sawa sawa, endelea na kama unadhani siyo sawa ni vizuri kubadilika, kwenda na mavazi ambayo yanakubalika humu ndani, bila bughudha zozote zile. Zipo *combat* nyeusi,

zipo za kaki na zipo za *blue*. Sasa kuna wale wanaotaka kuja na *combat* za kijani, mwisho itakuwa tabu kidogo. Kwa hiyo, hilo ninawaomba mjisomee wenyewe ili isijitokeze yale mambo ya kuombwa utoke nje.

Mwisho kabisa, tunao wageni ambao walichelewa kufika kidogo, ambao ninaomba niwakaribishe sana, wanatoka Mikoa ya Shinyanga, Morogoro, Mara, Mwanza, Arusha na Dar es Salaam, wamekuja kwa ajili ya mafunzo ya Bunge. Vilevile mafunzo kuhusu masuala ya upimaji ardhii, ambaao ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Anne Tibaijuka. Ninawakaribisheni sana. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, kwa mujibu wa *Order Paper* ya leo, shughuli zilizopangwa leo zote zimekamilika na muda wetu ndiyo huo. Kwa hiyo, ninaomba nichukue fursa hii kuahirisha shughull za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 1.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 14 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi*)